AALI BA ALAWIY

SEHEMU YA KWANZA

MKUSANYAJI

MANSOOR A. SAMEJA

UTANGULIZI:

Namshukuru Mwenyezi Mungu aliye tujaalia neema ya Uislamu baada ya neema ya kutuumba. Na rehema na amani zimshukie Mtume wetu Muhammad –Rehema za Mwenyezi Mungu na Amani zimshukie- aliye tumwa kututoa kwenye kiza cha ukafiri na kutuongoza kwenye nuru ya Uislamu, na ziwashukie pia jamaa zake tulio amrishwa kuwapenda ndani ya Qur-ani na zisiwawache pia masahaba wake na wafuasi wao hadi siku ya Kiyama.

Ama baada ya kumshukuru Mola na kumsalia Bwana Mtume (SAW), hatuna budi kushukuru neema ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia wakazi wa Afrika ya Mashariki; nayo ni kutuletea masharifu wanavyuoni wa Ba Alawy, kutufundisha Dini yetu na kutuongoza kwa vitendo katika njia sahihi ya kufuata Qur'ani na mwenendo wa mbora wa viumbe, Mtume Muhammad (SAW), pamoja na waja wema (salaf salalih). Hakika wao wamekuwa ni mfano mzuri mno wa kuigwa, "Alhamduli-Llah"! Kwa hivyo, katika kujenga imani na uislamu wetu, ni muhimu sana kwa waislamu kuwajua na kuelewa mienendo yao na tabia (akhlaqi) zao njema.

Cha kusikitisha, ni kwamba Waislamu wengi wa Afrika Mashariki au wenye asili yake hatutambui mchango wa masharifu wanavyuoni hawa wa Ba Alawy na wala hatuzijui historia zao; na kila kukicha tatizo hili linazidi kuwa kubwa. Pamoja na hili, hatufuati mwenendo na tabia zao njema ima kwa kutokujua au kwa sababu ya kutingwa na Dunia, sheitani, na matamanio ya nafsi.

Na kwa kuwa ni wajibu wetu kukumbushana, tumeandika kitabu hiki kueleza asili yao, mwenendo wao, tabia zao na matendo yao mema ili pamoja na kuwafahamu, tufuate mwenendo wao, kwani haiwezi kusilihi (kutengenea) sehemu ya mwisho ya Umma huu ila kwa kufuata njia sahihi ya wale wa mwanzo kama alivyo sema Imamu Malik(ra).

Hali kadhalika, kwa kufuata nasaha hizi na nyengine kama hizi huenda tukaingia kwenye bishara ya Mtume(saw) kwa kuhuisha Sunna yake na kutengeneza yale yaliyo haribika,. Katika bishara yake, Bwana Mtume(saw) alisema, **"Uislamu ulianza ukiwa mgeni (kwa watu) na utarudi kuwa mgeni kama ulivyo anza, basi** furaha iliyoje kwa hao watakaokuwa wageni**",** akaulizwa: Ewe Mtume(saw) wa Allah! Ni kina nani hao wageni? Akajibu**: "Ni wale watakao tengeneza (mambo) wakati wa kufisidika watu"**. Na katika riwaya nyengine: **"Ni wale wanao huisha Sunna yangu na kuwafundisha waja wa Mwenyezi Mungu".**

Na Habiib Abdillah Al-Haddaad anasema katika *Risalatul-Muawana*: "Na ama mwenye kulingania kuelekea kwenye mlango wa Mwenyezi Mungu pamoja na kuilaumu nafsi yake na kuizuia na kuwa na mapungufu (kwenye kutekeleza maamrisho yake) na akaihimiza kufanya jitihada, anategemewa zaidi kupata kuokoka kuliko yule anaye amrisha mema na kukataza mabaya na huku hatekelezi wala hana nia ya kweli. Na kwa hali yoyote ile , yule anaye jua na kufundisha na hatendi (kwa mujibu wa elimu yake) ni afadhali na anakaribia njia iliyo sawa na mwisho mwema kuliko yule asiye tenda wala hafundishi". *Mwisho wa kunukuu.* Na sisi tunakiri makosa yetu na tunafanya jitihada kufuata mwenendo wao huku tukitaka msaada wa Mwenyezi Mungu.

Kitabu hiki tunakiandika kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atutakabalie, na atupe Radhi Zake. Matumaini yetu ni kuwa kitakuja kuwa na manufaa kwetu na kwa vizazi vyetu, na kiwe ni kichocheo kwetu katika kuufuata mwenendo wa Mtume (SAW) na waja wema walio tangulia, tupate kufaulu duniani na akhera, kwani Yeye ni Muweza juu ya kila kitu, Aamiin.

Tanbihi: Kwenye kufasiri aya za Qur-ani tumetumia tafsiri ya Muntakhab ya Sheikh Ali Muhsin Barwani, Mwenyezi Mungu amrehemu.

YALIYOMO

UTANGULIZI: 2
UTUKUFU WA AHLIL BAYT 8
TARJAMA YA AHLIL KISAA 36
WAASISI WA BA ALAWIY 148
BAADHI YA VIONGOZI WA AALI BA ALAWIY 174
AALI BA ALAWIY AFRIKA MASHARIKI 240

AHLIL BAYT

- UTUKUFU WA AHLIL BAYT
- TARJAMA YA AHLIL KISAA

UTUKUFU WA AHLIL BAYT

- Aya za Qur-an zinazowaelezea Ahlil Bayt
- Hadithi za Mtume zinazowaelezea Ahlil Bayt
- Maneno ya Masahaba na Salaf katika kuwazungumzia Ahlil Bayt
- Wajibu wa Ahlil Bayt
- Masahaba wa Mtume

Kwa kuwa ukoo wa Ba Alawiy ni wajukuu wa Mtume(saw) na ni sehemu ya Ahlil bayt, tunaanza kitabu hiki na kuelezea utukufu wa Ahlil Bayt.

Aya za Qur-an zinazowaelezea Ahlil Bayt

1.

قُل لَّآ أَسۡـَٔلُكُمۡ عَلَيۡهِ أَجۡرًا إِلَّا ٱلۡمَوَدَّةَ فِي ٱلۡقُرۡبَىٰۗ

“Sema: Sikuombeni malipo ila kuwapenda jamaa zangu”. (Shuura, 23).

Imepokewa na Sahaba Ibn Abbas kuwa ilipo shuka aya hii, (masahaba) walimuuliza (Bwana Mtume (SAW),) “nani qaraaba (ndugu/jamaa) wako (waliotajwa kwenye aya) ambao tuliolazimishwa kuwapenda?” Mtume(SAW) akajibu: “Ali, Fatima na watoto wao wawili (yaani Hasan na Husain)”. Imepokewa na maimamu Ahmad, Tabraaniy, Ibn Abiy Hatim, na Al-Hakim. Na imetajwa kwenye tafsiri zifuatazo: *Ibn Kathiir, Qurtubiy*, na *Durrul-Manthur* ya *Suyutiy*.

Na katika hadithi nyingine:

إن اللّٰه تعالى جعل أجري عليكم المودة في أهل بيتي وإني سائلكم غدا عنهم أخرجه الملاء في سيرته

“Hakika Mwenyezi Mungu amejaalia ujira wangu kwenu katika kuwapenda Ahli bayti wangu na mimi ni mwenye kukuulizeni kwa hayo kesho (Kiyama)”**.** Imepokewa na Mulla kwenye Sira.

Na katika *Durrul-Manthur* yametajwa maneno ya Sayyidna Ali aliyoyapokea Abu Shaykh: “Kwetu sisi Aali Muhammad imeshuka aya: Hahifadhi mapenzi yetu ila kila muumini, kisha akasoma aya

قُل لَّآ أَسۡـَٔلُكُمۡ عَلَيۡهِ أَجۡرًا إِلَّا ٱلۡمَوَدَّةَ فِي ٱلۡقُرۡبَىٰۗ

Wamepokea maimamu Al-Bazzaar na Al-Tabraaniy: Kuwa Sayyidna Hasan bin Aliy alitoa khutba na katika jumla ya maneno aliyo yasema ni: “Mwenye kunifahamu amenifahamu na asiye nifahamu basi mimi ni Hasan bin Muhammad”, kisha akasoma aya:

وَٱتَّبَعْتُ مِلَّةَ ءَابَآءِىٓ إِبْرَٰهِيمَ

Na nimefuata mila za baba yangu Ibrahim …(Yusuf:38)

“Mimi ni mtoto wa ***Bashiir*** (Mbashiria watu wema Pepo), mimi ni mtoto wa ***Nadhiir*** (Mkhofishaji watu waovu na moto)”, kisha akasema “Mimi ni katika ***Ahlil-bayti*** ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amefaradhisha kuwapenda na kuwafanyia nusura na usaidizi”**.** Akaendelea kusema, “(Mwenyezi Mungu) katika aliyoyashusha kwa Muhammad-Rehema na Amani zimshukie:

قُل لَّآ أَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا ٱلْمَوَدَّةَ فِى ٱلْقُرْبَىٰ ۗ

Na imepokewa na Imaam Al-Tabraaniy kutoka kwa Zaynil Abidiin (Aliy bin Husain bin Aliy) alipo-letwa hali ya kuwa mateka baada ya kuuawa baba yake Husain, akasema mmoja wa watu wa Sham, “Sifa zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu aliyekuueni na akamaliza mzizi wenu na akakata shina la fitna”. Akasema (Bwana Ali - Zaynil-Abidin),: “Je, hujasoma (aya)

قُل لَّآ أَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا ٱلْمَوَدَّةَ فِى ٱلْقُرْبَىٰ ۗ

Akauliza: “Ndio nyie kwani?” Akajibu, ***“naam (ndio sisi)”.***

Na Imaam Shafiy-Allah amrehemu-anathibitisha hayo kupitia mashairi yake alipo sema:

يا أهل بيت رسول الله حبكم فرض من الله في القرآن انزله

كفاكم من عظيم الأجر أنكم من لم يصل عليكم لا صلاة له

Enyi Ahli bayti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, mapenzi yenu ni faradhi Aliyo ishusha Mwenyezi Mungu kwenye Qurani.

Unakutosheni ubora wa malipo kuwa asiye kuswalieni hana Swala (yaani haijakamilika).

2.

إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجْسَ أَهْلَ ٱلْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا

“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa Nyumba ya Mtume(saw) na kukusafisheni barabara”.
(Al-Ahzaab, 33).

Amesema Imaam Ibn Hajar Al-Haitamiy kuwa wafasiri wengi wanakubaliana kuwa aya hii imeshuka kwa ajili ya Mtume(saw), Sayyidna Ali, Sayyidatna Fatima, Sayyidna Hasan na Sayyidna Husain.

Amepokea Imaam Muslim katika hadithi ndefu ya Sayyidatna Aisha kuwa Mtume(saw) aliwaingiza hawa wanne ndani ya shuka (***kisaa***) na kisha akasoma aya hiyo hapo juu.

Amepokea Imaam Ahmad kwa riwaya ya Sahaba Abii Saiid Al-Khudriy: kwamba imeshuka aya hii kwa ajili ya watu watano; Mtume -Rehema na Amani zimshukie- Ali, Fatima, Hasan na Husain.

Imepokewa na Imaam Tabraaniy kwamba Mtume(saw) amesema:

أنزلت هذه الآية في خمسة، فيّ وفي علي والحسن والحسين وفاطمة

“Imeshuka aya hii kwa ajili ya watu watano; kwa ajili yangu na kwa ajili ya Ali, Hasan, Husain na Fatima”.

Kwa kuongezea, imepokewa na Maimamu Ahmad, Tirmidhiy na Tabraaniy kwa riwaya sahihi, na imetajwa na Imaam Suyuti katika Tafsiri yake na Haythamiy katika Majmaa kwamba, “Mtume(saw) aliwafunika na shuka na kusema:

أَللَّهُمَّ هَؤُلَاءِ أهل بَيْتِي وحامتي أذهب عَنْهُم الرجس وطهرهم تَطْهِيرا

‘Ewe Mwenyezi Mungu hawa ni Ahli bayti wangu na walio karibu zaidi kwangu, basi waondolee uchafu na wasafishe kuwasafisha ...’

Mama Ummu Salamah akasema, ‘Na mimi niko na wao’. Mtume(saw) akamwambia, ‘Wewe uko juu ya kheri’”.

Katika riwaya ya Imaam Tirmidhiy haya yote yalifanyika kwenye nyumba ya Ummu Salamah.

Imepokewa na Imaam Ahmad kwamba Mtume(saw) alikuwa anapotoka kwa ajili ya Swala ya Alfajiri anapitia nyumba ya mwanawe Sayyidatna Fatima na kusema, “Swalaa enyi Ahlil-bayti!” Na kisha husoma aya hii

إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجْسَ أَهْلَ ٱلْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا

Imepokewa na maimamu Bazzaar, Ibn Asakir na Tabraaniy kwamba Sayyidna Hasan alipokuwa Iraq, alipokuwa akiswali, akaja mtu akamchoma na jambia (kisu chenye ncha mbili) na yeye yuko kwenye hali ya kusujudu. Alipo maliza Swala akatoa khutba akasema, “Enyi watu wa Iraq! Mcheni Mwenyezi Mungu kwetu sisi (msitufanyie maovu) kwani sisi ni watawala wenu na ni wageni wenu na sisi ndio Ahlil-bayti ambao Mwenyezi Mungu amesema kuwakhusu wao:

إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذۡهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجۡسَ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِ وَيُطَهِّرَكُمۡ تَطۡهِيرًا

Basi hakuacha kuikariri aya hiyo hadi hakubakia mtu msikitini ila alilia (machozi).

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas - Mwenyezi Mungu amrehemu, "Ahlil bayti wanaendea na kujipamba (na yaliyo mema) na wasio wao huendea kujivua (na yaliyo mabaya) kwanza (kabla ya kujipamba na yaliyo mema), amesema Mwenyezi Mungu: **"Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu**". (Ahzaab:33) Akataja "***ankum"*** na hakusema "***minkum***". Na kwenye maneno yake mengine: "Ahlil bayti dhati zao zimesafika, na kwa hakika tabia mbaya zinaingia kwao kutokana na kukaa na walio wajinga na wenye kughafilika kwa neno la Mwenyezi Mungu aliye tukuka: **"Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu**" (Ahzaab:33), akataja ***ankum*** na hakusema ***minkum*** basi ***an*** haikuletwa kwa ***dharfiyya – uchombo/uelezi*** na hiyo haijulishi kingine ila kuwa ni kitu ambacho kinakuja juu yake (kinacho zuka). Na mfano ni kama johari yenye thamani unaiweka sehemu ambayo haistahiki kama kwenye rafu (ya vitabu) na jalalani, basi sifa zake zikatofautiana kwa kutofautiana sehemu ilipo, basi hukumu ni kwa sehemu ilipo wakati ule. Uhakika wake ni kuwa ni safi, ikiweko kwenye rafu imefunikwa na uchafu wa vumbi, na jalalani (imefunikwa na) najisi, na dhati yake haijabadilika".

3.

فَمَنۡ حَآجَّكَ فِيهِ مِنۢ بَعۡدِ مَا جَآءَكَ مِنَ ٱلۡعِلۡمِ فَقُلۡ تَعَالَوۡاْ نَدۡعُ أَبۡنَآءَنَا وَأَبۡنَآءَكُمۡ وَنِسَآءَنَا

وَنِسَآءَكُمْ وَأَنفُسَنَا وَأَنفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ ٱللَّهِ عَلَى ٱلْكَٰذِبِينَ

"Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo". (Aali Imran:61).

Aya hii ni mashuhuri; inaitwa *Ayatul-mubaahala*. Kisa chake ni kama kifuatavyo: Alijiwa Mtume(SAW)-rehema na amani zimshukie- na wakristo wa Najraan wakiwa na wanavyuoni wao, wakashindana na Mtume(saw) kuhusu Nabii Isa (AS), Mtume (SAW)-rehema na amani zimshukie- akawashinda kwa hoja wakakataa kukubali haki. Hapo Mtume(SAW) akaamrishwa na Mwenyezi Mungu afanye *mubaahala*, yaani kila kikundi kimwombe Mwenyezi Mungu aishushe laana kwa aliye mwongo. Wakristo wakawaomba ushauri maaskofu wao. Maaskofu wakajibu, "Wallahi hakuna aliye fanya *mubaahala* na nabii yeyote, akaishi mkubwa wao na akakua mdogo wao, na kama mukifanya mutamalizwa nyote" (Kisa hiki kimetajwa kwenye tafsiri ya Ibn Kathiir na zengine, kwenye sira ya Ibn Hishaam, na baadhi yake imepokewa na Bukhari na Muslim)

Mwandishi wa *Al-Kashhaaf* amesema: "Hakuna dalili yenye nguvu zaidi kuliko hii juu ya ubora wa watu wa *Kisaa* (watu walio funikwa shuka ya Mtume(SAW)), nao ni Aliy, Fatima na Hasanain (yaani Hasan na Husain), kwani iliposhuka aya hii (Mtume(saw)) aliwaita, akambeba Husain, akamshika mkono Hasan, na Fatima akatembea nyuma yao, na akatembea Aliy nyuma yao, basi ikajulikana kuwa wao ndio walio kusudiwa na Aya na kwamba watoto wa Fatima wananasibishwa kwake mnasaba ulio sahihi wenye kunufaisha duniani na akhera".

Bwana Mtume(SAW)-rehema na amani zimshukie- alipo kuja akiwa amembeba Husain na ameushika mkono wa Hasan, Fatma akiwa nyuma

yao na Aliy akiwa nyuma yao, alisema askofu, “Enyi wakristo hakika ninaona nyuso lau kama wangemwomba Mwenyezi Mungu aondoe jabali mahala lilipo angeliondoa kwa ajili yao, basi musifanye *mubaahala* nao mutaangamia, na hatobaki mkristo yeyote juu ya uso wa ardhi hadi siku ya Kiyama”. Wakaogopa na wakakataa *mubaahala*, wakaridhia kutoa kodi. Kuhusiana na kadhia hii, Bwana Mtume(saw) alisema, “Namwapia ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, hakika maangamizo yalishakuwa tayari kwa watu wa Najraan, na kama wangefanya ulaani wangegeuzwa ngedere na nguruwe, na wangwa wao ungeungua moto na Mwenyezi Mungu angekimaliza kizazi cha Najraan, hata ndege juu ya miti; na usingepita mwaka ila wangeangamia wakristo wote”.

Imepokewa na maimamu Daruqutniy na Ibn Asaakir kuwa Sayyidna Aliy alisema siku ya Shuura na akatoa hoja juu ya wengine, akasema: Ninakuapieni kwa Allah, je, kuna mmoja wenu ambaye ni karibu kiujamaa kwa Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu kuliko mimi, na ambaye Mtume(saw) amejaalia kuwa ni nafsi yake, na watoto wake kuwa ni watoto wake (Mtume(saw)) na wake zake kuwa ni wake zake (Mtume(saw)) asiye mimi?! Wakasema: Allahumma Laa, yaani hapana.

4.

إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلَٰٓئِكَتَهُۥ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِيِّۚ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ صَلُّواْ عَلَيۡهِ وَسَلِّمُواْ تَسۡلِيمًا

“Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu”. (Al-Ahzaab aya ya 56).

Imepokewa na Ka’ab bin Ujrah kuwa iliposhuka aya hii tukamwambia Mtume(saw): Hakika tumeshajua tukusalimu vipi, ama kukuswalia tukuswalie vipi? Akasema: Semeni *Allahumma Swalli alaa Muhammad wa alaa Aali Muhammad*”. Hadithi hii ni sahihi imepokewa na

maimamu wengi wa Hadithi akiwemo Bukhary, Muslim, Ahmad, Abu Daud, Tirmidhy, Nasaai na Ibn Maajah.

Na katika riwaya nyingine aliyoipokea Imaam Al-Haakim: Tulimwuliza ewe Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu vipi tukuswalieni Ahlil-Bayt? Akasema: *Allahumma Swalli alaa Muhammad wa alaa Aali Muhammad* ...".

Hadithi za Mtume(saw) zinazowaelezea Ahlil-bayt:

Mtume(saw) katuwachia kizazi chake:

قَامَ رَسُولُ اللَّهِ –صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ– يَوْمًا فِينَا خَطِيبًا بِمَا يُدْعَى خُمًّا بَيْنَ مَكَّةَ وَالْمَدِينَةِ فَحَمِدَ اللَّهَ وَأَثْنَى عَلَيْهِ وَوَعَظَ وَذَكَّرَ ثُمَّ قَالَ: "أَمَّا بَعْدُ, أَلَا أَيُّهَا النَّاسُ فَإِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ يُوشِكُ أَنْ يَأْتِيَ رَسُولُ رَبِّي فَأُجِيبُ, وَأَنَا تَارِكٌ فِيكُمْ ثَقَلَيْنِ: أَوَّلُهُمَا كِتَابُ اللَّهِ فِيهِ الْهُدَى وَالنُّورُ, فَخُذُوا بِكِتَابِ اللَّهِ وَاسْتَمْسَكُوا بِهِ". فَحَثَّ عَلَى كِتَابِ اللَّهِ تَعَالَى وَرَغَّبَ فِيهِ, ثُمَّ قَالَ: "وَأَهْلُ بَيْتِي, أُذَكِّرُكُمُ اللَّهَ فِي أَهْلِ بَيْتِي, أُذَكِّرُكُمُ اللَّهَ فِي أَهْلِ بَيْتِي, أُذَكِّرُكُمُ اللَّهَ فِي أَهْلِ بَيْتِي" فَقَالَ لَهُ حُصَيْنٌ: وَمَنْ أَهْلُ بَيْتِهِ يَا زَيْدُ؟ أَلَيْسَ نِسَاؤُهُ مِنْ أَهْلِ بَيْتِهِ؟ قَالَ: نِسَاؤُهُ مِنْ أَهْلِ بَيْتِهِ, وَلَكِنْ أَهْلُ بَيْتِهِ مَنْ حُرِمَ الصَّدَقَةَ بَعْدَهُ, قَالَ: وَمَنْ هُمْ؟ قَالَ: هُمْ آلُ عَلِيٍّ وَآلُ عَقِيلٍ وَآلُ جَعْفَرٍ وَآلُ عَبَّاسٍ. قَالَ: كُلُّ هَؤُلَاءِ حُرِمَ الصَّدَقَةَ؟ قَالَ: نَعَمْ.

Imepokewa na Muslim kwa riwaya ya Sahaba Zayd bin Arqam(ra), amesema: “Alisimama Mtume(saw) akitoa khutba sehemu inayoitwa Khum baina ya Makkah na Madina akamshukuru Mwenyezi Mungu na akamsifia, akatoa waadhi na akukumbusha kisha akasema,

‘Amma baadu, enyi watu! Hakika mimi ni mtu kama nyinyi, huenda nikaitwa na mjumbe wa Mola wangu Mtukufu (malaika wa mauti) nikaitika (nikafa). Na mimi nimekuachieni kwenu vizito viwili; cha kwanza ni kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani yake mna uongofu na nuru, basi chukueni kitabu cha Mwenyezi Mungu na mushikamane nacho (barabara)’, akahimiza na akawatia ***raghba*** (hamu ya kupenda) kisha akasema: ‘Na Ahli bayti wangu, nakukumbusheni kwa Mwenyezi Mungu kwa Ahli bayti wangu, nakukumbusheni kwa Mwenyezi Mungu kwa Ahli bayti wangu, nakukumbusheni kwa Mwenyezi Mungu kwa Ahli bayti wangu’,

Huswayn (mpokezi kwa sahaba Zayd) akamwambia, “Nani Ahli bayti wake ew Zayd ?, je wakeze ndio Ahli bayti wake?” Akasema, “wakeze ni Ahli bayti wake, lakini Ahli bayti zake khasa ni wale ambao wameharamishiwa sadaka”. Akaulizwa, “Ni kina nani hao? Akajibu,

“Ni Aali (familia ya) Aliy, Aali Ja’far, Aali Aqiil, na Aali Abbas”, akaulizwa wote hawa wameharimishiwa sadaka, akasema “Ndio”.

Lakini, kama tulivyo-ona kabla, Ahlil-bayti aliowataja Mtume(saw) kwa maneno yake mwenyewe ni: yeye mwenyewe, Ali, Fatima, Hasan na Husain. Na maulamaa wameeleza Ahlil-bayti makhsuusi ni hawa watano kwa ukaribu wao zaidi kwa Mtume(SAW) na kwa matamshi yake mwenyewe Bwana Mtume(SAW).

Watukufu hao watano wanafuatiwa kwa utukufu na jamaa zake wa karibu, nao ni wakeze, watoto wake, ammi zake na watoto wao, na baada ya hawa wanawafuata kwa utukufu Baniy Hashim na Baniy Muttalib. Hawa wote wanaingia kwa (haya ni kwa) mujibu wa hadithi ya Mtume(SAW) ifuatayo:

إنما بنو هاشم وبنو المطلب شيء واحد إنهم لم يفارقونا في جاهلية ولا إسلام

“Hakika Banu Hashim na Banu Muttalib ni kitu kimoja, hawajatengana nasi kwenye ujahiliyya wala kwenye Uislamu.(Bukhari, Abu Daud, Nasaai)

Hukumu ya kuwa ni haramu kuwapa zaka Ahli Bayti inawakusanya wote, wale wa karibu pamoja na hawa Baniy Hashim na Baniy Muttalib.

Ni muhimu sana kila mwislamu akaelewa kuwa kizazi cha Mtume(saw) kina nafasi muhimu katika imani na matendo yake. Kwa kutilia mkazo hoja hii tuzingatie Hadithi ifuatayo: imepokewa kutoka kwa (Imamu Tirmidhiy) kuwa Mtume(saw) - rehema na amani zimshukie – amesema

إِنِّي تَارِك فِيكُم مَا إِن تمسكتم بِهِ لن تضلوا بعدِي أَحدهمَا أعظم من الآخر كتاب اللّٰه عز وَجل حَبل مَمْدُود من السَّمَاء إِلَى الأَرْض وعترتي أهل بَيْتِي وَلنْ يفترقا حَتَّى يردا عَليّ الْحَوْض فانظروا كَيفَ تخلفوني فيهمَا

“Hakika mimi ninaacha kwenu ambavyo mukishikamana navyo hamtopotea baada yangu, cha kwanza ni kikubwa kuliko cha pili yake; Kitabu cha Mwenyezi Mungu - kamba inayotoka mbinguni kuja kwa watu wa ardhini - na kizazi changu, Ahli bayti wangu. Na

havitotengana viwili hivi mpaka vije pamoja kwenye hodhi (langu). Basi angalieni vipi mutakaa navyo baada ya kuondoka kwangu".

Mfano wa maneno haya yamepokewa na Imaam Ahmad. Katika riwaya nyingine aliyoipokea Imaam Al-Haakim, Bwana Mtume(saw) amesema,

إِنِّي تَارِك فِيكُم أَمريْن لن تضلوا إِن تبعتموهما وهما كتاب اللّٰه وَأهل بَيْتِي عِتْرَتِي

"Hakika mimi nakuachieni vitu viwili, mukishikamana navyo hamtopotea, navyo ni kitabu cha Mwenyezi Mungu na Ahli bayti wangu, kizazi changu".

Hadithi hii tuliyoitaja ya Ahlil-bayti imepokewa na masahaba zaidi ya ishirini, na ni sahihi, na imetajwa katika vitabu vingi vya hadithi. Katika riwaya mbali mbali za hadithi hii, kuna inayosema kuwa maneno haya Bwana Mtume(saw) ameyasema katika Hijja yake ya mwisho, siku ya Ghadiir, aliporudi Taif na katika maradhi yake ambayo alifariki. Bali kwa mujibu wa Imaam Tabraaniy, maneno ya mwisho aliyopokea Sayyidna Abdulla ibn Umar(ra) kutoka kwa Bwana Mtume(saw) ni kuwa,

أخلفوني فِي أهل بَيْتِي

"Kuweni badali yangu kwa Ahli bayti wangu". (Tabraaniy)

Na katika hadithi nyingine sahihi kuna neno **"sunna"** badala ya Ahlil-bayti. Riwaya zote mbili hizi ni sahihi. Kwa hivyo inatupasa waislamu kushikamana na vitu hivi vyote vitatu (yaani Qur'ani, Sunna, na kuwapenda na kuwatukuza Ahli Bayti) hadi siku ya Kiyama.

Mtu anaweza akajiuliza hawa mabwana Hasan na Husain wanaingiaje katika kizazi cha Mtume(saw) ilihali ya kuwa hakuwazaa, bali wamezaliwa na mtoto wake mwanamke, Bibi Fatima? Kwa kujibu swali hili tuzingatie Hadithi ifuatayo: Imepokewa kutoka kwa Imaam Tabraaniy kuwa Bwana Mtume(saw) amesema,

إِن اللّٰه عز وَجل جعل ذُرِّيَّة كل نَبِي فِي صلبه وَإِن اللّٰه تَعَالَى جعل ذريتي فِي صلب عَليّ بن أبي طَالب

“Hakika Mwenyezi Mungu amejaalia kizazi cha kila Nabii kwenye mgongo wake, na hakika Mwenyezi Mungu amejaalia kizazi changu kwenye mgongo wa Aliy bin Abi Talib”.

Jambo hili limethibiti pia katika Hadithi nyengine ya Bwana Mtume(SAW) iliyopokewa na Abu Yaali na Tabraaniy kwamba Mtume(SAW) amesema:

كل بني أم ينتمون إِلَى عصبَة إِلَّا ولد فَاطِمَة فَأَنا وليهم وَأَنا عصبتهم

“Kila watoto wa mama wananasibika na *asaba* (ndugu upande wa kiumeni) ila watoto wa Fatima kwani mimi ndio *walii* wao na mimi ndio *asaba* wao”.

Kwa kuongezea, imepokewa na maimamu Al-Haakim na Tabraaniy, Khatibul-Baghdadi na Abu Nuaym; kadhalika imetajwa na Qurtubi katika tafsiri yake na Ibn Hajar Asqalaani katika *Talkhiis*, kwamba Sayyidina Umar(ra) alikwenda kumposa mtoto wa Sayyidna Aliy (ra), Ummu Kulthum. Sayyidna Aliy akamjibu kuwa ni mdogo na kwamba amemwekea mtoto wa ndugu yake Ja’afar. Sayyidina Umar(ra) akamwambia Sayyidina Aliy(ra), “Wallahi sikumtaka kwa matamanio lakini nilimsikia Mtume(SAW) akisema:

كل سَبَب وَنسب يَنْقَطِع يَوْم الْقِيَامَة مَا خلا سببي ونسبي وكل بني أُنْثَى عصبتهم لأبيهم مَا خلا ولد فَاطِمَة فَإِنِّي أَنا أبوهم وعصبتهم

“Kila nasabu ya mama na nasabu ya baba itakatika siku ya Kiyama ila nasabu yangu na kamba yangu, na kila watoto wa mwanamke nasabu yao ni kwa baba yao ila watoto wa Fatima, kwani mimi ni baba yao na mimi ndio ndugu wa kiumeni wao”.

Kwa maana hii, Sayyidna Hasan na Sayyidna Husain wanaingia katika kizazi cha Mtume(SAW) kwani imepokewa pia kuwa Mtume(SAW)

alisema kuhusu Sayyidna Hasan: “Hakika mtoto wangu huyu ni Sayyid (Bwana)”. (Bukhari)

Mahdy ni mjukuu wa Mtume(saw):

Imepokewa na maimamu Muslim, Abu Daud, Nasaai, Ibn Majah, na Bayhaqiy: “Al-Mahdiy ni katika kizazi changu katika watoto wa Fatima”.

Na Katika hadithi sahihi pia: “Lau isinge bakia katika Dunia ila siku moja Mwenyezi Mungu angeirefusha hadi amlete mtu katika kizazi changu, jina lake kama langu na jina la baba yake kama jina la baba yangu, ataeneza katika ardhi uadilifu na usawa kama ilivyo enea dhuluma na jeuri”. (Ahmad, Abu Daud, Tirmidhiy)

Na Imaam Al-Haakim amepokea pia kuwa amesema Mtume(saw)-Rehema na Amani zimshukie: “Itawapata umma wangu mwisho wa zama (karibu na Kiyama) balaa kubwa sana kutoka kwa watawala wao, haijawahi kusikiwa balaa kama hiyo mpaka mtu atakuwa hana pa kwenda. Hapo Mwenyezi Mungu atamleta mtu kutoka katika Ahli bayti wangu ambaye ataeneza usawa na uadilifu kama ilivyo enea dhulma na jeuri, watampenda wakaazi wa ardhini na wakaazi wa mbinguni. Na mawingu yatanyesha mvua, na ardhi itatoa miti yake wala haitozuia kitu (ndani ya ardhi kisiote), ataishi ndani yake miaka saba au nane au tisa. Watatamani walio kufa wapate uhai kwa kuona kheri za Mwenyezi Mungu alizozishusha kwa watu wa ardhini”.

Na katika riwaya nyingine ya Imaam Tirmidhiy: “Katika umati wangu yuko Mahdiy, ataishi (miaka) mitano au saba au tisa atajiwa na mtu atakaye mwambia: Ewe Mahdiy, nipe, nipe! Atamwekea kwenye nguo yake kiasi anachoweza kubeba”.

Na hakika Imaam Mahdiy kama inavyothibitisha hadithi nyingine kuwa atamswalisha Nabii Isa, na kwamba atataka Nabii Isa atangulie, lakini Nabii Isa atamtanguliza yeye. Na kama ilivyothibiti kwamba Mtume(SAW) amesema:

“Nabii Isa ataswali nyuma ya mjukuu wangu.” (Tabraaniy).

Na hii ndiyo iliyothibiti kuwa Nabii Isa ataswali nyuma yake, kwani pamoja na kuwa yeye ni Nabii lakini atakuja kama mfuasi wa Mtume Muhammad(SAW), na mwenye kufuata sheria zake, na sio mwenye kuleta sheria mpya, na kumfuata kwake mmoja wa umati Muhammad kunadhihirisha kuwa amekuja kama mfuasi.

Na Imaam Mahdiy atakuwa mjukuu wa Sayyidna Hasan kama ilivyo katika hadithi aliyoipokea Imaam Abu Daud, na siri yake kama alivyoeleza Ibn Hajar Al-Haitamy kwenye *Sawaaiqul Muhriqa*, ni kuwa Sayyidna Hasan alipoacha Ukhalifa kwa kuogopa kumwagika damu ya Waislamu, Mwenyezi Mungu atamjaalia mjukuu wake kushika ukhalifa wakati zitakapoharibika zama, ili aeneze uadilifu. Na Imaam Mahdiy kama ilivyothibitisha hadithi atakuwa na jina la Muhammad bin Abdillah kama jina la Mtume(SAW). Riwaya nyengine inasema kuwa Imaam Mahdiy ni mjukuu wa Mtume(SAW) kwa Sayyidna Husain.

Ubora wa Ahlil-Bayti.

Imepokewa kuwa Mtume(saw)-rehema na amani zimshukie- amesema:

“Amenipa ahadi Mola wangu kuwa katika Ahli bayti wangu, ambaye amekiri upweke wa Mwenyezi Mungu (amekufa mwislamu) na akanikiria mimi kuwa nimefikisha ujumbe, kuwa Hatowaadhibu”. (Al-Haakim)

Imepokewa na Bukhariy na Muslim kwamba Sayyidna Umar(ra) alimwambia Sayyidna Zubair(ra): “Twende tukamzuru Hasan bin Aliy”. Akarudi nyuma Sayyidna Zubair. Sayyidina Umar(ra) akasema: "Je, hukujua kuwa kuwazuru Baniy Hashim wakiwa wagonjwa ni faradhi na kuwazuru bila ya ugonjwa ni sunna?” Hadithi hii pia imepokewa na maimamu Malik, Ahmad, Abu Daud, Nasaai, Bayhaqiy, Ibn Khuzaimah, Ibn Hibban, na Daarimy.

Maana ya ufaradhi hapa ni kuwa imehimizwa sana. Hivyo kiimani, mwislamu hana budi kujilazimisha katika kuwafanyia wema Ahlil Bayt. Hata hivyo, hii si faradhi kama ilivyo swala, saumu, n.k.

Hoja ya kuwaheshimu, kuwaenzi, kuwatanguliza na, kwa jumla kuwafanyia wema Ahlil bayt ni hoja muhimu sana katika imani ya mwislamu, na ina Hadithi nyingi. Tunanakili hapa chini baadhi ya Hadithi hizo ili kuthibitisha imani ya msomaji.

“Mbora wenu ni mbora wenu kwa ahli yangu baada ya kufa kwangu”. (Al-Haakim)

“Nimemwomba Mola wangu, kuwa sitooa kwa mtu yeyote katika umati wangu wala hatooa kwangu yeyote katika umati wangu ila awe na mimi Peponi, akanipa hilo”. (Al-Tabraany, Al-Haakim)

“Mpendeni Mwenyezi Mungu kwa vile anavyokupeni riziki na nipendeni mimi kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na wapendeni Ahlil-bayti wangu kwa mapenzi yangu”. (Tirmidhiy na Al-Haakim)

“Atakayethibiti zaidi juu ya ***sirati*** (daraja jembamba mno la kuvukia kwendea Peponi), ni yule anayewapenda zaidi Ahli bayti wangu na masahaba wangu”. (Ibn Adiy na Daylamiy)

“Imekuwaje watu wanazungumza, akija mtu katika Ahli bayti wangu hukatiza mazungumzo yao (kwa kumchukia), naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, haitoingia imani kwenye moyo wa mtu mpaka awapende (Ahli Bayti) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya ujamaa kwangu”. (Ibn Majah na Al-Haakim)

Sayyidna Abubakr Siddiiq(ra) amesema,

“Muhifadhini Muhammad kwenye Ahli bayti wake”. (Bukhariy na Muslim)

Yaani muhifadhini kwa kupitia Ahli bayti wake, musiwaudhi.

Imepokewa na maimamu Ibn Sa’ad na Mulla katika Sira yake:

“Nakuusieni kheri kwa Ahli bayti wangu (muwafanyieni wema), kwani mimi ni mgomvi wenu kwao kesho (Kiyama) na ambaye mimi nitakuwa mgomvi wake nitafanya hasama (ugomvi) naye na ambaye nitafanya hasama naye ataingia Motoni”

Na hadithi nyengine waliyoipokea “Mwenye kunihifadhi mimi kwenye Ahli bayti wangu basi Mwenyezi Mungu amechukua ahadi (ya kumuingiza peponi)”.

Imepokewa na Imaam Tirmidhiy na kutajwa na Imaam Suyuti katika Tafsiri yake na Imaam Hindiy katika *Kanzul-Ummaal*,

“Hakika jamaa zangu na ndugu zangu ni Ahli bayti wangu na Ansari, basi mkubalini anayefanya mema baina yao, na wasameheni ambao watakosea”.

“Nyota ni amani ya watu wa ardhini na kughariki baharini, (kwani hutumia nyota kuwaonyesha njia) na Ahli bayti wangu ni amani ya ummati wangu na kufarikiana”. Imepokewa na Al-Haakim na akasema ni sahihi kwa sharti ya Bukhariy na Muslim

“Ahli bayti wangu ni mfano wa safina ya Nuhu, mwenye kuipanda ataokoka na mwenye kuiwacha atazama”. (Muslim)

Baadhi ya Maulamaa wamesema kuwa wanao kusudiwa hapa ni wale waliokuwa wanachuoni miongoni mwa Ahlil-bayti, kwani ndio wanaoonyesha njia. Ibn Hajar Al-Haytamiy(ra) amekwenda mbali zaidi katika kufafanua umuhimu na faida za kuwapenda na kuwatukuza Ahlil bayti. Amesema, “iliyo kuwa dhahiri zaidi kwangu ni Ahlil-bayti wote (na si lazima wanachuoni tu peke yao). Hii pia ni kwa kuwa Ahlil-bayti wanatokana na Mtume(saw), na umma wake hawakuadhibiwa wakati wake, kwa sababu ya kuwa Mtume(SAW) yuko pamoja nao. Ibn Hajar ameendelea kusema kuwa kwa mantiki hii, baada ya Mtume(SAW) kufariki, watu hawatoadhibiwa kwa sababu ya Ahlil-bayti.

“Mwenye kunipenda mimi na akawapenda hawa (Hasan na Husain), na akampenda baba yao na mama yao, atakuwa pamoja nami kwenye daraja yangu siku ya Kiyama”. (Ahmad na Tirmidhiy)

“Hatoamini mja mpaka niwe mimi ni mwenye kupendwa zaidi kuliko nafsi yake, na akakipenda kizazi changu kuliko kizazi chake, na akawapenda Ahli bayti wangu zaidi ya Ahli bayti wa kwake, na iwe dhati yangu inapendwa zaidi kuliko dhati yake”. (Bayhaqiy na Abu Shaikh na Daylamiy)

“Wafundisheni watoto wenu mambo matatu; kumpenda Mtume(saw) wenu, kuwapenda Ahli bayti wake na kusoma Qur-ani”. (Daylamiy) Hadithi hii pia imetajwa na Hindiy katika *Kanz* na Ajluni katika *Kashful-khafaa*.

“Mwenye kumpenda Mwenyezi Mungu ataipenda Qur-ani, na mwenye kuipenda Qur-ani atanipenda mimi, na mwenye kunipenda mimi atawapenda masahaba wangu na jamaa zangu”. (Daylamiy)

“Mwenye kuswali swala na asiniswalie mimi (asiniombee rehema) na asiwaswalie Ahli bayti wangu, haitokubaliwa (swala yake)”. (Daaruqutniy na Bayhaqiy) Na Ibn Hajar Al-Haitamiy anasema: huenda ikawa hii ndiyo hadithi aliyoitegemea Imaam Shafiy kuwa kuwaswalia Ahli bayti wake ni lazima katika swala."

Kujihadhari na kuwachukia Ahlil-bayti.

Imepokewa na Al-Haakim na akasema kuwa ni sahihi kwa sharti ya Muslim, kwamba Mtume(SAW) amesema: “Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, (mtu yoyote) hatuchukii sisi Ahlil-bayti ila Mwenyezi Mungu atamwingiza motoni”. Hadithi hii imepokewa pia na Ibn Hibban, na imetajwa na Haithamiy na Suyutiy katika Tafsiri yake.

“Mwenye kutuchukia sisi Ahlil-bayti, basi yeye ni mnafiki”. (Ahmad)

Sahaba Jabir bin Abdillah(ra) amesema: “Hatukuwa tukiwajua wanafiki ila kwa kumchukia kwao Aliy”. (Ahmad na Tirmidhiy)

”Enyi watoto wa Abdil-Muttalib! Hakika nimekuombeeni kwa Mwenyezi Mungu vitu vitatu; amthibitishe mwenye kusimama baina yenu, amwongoze mwenye kupotea baina yenu, na amfundishe asiye na elimu baina yenu. Na nimemwomba Mwenyezi Mungu awajaalie kuwa ni wakarimu, (katika riwaya nyingine mashujaa), ***wapaji*** na wenye kurehemu watu. Basi lau mtu angeliikusanya miguu yake baina ya nguzo (ya Ka’aba) na maqamu (Ibrahim) akaswali na kufunga, kisha akakutana na Mwenyezi Mungu, hali anawachukia Ahli bayti wa Muhammad ataingia motoni”. (Al-Haakim na akasema kuwa ni sahihi, pia na Tabraaniy).

“Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu imekuwa kali mno juu ya mwenye kuniudhi katika kizazi changu”. (Daylamiy na Ibn Adiy)

Kwa hiyo ni wazi katika hadithi hizi zilizotangulia kuwa ni lazima kuwapenda Ahlil-bayti, na ni haramu sana kuwachukia. Hivi ndivyo alivyosisitiza Imaam Shafiy kama tulivyoona kwenye mashairi yake, Bayhaqiy, Baghawiy na wengineo. Na katika kitabu *Tawthiiq ural-iimani* cha Al-Baarizy, akiyakariri maneno ya Imaam Harraliy: “Hakika wanachuoni waliobobea wanakuta kwenye mioyo yao mapenzi kamili juu ya Mtume(SAW)-rehema na amani zimshukie-kisha kupenda kizazi chake kwa kujua kwao kuwa Mwenyezi Mungu amewachagulia nasabu tukufu. Kisha kupenda watoto wa watu kumi walio bashiriwa pepo, na kisha watoto wa masahaba wengine na wanawaangalia wao leo, mwangalio wa baba zao siku zilizo pita kama wangewaona. Inabidi kujiepusha na kuwatolea maneno makali. Na mwenye kuasi katika Ahlil-bayti inabidi tuchukie matendo yake ya maasi lakini siyo dhati yake, kwani yeye (dhati yake) ni sehemu ya Mtume(SAW) hata kama kuna watu wengi kwenye nasaba mpaka kumfikia Mtume(SAW)”.

Imaam Ibn Hajar Al-Haitamiy anasema katika *Sawaaiq*: Ndio maana wameeleza wazi wanavyuoni kwamba inabidi kuwatukuza wakaazi wa mji wake (Mtume(SAW)) hata kama kuna uhakika wa maasi yao. Hii ni kwa ajili ya kuchunga utukufu wa ujirani wao (kwa Mtume(SAW)), basi hali itakuwaje kwa kizazi chake ambao ni sehemu/pande linalotokana na yeye!

Na Bwana Ja’afar Sadiq amepokewa akisema, “Tuhifadhini kwa jinsi alivyowahifadhi Mwenyezi Mungu mayatima kwa ajili ya wema wa baba zao (suratil kahf), basi na mwenye kumpenda Mtume(SAW) hawezi kuwadharau wajukuu wake” (Tafsir ya Raaziy)

Amesema Imaam Qurtubiy: “Hadithi zilizopokewa kwa Mtume(saw) zinatoa hukumu ya ulazima wa kuwaheshimu Ahlil bayt, kuwaenzi na kuwapenda, wajibu wa ufaradhi ambao hakuna udhuru kwa yeyote kukaa nyuma. Hii ni pamoja na kujulikana kwao ni sehemu ya Mtume(saw) kwani wao ni kizazi ambacho kimetokana na yeye”. Kwa ajili ya hilo, amesema Qadhi 'Iyaadh, “Mwenye kumtukana yeyote

katika kizazi cha Mtume(SAW) na haikupatikana dalili ya kurejea kwake, huuawa".

Mwenye kuwafanyia wema atalipwa na Mtume(SAW).

Imaam Al-Tabraaniy amepokea kauli ifuatayo ya Bwana Mtume(SAW), "Mwenye kutenda wema kwa yeyote katika watoto wa Abdil-Muttalib na asipate malipo yake duniani, basi mimi nitampa malipo yake kesho (Kiyama) akikutana nami"**.**

Kauli hii hii pia imepokewa na Ibn Adiy na kutajwa katika Tafsiri ya Qurtubiy. Hadithi ifuatayo yenye maana kama hiyo imepokewa na Ibn Asaakir,

"Mwenye kufanya wema kwa yeyote katika Ahli bayti wangu nitamlipa kwa hilo mimi siku ya Kiyama".

Ufafanuzi zaidi unapatikana katika Hadithi ifuatayo iliyotajwa na Zabiidiy na Muhibbut-Tabary na Hindiy:

"Watu wanne mimi ni mwenye kuwaombea siku ya Kiyama; mwenye kukifanyia wema kizazi changu, na mwenye kuwakidhia haja zao, na mwenye kuwasaidia kwenye mambo yao (ya Dunia) wakiwa na haja nayo, na mwenye kuwapenda kwa moyo wake na ulimi wake".

Ahlul-Bayti watapata matatizo sana duniani.

Imepokewa na Ibn Majah, kwamba Mtume(SAW) aliwaona vijana wa Baniy Hashim, akatokwa na machozi, akaulizwa akasema: "Hakika sisi Ahlil-bayti, Mwenyezi Mungu ametuchagulia akhera juu ya dunia, na Ahli bayti wangu baada ya kufa kwangu watapata balaa, na kufukuzwa kabisa na kutolewa kwenye miji".

Maneno ya Masahaba na Salaf katika kuwazungumzia Ahlil-bayti.

Imepokewa na Imaam Bukhariy kwamba Sayyidna AbuBakr(ra) alisema: “Namwapia yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, jamaa wa Mtume(SAW) wa Mwenyezi Mungu ni wapendwa zaidi kwangu kuliko kuwaunga jamaa zangu”. Katika riwaya nyingine: kuliko kuwapenda jamaa zangu.

Na katika riwaya ya Imaam Muslim: Sayyidina Abubakar alisema, “Wallahi kuwaunga nyie (kwa kuwafanyia wema) ni jambo lenye kupendeza kwangu kuliko kuwaunga jamaa zangu kwa ajili ya ujamaa wenu kwa Mtume(SAW) wa Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya ukubwa wa haki zenu juu ya kila mwislamu”.

Imepokewa na Imaam Bukhariy pia, kuwa Sayyidina Abubakar(ra) alimbeba Sayyidna Hasan shingoni kwake na huku akifanya mzaha na Sayyidna Aliy-Mwenyezi Mungu awarehemu wote-kwa kusema huku amembeba: “Nakufidia kwa baba yangu, umefanana na Mtume(SAW) na hujafanana na Aliy", na huku Sayyidna Aliy akicheka.

Na hii inathibitishwa kwa maneno ya Anas, kuwa hakuna aliye kuwa akifanana na Mtume(SAW) zaidi ya Sayyidna Hasan. Na katika riwaya nyingine: Sayyidna Hasan amefanana na Mtume(SAW) kutoka kichwani hadi kifuani, na Sayyidna Husain amefanana na Mtume(SAW) kutoka hapo (kifuani) na chini yake.

Na amepokea Ibn Abi-Dduniyaa kuwa Sayyidna Umar alipo taka kugawa mali kwa watu akaambiwa: Anza kujigawia mwenyewe, akakataa, akaanza na walio kuwa karibu zaidi kwa Mtume(SAW), hakuja kwenye kabila lake ila baada ya makabila matano. Akawapa watu wa vita vya Badr elfu tano, Sayyinda Abbas elfu kumi na mbili, Hasanayn (Sayyidna Hasan na Sayyidna Husain) sawa na baba yao. Na ndio maana Ibn Abbas akasema kwamba: Alikuwa akiwapenda wote wawili (yaani Sayyidna Hasan na Sayyidna Husain) kwani aliwatanguliza kuliko watoto wake.

Aliingia Sayyidina Abdallah bin Hasan (Muthanna) bin Hasan kwa Khalifa Umar bin Abdul-Aziz na yeye ni kijana mdogo, akavunja Khalifa Umar mkutano wake, na akakaa kumsikiliza mgeni wake. Waliokuwepo wakamlaumu, naye akasema, “Hakika nimeambiwa na mtu mwaminifu ikawa kama namsikia Mtume(saw) mwenyewe akisema, ‘Hakika Fatima ni sehemu/pande linalo tokana na mimi, kinanifurahisha kinachomfurahisha.’ Na mimi nina yakini kuwa Fatima angekuwa hai angefurahikiwa na kitendo changu kwa mtoto wake. Khalifa Umar bin Abdul-Aziz alimwambia Bwana Abdallah bin Hasan (Muthanna) bin Hasan, “Ukiwa na haja yoyote niandikie, kwani naona haya kwa Mwenyezi Mungu akikuona juu ya mlango wangu”.

Na Khalifa huyu alipo jiwa na Bibi Fatima bint Aliy bin Husain, na yeye wakati huo ni kiongozi wa Waislamu, akamwambia: Hakuna juu ya ardhi watu wa nyumba yoyote ninaowapenda kuliko nyie, na hakika nyie ni wenye kupendwa zaidi kwangu kuliko watu wa nyumbani kwangu.

Ja’afar bin Sulaiman Al-Abbasiy, liwali wa Madina, alimpiga Imaam Malik(ra) mpaka akazimia, alipozinduka akasema, “Nakushuhudisheni kuwa nimemsamehe aliyenipiga”. Alipoulizwa zaidi akasema, “Naogopa nisije kufa nikakutana na Mtume(saw), nitaona haya kwake kwa kuingizwa mmoja wa jamaa zake motoni kwa ajili yangu”. Alipo tawala Mansuur Madina, alimtaka Imaam Malik alipe kisasi kwa Ja’afar. Imaam akasema, “Ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu (na kutenda hilo), Wallahi hakunyanyua bakora ila nilimsamehe kwa ajili ya ujamaa wake na Mtume(SAW) wa Mwenyezi Mungu”.

Kwa upande wa maimamu, alikuwa Imaam Abu Hanifa(ra) anawatukuza sana Ahlil-bayti, na anajikurubisha kwao kwa kuwapa sadaka wale ambao ni mafakiri wa dhahiri, na wale wanaojificha wasidhihirishe haja zao.

Imaam Shafiy(ra) alikuwa akiwapenda sana Ahlil-bayti, hata akatuhumiwa kuwa ni Shia. Watu walikuwa wanamsingizia mengi, lakini akiwajibu kwa mashairi, mojawapo ni hili:

آل النبي ذريعتي وهمُ اليه وسيلتي

ارجوا بهم اعطى غدا بيدي اليمين صحيفتي

Aali wa Mtume(SAW) ni tawasuli yangu

Nao kumuendea yeye (Mtume(SAW)) wao ndio wasila wangu

Nataraji kwa jaha yao kupewa kesho

Sahifa yangu kwa mkono wangu wa kuume.

Kadhalika Imaam Ahmad(ra) alikuwa anapojiwa na mtu mzima au kijana wa kikureshi, au katika masharifu huwatanguliza mbele yake, na hutembea nyuma yao akiwasindikiza. Imamu Ahmad mara moja alimtukuza mtu katika Ahli bayti ambaye alikuwa Shia, wakamlaumu watu wake, akasema, "***Subhanallah*** - utakasifu ni wake Allah! Mtu amempenda mtu katika Ahli bayti wa Mtume(saw) na yeye ni mtu mwaminifu wa kutegemewa".

Amesema Sayyidna Hasan bin Aliy, "Mwenye kutufanyia uadui basi anamfanyia uadui Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu"

Imepokewa na Al-Hafidhu Taqiiyu bin Fahd Al-Hashimiy kwamba alisema "Alinijia Sharifu Aqiil bin Humayl akaniomba chakula cha usiku sikumpa, nikatoa udhuru. Nikamwona Mtume(saw) usiku ule, akanipa mgongo, nikamwuliza, 'Vipi unanipa mgongo ewe Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu na mimi ni mtumishi wa hadithi zako?' Akanijibu, 'Vipi nisikupe mgongo na anakuja kwako mtoto katika watoto wangu anakuomba chakula cha usiku (***ashaa***) usimpe?' Kulipopambazuka asubuhi nikaenda kwa yule Sharifu, nikamwomba msamaha na kumpa nilicho kuwa na uwezo nacho"..

Imepokewa kutoka kwa Jamaal Abdul-Ghifaariy Al-Ansariy maarufu kwa jina la Ibn Nuuh, kutoka kwa Ummu Najmuddiin bin Matruuh nae alikuwa mwanamke mwema, alisema, "Ilipatikana njaa kali Makka hata watu wakawa wanakula ngozi, na sisi tulikuwa watu kumi na nane. Tukawa tunatengeneza chakula kiasi cha nusu bamba na tunajitosheleza na hicho tu, tukaletewa makorobasi (makapu makubwa) kumi na nne ya unga, mume wangu akatoa kumi kwa watu wa Makka na tukabakiwa na

manne. Alipolala (mume wangu) akashtuka usingizini na kulia, nikamuuliza imekuwaje, akasema: Nimemwona kwenye ndoto sasa hivi Sayyidatna Fatima Zahraa(ra), na yeye akiniambia: 'Ewe Siraaj! Je, unakula ngano na watoto wangu wana njaa?' Akaamka na kutoa kilichobaki kwa masharifu, tusibakiwe na kitu, na tulikuwa hatuwezi kusimama kwa njaa kali".

Wajibu wa Ahlil-bayti:

Hapa tutanukuu kwa ufupi maneno ya Imaam Ibn Hajar Al-Haitamiy katika kitabu cha *Sawaaiq*. Mambo yafuatayo ni muhimu sana kwa ajili ya Ahlil-bayti khasa na kwa watu wengine kwa ujumla:

1 Kuwa na hima ya kutafuta elimu za dini, kwani hamna faida kwenye nasabu bila ya elimu.

2 Kuacha kujifakharisha kwa wazazi na kutokuegemea kitu hicho bila ya kufanya amali. Imepokewa na Imaam Muslim(ra) kuwa Mtume(saw) amesema, "Mwenye kucheleweshwa (kuwekwa nyuma) na amali zake, hatopelekwa mbele na nasabu yake".

3 Kuwa wacha Mungu zaidi, na wenye kumuogopa Mwenyezi Mungu zaidi. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema, "**kwa hakika mbora wenu kwa Mwenyezi Mungu ni mcha Mungu"**. Imepokewa kutoka kwa Hasan Muthanna bin Hasan Sibti, "Lau kama Mwenyezi Mungu angenufaisha kwa ajili tu ya ujamaa (qaraaba) kwa Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu bila ya amali njema, basi ungemnufaisha aliye kuwa karibu zaidi (kwa Mtume(saw)) kuliko sisi. Wallahi hakika mimi nakhofia kuwa mwenye kuasi katika sisi kupewa adhabu mara mbili, na mwenye kufanya mema atalipwa ujira wake mara mbili". (Maneno haya ya Hasan Muthanna yamepokewa na maimamu Ibn Sa'ad, Ibn Asaakir, na yametajwa na Dhahaby katika Sira yake).

   Pia wametaja watu wa Tarikh, kuwa Bwana Zayd bin Musal-Kadhim, alimpinga Al-Maamuun na kupigana naye vita, akakamatwa, akaitwa ndugu yake, Bwana Aliy Ridhaa. Bwana Aliy

Ridhaa alimkaripia kwa maneno makali, miongoni mwa maneno hayo ni haya yafuatayo, “Utamwambia nini Mtume(SAW) wa Mwenyezi Mungu ukimwaga damu (za Waislamu) na ukakata njia (za watu) kwa kuwatisha, na ukanyang’anya mali bila ya haki? Je, wamekupotosha wapumbavu wa Koufa? Hakika Mtume(SAW) amesema, **‘**Hakika Fatima ameuhifadhi utupu wake, na Mwenyezi Mungu akakiharimisha kizazi chake na moto’. Hili ni kwa waliotoka tumboni mwake mfano wa Hasan na Husain peke yao, si mimi na wewe. Wallahi hawakupata daraja hizo ila kwa kumtiii Mwenyezi Mungu, ukitaka uipate kwa maasi ya Mwenyezi Mungu waliyopata kwa kumtii Mwenyezi Mungu basi utakuwa wewe ni mbora zaidi kuliko wao."

Mwenye kuzingatia na ayazingatie haya, na asitegemee nasabu yake, bali afanye amali za kheri zaidi ya wengine, na arejee kwenye nyendo za wazee wake, na kufanya mambo ya kheri waliyoyafanya, na ucha Mungu wao, na ibada zao, na kujipamba kwao kwa elimu tukufu. Mwenyezi Mungu aturudishie baraka zao, na atufufue kwenye kundi la wanaowapenda, amin.

4 Kuwatukuza masahaba na kuwapenda, kwani wao ni bora wa umma, na tutakuja kuona kuwa Ahlil-bayti wote mashuhuri walio tangulia na ambao wamesifika kwa ucha mungu, walikuwa wakiwatukuza masahaba, na wala hawakubali mtu awatukane, wala kuwataja kwa ubaya. Basi wao wawe ni mfano wa kufuatwa, na sio kufuata mkumbo wa vikundi vya wanao wasema vibaya masahaba. Aliwahi kuulizwa Muhammad Baaqir, “Je, alikuwepo yeyote katika Ahlil-bayti aliyekuwa akiwatukana Abubakar na Umar?” Akajibu, “Mwenyezi Mungu awakinge na hilo**,** bali huwaweka wao mbele, huwaombea maghfira na huwaombea rehma. (Imepokewa mfano wake na Tabary katika Tafsiri yake).

Imepokewa pia kutoka kwa Ja’afar Sadik kuwa alipo kuwa mgonjwa alisema, “Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nawapenda Abu Bakr na Umar na ninawatanguliza, ewe Mwenyezi Mungu nikiwa nina chochote kwenye nafsi yangu kisichokuwa haya

basi usinipe *shafaa* (uombezi) ya Muhammad". Imepokewa na Abu Nuaym.

5 Kuhifadhi nasaba yao, na kuidhibiti barabara, usiwepo upenyo wa mtu kujinasibisha kwa Mtume(saw) bila ya haki, na Al-hamdu lillahi nasabu ya Mtume(saw) imehifadhiwa na wanachuoni wakubwa, na kila zama anatokea ambaye anaihifadhi na kuisahihisha, na khasa wajukuu wa Sayyidatna Fatima. Na wakati wa utawala wa Al-Maamuun walipewa vazi maalum la kijani ili kuwatofautisha na watu wengine, na alama hii iliendelea, ijapokuwa baadaye ikawa ni kitambaa cha kijani juu ya vilemba vyao, kama alivyo kuja kuthibitisha hayo Mfalme Shaaban bin Husain bin Nasir Muhammad bin Qalaawuun; mfalme wa Misr na Shaam. Na hakika imethibiti adhabu kali kwa mwenye kujinasibisha na nasabu isiyo yake. Katika Sahiih Bukhariy amesema Mtume(SAW), "Mwenye kujinasibisha kwa asiyekuwa baba yake au kuwa mwachwa huru kwa wasiomwacha huru, basi juu yake ishuke laana ya Mwenyezi Mungu na malaika na watu wote".

6 Kufuata nyendo za wazee wao waliotangulia kwa elimu, itikadi, kuupa nyongo ulimwengu, na ucha Mungu, na wazingatie maneno ya Mtume(SAW) yaliyomo katika hadithi waliyoipokea maimamu Ahmad, Tabraaniy, Baihaqiy na Ibn Hibban: "Hakika Ahli bayti wangu hawa, wanaona kuwa wao ni wa karibu zaidi kwangu, na hakika sio hivyo, bali mawalii (walio karibu kwangu zaidi) wangu ni wacha Mungu miongoni mwenu, yeyote atayekuwa, popote atakapokuwa".

Masahaba wa Mtume(SAW).
Hakika kuwapenda Ahlil bayt kunaenda sanjari na kuwapenda masahaba. Na hapa tutataja utukufu wao kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume(SAW)-rehema na amani zimshukie-asije akafikiria mjinga kuwa kuwapenda Ahlil bayt kunashusha hadhi ya masahaba.

Mtume(SAW) amesema, “Hakika Mwenyezi Mungu amenichagua na amenichagulia masahaba akajaalia kati yao mawaziri, Ansaar (wenye kuninusuru) na wakwe, basi mwenye kuwatukana imshukie laana ya Mwenyezi Mungu na malaika na watu wote. Mwenyezi Mungu hatokubali kwake siku ya Kiyama toba wala amali yoyote”**.** (Al-Haakim).

Vile vile Bwana Mtume(SAW) amesema,
“Allah Allah (nakuusieni) kwa masahaba musiwafanye dango la shabaha baada yangu, (mukawa munawapopoa kwa maneno machafu). Mwenye kuwapenda amewapenda kwa ajili yangu na mwenye kuwachukia amewachukia kwa ajili yangu. Na mwenye kuwaudhi ameniudhi mimi, na mwenye kuniudhi mimi amemwudhi Mwenyezi Mungu, na mwenye kumuudhi Mwenyezi Mungu inahofiwa kuwa (Mwenyezi Mungu) atamwangamiza”. (Tirmidhiy)

Na Imaam Muslim(ra) amepokea maneno ya Bwana Mtume(SAW) kama ifuatavyo, “Musiwatukane masahaba wangu, kwani namwapia ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, lau kama mmoja wenu atatoa (sadaka) kiasi cha jabali Uhud dhahabu hatofikia kibaba cha mmoja wao wala nusu yake”.

TARJAMA YA AHLIL KISAA

- Mtume Muhammad(SAW)
- Sayyidatna Fatma
- Sayyidna Aliy
- Sayyidna Hasan
- Sayyidna Husain

Mtume Muhammad (SAW):

Huyu ndiye msingi wa Ahlil-bayti na masahaba wote, na Ahlil-bayt wamepata utukufu kwa ajili yake, bali umma mzima wa Kiislamu umepata utukufu kwa ajili yake.

Ni Mtume(saw) wa mwisho, na ni katika kizazi cha Nabii Ibrahim(as).

Amesema Mtume SAW,

"أنا دعوة أبي إبراهيم، وبشرى أخي عيسى، ورأت أمي حين حملت بي أنه خرج منها نور أضاء له قصور الشام " وإسناده صحيح، وصححه الحاكم، ووافقه الذهبي.

“Mimi ndio dua ya baba yangu Ibrahim, na bishara ya ndugu yangu Isa, na aliona mama yangu nilivokuwa nimebebwa na yeye (alivokuwa na mimba yangu) kuwa ilimtoka nuru iliyoangaza kasri (majumba ya kifalme) za Shaam” Hadithi hii ni sahihi imepokewa na Imaam Al-Haakim, na Imaam Dhahabiy pia kawafikiana naye kuwa ni sahiih.

Nasabu ya Mtume(saw):

Ni Muhammad bin Abdillah bin Abdil-Muttalib bin Hashim, bin Abdi Manaaf bin Qusayy bin Kilaab bin Murrata bin Ka’ab bin Luayyi bin Ghalib bin Fihr bin Malik bin Nadhr bin Kinaana bin Khuzaymah bin Mudrikata bin Ilyaas bin Mudhara bin Nizaar bin Ma’add bin Adnaan.

Mama yake ni Bibi Aminah bint Wahab bin Abdi Manaaf bin Zuhrah bin Hakiim, na Hakiim ndiye Kilaab bin Murrata.

Na mpaka Adnaan ndiyo nasabu iliyo thibiti, na zaidi ya hapo mpaka kwa Nabii Ibrahim kuna tofauti kubwa sana (*ikhtilaaf*) baina ya wanazuoni, na mpaka kufika kwa Nabii Adam ndio zaidi. Na Mtume(saw) alikuwa akifika kwa Adnaan husema, “Wamesema uongo wanao hifadhi nasabu”, yaani wamesema uongo baada ya Adnaan kwani haijahifadhiwa sawa sawa.

Historia ya wazee wake:

Mtume(saw) amechaguliwa wazee na hayakugawanyika matumbo ila Mtume(saw) alikwenda kwenye tumbo lililo kuwa tukufu zaidi. Anasema Mtume(saw) katika hadithi iliyopokewa na Imaam Muslim,

“Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Ismail kutoka katika watoto wa Ibrahim, na akawachagua Baniy Kinaana katika watoto wa Ismail, na akamchagua Qurayshi kutoka katika watoto wa Kinaana na akawachagua Banii Hashim kutoka kwa Qurayshi, na akanichagua mimi kutoka kwa Baniy Hashim”.

Basi bila shaka Mtume(saw) ni mchaguliwa kutoka kwa mchaguliwa kutoka kwa mchaguliwa.

Na katika hadithi nyingine iliyopokewa na Imaam Ahmad, Mtume(saw) aliposikia maneno yanayosemwa kumuhusu yeye, alisimama kwenye mimbari, akauliza,

“Mimi ni nani?” Wakajibu (maswahaba), “Wewe ni Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu.” Akasema, “Mimi ni Muhammad bin Abdillah bin Abdil-Muttalib, hakika Mwenyezi Mungu alipoumba viumbe, alinijaalia mimi katika waliobora zaidi. Akawajaalia (akawafanya hao viumbe) kuwa vikundi viwili, akanijaalia katika kundi bora zaidi, akaumba makabila na akanijaalia mimi katika kabila lililo bora zaidi. Akawajaalia kwenye nyumba, akanijaalia mimi kuwa kwenye nyumba bora zaidi, basi mimi ni mbora wenu kwa nyumba na ni mbora wenu kwa nafsi”.

Na imepokewa na Imaam Bayhaqiy pia, kwa riwaya ya Sahaba Anas(ra), Mtume(saw) alisema, “Nimetoka kupitia ndoa, na sijatoka kwa kupitia uchafu (zinaa) toka kwa Adam, mpaka kwa baba yangu na mama yangu, basi mimi ni mbora wenu kwa nasabu na mbora wenu kwa baba”.

Kisa cha nuru ya Mtume(saw):

Imepokewa kwamba Bwana Abdillah alipokuwa akipita njiani baada ya kumuoa Bi Amina, alikutana na mwanamke mmoja kutoka kabila la Khath-'am, jina lake Fatimah bint Murr. Mwanamke huyu alikuwa mzuri sana, na alikuwa msomaji wa vitabu. Yule mwanamke akaiona nuru ya Mtume(saw) kwenye uso wa Abdillah, na baada ya kumwuliza maswali akamtaka afanye naye tendo la ndoa, na atampa ngamia mia moja. Bwana Abdillah Akamwangalia na akasema mashairi yake maarufu, kuwa hawezi kufanya haramu. Siku nyengine walipokutana tena, baada ya kuonana na mkewe Bi Amina, Bwana Abdillah akamwuliza mbona leo huniambii kama ya siku ile? Akamwambia, "Kwa hakika mimi sio mzinzi, ila siku ile niliona Nuru ya utume usoni mwako, nikataka nuru ile ije kwangu, lakini Mwenyezi Mungu ameiweka sehemu alipoitaka."

Kushika mimba ya Mtume(saw) na kufariki kwa Bwana Abdillah:

Imepokewa kuwa Bibi Amina alisema, "Sikuhisi kama nimeshika mimba wala sikuona uzito kama wanavyoona kina mama wengine, ila nilihisi tu kuwa hedhi yangu imekatika, na nilijiwa na mtu usingizini akaniambia, 'Je, unajua umeshika mimba ya nani? Hakika umebeba mimba ya Bwana wa umma huu na Mtume(saw) wake'".

Bwana Abdillah alikwenda safari ya Shaam pamoja na Makureshi, waliporudi walipitia Madina, na Bwana Abdillah akaomba abaki kwa wajomba zake Baniy Najjar kwani alipatwa na homa kali. Akakaa mwezi mzima Madina. Na walipo rudi wasafiri wenzake, walimwambia Abdul-Muttalib kuwa wamemwacha mtoto wake Madina. Mzee Abdul-Muttalib akamtuma Al-Harith aende huko Madina. Alipofika akakuta Abdillah ameshafariki. Akarudi na khabari ile kwa baba yake, ambaye alihuzunika sana. Wakati huo Mtume(saw) alikuwa bado hajazaliwa.

Kuzaliwa kwake Mtume(saw):

Wanahistoria wanakubaliana kuwa Mtume(saw) alizawa siku ya Jumatatu, mwezi wa Rabiul-Awwal (Mfunguo Sita) mwaka wa tembo. Na siku ya kuzaliwa kwake, kuna riwaya nne, riwaya ya kwanza inasema tarehe 2, ya pili inasema tarehe 8, ya tatu inasema tarehe 10 na ya nne inasema tarehe 12.

Imepokewa kuwa Bi. Amina alisema wakati wa kumzaa Mtume(saw) hakupata maumivu, na alipozaliwa ilitoka nuru ambayo ilizagaa ulimwengu mzima, Mashariki na Magharibi. Bwana Abbas bin Abul-Muttalib alisema, "Alizawa Mtume(saw) hali ya kuwa ametahiriwa na mwenye furaha, na babu yake alipomuona alifurahi sana na akasema, 'Hakika mtoto wangu huyu atapata utukufu', na kweli akaja kupata utukufu mkubwa sana".

Majina ya Mtume(saw):

Bila ya shaka majina ya Mtume(saw) ni mengi sana, sisi tutataja hapa baadhi yake tu.

Imepokewa na Maimamu Bukhariy na Muslim kwamba Mtume(saw) amesema: "Nina majina matano, mimi ni Muhammad, na Ahmad, na mimi ni *Al-Maahiy* (mwenye kufuta) - Mwenyezi Mungu anafuta kufuru kwangu mimi, na mimi ni *Al-Hashir* - ambaye watafufuliwa watu kwenye miguu yangu [yaani atafufuliwa yeye Mtume(saw) kabla ya watu wote, kisha watafuatia wengine], na mimi ni *Al-Aqib (yaani*, yeye ni wa mwisho katika Mitume)".

Na katika hadithi nyingine aliyoipokea Imaam Muslim, "Mimi ni Muhammad, na Ahmad, na *Al-Muqaffi* (yaani Nabii wa mwisho), na *Al-Maahiy*, na *Al-Hashir*, na ni Nabii wa msamaha, na Nabii wa vita".

Waliomnyonyesha Mtume(saw)

Mtume(saw) alinyonyeshwa kwanza na mama yake, kisha na Bi Thuwayba, kijakazi wa Abii Lahab, ambaye alishamnyonyesha Sayyidna Hamza kabla yake. Hii ndio maana Mtume(saw) alikuwa akisema kuwa Hamza ni ndugu yake kwa kunyonya. Mwanamke wa pili kumnyonyesha Mtume(saw), baada ya mama yake, alikuwa ni Bi Salamah bin Abdul-Asad; na baadaye akanyonyeshwa na Bi Halimah As-Sa'adiyya.

Kisa cha Bi Halimah ni maarufu. Alimchukua Mtume(saw) kwa kuwa hakupata mtoto mwengine wa kumnyonyesha. Bi Halima alikuwa hana maziwa kifuani kwake, na mtoto wake akilia usiku mzima. Lakini alipombeba Mtume(saw) tu maziwa yakatoka, akamnyonyesha Mtume(saw) pamoja na mwanawe mwenyewe. Wakati wa kurudi kitongojini kwao, punda wake, aliyekuwa dhaifu wakati wa kwenda Makka, akawa na mbio kuliko wenzake mpaka wenzake wakashangaa. Mbuzi wake walikuwa hawana maziwa. Lakini tangu kuja kwa Mtume(saw)mbuzi wake walitoa maziwa mengi ya kuwatosha, hata wachungaji wakiambiwa wawafuate mbuzi wa Bi Halimah, wakitegemea na mbuzi wao pia watapata lishe inayofanana. Lakini haikuwa hivyo kwani ile haikuwa lishe bali ni baraka ya Mtume(saw). Bwana Mtume(saw) alipofikia umri wa miaka miwili, Bi Halima alimuomba mama yake aendelee kukaa naye, kwa ajili ya baraka walizokuwa wanazipata kwa kukaa na mtoto huyo. Wakakubaliwa, na hawakumrudisha mpaka pale Mtume(saw) alipojiwa na Malaika Jibril(as) akapasuliwa kifua. Hapo ndipo Bi Halimah akaona kisije kumtokea kitu kibaya mtoto wakalaumiwa, ndipo akamrudisha kwa mama yake.

Bi Halimah, alikuja kwa Mtume(saw) baada ya Utume na alisilimu pamoja na mumewe na wanawe. Kwa taadhima ya Mama yake huyo aliyemnyonyesha, Mtume(saw) alimtandikia Bi Halimah kishali chake akae juu yake.

Ama Bi Thuwayba, hakujathibiti kusilimu kwake. Lakini Mtume(saw) alikuwa akimkirimu, na kumfanyia wema alipokuwa Makka.

Alipohamia Madina alikuwa akimpelekea nguo na mahitaji mengine. Ilimfikia Mtume(saw) habari ya kufariki Bi Thuwaiba aliporudi kutoka Khaybar.

Kufariki Mama yake:

Mtume (saw) alipofikia umri wa miaka sita, mama yake alitoka naye kwenda Madina kuwazuru wajomba zake, akifuatana na mtumishi wake Ummu Ayman. Akakaa Madina mwezi mmoja, na akafariki njiani wakati wakirejea Makka, katika sehemu inayoitwa "*Abwaa*". Mtume (saw) alilia alipolizuru kaburi la mama yake katika safari yake ya Umra.

Kulelewa na Babu yake:

Mtume(saw) alilelewa na Babu yake Bwana Abdul-Muttalib baada ya kufariki kwa mama yake Bibi Amina. Bwana Abdul-Muttalib alimpenda na kumtanguliza Mtume(saw) zaidi kuliko watoto wake mwenyewe. Bwana Abdul-Muttalib alifariki dunia pale Mtume(saw) alipokuwa na umri wa miaka minane, na alizikwa Al-Hujuun.

Kulelewa na Ammi yake:

Baada ya kufariki babu yake, Mtume(saw) alilelewa na Ammi yake Bwana Abi Talib. Ami yake huyu alikuwa ndugu wa baba mmoja na mama mmoja na Baba yake Bwana Abdillah. Kadhalika, Bwana Abi Talib alikuwa akimpenda na akimtanguliza Mtume(saw) kuliko watoto wake aliowazaa.

Safari ya Shaam:

Mtume(saw) alipofikia umri wa miaka kumi na mbili, alisafiri na ammi yake Abi Talib kwenda Shaam kwa ajili ya biashara. Huko akakutana na padre wa kinasara, jina lake Bahira, ambaye alimjua kuwa atakuja kuwa Mtume(saw) kwa dalili alizoziona. Mojawapo katika dalili hizo

ni kuwa Mtume(saw) alikuwa kila aendapo anafunikwa na kiwingu, hapati jua. Baada ya yule padre kumwuliza ammi yake na yeye mwenyewe kuhusu hali yake ya usingizini na nyingine, alithibitisha kuwa yule kijana ndiye Mtume aliyebashiriwa katika vitabu vilivyotangulia. Mwishowe akamwambia Mtume amwonyeshe mgongo wake na akaona Muhuri wa mwisho wa Utume. Hapo yule padre akamshauri Ami yake arudi naye na akamhimiza amhifadhi sana na Mayahudi kwa kuhofia wasije kumdhuru wakiijua hali yake.

Kwenda Shaam kwa mali ya Bibi Khadija:

Bi. Khadija alikuwa ni mwanamke tajiri na akiwapa baadhi ya watu raslimali yake, waende wakafanye biashara Shaam, na hugawana nao faida. Aliposikia uaminifu wa Mtume(saw) akataka aende Shaam ili akafanye biashara na kumwahidi kumpa faida zaidi ya anayowapa wengine. Katika safari hiyo Mtume(saw) alifuatana na Maysarah, mtumishi wa Bibi Khadija. Wakiwa safarini, Maysarah alikuwa akiona Mtume(saw) anafunikwa na kiwingu wakati wa jua kali. Katika safari hiyo walipokuwa Basrah Maysarah alikutana na padre jina lake Nastura. Yule padre alimwuliza Maysarah kuhusu Mtume(saw), na kisha akamwambia kuwa huyo ni Mtume wa mwisho na kwamba asiachane naye. Katika msafara hyo, Mtume(saw) alipata faida kubwa. Waliporudi Makka, Maysarah alimweleza Bibi Khadija aliyoyaona kwa Mtume(saw), pamoja na taarifa alizopewa na padre Nastura.

Kuolewa Bi. Khadija na Mtume(saw):

Bi. Khadija alikuwa ni mwanamke tajiri, mwenye nasabu nzuri, na mwenye tabia nzuri. Wengi katika jamaa zake walitaka kumuoa na walimuahidi mali lakini hakukubali. Bi Khadija alimtuma Bi Nafisa bint Munyah kumshawishi Muhammad amwoe. Bi Nafisa alieleza yaliyotokea kama ifuatavyo: “Nikamwambia Muhammad, ‘Nini kinacho kuzuia usioe?” Akasema, ‘Sina kitu mkononi cha kuolea (yaani mali)’. Nikamwambia, ‘Ukipata anaye kutoshea hayo yote, na

pia ana uzuri wa sura, mali, utukufu na kuwa sawa yako utakubali?' Akauliza, 'Ni nani huyo?' Nikasema, 'Khadija'. Akauliza, 'Yatakuwaje hayo?' Nikasema, 'Niachie mimi'. Akakubali, na mimi nikaenda kwa Bi. Khadija na khabari ile. Bibi Khadija akaandaa harusi na kumwita ammi yake Amru bin Asad, ili amwoze, na akahudhuria. Na Mtume(saw) akaenda pamoja na ammi zake, naye wakati huo ana miaka 25 na Bi. Khadija ana miaka 40, na akamwoa".

Baadhi ya wanachuoni wametaja kuwa Abi Talib alipohudhuria pamoja na jamaa zake alitoa khutba ifuatayo, "Himda zote njema ni stahiki yake Allah ambaye ametujaalia sisi kuwa ni watoto wa (Nabii) Ibrahim(as) na kizazi cha (Nabii) Ismail(as) na ni chimbuko la Ma'ad na ni ukoo wa Mudhwar. Na ametufanya kuwa ni walezi wa nyumba yake na walinzi wa *Haram* yake. Na ametupa nyumba inayokusudiwa kwa Hijja na *Haram* yenye amani na akatufanya sisi kuwa ndio watawala wa watu. Kisha (baada ya yote hayo), hakika mwana wa ndugu yangu huyu, Muhammad bin Abdillah, hapimwi na mtu yeyote ila yeye atamshinda mtu huyo. Ingawa ni mchache wa mali, hakika mali ni kivuli kiondokacho na ni jambo hemezi. Na (huyu) Muhammad ni yule ambaye mmekwisha ujua ukoo wake, nae amemposa Khadija bint Khuwaylid na amempa mahari aliyoitanguliza na kubakisha nyingine katika mali yangu. Naye baada ya leo, wallah atakuwa na khabari kubwa na jambo tukufu".

Kutetea madhaifu (wanyonge):

Mtume(saw) alikuwa akishirikiana na jamaa zake katika kila jambo jema. Katika mambo mema aliyoshirikiana nao ni ahadi ya kutetea madhaifu, ambayo ilikuwa mashuhuri kama "*hilful-fudhuul*", yaani viapo vya watu watukufu. Imepokewa na Ibn Is-haq kwamba Mtume(saw) amesema: "Nimeshuhudia kupeana ahadi kwenye nyumba ya Abdallah bin Jad-an, hiyo ahadi ni bora kwangu kuliko wanyama wekundu, na lau ningeitiwa jambo hilo katika Uislamu ningeitika".

Ahadi yenyewe ya "*hilful-fudhuul*" ilikuwa kama ifuatavyo, "Alikuja mtu kutoka Zabiid na biashara yake. Aasi bin Waail akachukua bidhaa

na akakataa kumlipa. Yule mtu akaenda kwenye makabila tofauti likiwemo Abdid-Daar, Makhzuum, na Adiy bin Ka'ab wasiweze kumsaidia kumpatia haki yake. Akasimama juu ya Jabal Abi Qubays, na kunadi, 'Enyi Jamaa za Fihr (Fihr ndio Qureshi), msaidieni mwenye kudhulumiwa bidhaa yake ndani ya Makka, aliyekuja kutoka mbali, asiye na watu (hapa) na (amekuja) akiwa amehirimia Umra, akiwa timtim wa nywele, akiwa bado hajaikidhi Umra yake. Enyi mlo kuja kwa miguu nyie! Na baina ya jiwe (jabali) na jiwe hakika haramu ni ya yule uliopomoka utukufu wake na wala hapana haramu kwa nguo ya mtu muovu, mfanya khiana'. Akasimama Zubeir bin Abdil-Muttalib na kusema inakuwaje mtu anakuja kwetu tunashindwa kumnusuru.Wakakusanyika Baniy Hashim, Baniy Muttalib, Baniy Asad bin Abdil-uzza, Baniy Zuhra, Baniy Taym bin Murrah katika nyumba ya Abdallah bin Jad-a'n Al-Taymiy kwa ajili ya utu uzima wake na utukufu wake. Wakapeana ahadi, kuwa hawatomkuta Makka mwenye kudhulumiwa akiwa mkazi wa pale au mgeni aliye kuja pale, ila watakuwa pamoja katika kumnusuru mwenye kudhulumiwa hadi wampatie haki yake. Kisha wakaenda kwa Aasi na kumnyang'anya bidhaa yake na kumkabidhi yule mtu wa Zabiid".

Katika riwaya nyengine, alisema Muhammad bin Is-haaq bin Yasaar, ".....na yakaitana makabila ya Kikureishi kwenye kiapo, basi wakakusanyika kwa ajili yake katika nyumba ya Abdallah bin Jad'aan kwa sababu ya utukufu wake na utu uzima wake. Na waliapa mbele yake Baniy Hashim, Banil-Mutwalib, Baniy Asad bin Abdil-uzza na Baniy Zuhrah bin Kilaab na Taym bin Murrah, wakapeana na kufunga ahadi ya kwamba wasimpate mdhulumiwa Makka; katika wenyeji wa hapo au katika wa kuja miongoni mwa watu wengine, ila watakuwa pamoja nae. Na watakuwa dhidi ya aliye mdhulumu mpaka amrejeshee alicho mdhulumu na Makureishi wakakiita kiapo hicho kwa jina la "*Hilful-Fudhuul*".

Katika yaliyopokewa pia ni kuwa Sayyidna Husain bin Aliy alikuwa na ugomvi na Waliid bin Utbah bin Abi Sufyan aliyekuwa Liwali wa Madina juu ya mali, akawa Waliid hataki kumlipa kwa ajili ya cheo chake. Akasema Sayyidna Husain: Namwapia Mwenyezi Mungu, utanipa haki yangu au nitachukua upanga wangu na nisimame kwenye

msikiti wa Mtume(saw) na kisha nitanadi kwa kiapo cha *Fudhuul*. Akasema Sayyidna Abdallah bin Zubair, naye alikuwa amehudhuria hapo: Wallahi akilingania hayo, na mimi nitachukua upanga mpaka apate haki yake au tufe wote. Khabari hii ikamfikia Miswar bin Makhramah bin Naufal Al-Zuhry, naye akasema kama hayo, na ikamfikia Abdul-Rahman bin Uthman bin Ubaydillah Al-Taymiy, naye pia akasema hivyo. Zilipo mfikia khabari hizo Waliid bin Utbah, akampa haki yake Sayyidna Husain hadi akaridhia.

Kujenga Ka'aba:

Mtume(saw) alipo fikia umri wa miaka 35 alishuhudia kujengwa kwa Ka'aba na alishirikiana nao kwenye ujenzi, na ulitokea ugomvi juu ya nani alihamishe jiwe jeusi na kuliweka sehemu yake, wakakubaliana kwamba mtu wa kwanza atakayeingia msikitini humo ndiye awe hakimu wa mzozo wao huo. Ikasadifu kuwa Mtume(saw) ndio wa kwanza mwenye kuingia, wote wakasema, "Huyu ni mwaminifu." Makureshi walikuwa wakimwita mtu mwaminifu, na wakiweka kwake amana hata baada ya Utume. Baada ya kupewa khabari, akatandika kishali chake, na kumwambia kila mkubwa wa kabila ashike pembe moja, na walipo fika sehemu yake, Mtume(saw) akalichukua kwa mkono wake mtukufu na kuliweka sehemu yake tukufu.

Dalili za utume wake kabla ya kushuka kwa wahyi:

Tumeshaona kuwa Bibi Amina aliona nuru alipozaliwa Mtume(saw) ambayo ilizagaza Mashariki na Magharibi, na pia khabari ya mapadre Bahira na Nastura ambazo zilionyesha kuwa yeye ndiye Mtume mtarajiwa.

Pia kuna hadithi iliyopokewa na Sahaba Ibn Abbas kwamba kitu cha kwanza ambacho Mtume(saw) alichokisikia naye ni kijana mdogo, ni sauti ikimwambia jisitiri, basi haukuonekana utupu (uchi) wake baada ya siku hiyo.

Na katika hadithi iliyo pokewa na maimamu Muslim na Ahmad: kwamba Mtume(saw) amesema: “Mimi nalijuwa jiwe Makka, lililokuwa likinisalimia kabla ya utume, hata hivi sasa nalijuwa”.

Na imepokewa pia kuwa alipokuwa anatoka kwa ajili ya kukidhi haja yake, sehemu mbali na watu, kwenye majabali na katikati ya jangwa, alikuwa halipitii jiwe au mti ila husema (hilo jiwe/mti): “*Assalaam Alayka Yaa Rasulullah*!” akigeuka kulia, kushoto na nyuma hamuoni mtu.

Jinsi ulivyokuwa ukishuka wahyi:

Imepokewa katika maimamu Bukhariy na Muslim, kwamba Mtume(saw) aliulizwa vipi unateremka wahyi kwako, akasema, “Baadhi ya wakati inanijia kama kelele ya kengele na hiyo ndio hali ngumu kabisa, unafunguliwa (unafunuliwa) wahyi kwangu, na huwa nimeshahifadhi kila alichosema. Na baadhi ya nyakati malaika anakuja katika sura ya binadamu, hunisemesha nami huhifadhi alichokisema. Amesema Sayyidatna Aisha, “Hakika nilimuona [Mtume(saw)] akishushiwa wahyi katika siku yenye baridi kali, hufunguliwa (wahyi) na kipaji chake cha uso kikitoka jasho”.

Na imepokewa kwamba Sahaba Zayd bin Thabit, amesema, “Nilikuwa nimekaa pembezoni mwa Mtume(saw), akajiwa na wahyi, na akafunikwa na utulivu, na paja lake likaangukia la kwangu alipokuwa akishushiwa wahyi. Basi namwapia Mwenyezi Mungu, sikuona kitu kizito kuliko paja la Mtume(saw) kisha akatoka kwenye wahyi na kunisomea niandike wahyi”. Na katika riwaya iliyopokewa na Imaam Bukhariy, likawa zito paja lake hata nikahisi atalivunja paja langu.

Na katika riwaya nyingine, mmoja wa masahaba anasema, “Niliona wahyi ukishuka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) na yeye yuko juu ya kipando chake, (kile kipando) kikajaribu kututumua mikono yake mpaka nikadhania kuwa miguu yake itakatika. Na huenda kile (kipando-mnyama) hukaa chini kabisa na huenda husimama akiwa amejitahidi kunyoosha mikono yake mpaka wahyi umalizike kwa uzito

wa wahyi, na jasho likiwa linamtoka Mtume(saw) na kung'ara kama lulu".

Kulingania Uislamu kwa siri:

Imepokewa kwamba Mtume(saw) alilingania kwa siri kwa miaka mitatu, kisha akaamrishwa adhihirishe. Imepokewa pia kuwa Sayyidna Abubakr, Sayyidna Uthman, Sayyidna Said bin Zayd na Sayyidna Ubaydah bin Jarrah walikuwa wakilingania Uislamu kwa siri, na Sayyidna Umar na Sayyidna Hamza walikuwa wakilingania kwa dhahiri.

Watu wa mwanzo kusilimu:

Wanachuoni wa Tarikh (Historia) wamekubaliana kwamba mtu wa kwanza kusilimu alikuwa ni Bi. Khadija(ra), ila wamekhitalifiana katika watu hawa watatu, nani anayefuatia, Sayyidna Abu Bakr(ra), Sayyidna Aliy(ra) na Sayyidna Zayd bin Harith(ra), "huru" wa Mtume(saw). Kwa ujumla, wa kwanza kusilimu katika watu wazima, wanaume, na waliokuwa huru ni Sayyidna Abu Bakr(ra), katika akina mama ni Bi. Khadija(ra), katika vijana wadogo ni Sayyidna Aliy(ra), katika walio achwa huru ni Sayyidna Zayd bin Harith(ra), na katika watumwa ni Sayyidna Bilaal bin Rabaah(ra). Watu watano hawa ndio wa mwanzo kusilimu na ndio vinara wa Uislamu.

Kulingania kwa dhahiri:

Baada ya miaka mitatu ya kulingania watu kwa siri, Mwenyezi Mungu alimwamrisha kudhihirisha mlingano wake kwa neno lake tukufu,

فَٱصۡدَعۡ بِمَا تُؤۡمَرُ وَأَعۡرِضۡ عَنِ ٱلۡمُشۡرِكِينَ

"Na tangaza uliyo amrishwa na wapuuze makafiri". (Hijr:94)

Akasimama Mtume(saw) juu ya mlima Safaa kama ilivyopokewa kwa Sahaba Ibn Abbas(ra), na akawalingania watu wake, walipofika akawaambia, “Mnaonaje kama nikikupeni khabari kuwa nyuma ya mlima huu kuna adui atakujieni asubuhi au jioni, je mutanisadikisha?” Wakasema: Naam bila ya shaka, kwani hatukuwahi kukusikia ukisema uongo. Akasema: “Basi mimi ni mwenye kukuonyeni na adhabu kali inayokukabilini.” Akasema Abi Lahab, “Umeangamia! Je, hili ndilo ulilotuitia?” Ndipo ikashuka,

تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ

“Imeangamia mikono ya Abi Lahab na ameangamia (yeye mwenyewe pia).” (Masad:1)

Makureshi na mlingano wao kwa Abi Talib:

Imepokewa kutoka kwa Imaam Ibn Is-hak kwamba Mtume(saw) alidhihirisha mlingano wake, na akaikosoa miungu yao na wakaona kuwa ammi yake Bwana Abi Talib anamlinda. Wakubwa wa kikureshi wakamwendea Bwana Abi Talib na kumwambia, “Ewe Abi Talib! Hakika mtoto wa ndugu yako ameitukana miungu yetu, akaiaibisha dini yetu, na akazitia upotofu akili zetu na akawatia katika upotofu wazee wetu, basi ima umzuie au utuachie sisi tumzuie". Bwana Abi Talib akawajibu jibu zuri, wakaondoka lakini Mtume(saw) akaendelea na mlinganio wake. Makureshi wakachukia zaidi, hasa walipoona kuwa Abi Talib hamzuii. Wakamwendea tena na kumwambia, “Ewe Abi Talib! Hakika wewe ni mwenye umri mkubwa na mwenye utukufu, tumekwambia umkataze mtoto wa ndugu yako na hukumkataza, na sisi wallahi hatusubiri juu ya haya ya kutukanwa wazee wetu na kuzitia upotofu akili zetu na kuaibisha miungu yetu, kwa hiyo ima umzuie au tupigane vita na wewe na yeye mpaka kiangamie kikundi kimojawapo”. Bwana Abi Talib akaona uzito kutengana na watu wake na uadui wao na wala hakutaka kumsalimisha Mtume wa Mwenyezi Mungu kwao wala kumdhalilisha. Basi akamwita Mtume(saw) na kumwambia

kwamba walikuja jamaa zako na akamueleza waliyoyasema, kisha akamwambia, "Basi usinibebeshe mzigo nisiouweza". Mtume(saw) akahisi kuwa ammi yake amechoka kumnusuru na kusimama naye, akasema neno lake tukufu:

“Ewe Ammi yangu, Wallahi lau wangeweka jua kwenye mkono wangu wa kulia na mwezi kwenye mkono wangu wa kushoto, ili niache jambo hili nisingeliwacha, hadi Mwenyezi Mungu alidhihirishe au niangamie mimi”. Kisha akalia. Alipompa mgongo ammi yake aondoke, Ammi yake akamwita, “Njoo ewe mtoto wa ndugu yangu!” Alipokwenda akamwambia, “Nenda ewe mtoto wa ndugu yangu, useme unayoyataka, wallahi sitakusalimisha kwa lolote”.

Walipoona Makureshi kuwa Bwana Abi Talib ameahidi kumnusuru mtoto wa ndugu yake kwa lolote, wakamwendea Abi Talib na Ammara bin Waliid, wakamwambia, “Mchukue kijana huyu mzuri kwa sura na mwenye akili, awe wako, na utupe mtoto wa ndugu yako huyu, ambaye amekhalifu dini yako na dini ya wazee wako, na akavunja umoja wa watu wako, na akazitia upotofu akili zetu, na tumwulie mbali kwani tunakupa mtu badala ya mtu”. Akasema, “Mnanipa mtoto wenu nimlishe kwa ajili yenu na nikupeni mtoto wangu mumwue, hilo wallahi haliwi”.

Kukatwa pande Baniy Hashim na Baniy Muttalib na kwenda kwao kwenye Shiib (kiunga cha) Abi Talib:

Na walipoona Makureshi kuenea kwa Uislamu na kupata nguvu kwake wakakusanyika kuandika mkataba baina yao, kuwa wasioe Baniy Hashim wala Baniy Muttalib, wala wasiwaoze wao, wala wasiuze wala kununua bidhaa zao. Na wakaandika katika karatasi na kuitundika kwenye Ka’aba. Walipo fanya hayo, wakakusanyika Waislamu pamoja na Baniy Hashim na Baniy Muttalib (isipokuwa Abi Lahab) kwenye shiib Abi Talib, na wakakaa huko miaka mitatu hadi wakapata njaa kali na shida, na hawakuwa na chakula ila walicholetewa kwa siri na jamaa zao. Na Mtume(saw) akawa analingania kwa Mwenyezi Mungu kwa siri na dhahiri, na wahyi ukiendelea kushuka, mpaka kikatokea kikundi

katika Makureshi ambao iliwauma sana shida wanayoipata ndugu zao. Akaenda Hishaam bin Amru kwa Zuhayr bin Umayya na kumwambia, “Je, umeridhia kula chakula na kuvaa nguo na kuoa wanawake wakati wajomba zako wako katika hali unayoijua!” Zuhayr akamwambia, “mimi ni mtu mmoja nitafanya nini, wallahi ningekuwa na mwingine ningeuvunja huu mkataba”. Hishaam akamwambia umempata mtu mmoja, mimi mwenyewe, tumtafute wa tatu. Akaenda Hishaam kwa Mut-im bin Adiy, akamwambia, “Unaridhia matumbo mawili ya Abdi Manaaf yaangamie na wewe unashuhudia na kuridhia hayo?” Mut-im akajibu, “mimi mtu mmoja, nitafanya nini? Hishaam akamwambia, “Umempata wa pili”. Mut-im akasema, “Tumtafute wa tatu”. Hishaam akamjibu, “Ninaye wa tatu, Zuhayr bin Umayya”. Mut-im akashauri, “Mtafute wa nne”. Akaenda Hisham kwa Abil-Buhtury bin Hisham, na kumwambia aliyomwambia Mut-im. Naye akamwuliza, “Je kuna mwingine mwenye kusaidia hili?” Hishaam akajibu, “Naam, mimi, na Zuhayr na Mut-im”. Abil-Buhtury Akasema tumtafute wa tano. Hisham akaenda kwa Zam’a bin Aswad bin Muttalib, akamwambia na kumtajia udugu wao. Zam’a akamwuliza, “Je, kuna msaidizi wa jambo hili?” Hishaam akamtajia aliokubaliana nao, wakakusanyika usiku na wakakubaliana kuuvunja mkataba. Wakasimama kuuvunja. Aliposimama Mut-im kuuchana ule mkataba, akakuta kuwa wadudu wameula ule mkataba ila jina la Mwenyezi Mungu. Wakapata faraja Waislamu na kutoka kwenye janga hilo.

Katika riwaya nyingine, Mtume(saw) aliambiwa na Jibriil kuwa mkataba ule umeliwa na wadudu ila jina la Mwenyezi Mungu. Mtume(saw) akamwambia ammi yake ambaye hakuwa na shaka na maneno yake. Bwana Abi Talib akawaendea Makureshi na kuwaambia, “Mtoto wa ndugu yangu, ameniambia kuwa Mwenyezi Mungu ametuma wadudu na wamekula mkataba wenu ila jina la Mwenyezi Mungu. Basi uleteni mkataba, ikiwa ni kweli aliyoyasema basi mtajua kuwa nyie mumetudhulumu na mumekata udugu. Na ikiwa si kweli aliyoyasema, basi tutajua kuwa nyie muko juu ya haki, na mimi niko juu ya batili”. Wakainuka haraka na kuuleta mkataba, wakaona kama alivyosema Mtume(saw).

Kwenda Twaif:

Imepokewa na maimamu Bukhariy na Muslim(ra), kwamba Sayyidatna Aisha(ra) alimwuliza Mtume(saw): “Je, uliwahi kupata matatizo zaidi ya yale ya siku ya Uhud? Akajibu, “Nimepata shida kutoka kwa jamaa zako na ilikuwa kubwa zaidi, siku ya Aqaba, nilipo enda kwa Ibn Abdi Yalayl (wakubwa wa Thaqiif, waliokuwa wakikaa Twaif), na hawakujibu ulinganio wangu. Nikaondoka hali ya kuwa nina huzuni usoni, sikuzindukana ila niko Qarn Thaaliba. Nikanyanyua uso wangu, kutahamaki nikaona kiwingu kimenifunika, nikaangalia nikamuona Jibriil ndani yake, akininadia, “Hakika Mwenyezi Mungu amesikia maneno ya watu wako kwako na waliyokujibu, na amekutumia Malaika wa majabali uwaamrishe unachotaka, ukitaka niwaponde kwa kukusanya majabali mawili (Jabali la Abu Qubays, na jabali lililo kuwa mkabala wake)”. Mtume(saw) Akasema, “La, nataraji Mwenyezi Mungu atawatoa katika migongo yao watakaomwabudu Mwenyezi Mungu peke yake na wasimshirikishe na chochote”.

Mtume(saw) alikwenda Twaif baada ya kufariki kwa Ammi yake na kupata maudhi makubwa sana Makka. Akatoka na huru wake Sayyidna Zayd bin Harith(ra), akawalingania viongozi wa Twaif nao ni ndugu watatu: Abdi Yalayl, Mas-ud na Habiib, watoto wa Amr. Wa kwanza akamwambia Mtume(saw) yeye akiwa ni Mtume kweli, basi ataivika guo Ka’aba. Akasema wa pili wao, ama Mwenyezi Mungu hakumpata yeyote wa kumpa utume ila wewe! Na wa tatu akasema, “Wallahi siwezi kuzungumza nawe kabisa, ukiwa kweli ni Mtume, wewe ni mbora zaidi, kuliko nirejeze maneno yako, na ukiwa mwongo haitakiwi nizungumze na wewe”. Akatoka Mtume(saw) naye akiwa amekata tamaa na kunusuriwa na Thaqiif. Wakawatuma wahuni wao, wakimtukana na kumrembea mawe. Akarudi amekata tamaa na damu zinamchuruzika, na akatulia chini ya kivuli cha mti na kuomba dua yake mashuhuri, “*Allahumma ilayka ashkuu* ...” Hapo ndipo Malaika Jibril(as), akifuatana na Malaika wa milima, alipomjia Mtume(saw) kama tulivyoeleza hapo juu.

Israi na Miiraji:

Baada ya kutoka Twaif, na baada ya kupata matatizo aliyoyapata, alihuzunika sana Mtume(saw), Mwenyezi Mungu akamtunuku safari tukufu ya Israai na Miiraji, akamthibitishia daraja yake kubwa kuwapita Mitume wote na akamwonyesha utukufu wake. Israai ni safari yake ya kutoka Makka hadi Baytil-Muqaddas iliyoko Jerusalem, Palestina, na Miiraji ni safari yake ya kutoka hapo na kwenda mbinguni. Huko mbinguni alifaradhiwa swala khamsini, kisha zikapunguzwa hadi zikawa tano. Moja katika neema alizokirimiwa Mtume(saw) akiwa huko mbinguni katika Safari hii ya Miiraji, kama ilivyopokewa katika hadithi sahihi na Imaam Ahmad kupitia kwa Sahaba Ibn Abbas(ra), "Nimemwona Mola wangu, aliyetukuka".

Wanachuoni wamekubaliana kwamba Israi na Miiraji ilikuwa kwa mwili na roho yake, na si usingizini kwani mtu usingizini anaona mengi, na si sawa na mtu kushuhudia (kuona kwa macho).

Maudhi aliyoyapata Mtume(saw) kutoka kwa washirikina:

Mtume(saw) alipata maudhi ya kila aina, lakini maudhi haya yalikuwa yana nafuu wakati wa uhai wa ammi yake Bwana Abi Talib, kwani alikuwa akimkinga Mtume(saw) na watu wake, na Makureshi walikuwa wakimuheshimu na kumwogopa Bwana Abi Talib kwa ajili ya cheo chake na kwa kuwa ni kiongozi wao.

Alipofariki Bwana Abi Talib, Mtume(saw) alipata maudhi makubwa sana. Imepokewa kutoka kwa Sahaba Abdillah bin Mas-ud kwamba hakumuona Mtume(saw) akiwaapiza Makureshi ila siku moja. Siku hiyo alikuwa akiswali na kikundi cha Makureshi wamekaa na utumbo wa uzazi wa ngamia ukiwa mbele yao. Wakasema nani auchukue utumbo huu na kumwekea mgongoni Muhammad(saw). Akajitokeza Uqbah bin Abi Muayt, akauchukua utumbo ule na kuuweka juu ya mgongo wa Mtume(saw). Mtume(saw) akaendelea kusujudu mpaka akaja Sayyidatna Fatima(ra) na akauondoa mgongoni mwake. Akasema Mtume(saw), "Ewe Mwenyezi Mungu waangamize viongozi wa

Kureshi! Ewe Mwenyezi Mungu, kuangamia kushuke juu ya Utbah bin Rabiah! Ewe Mwenyezi Mungu, juu ya Shaybah bin Rabia. Ewe Mwenyezi Mungu juu ya Abi Jahl bin Hisham. Ewe Mwenyezi Mungu, juu ya Uqbah bin Abi Muayt. Ewe Mwenyezi Mungu juu ya Ubayy bin Khalaf au Umayya bin Khalaf". Anasema Abdillah bin Mas-ud nikawaona hawa wote wameuawa siku ya Badr, kisha wakakokotwa na kutupwa kwenye kisima cha zamani, isipokuwa Ubayy au Umayya kwani alikuwa mtu mnene, akapasuka. (Bukhariy na Muslim).

Imepokewa na Imaam Bukhariy, kwamba aliulizwa Sahaba Abdillah bin Amr bin Al-Aas, Kitu kiovu sana mushrikina walichomfanyia Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akajibu, Alipokuwa Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu ndani ya Ka'aba alikuja Uqbah bin Abi Muayt akayashika mabega ya Mtume(saw), na kumkaba na nguo yake shingoni, akamkaba vibaya sana. Akaja Sayyidna Abu Bakr akamfungulia Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu na kusema, "Munamuua mtu kwa kuwa tu anasema kuwa Mungu wangu ni Allah, na wakati zimekujilieni dalili za wazi kutoka kwa Mola wenu?!"

Imepokewa kutoka kwa maimamu Ahmad na Tirmidhiy kwamba Mtume(saw) amesema: "Nimepata maudhi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, maudhi asiyoyapata mtu mwengine, na nimetishwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na hakutishwa mtu mfano wangu ...."

Kulingania kwake wakati wa misimu:

Imepokewa na Sahaba Jabir bin Abdillah amesema, Alikuwa Mtume(saw) analingania katika mahala wanaposimama watu katika msimu wa Hijja na akisema, "Je, kuna mtu atakayenichukua kwa watu wake, kwani Makureshi wamenizuia kufikisha maneno ya Mola wangu". Imepokewa na Tirmidhiy.

Na imepokewa na maimamu Ahmad na Al-Hakim kwa riwaya sahihi kupitia kwa Sayyidina Jabir bin Abdillah(ra), "Alikaa Mtume(saw) miaka kumi, akiwafuatilia majumbani mwao, (kwenye soko la) *Ukadh*, na *Majannah* na kwenye misimu Minaa. Akisema, 'Nani mwenye

kunikaribisha kwake, nani mwenye kuninusuru mpaka nifikishe ujumbe wa Mola wangu na yeye atapata Pepo'. Hata ikawa mtu anatoka Yaman au Misri anaambiwa na watu wake, 'Jihadhari na kijana wa kikureshi asikufitini. Anapitia kwenye makazi yao na wao wanamuashiria kwa vidole, mpaka alipotuleta Mwenyezi Mungu kutoka Yathrib (Madina) tukamkaribisha na kumnusuru na kumuamini. Akawa anatoka mmoja wetu anamwamini, anasomeshwa Qur-ani na anarudi kwa watu wake, na wao wanasilimu kwa Uislamu wake, mpaka haikubaki nyumba katika nyumba za Ansaari ila kilikuwemo ndani yake kikundi cha Waislamu kinachoudhihirisha Uislamu wao. Kisha tukafanya shauri sote, na tukasema, hadi lini tutamwacha Mtume wa Mwenyezi Mungu akifukuzwa huku na huku kwenye majabali ya Makka huku ikiwa imemjaa khofu? Wakamwendea katika sisi watu sabini, mpaka wakamjia kwenye msimu, tukapeana ahadi ya kukutana kwenye pango la Aqaba (panapo tupiwa mawe). Tukajumuika kwenye sehemu hiyo, mmoja mmoja hadi tukakusanyika sote tukamwambia, 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, tukupe ahadi ya utii kwa lipi?' Akasema, "Nipeni ahadi juu ya usikivu na utii katika hali ya uchangamfu na machofu, na kujitolea kwa mali wakati wa raha na wakati wa shida. Na juu ya kuamrisha mema na kukataza mabaya, na museme (haki) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na wala msiogope lawama ya mwenye kulaumu, na juu ya kuninusuru na kunilinda nikija kwenu kwa mnayozilinda nafsi zenu na wake zenu na watoto wenu, nanyi mtapata Pepo".

Akaendelea kusema Sayyidina Jabir(ra), "Tukasimama na tukampa ahadi na akamshika mkono wake As-ad bin Zuraara naye ni mdogo wao na akasema, 'Pole pole enyi watu wa Yathrib! Kwani sisi hatukuja juu ya vipando vya ngamia ila sisi tunajua kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Kumtoa kwake leo ni kutengana na Waarabu wote, na kupigana na waliowabora kwenu hata kama yatakulazimuni mapanga. Basi ima nyie mutasubiri juu ya hayo na ujira wenu uko kwa Mwenyezi Mungu, au mutaogopa kwa ajili ya nafsi zenu, basi bainisheni kabisa, kwani hilo ndilo litakalokupeni udhuru kwa Mwenyezi Mungu." Wakasema, 'Hebu tuache ewe As-ad! Kwani Wallahi hatutoacha ahadi hii milele, na wala hatutaipoka Milele'. Basi

tukanyanyuka na kumpa ahadi Mtume(saw). Naye Mtume(saw) akachukua kwetu ahadi kwa sharti zake, na atatupa Pepo kwa ajili ya hayo".

Kuhama Mtume(saw) kwenda Madina:

Hapa tutaelezea kuhama kwa Mtume(saw), tukifupisha kutoka katika hadithi aliyoipokea Imaam Bukhariy kwa riwaya ya Bibi Aisha:

Mtume(saw) aliota kuwa watahamia sehemu yenye mitende, na masahaba wakaanza kuhamia Madina. Akataka Sayyidina Abu Bakr(ra) kuhama na akafanya matarayarisho ya kuhama lakini Mtume(saw) akamwambia asubiri, huenda na yeye Mtume(saw) akapewa ruksa ya kuhama. Akajizuia Sayyidina Abu Bakr(ra) ili asuhubiane na Mtume wa Mwenyezi Mungu, na akatayarisha vipando viwili.

Anasema Bibi Aisha, tulipokuwa tumekaa nyumbani wakati wa jua kali, akasema mtu kumwambia (Sayyidina) Abu Bakr(ra), "Huyo Mtume anakuja akiwa amejifunika (kuficha sura) na si kawaida yake kuja kwetu muda huu. Akasema Sayyidina Abu Bakr(ra), "Amfidie kwa baba yangu na mama yangu, wallahi hakuja muda huu ila kuna jambo. Akabisha hodi, akapewa ruhusa na kuingia ndani. Mtume(saw) akamwambia Sayyidina Abu Bakr, "Waondoe waliopo kwako nina jambo muhimu la kusema". Akasema Sayyidina Abu Bakr, "Hakika hawa ni watu wako, nakufidia kwa baba yangu na mama yangu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu". Akasema Mtume(saw), "Hakika nimepewa ruhusa kuondoka". Akasema Sayyidina Abu Bakr, "Naomba niwe na wewe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Akasema, "Ndio". Akasema Sayyidina Abu Bakr, Chukua kimojawapo cha vipando hivi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu, "(nakubali kuchukua) kwa thamani".

Anasema Bibi Aisha, Tukatengeneza vipando hivyo viwili vizuri kabisa, na tukawatengenezea chakula tukakiweka katika mfuko. Asmaa bint Abi Bakr akakata kamba yake (ya kujifungia kwenye nguo) na akafunga mojawapo juu ya mdomo wa kiriba. Kwa ajili hiyo ndio anaitwa "*Dhaatul Nutaaqein*" (mwenye kamba mbili). Anasema,

“Kisha (Sayyidina) Abu Bakr na Mtume wa Mwenyezi Mungu wakaelekea katika pango la Thaur, wakakaa humo masiku matatu. Analala kwao Abdillah bin Abi Bakr, naye ni kijana mahiri na mweledi, anatoka kwao wakati wa kula daku kwenda kwa Makureshi. Anakuwa na Makureshi kama vile amelala (huko Makka). Kila analolisikia huliweka kichwani mpaka humletea Mtume(saw) na Sayyidina Abu Bakr habari hiyo wakati kinapoingia kiza. Na Amir bin Fuhayra - huru wa Abu Bakr - huwaletea maziwa ya mbuzi baada ya kupita saa moja tangu kuingia kiza. Alifanya hivyo Amir bin Fuhayra siku zote tatu. Mtume wa Mwenyezi Mungu na Sayyidina Abu Bakr walimkodi mtu katika kabila la Baniy Abd bin Adiy awe ndio mwenye kuwaonyesha njia. Mtu huyo alikuwa rafiki wa Jamaa wa Aas bin Wail, naye yuko katika dini ya ukafiri ya Makureshi. Lakini walimwamini na kumwachia vipando vyao, na wakamwahidi wakutane naye kwenye pango la Thaur asubuhi ya siku ya tatu. Mwenye kuwaonyesha njia akawapitisha njia ya pwani. Wakaondoka na Amir bin Fuhayra.

Imepokewa na Imaam Bukhariy kuwa Suraaqa bin Ju’shum amesema, “Walikuja kwetu makafiri wa kikureshi wakaweka dau la ngamia mia moja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakr kwa kila mmoja, kwa mwenye kumwua au kumkamata. Nilipokuwa nimekaa na watu wangu wa Baniy Mudlaj, akasema mtu na sisi tukiwa tumekaa, ‘Ewe Suraaqa nimeona sasa hivi kundi likipita pwani, nahisi ni Muhammad na watu wake’. Nikajua kuwa ndio wao, nikasema sio wao lakini wewe umewaona fulani na fulani wametoka kwetu sasa hivi. Kisha nikakaa muda kidogo na nikaingia ndani na kumwamrisha kijakazi wangu atoke na farasi wangu kwa mlango wa nyuma na anisubiri, na nikatoka na mkuki wangu. Nikapanda farasi wangu nikakimbia naye, hadi nikawakaribia, akateleza farasi wangu na kuanguka, nikapeleka mkono wangu kwenye sehemu ya kuwekea mishale na kutoa ramli, nikapiga ramli niwadhuru au la, ikatokea ninayochukia (ikinikataza nisiwadhuru). Nikapanda farasi na nikaenda kinyume na ramli, nikawakaribia, nikamsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu anasoma wala hageuki, na Abu Bakr akigeuka kila mara, ikazama mikono ya farasi wangu mpaka ikafikia kwenye vifundo. Nikamtutumua kwa nguvu na ilikuwa mikono yake imekwama sana. Niliposimama naye, likatoka

vumbi kama moshi, nikapiga ramli ikaja kinyume na ninavyotaka, nikawataka amani, wakasimama nikapanda farasi wangu mpaka nikawafikia. Na nikapata hisia baada ya kutokuweza kuwafikia kuwa litadhihiri jambo (dini) la Mtume wa Mwenyezi Mungu. Nikamwambia, 'Hakika watu wako wameweka kwako zawadi (dau) nono'. Na nikamwambia yote waliyokusudia watu kuwafanya. Na nikawawekea mbele yao chakula cha safari wasiniombe chochote, ila alisema Mtume, 'Tufanyie wepesi (usiwaelekeze watu kwenye njia yetu)'. Nikamwomba aniandikie amani, akamwambia Amir bin Fuhayra akaniandikia kwenye kipande cha ngozi".

Amesema Urwa bin Zubayr kwamba, "Waislamu waliokuwa Madina walisikia kuwa Mtume(saw) ametoka Makka wakawa wanatoka kila siku wakiwasubiri hadi jua likiwa kali sana ndio huwarudisha majumbani mwao. Wakarudi siku moja wakiwa wameshasubiri sana. Walipofika majumbani, alipanda mtu mmoja katika Mayahudi ngome yao kwa ajili ya kutizama kitu, akamwona Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu na masahaba wake wakiwa wamevaa nguo nyeupe. Hakuweza kujizuia yule yahudi akasema kwa sauti kubwa: Enyi Waarabu amekuja mtu wenu muliokuwa mukimsubiria! Wakatoka Waislamu wakampokea Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume(saw) akashukia katika boma la Baniy Amr bin Auf, na hiyo ilikuwa ni siku ya Jumatatu ya Rabiul-Awwal. Akasimama Abu Bakr na Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu akiwa amekaa chini kimya, wakawa wanakuja ambao hawajawahi kumwona Mtume wa Mwenyezi Mungu kabla wanamsalimia Abu Bakr, hadi Mtume wa Mwenyezi Mungu lilipo mpiga jua, akaja Abu Bakr akimkinga kwa radi yake, hapo ndipo watu wakamjua Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu. Akakaa Mtume(saw) kwa Baniy Amr bin Auf zaidi ya siku kumi na akaweka msingi wa Msikiti (wa Kubaa) ambao uliasisiwa kwa ucha Mungu na akaswali ndani yake. Kisha akapanda kipando chake, akawa anakwenda na watu hadi kilipotulia kipando chake kwenye msikiti wa Mtume(saw) Madina. Huo ndio unaoswaliwa hivi sasa. Mahala hapo ilikuwa ni sehemu ya kukaushia mitende ya Sahl na Suhail, vijana wawili mayatima walio kuwa wakikaa kwa As'ad bin Zuraara. Akasema Mtume(saw) kilipokita hapo kipando chake, "Hapa ndio nyumba (makazi) Inshallah". Kisha

akakubaliana Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu na vijana wawili wale (kuinunua ile) sehemu ya kukaushia (tende) kwa ajili ya msikiti. Wale vijana wakasema bali tunaitoa kama zawadi kwako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Kisha akajenga Msikiti, na akawa anabeba pamoja nao matofali katika nguo yake na akisema huku akibeba matofali,

هذا الحمال لا حمال خيبر هذا أبر ربنا وأطهر

Twika (mzigo) hii si kama twika ya Khaybar,

hii ni (twika) iliyo bora na tukufu zaidi.

(Maana ya ubeti huu ni kwamba, twika hii ya matofali kwa ajili ya ujenzi wa msikiti, ni bora mbele za Mwenyezi Mungu kuliko ile biashara inayobebwa Khaybar).

Na akisema pia:

اللهم إن الأجر أجر الآخرة فاغفر للأنصار والمهاجرة

Ewe Mola wa haki! Hakika ya ujira bora ni ule ujira wa Akhera,

Nakuomba uwaghufirie Answaari na Muhajirina.

Akawa anasoma shairi la mtu ambaye hakutajwa. Amesema Ibn Shihaab, na haijatufikia katika Hadithi kuwa Mtume(saw) amesoma shairi lililo timia lisio kuwa hili".

Imepokewa pia na Imaam Bukhariy, kwamba Abu Bakr(ra) amesema, "Nilimwambia Mtume(saw) nilipo kuwa pangoni, lau mmoja wao ataangalia chini ya miguu yake basi atatuona". Akasema, "Nini dhana yako kwa watu wawili ewe Abu Bakr akiwa Mwenyezi Mungu ndiye wa tatu wao!"

Mwaka wa kwanza baada ya Kuhama:

Matukio muhimu:

- Mtume(saw) ajenga msikiti wa Madina.
- Adhana yaanza kwa ndoto ya kweli ya Sahaba Abdullah bin Zayd Al-Ansary.

- Mtume(saw) aandikiana ahadi (mkataba wa amani) na Mayahudi.
- Waislamu wapewa ruhusa na Mwenyezi Mungu ya kupigana vita na makafiri.
- Sahaba Abdullah bin Zubayr azaliwa naye ni mwislamu wa kwanza kuzaliwa baada ya kuhama.

Mwaka wa pili baada ya Kuhama:

- Kuhawilishwa (kugeuzwa) kibla kuelekea Ka'aba badala ya Baytil-Muqaddas.
- Vita vikubwa kabisa katika Uislamu, vita vya Badr ambapo Waislamu walipata ushindi mkubwa.
- Sahaba Uthman bin Madh-un afariki, naye ni muhajirina wa kwanza kufariki Madina, na azikwa Baqii.
- Binti wa Mtume(saw), Sayyidatna Ruqayya afariki.
- Mayahudi wa Baniy Qaynuqai walivunja heshima ya mama wa kiislamu na kuvunja mkataba, na kuzuka Vita vya Baniy Qaynuqai. Waislamu walishinda vita hivi na Mayahudi hawa wakafukuzwa Madina.
- Sayyidna Ali amwoa Sayyidatna Fatima. Sayyidna Ali alikuwa na miaka 21 wakati huo na Sayyidatna Fatima miaka 15.
- Mtume(saw) aingia nyumbani kwa Sayyidatna Aisha.

Mwaka wa tatu baada ya kuhama:

- Vita vya Uhud, ambavyo ndani yake Waislamu walipata mtihani mkubwa kwa kukhalifu kwao amri ya Mtume(saw). Sayyidna Hamza aliuawa katika vita hivi.

- Mtume(saw) amwoza binti yake wa pili Sayyidatna Ummu Kulthum kwa Sayyidna Uthman bin Affan.
- Pombe yaharamishwa na Qur'ani.
- Mtume(saw) amwoa Bi. Zaynab bint Khuzaymah.

Mwaka wa nne baada ya kuhama:

- Mayahudi wa Bani Nadhiir walivunja mkataba kwa kutaka kumwua Mtume(saw). Vikapiganwa vita vya Bani Nadhiir ambao ni kabila la pili la Mayahudi. Wakazingirwa siku sita huku wakiwa kwenye ngome zao, kisha wakaomba waachiwe waondoke na kila kinachoweza kuchukuliwa na ngamia wao. Wakahamia Khaybar na wengine wakaenda Sham.
- Kufariki kwa Sayyidatna Zaynab bint Khuzaymah, mkewe Mtume(saw).
- Kufariki kwa Abu Salamah na Mtume(saw) kumwoa Sayyidatna Ummu Salamah kwa wasita wa Najashi, mfalme wa Uhabeshi.

Mwaka wa tano baada ya kuhama:

- Vita vya Baniy Mustaliq, ambapo Mtume(saw) alimwoa Sayyidatna Juwayriya, mmoja wa mateka na ikawa ndio sababu ya kuwachwa huru watu wake wote na kusilimu kwao.
- Vita vya Ahzaab (Khandaq) na kushinda kwa Waislamu baada ya khofu kubwa iliyowajaa.
- Mayahudi wa Baniy Quraydha walivunja mkataba na kuazimia kuwafungulia njia Makureshi wakati wa vita vya Ahzaab.
- Vita vya Baniy Quraydha ambapo waliuawa Mayahudi wanaume watu wazima; wanawake na watoto wakachukuliwa mateka.

- Kufariki kwa Sayyidna Sa’ad bin Muadh mkubwa wa Aws, bali mkubwa wa Ansaar.

Mwaka wa sita baada ya kuhama:

- Sulhu ya Hudaybiyya, Mtume(saw) kuelekea Makka kufanya Umra na baadaye ikaishia kwenye sulhu na Makureshi.
- Mtume(saw) awaandikia wafalme akiwalingania Uislamu.

Mwaka wa saba baada ya kuhama:

- Vita vya Khaybar, sehemu ya mwisho walipokuweko Mayahudi Madina. Hivi vilikuwa vita vikubwa na Waislamu walivunja ngome za Mayahudi.
- Waislamu wafanya Umra kwa mujibu wa sulhu ya Hudaybiya.
- Mtume(saw) amwoa Bibi Safiyya, Bibi Maymuna na Bibi Ummu Habiba.
- Waliohama kwenda Habasha warudi Madina wakiongozwa na Sayyidna Ja’afar bin Abi Talib.

Mwaka wa nane baada ya kuhama:

- Vita vya Mu-ta ambamo aliuawa Sayyidna Zayd bin Harith, Sayyidna Ja’afar bin Abi Talib na Sayyidna Abdullah bin Rawaaha, ambao walishika bendera ya Mtume(saw), na hatimaye jeshi kuongozwa na Sayyidna Khalid bin Waliid aliye shindisha vita hivyo.
- Kufunguliwa Makka na kuwa chini ya Waislamu.
- Vita vya Hunain na Twaif ambavyo vyote walishinda Waislamu.

- Kufariki mtoto mkubwa wa Mtume(saw), Sayyidatna Zainab.

Mwaka wa tisa baada ya kuhama:

- Vita vya Tabuuk.
- Kisa cha masahaba watatu waliobaki nyuma (wasiende) katika vita, na hatimaye wakasamehewa kwa ajili ya ukweli wao.
- Kuvunjwa kwa msikiti wa wanafiki.
- Sayyidna Abubakr(ra) awaongoza Waislamu kwenye Hijja.
- Kufariki kwa Sayyidatna Ummu Kulthum bint wa Mtume(saw).

Mwaka wa kumi baada ya kuhama:

- Hijja ya kuaga, nayo ni Hijja ambayo Mtume(saw) aliwaaga Waislamu na kuwapa mafundisho muhimu ya dini.
- Kuja makundi kwa makundi kwa Mtume(saw) kusilimu.
- Kufariki kwa Sayyidna Ibrahim mtoto wa Mtume(saw).

Mwaka wa kumi na moja baada ya kuhama:

- Kuumwa kwa Mtume(saw), na Sayyidna Abubakar(ra) kuongoza swala.
- Kufariki kwa Mtume(saw).

Kufariki kwa Mtume(saw):

Mtume(saw) alianza kwa kuumwa kichwa naye akiwa kwa Sayyidatna Aisha(ra), kisha hali yake ikazidi kuwa mbaya alipo kuwa kwa Sayyidatna Maymuna(ra), akawaomba wake zake augulie kwa

Sayyidatna Aisha(ra), nao wakakubali. Na tangu kuumwa kwake hadi kufariki ni siku 12.

Imepokewa pia kuwa Mtume(saw) aliwatokea maswahaba siku moja alipokuwa anajisikia hali yake afadhali, kichwa chake kikiwa kimefungwa kitambaa akimwegemea Sayyidna Abbas(ra) na Sayyidna Aliy(ra), hadi wakamfikisha kwenye mimbari. Mtume(saw) akamuhimidi Mwenyezi Mungu kisha akasema, "Hakika mja amepewa khiyari achague Dunia au Aliyonayo Mwenyezi Mungu, akachagua Aliyonayo Allah". Masahaba wote wasifahamu maana ya maneno hayo, ila Sayyidna Abubakr. Yeye akaelewa kuwa ajali ya Mtume(saw) imeshakaribia; akalia na kusema, "Tunakufidia kwa nafsi zetu na watoto wetu". Mtume(saw) akasema, "Fungeni milango yote (inayoingia msikitini) ila mlango wa Abubakar(ra), Wallahi ningekuwa mwenye kuchagua rafiki basi ningali mchagua Abubakar(ra)".

Imepokewa kuwa Sayyidna Abubakar(ra) aliswalisha swala kumi na saba. Katika riwaya nyingine aliswalisha swala siku tatu. Na Mtume(saw) ndiye aliyeamrisha aswalishe Sayyidna Abubakar(ra).

Imepokewa pia na Maimamu Bukhariy na Muslim, kwamba Mtume(saw) alipokuwa kwenye maradhi yake, siku ya Jumatatu, wakiwa Waislamu wanaswalishwa na Sayyidna Abubakar(ra), akainua pazia na kuwaangalia huku uso wake uking'ara kama fedha, akatabasamu. Masahaba wakakaribia kufitinika wakaharibu swala kwa furaha ya kumwona Mtume(saw). Hata Sayyidna Abubakar(ra) akataka kurudi nyuma ili amwachie Mtume(saw) aswalishe, Mtume(saw) akaashiria watimize swala yao, akaingia chumbani kwake na ndio siku aliyofariki.

Imepokewa pia katika Bukhariy na Muslim, kwamba Mtume(saw) alikuwa akiomba dua ya kupata afya akiwa mgonjwa:

أذهب البأس رب الناس اشف وأنت الشافي لا شفاء إلا شفاؤك شفاء لا يغادر سقما

"Ondosha ubaya (maradhi) ewe Mola Mlezi wa watu! Ponya nawe ndiwe Mponyaji, hapana ponyo ila ponyo lako, ponyo lisilo bakisha ugonjwa".

Akasema Sayyidatna Aisha, alipokuwa katika maradhi yake ya kufa: Nikawa napangusa mikono yake na kusoma dua hiyo, akaondoa mikono yangu na kusema:

رب أغفر لي وألحقني بالرفيق الأعلى

“Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe na nikutanishe na rafiki wa juu”. Yakawa ndio maneno ya mwisho niliyo yasikia kutoka kinywani mwake.

Na katika riwaya nyingine aliyoipokea Imamu Ahmad, anasema Sayyidatna Aisha, Alipo kuwa Mtume(saw) katika pumzi zake za mwisho, aliingia Abdul-Rahman bin Abubakr akiwa na mswaki. Mtume(saw) akamwangalia, nikaelewa kuwa anautaka, nikauchukua, nikautafuna kuulainisha, kisha nikampa, akapiga mswaki vizuri, kama ambavyo alikuwa akipiga. Kisha akanyanyua kichwa kutaka kunirudishia, ukaanguka kutoka mkononi mwake. Kisha nikamwomba Mwenyezi Mungu kwa dua aliyofundishwa Mtume(saw) na Jibril, na ambayo alikuwa akiiomba katika maradhi yake, lakini kwenye maradhi haya hakuiomba. Akainua macho yake mbinguni na kusema, “(Naenda kwa) Rafiki wa Juu, Rafiki wa Juu!” Na ikatoka roho yake, basi namshukuru Mwenyezi Mungu aliyekutanisha mate yangu na mate yake katika siku yake ya mwisho ya Dunia.

Kupigwa na butwaa kwa masahaba kwa kufariki Mtume(saw) na khutba ya Sayyidna AbuBakr:

Alipofariki Mtume(saw), masahaba walipigwa na butwaa, wasijue la kufanya, ama Sayyidna Uthman(ra) akawa bubu asiweze kutamka, Sayyidna Aliy(ra) akakaa chini asiweze kuinuka. Sahaba Abdullah bin Unays(ra) akafariki kwa huzuni, Sayyidna Umar(ra) alichanganyikiwa na kupiga mayowe na kusema kuwa Mtume(saw) hajafariki. Na wakati huo Sayyidna Abubakar(ra) alikuwa nje ya mji, aliporudi, akapewa khabari. Yeye hakumsemesha mtu, akaingia ndani na kumbusu Mtume(saw) na kulia na kusema, “Wallahi Mwenyezi Mungu hatokukusanyia vifo viwili”. Akatoka na kuingia msikitini, akajaribu

kumnyamazisha Sayyidna Umar(ra), isiwezekane, akasimama juu ya mimbari na kutoa khutba yake maarufu akasema: Mwenye kumuabudu Muhammad, basi Muhammad kesha kufa, na mwenye kumuabudu Allah, basi yeye yuko hai milele. Kisha akasoma aya, **"Na hakuwa Muhammad ila Mtume, ametanguliwa na mitume wengine, basi akifariki au akauawa, mutarudi nyuma kwa visigino vyenu ..."** hadi mwisho wa aya. Sayyidna Umar(ra) akasema: Nikahisi kama sijawahi kuisoma aya hiyo ila siku hiyo na masahaba wengine pia walikuwa wameisahau aya hiyo, wakaisikia kwa Sayyidna Abubakar(ra), akawa kila mtu anaisoma. Sayyidna Umar(ra) anasema, "Wallahi nilipoisikia aya hii nikajua kuwa ni haki nikaishiwa nguvu, hata miguu yangu isiweze kuninyanyua".

Mtume(saw) alishushiwa wahyi akiwa na umri wa miaka arobaini, akakaa Makka miaka kumi na tatu na Madina miaka kumi. Amefariki akiwa na umri wa miaka 63.

Kuoshwa kwa Mtume(saw) na kuzikwa kwake:

Mtume(saw) alioshwa na Sayyidna Aliy, akisaidiwa na Sayyidna Abbas ammi yake, pamoja na mabwana Saleh (ambaye ndiye aliye kuwa anaitwa Shaqaraan); huru wa Mtume(saw), Usama bin Zayd, Quthm na Fadhl watoto wa Sayyidna Abbas. Baada ya kukoshwa na kukafiniwa, wakaingia watu kumswalia bila ya Imamu. Masahaba walitofautiana wapi wamzike Mtume(saw). Mzozo ulikwisha Sayyidina Abubakar(ra) alipoinukuu Hadithi ya Mtume kuwa, "Nabii yeyote akifariki huzikwa pale pale alipofia." (Ahmad, Tirmidhiy) Hivyo, akazikwa chini ya kitanda chake.

Tabia njema za Mtume(saw):

Imepokewa kwamba Mtume(saw) alikuwa mbora wa watu wote kwa tabia, hasemi maneno machafu, na wala akifanyiwa maovu halipi kwa maovu, bali husamehe. Amesema Anas: Nimemtumikia Mtume(saw) miaka kumi, hakuniambia ha! hata mara moja, au kwa nini nimefanya

kitu fulani, wala kwa nini sikufanya kitu fulani. Imepokewa na Bukhariy.

Mifano ya Unyenyekevu wake:

Amesema Anas, alikuwa anakuja kijakazi katika watu wa Madina, huchukua mkono wa Mtume(saw) na kwenda naye ili Mtume(saw) amkidhie haja zake. (Bukhariy).

Alipoulizwa Sayyidatna Aisha(ra) juu ya matendo ya Mtume(saw) akiwa nyumbani, akasema huwasaidia watu wake kazi za nyumbani, ukiingia muda wa swala hutoka kwa ajili ya kuswali. (Bukhariy).

Amesema Sayyidina Anas bin Maalik(ra) kuwa alikuwa Mtume(saw) akitembelea wagonjwa, akihudhuria janaza, akijibu wito wa wafalme, na akipanda punda. Hakika nilimwona siku moja amepanda punda, na hatamu yake ni usumba (aina fulani ya nyuzi nyuzi).

Alitajwa Mtume(saw) mbele ya Al-Hasan, naye akasema, "Hapana, wallahi haikuwa milango yake ikifungwa, na wala hakuna bawaba baina yake, na wala hakuwa akila kwenye sinia kubwa, na alikuwa akitoka mbele ya watu. Mwenye kutaka kuonana na Nabii wa Mwenyezi Mungu huonana naye; na alikuwa akikaa juu ya ardhi na chakula chake huwekwa juu ya ardhi. Akivaa nguo nzito, akipanda punda, akimsaidia mtumwa wake, na humsafisha mnyama wake kwa mkono wake mtukufu(saw).

Mfano wa Huruma yake:

Imepokewa na Sayyidina Anas(ra), kwamba Mtume(saw) amesema, "Hakika naingia kwenye swala nikiwa na nia ya kuirefusha, nikisikia mtoto analia, huifupisha kwa kufahamu huzuni ya yule mama kwa kulia mtoto wake". (Bukhariy na Muslim).

Mifano ya Kusamehe kwake:

Imepokewa na Sayyidina Anas bin Malik(ra), "Nilikuwa nikitembea na Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu-Rehema na Amani zimshukie-akiwa amevaa shali la Najran lenye pembe zenye kuning'inia, akaja mtu wa mashamba, akaivuta shali yake kwa nguvu sana, hata nikaona shingo ya Mtume(saw) imeathirika kwa kubanwa kwake na ile shali. Kisha akamwambia, 'Ewe Muhammad! Nipe mali ya Mwenyezi Mungu iliyo kwako. Mtume(saw) akageuka, akamwangalia kisha akatabasamu, na akaamrisha apewe chochote. (Bukhariy na Muslim)

Sayyidatna Aisha, amesema, "Hakuwahi Mtume(saw) kumpiga mtumishi hata mara moja, wala hakuwahi kumpiga mwanamke hata mara moja, na wala hakuwahi kumpiga mtu kwa mkono wake ila katika vita vya jihadi. Na wala hakufanyiwa uovu akaulipa kwa aliyemfanyia, ila ikivukwa mipaka ya Mwenyezi Mungu, hapo hutekeleza adhabu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na wala hakujiwa na moja ya mambo mawili ila huchagua lililokuwa na wepesi maadam si madhambi, na ikiwa ni dhambi, huwa yeye ni mbali zaidi kuliko watu wengine". (Bukhariy na Muslim).

Mifano ya Ukarimu wake:

Imepokewa kutoka kwa Sahaba Ibn Abbas(ra), "Alikuwa Mtume(saw) mkarimu sana, na alikuwa mkarimu zaidi katika mwezi wa Ramadhani. (Bukhariy na Muslim).

Imepokewa na Sahaba Anas(ra), kwamba, "Hakuwa Mtume(saw) akiombwa kitu kwa ajili ya Uislamu ila hutoa. Akimjia mtu kumwomba, humjazia mbuzi wa sadaka baina ya majabali mawili; yule mtu akarudi kwa watu wake huku akisema, 'Enyi watu ingieni kwenye Uislamu, kwani Muhammad anatoa kiasi kikubwa, utoaji wa mtu asiyeogopa ufakiri". (Muslim).

Mifano ya Ushujaa wake:

Amesema Sayyidina Anas(ra), “Alikuwa Mtume(saw) mbora wa watu na shujaa zaidi kuliko watu wote, na mkarimu zaidi kuliko watu wote. Ilisikika mara moja sauti kubwa ya kuogofya Madina, wakatoka watu wapate kujua ile sauti imetokana na nini, wakakutana na Mtume(saw) akiwa ameshawatangulia, naye anarudi akiwa amempanda farasi wa Abi Twalha, bila ya tandiko, na shingoni kwake kuna upanga. Akawaambia, ‘Musiogope’..... (Bukhariy na Muslim).

Aliulizwa Sahaba Al-Baraa (ra): Mulimkimbia Mtume(saw) siku ya Hunain? Al-Baraa akajibu, “Lakini Mtume(saw) hakukimbia, walikuwa Hawaazin mahodari wa mishale, na sisi tulipowafikia walikimbia. Basi tukakimbilia kukusanya ngawira, wakatukabili na mishale. Hakika nilimwona Mtume(saw) amesimama imara juu ya nyumbu wake mweupe, na Abu Sufyan bin Al-Harith amekamata kamba yake, naye (Mtume(saw)) akisema:

أنا النبي لا كذب أنا ابن عبدالمطلب

Mimi ni Nabii khasa, si uwongo

Mimi ndiye mwana wa Abdul-Mutwalib

(Bukhariy na Muslim).

Mifano ya Ibada za Mtume(saw) na jitihada zake:

Bwana Alqama alimwuliza Sayyidatna Aisha(ra), “Je, Mtume(saw) alikuwa akiyakhusisha baadhi ya masiku (kwa kufanya ibada zaidi)?” Akajibu, “Hapana, alikuwa akidumu juu ya amali. Na nani kati yenu anaweza kufanya aliyokuwa akiyafanya Mtume(saw)? (Bukhariy na Muslim).

Aliulizwa Sahaba Anas bin Malik(ra) kuhusiana na swala ya Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) wakati wa usiku, akasema, “Hatukuwa tukitamani tumwone akiswali usiku ila tulimwona akiswali, na tukitamani tumwone amelala ila tulimwona amelala. Na alikuwa

akifunga ndani ya mwezi hadi tunasema kuwa hatofuturu". (Bukhariy na Muslim)

Amesimulia Sayyidina Abdillah bin Mas-ud(ra), "Niliswali mara moja na Mtume(saw) usiku mmoja, basi hakuacha kusimama (akisoma) hadi nikaazimia kitu kibaya. Tulimwuliza uliazimia kitu gani? Akasema niliazimia nikae chini na nimwache aendelee (peke yake). (Bukhariy na Muslim)

Amesimulia Sayyidatna Aisha(ra), "Alikuwa Mtume(saw) akiswali, husimama hadi miguu yake inavimba". Nikamwambia, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa nini unafanya hivi, wakati umeshasamehewa madhambi yako yote - yaliyotangulia na yatakayokuja baadaye?" Akasema: "Ewe Aisha! Basi nisiwe hata mja mwenye kushukuru?" (Bukhariy na Muslim)

Mifano katika maisha yake na hali ya uduni aliyokuwa nayo:

Bwana Abi Hazim(ra), alisema, "Nilimwona Abu Hurayrah mara nyingi akiashiria kwa kidole chake cha shahada akisema, 'Naapa kwa ambaye nafsi ya Abi Hurayrah iko mkononi mwake, hakushiba Mtume(saw) mkate wa ngano siku tatu mfululizo hadi ameondoka duniani'". (Bukhariy na Muslim)

Amesimulia Abi Hurayrah(ra) kwamba alipita kwa watu ambao mbele yao kuna mbuzi aliyechomwa, wakamwita akakataa kula, akasema: "Ametoka Mtume wa Mwenyezi Mungu duniani wala hakuwahi kushiba kwa mkate wa shayiri". (Bukhariy)

Imepokewa na Bwana Urwa, kwamba alimsikia Sayyidatna Aisha(ra) akisema, "Ulikuwa unapita kwetu mwezi na mwezi mwengine, na hakuna moto unaowashwa (kwa ajili ya kupika) kwenye nyumba yoyote ya Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw)? Nikamuuliza, 'Ewe mama mdogo, mulikuwa mukiishi vipi?' Akasema, 'Juu ya vyeusi viwili: tende na maji'". (Ahmad)

Imepokewa na Sahaba Ibn Abbas(ra), amesema: Alifariki Mtume(saw) na nguo yake ya vita ikiwa imewekwa rahani kwa Yahudi kwa ajili ya

pishi thelathini za shayiri, alizozichukua kama nafaka kwa ajili ya watu wake wa nyumbani". (Ahmad)

Imepokewa na Sayyidina Anas bin Malik(ra), kwamba "alikuja Bibi Fatima(ra) na kipande cha mkate kwa Mtume(saw), akamuuliza 'Ni kipande gani hiki'? Akasema, 'Kipande cha mkate nilioutengeneza, sikuweza kuula bila ya kuja nao kwako'. Mtume(saw) akasema, 'Ama hiki kipande cha mkate ni chakula cha mwanzo kimeingia kinywani mwa baba yako tangu siku tatu'". (Ahmad)

Miujiza yake:

Miujiza ya Mtume(saw) ni mingi mno, na hapa tutataja baadhi tu, muujiza mkubwa kabisa ni Qur-ani ambao wakikusanyika watu wote hawatoweza kuleta mfano wa sura ndogo kabisa.

Miujiza mwingine ni kupasuka kwa mwezi vipande viwili kama ilivyo pokewa katika hadithi sahihi.

Miujiza mwingine ni kutoka maji kwenye vidole vyake wakatumia maji yale kutawadhia waliokaribia watu mia tatu. (Bukhariy na Muslim) Miujiza hii pamoja na miujiza ya kuongezeka chakula imetokea zaidi ya mara moja.

Miujiza mwengine ni kunyesha mvua kwa dua yake Mtume(saw), wakati hakukuwa hata na kiwingu kimoja, ikanyesha mvua kwa wiki nzima hadi wakaomba ipungue mjini na iende kwenye mashamba.

Utukufu wake juu ya manabii wengine:

Imepokewa na Sahab Jabir bin Abdillah, kwamba Mtume(saw) amesema, "Nimepewa vitu vitano na hakupewa mtu kabla yangu, nimenusuriwa kwa khofu kwa mwendo wa mwezi mmoja, na nimejaaliwa ardhi yote kuwa ni msikiti na ni safi, basi yeyote itakayemkuta swala popote basi aswali. Nimehalalishiwa ngawira na haikuhalalishwa kwa yeyote kabla yangu, na nimepewa shafaa (daraja ya kuwaombea watu siku ya Kiyama). Na walikuwa Mitume

wakipelekwa kwa watu makhsusi nami nimetumwa kwa watu wote”. (Bukhariy na Muslim)

Imepokewa na Sahaba Anas(ra), amesema Mtume(saw), “Nitaujia Mlango wa Pepo (siku ya Kiyama), na kuomba kuingia. Atauliza mlinzi, ‘Nani wewe?’ Nitajibu, ‘Muhammad’. Atasema, ‘Nimeambiwa nikufungulie na nisimfungulie yeyote kabla yako’”. (Muslim)

Imepokewa na Sayyidina Anas, kwamba Mtume(saw) amesema, “Mimi ni wa mwanzo kutoka ndani ya tumbo la ardhi watakapofufuliwa watu, na mimi ndio khatibu (msemaji) wao watakapokusanyika. Na mimi ndio mwenye kuwabashiria (kuwapa matumaini) wakikata tamaa, bendera yenye kushukuriwa ***(liwaaul-hamd)*** itakuwa mkononi mwangu, na mimi ni mbora wa watoto wa Adam mbele ya Mwenyezi Mungu na wala si fakhari”. (Tirmidhiy)

Imepokewa pia na Sayyidina Anas(ra), kwamba Mtume(saw) amesema, “Mimi ni mtu wa mwanzo kuwaombea wengine siku ya Kiyama, na mimi ndiye mwenye wafuasi wengi zaidi kuliko manabii wengine, na mimi ni wa mwanzo kupiga hodi mlango wa Peponi”. (Muslim)

Imepokewa na Sahaba Jabir bin Abdillah(ra), kwamba Sayyidna Umar bin Khataab(ra) alimjia Mtume(saw) na kitabu cha Mayahudi, akamsomea Mtume(saw). Mtume(saw) akakasirika na kusema: “Je, tunajiingiza kwenye mambo haya ewe Ibnul-Khattaab? Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, hakika nimekujilieni na (dini) iliyo nyeupee safi kabisa. Musiwaulize (Ahlil-kitaab) wakakuambieni kwa lililo haki mukawakadhibisha au wakakwambieni kitu ambacho si sawa mukawasadikisha. Namwapia ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, lau Musa angekuwa hai, asingeweza lolote ila kunifuata”. (Ahmad)

Imepokewa kutoka kwa Sahaba Abu Hurayrah amesema, Amesema Abul Qasim [yaani Mtume(saw)] “Mfano wangu na mfano wa manabii kabla yangu, ni mfano wa mtu aliyejenga nyumba nzuri sana, akaikamilisha na kuipamba vizuri ila sehemu ya tofali moja katika mojawapo ya pembe (kona) zake. Wakawa watu wanaizunguka na wanapendezewa sana na lile jengo, wakawa wanasema lau ingewekewa

tofali moja kwenye sehemu hii lingetimia jengo lake. Akasema Muhammad(saw), “Basi mimi ndio lile tofali”. (Bukhariy na Muslim)

Mapenzi ya Mtume(saw):

Kumpenda Mtume(saw) ni katika Imani:
Imepokewa na Imaam Bukhariy kwamba Mtume(saw) amesema: “Hatoamini mmoja wenu mpaka niwe mimi ni mpenzi zaidi kwake kuliko mtoto wake, mzazi wake, mali yake na watu wote”. Na katika riwaya ya Imaam Ahmad imeongezeka “kuliko nafsi yake”.

Mwenye Kumpenda Mtume(saw) ataonja ladha ya Imani:
Mtume(saw) amesema: “Mambo matatu mwenye kuwa nayo ataonja ladha ya imani: awe Allah na Mtume wake ni wapenzi zaidi kwake kuliko asiyekuwa wao, ampende mtu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, na achukie kurudi kwenye kufuru baada ya kuokolewa na Mwenyezi Mungu kama anavyo chukia kutupwa motoni”. (Bukhariy na Muslim)

Kumpenda Mtume(saw) ni wajib:
Imepokewa na Imaam Al-Hakim kuwa Mtume(saw) amesema: “Mpendeni Mwenyezi Mungu kwa neema zake anazokuneemesheni na nipendeni mimi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na wapendeni Ahli bayti wangu kwa ajili yangu”. Na katika riwaya nyengine iliyo pokewa na Imaam Tirmidhiy: “Nipendeni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ananipenda”.

Kumpenda Mtume(saw) kutasababisha kuwa naye siku ya Kiyama:
Imepokewa na maimamu Bukhariy na Muslim kwamba alikuja mtu kwa Mtume(saw) akasema, “Unaonaje kama mtu anawapenda watu fulani lakini hajafanya amali kama za kwao?”. Akajibu Mtume(saw), “Mtu atakuwa na anayempenda”. Na katika riwaya nyengine: “Atakuwa na anayempenda siku ya kiyama”.

Imepokewa pia na maimamu Bukhariy na Muslim kutoka kwa Sahaba Anas kwamba alikuja mtu akamwuliza Mtume(saw), “Lini Kiyama?” Akamjibu, “Na umekiandalia nini?” Akasema, “Sina kitu ila nampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake”. Na katika riwaya nyengine: Sijakiandalia wingi wa swala au funga ila nampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Akasema Mtume(saw): “Wewe utakuwa na unayempenda”. Akasema Sayyidina Anas(ra): Hawakufurahi masahaba wa Mtume(saw) kwa kitu baada ya Uislamu kama walivyofurahi kwa maneno haya (utakuwa na unayempenda). Akasema Anas: Na mimi nampenda Mtume(saw) na Abubakr na Umar na nategemea kuwa nao ijapo kuwa sijafanya amali kama za kwao. Na katika riwaya nyengine iliyopokewa na Imamu Ahmad, amesema Sayyidina Anas(ra), Na sisi tunampenda Mtume(saw) na hatuna uwezo wa kufanya amali kama za kwake, na tukiwa naye hilo linatutosha (hatutamani jengine tena).

Imepokewa na Imaam Tabraaniy kuwa Bi. Aisha amesema, “Alikuja mtu kwa Mtume(saw) akasema, ‘Hakika mimi nakupenda kuliko nafsi yangu, na kuliko familia yangu, na ninapokuwa nyumbani ninapokukumbuka huwa siwezi kujizuia mpaka nije nikuone. Na nikikumbuka kufa kwako na kufa kwangu naelewa kuwa ukiingia Peponi utanyanyuliwa na Mitume (wengine) na nikiingia Peponi nakhofia kuwa sitokuona’”. Mtume(saw) hakumjibu kitu mpaka ikashuka Aya ifuatayo:

وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ فَأُوْلَٰٓئِكَ مَعَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِم مِّنَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ وَٱلصِّدِّيقِينَ وَٱلشُّهَدَآءِ وَٱلصَّٰلِحِينَۚ وَحَسُنَ أُوْلَٰٓئِكَ رَفِيقٗا

“Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume(saw) basi watakuwa pamoja na walioneemeshwa miongoni mwa manabii ...” (Nisaa:69)

Mapenzi ya Mtume(saw) juu ya Waislamu:
Katika hadithi iliyopokewa na Imaam Muslim, Mtume(saw) alitaja maneno ya Nabii Ibrahim, "ewe Mola hakika wao (masanamu) wamepotosha watu wengi sana, basi na mwenye kunifuata yuko na mimi, mwenye kuniasi basi wewe ni mwenye kusamehe mno na mwenye rehema nyingi"; Na neno la Nabii Isa, "ukiwaadhibu basi wao ni waja wako". Kisha akanyanyua mikono na kusema: "Umati wangu! Umati wangu!" na akalia. Mwenyezi Mungu akamwambia Jibriil nenda kwa Muhammad, na Mwenyezi Mungu ni mwenye kujua zaidi muulize nini kinakuliza, Jibriil akamwuliza, naye Mtume(saw) akampa khabari aliyoyasema, na Yeye anajua zaidi, Mwenyezi Mungu Akamwambia, "Ewe Jibriil nenda kwa Muhammad, umwambie hakika sisi tutakuridhisha katika umati wako wala hatutokuonyesha ubaya kwao".

Mapenzi ya Mtume(saw) juu ya watakao kuja baada yake na kumuamini:
Imepokewa na Abu Shaikh na kutajwa kwenye *Kanzul-Ummaal* kwamba Mtume(saw) alisema, "Lini nitakutana na wapenzi wangu". Wakauliza masahaba, "Je, sisi sio wapenzi wako?" Akajibu, "Nyie ni masahaba wangu, wapenzi wangu ni watu ambao hawajaniona na wakaniamini, nina shauku kubwa ya kukutana nao".

Kumpenda Mtume(saw) ni kufuata aliyokuja nayo:
Amesema Mwenyezi Mungu:

قُلۡ إِن كُنتُمۡ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِي يُحۡبِبۡكُمُ ٱللَّهُ

"**sema ikiwa munampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni, atakupendeni Mwenyezi Mungu**". (Aali Imran:30)
Na kama tulivyo sema kumpenda Mtume ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kumwona Mtume(saw) usingizini:
Imepokewa na Imaam Bukhariy Mtume(saw) amesema: "Zitakujieni zama ambazo mmoja wenu atatamani kuniona kuliko kuwa na mfano wa ahli yake na mali yake". Na katika riwaya nyengine iliyo pokewa na maimamu Muslim na Ahmad, "Mwenye mapenzi zaidi juu yangu katika umati wangu ni watu watakao kuja baada yangu, atatamani mmoja wao apoteze ahli yake na mali yake ili apate kuniona".

Imepokewa na maimamu Bukhariy na Muslim kwamba Mtume(saw) amesema: "Mwenye kuniona usingizini, (huyo) ameniona kweli kwani shetani hawezi kujishabihisha na mimi".

Kutukuzwa kwake na masahaba wake na mapenzi yao juu yake:

Sayyidina Anas(ra) amesema, "Nilimwona Mtume(saw) akinyolewa na kinyozi, naye amezungukwa na masahaba wake, hawataki unywele wake uanguke ila kwenye mkono wa mtu". (Muslim)

Na imepokewa na maimamu Bukhariy na Muslim, katika hadithi ya Abi Juhayfah(ra) kwamba amesema: Nilikuja kwa Mtume(saw), akatokea Bilaal na maji yake ya udhu, nikaona watu wanayafuatilia yanayodondoka kwenye udhu wake, akipata kitu mtu hujipangusa nacho, na ambaye hajapata huchukua unyevu wa mwenzake. Wakasimama watu wakichukua mkono wake na wanajipangusia nyuso zao, nikachukua mkono wake nikaweka juu ya uso wangu, kutahamaki ni baridi kuliko barafu na una harufu nzuri zaidi kuliko udi wa misk".

Ameelezea Sayyidina Anas(ra), kwamba ilipokuwa siku ya vita vya Uhud, watu walivumisha uvumi na wakasema Mtume(saw) ameuawa; yakawa mengi makelele katika pande za Madina. Akatoka mwanamke mmoja wa Kianswari akakutana na (maiti ya) kaka yake, baba yake na mume wake, sijui alikutana na nani kwanza. Basi alipompitia wa

mwisho wao, akauliza, “Huyu ni nani?” Wakamjibu: Huyu ni kaka yako, baba yako, mume wako na mwanao. Akauliza, “Mtume(saw) ana hali gani? Wakamwambia, “Huyo mbele yako.” Akaenda mpaka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw), akaishika ncha ya nguo yake, kisha akawa anasema, “Nakufidia baba na mama yangu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi sijali (msiba wowote) ikiwa wewe umesalimika na hilaki. (*Sifat Safwa*)

Kufikishwa kwake salamu za umma wake:

Imepokewa na Sayyidina Abdillah bin Mas-ud(ra), Mtume(saw) amesema, “Hakika Mwenyezi Mungu ana malaika watembeao ardhini wananifikishia salamu kutoka kwa umati wangu”. (Imaam Ahmad)

Wakeze Mtume(saw)- Mamama wa Waislamu:

Mama Khadija bint Khuwaylid(ra).

Mtume(saw) alimwoa alipokuwa na miaka 25 na Bibi Khadija akiwa na miaka 40. Bibi huyu aliwahi kuolewa na watu wawili kabla ya kuolewa na Bwana Mtume(saw). Watu wenyewe ni Abi Halah bin Zuraara Atamiymiy na Atiiq bin Aidh. Mama huyu alijitolea kwa mali yake yote kwa ajili ya Mtume(saw) na alikuwa wa kwanza kusilimu kwa ijmai ya wanachuoni wa Tarikh. Watoto wa Mtume(saw) wote walitokana na yeye ila Ibrahim. Mtume(saw) aliishi naye miaka 25. Mwaka aliofariki Sayyidatna Khadija(ra) ndio mwaka aliofariki Abi Talib. Ndiyo maana mwaka huu ukaitwa mwaka wa Huzuni, kwani Mtume(saw) aliwapoteza watu wawili waliomsaidia sana kufikisha Ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Huu ulikuwa mwaka wa kumi tangu kupewa Utume. Mtume(saw) hakumwoa mwanamke yeyote katika uhai wa Sayyidatna Khadija; wake wote aliowaoa ilikuwa ni baada ya kufariki Bibi huyu. Sayyidatna Khadija alitumiwa salamu na Mwenyezi Mungu kwa wasita (njia) wa Jibriil, ama Sayyidatna Aisha alipewa salamu na Jibriil mwenyewe.

Imepokewa kwamba Mtume(saw) aliletewa zawadi ya nyama ya ngamia aliyekwishapikwa, akachukua mfupa na kutaka kutafuna kisha akaurudisha na kusema, “Nenda mpelekee fulani”. Akauliza Sayyidatna Aisha, “Mbona umerudisha mkono wako (umeacha kula)? Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu, “Hakika Khadija aliniusia kumfanyia wema”. Sayyidatna Aisha akaona wivu na kusema, “Kama vile hakuna mwanamke yeyote duniani ila Khadija”. Mtume(saw) akakasirika sana na kunyanyuka, akawa mbali kiasi anachotaka Mwenyezi Mungu, kisha akarudi. Akatokea Bibi Ummu Ruman (mama yake Sayyidatna Aisha), akauliza, “Una nini na Aisha, hakika yeye ni mdogo, na wewe ni mbora wa kusamehe.” Mtume(saw) akashika sehemu ya shavu la Bibi Aisha (iliyo karibu na mdomo) na kusema, “Wewe si ndio umesema kama vile hakuna mwanamke duniani ila Khadija, wallahi aliniamini walipokataa kuniamini watu wako. Na nimepewa watoto kupitia kwake, na mukanyimwa nyie."

Maimamu Bukhari na Muslim wamepokea maneno yafuatayo kutoka kwa Mama Aisha, “Sikuwa na wivu juu ya wakeze Mtume(saw) zaidi ya wivu wangu juu ya Khadija. Sikuwahi kumwona lakini Mtume(saw) alikuwa akimtaja sana. Huenda akachinja mbuzi na kuwapelekea marafiki wa Khadija, na huenda nikasema kama vile hakuna mwanamke duniani ila Khadija, akijibu: Hakika alikuwa na alikuwa... na mimi nilipata watoto kupitia kwake.

Kadhalika, Mama Aisha amesema, “Alikuwa Mtume(saw) hatoki nyumbani hadi amemtaja Khadija kwa wema na kumsifia. Siku moja akamtaja, nikapatwa na wivu, nikasema, ‘He! Kwani hakuwa ila kizee, Mwenyezi Mungu amekupa badali yake aliyekuwa bora zaidi’. Mtume(saw) Akaghadibika sana mpaka zikasimama nywele zake za mbele ya kichwa kwa ghadhabu, kisha akasema, ‘Wallahi sikupata aliyekuwa bora kuliko yeye; hakika aliniamini walipokataa kuniamini watu; akanisadiki waliponikadhibisha watu; akanipa mali yake waliponinyima watu; na Mwenyezi Mungu Mtukufu akaniruzuku watoto kupitia kwake wakati sikupata watoto kwa wanawake wengine’. Nikajiambia nafsini mwangu, wallahi sitomtaja kwa ubaya tena.

Sayyidatna Khadija ni bora ya wanawake wa ummati huu baada ya Sayyidatna Fatima(ra), binti ya Mtume(saw). Na yeye ni mbora wa wakeze Mtume(saw). Na baada yake kwa ubora ni Sayyidatna Aisha. Ilitokea Mama Aisha(ra) na Bibi Fatima(ra) walishindana. Mama Aisha(ra) alisema, "Mtume(saw) amenioa mimi nikiwa Bikira, na alimwoa mama yako wakati yeye ni mwanamkuu (amesha olewa kabla). Maneno hayo yakamfikia Mtume(saw), akamwambia (Bibi Fatima), amwambie kuwa ikiwa Mtume(saw) amemwoa yeye (Mama Aisha) akiwa Bikira, basi Bi Khadija aliolewa na Mtume(saw) wakati Mtume(saw) akiwa ni bikira.

Mama Sawda bint Zam-ah(ra).

Mtume(saw) alimwoa baada ya kufariki kwa Mama Khadija, kabla yake alikuwa ameolewa na Bwana Sakaran bin Amr. Alipofikia umri mkubwa, Mtume(saw) akataka kumwacha, akamwambia Mtume(saw), "Usiniwache kwani nataka nifufuliwe katika wake zako". Akampa zamu yake Sayyidatna Aisha. Alifariki katika zama za ukhalifa wa Sayyidna Umar.

Mama Aisha bint Abi Bakr(ra).

Mtume(saw) alimwoa Mama Aisha kabla ya Hijra. Alipelekwa nyumbani kwa mumewe, Mtume(saw) baada ya kuhamia Madina. Huyu ndiye bikira pekee ambaye Mtume(saw) alimwoa. Ama wake zake wengine wote walipata kuolewa kabla. Mtume(saw) alikuwa akimpenda sana, na ndiye aliyepokea Hadithi nyingi za Mtume(saw) kuliko wake zake wengine. Mtume(saw) aliulizwa nani anayempenda zaidi katika watu akasema Aisha. Akaulizwa na katika wanaume, akajibu baba yake, akaulizwa kisha nani, akasema Umar. (Bukhari na Muslim). Mama Aisha pia amepata utukufu kwa kuwa Mtume(saw) amefariki akiwa pamoja naye, chumbani kwake na akiwa amelala kwenye mapaja yake.

Sahaba Abu Musa Al-Ash-ariy(ra) amesema, “Hawakupata mushkili masahaba wa Mtume(saw) katika hadithi hata mara moja, tukamuuliza Aisha ila tulikuta kuwa ana elimu juu ya jambo hilo”. Masruuq pia amesema, “Tunamwapia Mwenyezi Mungu tumeona masahaba wakubwa na watu wazima wa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) wakimuuliza Aisha kuhusu mirathi”. Na amesema Urwa bin Zubair, “Sikuona mwanamke mwenye elimu ya utabibu, wala fiqh, wala mashairi kuliko Aisha”.

Sufyaan bin U’yayna amesema kutokana na Imamu Zuhriy, “Lau ingekusanywa ilmu ya Aisha(ra) ikawekwa (upande mmoja) na ilmu za wake wengine wote wa Mtume(saw) na wanawake wote (upande mwengine), ilmu ya Aisha ingekuwa zaidi”.

Imepokewa pia kuwa watu walikuwa wakituma zawadi wakati Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu akiwa nyumbani kwa Mama Aisha(ra). Wakakutana wakeze Mtume(saw) kwenye nyumba ya Mama Ummu Salamah(ra) wakamwambia Ummu Salamah, kuwa watu wanatuma zawadi zao siku ya Aisha, na kuwa wao pia wanataka kheri kama anavyoitaka Aisha. Mama Ummu Salamah akamwambia Mtume(saw), Mtume(saw) asimjibu kitu, alipomwambia mara ya tatu, Mtume(saw) akasema, “Ewe Ummu Salamah usiniudhi kwa Aisha, kwani Wallahi hakuna katika wake zangu ambaye unashuka wahyi nikiwa kwenye shuka yake ila Aisha”.

Mama Aisha(ra) alikuwa mkarimu sana. Imepokewa na Imaam Bukhariy kuwa mtoto wa dada yake Mama Aisha (na ambaye kalelewa na yeye), Bwana Abdullah bin Zubeir alisema kuwa Mama Aisha(ra) awache kutoa sadaka kila alichonacho au watamwekea kizuizi (yaani asiwe na uwezo wa kutumia mali yake ila kwa amri ya hakimu). Mama Aisha(ra) alipopata habari hizo akasema, “Basi Wallahi ninatia nadhiri (ya kukata udugu naye na) sitamsemesha tena”. Ibn Zubair akamtumia mtu amwombee msamaha ulipozidi muda wa kutokumsemesha. Akasema, “Wallahi sitokubali maombi ya yeyote kwa suala lake, wala sitotoa kafara ya nadhiri yangu”. Ulipozidi muda kuwa mkubwa Ibn Zubair akazungumza na Miswar bin Makhrama na Abdullah bin Al-aswad bin Abd Yaghuth ambao ni katika Baniy Zuhra bin Kilaab,

akawaambia, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu ila mutaniingiza kwake Aisha, kwani si halali yeye kutia nadhiri ya kukata udugu na mimi”. Wakaenda Miswar bin Makhramah na Abdul-Rahman wakiwa na radi zao, wakaomba ruhusa kwa Mama Aisha(ra) wakamwambia, “Assalaam Alayki Warahmatullah Wabarakatuh! Je tuingie?” Akasema Aisha, “Ingieni”. Wakauliza, “Jee sote?” Akasema, “Naam nyote”. Hakujua kuwa Ibn Zubair yuko pamoja nao. Walipoingia, akaingia Ibn Zubair ndani ya Hijaab akamkumbatia Aisha akawa anabusu kichwa chake huku akilia, na wakawa Miswari na Abdul-Rahman wanamwapia azungumze naye na wakimwambia Mtume(saw) amekataza kama unavyojua kuhusu mtu kumhama mwenzie, kwani si halali mwislamu kumhama nduguye zaidi ya siku tatu. Walipomwambia sana kwa kumkumbusha na kumfahamisha makosa, akawa anawakumbusha huku akilia kuwa ameweka nadhiri na nadhiri ni kitu kizito. Ibn Zubair hakuacha kumnasihi Mama Aisha(ra) mpaka akavunja ukimya na akazungumza na naye. Kwa ajili ya kuvunja nadhiri yake Mama Aisha(ra) akawaacha huru watumwa arobaini. Alikuwa kila akiikumbuka nadhiri yake analia mpaka akijaza machozi kwenye hijabu (nguo ya kujitanda) yake.

Amefariki Sayyidatna Aisha siku ya Jumanne, tarehe 17 Ramadhan mwaka wa 58 A.H. Na aliomba azikwe Baqii na wake wengine wa Mtume(saw), kwani alichukulia kuwa alifanya makosa makubwa kumpiga vita Sayyidna Ali katika vita vya Jamal. Aliswaliwa na Sayyidna Abu Hurayrah(ra), na liwali wa Madina wakati huo alikuwa Bwana Marwaan.

Mama Hafsa bint Umar bin Khattab(ra).

Aliolewa na Bwana Khunays bin Hudhafa(ra), akafariki baada ya kuhama Madina wakati Mtume(saw) akirejea kutoka katika vita vya Badr. Alipofiwa Hafsa na mumewe Khunays ambaye alikuwa sahaba na ameshiriki katika vita vya Badr, Sayyidna Umar(ra) alimwambia Sayyidna Uthman(ra), “Ukitaka nitakuoza Hafsa.” Sayyidina Uthman(ra) hakumjibu kitu. Sayyidina Umar(ra) akamwambia Sayyidna Abubakr(ra), naye pia hakumjibu kitu. Hapo Sayyidina

Umar(ra) akaenda akamwambia Mtume(saw). Mtume(saw) akamjibu kuwa ataolewa Hafsa na aliyekuwa bora zaidi kuliko Uthman, na Uthman atamwoa aliyekuwa bora zaidi kuliko Hafsa. Sayyidina Umar(ra) akamwuliza Mtume(saw), litakuwaje hilo? Mtume(saw) akamwambia yeye atamwoa Hafsa, na Uthman atamwoa binti yake wa pili, naye ni Bibi Ummu Kulthum. Wakati huo mke wa Sayyidina Uthman(ra), Bibi Ruqayya alishafariki.

Mtume(saw) alitaka kumwacha Hafsa(ra), lakini akajiwa na Jibriil na kuambiwa asimwache, kwani Hafsa(ra) ni mwenye kufunga sana na ni mwenye kusimama sana usiku, na ni mke wake wa Peponi.

Kuna khitilafu kuhusu tarehe ya kufariki kwa Mama Hafsa(ra). Mapokezi mamoja ni kwamba alifariki katika zama za Ukhalifa wa Bwana Muawiya(ra). Na katika riwaya nyingine alifariki katika Ukhalifa wa Sayyidna Uthman(ra).

Mama Zaynab bint Khuzaymah(ra).

Huyu aliolewa kabla na sahaba Ubayda bin Al-Harith bin Abdul-Muttalib(ra), ambaye aliuawa kwenye vita vya Badr. Pamoja na kufa mumewe Mama huyu aliendelea na kazi yake ya kuwaangalia majeruhi wa vita hivyo. Mama huyu hakukaa sana na Mtume(saw). Alifariki baada ya miaka miwili. Yeye na Mama Khadija(ra) ni wake wawili wa Mtume(saw) waliofariki katika uhai wa Mtume(saw). Mama huyu alikuwa akiitwa *Ummul-Masaakin* kwa kuwa alikuwa akitoa sadaka sana kwa masikini na kuwalisha.

Mama Ummu Salamah Hind bint Abi Umayya Al-Makhzumiya(ra).

Huyu aliolewa kabla na sahaba Abdallah bin Abdul-Asad (yaani Abu Salamah)(ra). Katika Hijra ambayo masahaba walihama kwenda Habash, Mama Ummu Salamah(ra) alikwenda pamoja na mumewe. Mumewe aliuawa kwenye vita vya Uhud. Baada ya kumaliza eda ya kufiwa na mumewe, Mtume(saw) akamposa. Jibu la Mama Ummu Salamah(ra) ni kuwa yeye ni mwenye umri mkubwa, na ni mama wa

mayatima, na ni mwenye wivu sana. Mtume(saw) akamjibu, “Ama mayatima nitawaweka kwangu, na ninamwomba Mwenyezi Mungu akuondolee wivu moyoni kwako”.

Kwa bahati Bwana Abu Salamah(ra) alipokea Hadithi kwa Mtume(saw) na kuifikisha kwa mkewe, kwamba “ambaye hufiwa na mtu wa karibu akasema, ‘***Innaa Lillaahi wa innaa ilayhi raajiun***’, na kisha akaongeza dua kwa kusema, ‘Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba thawabu ya msiba huu, na unipe aliye bora kuliko huyu,’ ila Mwenyezi Mungu humpa (aliye bora)”. Mama Ummu Salamah(ra) amenukuliwa akisema alipofariki mumewe aliomba dua hiyo ila alipoomba apewe aliye bora kuliko Abu Salamah(ra), ilimpitikia moyoni “nani bora kuliko Abu Salamah(ra)”. Na Mwenyezi Mungu akamjaalia akaolewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw).

Mama huyu alikuwa mwenye hekima, katika Sulhu ya Hudaybiya, masahaba waliposita kunyoa alipowaamrisha Mtume(saw), aliingia Mtume(saw) kwake, huku akisema, “Wameangamia watu, nimewaamrisha wanyoe hawatekelezi”. Mama Ummu Salamah(ra) akampa ushauri kuwa yeye afanye kwanza, aonyeshe mfano, na masahaba hawatokaa nyuma, na wao pia watanyoa. Akatoka nje Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) na kunyoa. Hapo masahaba wakakimbilia kutekeleza na wao pia kunyoa.

Alifariki Mama Ummu Salamah(ra) mwaka wa 61 A.H.

Mama Ummu Habiba Ramlah bint Abi Sufyaan(ra).

Aliolewa kabla na Ubaydillah bin Jahsh, na akahama naye Habash, kisha mumewe akaingia kwenye dini ya ukristo na akafariki huko huko Habash. Ama yeye alithibiti juu ya Uislamu, Mtume(saw) akamwoa kwa wasita wa Najashi. Na Najashi akamtolea mahari ya dirham mia nne, na akampa mafuta mazuri ya kila aina, na akamfanyia walima pia ambayo walihudhuria masahaba waliokuwa Habasha wakiongozwa na Sahaba Ja’afar bin Abi Talib.

Baba yake Mama Ummu Habiba(ra), Abu Sufyan, ilipomfikia khabari ya kuolewa binti yake na Mtume(saw) na yeye bado ni kiongozi wa makafiri na hajasilimu bado, akaikiri ile ndoa, na kusema: “Yeye ni fahali isiyogongwa pua yake”. Na akajifakharisha na ukwe wa Mtume(saw), hadi aliposilimu.

Abu Sufyan, akiwa kiongozi wa makafiri, alipokuja Madina ili kuitia nguvu Sulhu ya Hudaybiya, baada ya kuwa wao wamevunja masharti yake, akaenda kwa binti yake, akataka kukaa juu ya tandiko la Mtume(saw). Ummu Habiba akalivuta kuliondoa. Akauliza baba yake, “Je, umeona hili tandiko ni bora zaidi kuliko mimi?” Mama Ummu Habiba(ra) akajibu, “Bali hili ni tandiko la Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) na wewe ni mtu kafiri najisi”.

Bibi Aisha anasema, “Aliniita Ummu Habiba wakati wa kufa kwake, akaniambia, ‘Mwenyezi Mungu atusamehe yaliyokuwa baina yetu kama yanavyotokea baina ya wake wenza’. Nikamwambia, ‘Mwenyezi Mungu akusamehe yote’. Akasema, ‘Umenifurahisha, Mwenyezi Mungu akufurahishe nawe’”. Vile vile alimwita Ummu Salamah na kumwambia hayo hayo.

Mama Ummu Habiba(ra) alifariki mwaka wa 44 A.H. wakati wa ukhalifa wa Bwana Muawiya.

Mama Zaynab bint Jahsh(ra).

Huyu ni mtoto wa Shangazi yake Mtume(saw), Umayma binti Abdil-Muttalib. Aliolewa kabla na huru wake Mtume(saw), Sahaba Zayd bin Harith(ra). Baada ya kuachwa na kumaliza eda, Mama Zainab(ra) aliozeshwa Mtume(saw) na Mwenyezi Mungu. Hatua hii imevunja tabia ya kumnasibisha huru wa mtu kama mtoto wa aliyemwacha huru, kwani sahaba Zayd alikuwa akiitwa Zayd bin Muhammad kabla ya kushuka kwa Aya iliyoharimisha kunasibisha mtumwa kwa mwenye kumuacha huru. Mtume(saw) alimwoa Mama Zainab(ra) mwaka wa tano tangu kuhamia Madina.

Imepokewa na Imaam Bukhariy kwamba Mama Zaynab alikuwa akijifakharisha juu ya wake wengine kwa kusema, “Nyie mumeozwa na wazee wenu, ama mimi nimeozwa na Mwenyezi Mungu”.

Mtume(saw) alilisha mkate na nyama katika harusi yake hii kama walima. Baada ya kula masahaba wakabaki wakizungumza nyumbani kwa Mtume(saw). Mtume(saw) akaingia na kutoka akitegemea wataondoka, lakini hawakuondoka. Jambo hili lilimpa uzito Mtume(saw) hadi ukaonekana juu ya uso wake. Hapo ndipo iliposhuka aya ya Hijaab.

Mama Zaynab alikuwa mtoaji sana sadaka, imepokewa na Bibi Aisha kwamba Mtume(saw) alisema, “(Katika wake zangu), wa kwanza kuja kwangu (baada ya kufa kwangu. Atakuwa ni) mwenye mkono mrefu”. Anasema Bibi Aisha, “Tukawa baada ya kufariki Mtume(saw), tunapima mikono yetu, tuone nani ana mkono mrefu. Hadi alipofariki Zaynab bint Jahsh, naye alikuwa ni mwanamke mfupi na wala si mwenye mkono mrefu, tukaelewa kuwa makusudio ya Mtume(saw) urefu wa mkono una maana ya sadaka. (Mama Zainab) alikuwa ni fundi, anafanya kazi, kisha anachopata anatoa sadaka”. Katika Ukhalifa wa Sayyidna Umar Mama Zainab(ra) aliletewa sehemu yake kama Mama wa waislamu na akaitoa karibu yote sadaka. Baada ya hapo akaomba dua ifuatayo, “Ewe Mwenyezi Mungu! Lisinifikie fungu atowalo Umar baada ya mwaka huu”. Dua yake ikakubaliwa na akafariki mwaka ule ule. Amefariki Mama Zaynab mwaka wa 20 A.H. naye akiwa na miaka 53.

Mama Juwayriya bint Al-Harith(ra).

Bibi huyu alikuwa mateka kwenye vita vya baniy Mustalik. Akawa kwenye fungu la sahaba Thabit bin Qays(ra). Akamwomba amwandikie mkataba wa kujikomboa kwa mali ili apate kuwa huru. Akamwandikia, akaenda kwa Mtume(saw) na kumwambia, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni Juwayriya bint Al-Harith, kiongozi wa watu wake, na hakika limenisibu jambo ambalo unalijua, na nimeangukia kwenye fungu la Thabit bin Qays, ameniandikia mkataba wa uhuru kwa

kutoa wakia tisa (28.349gx9), basi nisaidie katika kulipa mkataba wangu. Mtume(saw) akamwambia, “Je, unataka bora ya hayo?” Akamwuliza, “Nini hicho?” Akasema, “Nitakutolea mali yote na nikuoe”. Akasema, “Ndio, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu”.

Ilipofika habari kwa masahaba, wakasema wakweze Mtume(saw) hawawezi kuwa watumwa, wakawaacha huru wote. Walioachwa huru katika mkumbo huo wakafikia zaidi ya nyumba 100. Kisha watu wake walipoona waliyoyafanya Waislamu, wakaja wote kusilimu, ikawa kuolewa kwake ni baraka kwa watu wake.

Mama Juwairiya(ra) alifariki mwaka wa 50 A.H. naye akiwa na miaka 65.

Mama Safiyya bint Huyay bin Akhtab(ra).

Bibi huyu alichukuliwa mateka baada ya vita vya Khaybar, na baba yake alikuwa ndiye kiongozi wa Mayahudi wa kabila la Baniy Quraydha. Alipochukuliwa mateka, mumewe akiwa ameuawa vitani, Waislamu wakasema kuwa huyu ni mwanamke mtukufu wa Baniy Quraydha, hawezi kumfaa ila Mtume(saw). Wakampeleka kwa Mtume(saw), Mtume(saw) akamkhiyarisha moja ya mawili, alimwambia, “Chagua, ukitaka Uislamu nitakuweka kwangu (uwe mke wangu), na kama ukichagua uyahudi huenda nikakuacha huru ukarudi kwa watu wako”. Akasema, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika nimeupenda Uislamu na nimeuamini kabla hujanilingania. Sina haja na uyahudi, sina baba wala ndugu, na umenikhiyarisha baina ya Uislamu na ukafiri, basi Mwenyezi Mungu na Mtume(saw) wake ni bora zaidi kuliko kuachiwa huru na kurudi kwa watu wangu”. Hapo Mtume(saw) akamwoa. Walisilimu kwa ajili yake watu wengi.

Alifariki Bibi Safiyya mwaka wa 50 A.H. na akazikwa Baqii.

Mama Maymuna bint Al-Harith Al-Hilaaliyya.

Huyu ndiye mke wa mwisho kuolewa na Mtume(saw). Aliolewa kabla yake na sahaba Abi Ruhm bin Abdil-Uzza. Imepokewa kwamba yeye mwenyewe alijitolea kwa ajili ya Mtume(saw).

Imepokewa kutoka kwa Mama Aisha kuwa Mama Maimuna(ra) ndiye aliyekuwa mcha Mungu zaidi (katika wakeze Mtume(saw)), na mwenye kuunga zaidi udugu.

Imepokewa pia, yeye ndiye wa mwisho kufariki katika wakeze Mtume(saw), amefariki mwaka wa sitini na kitu baada ya Hijra.

Hawa ndio wakeze Mtume(saw). Ambao walimkalia eda ni tisa, ukiwaondoa Bibi Zaynab bint Khuzaymah na Bibi Khadija ambao walifariki katika uhai wa Mtume(saw).

Watoto wa Mtume(saw):

Watoto wa Bwana Mtume(saw) ni saba, watatu wanaume nao ni Qaasim, Abdulla, na Ibrahim; na wanne wanawake, nao ni Zainab, Ruqayya, Ummu Kulthum, na Fatma. Qaasim na Abdulla, pamoja na watoto wote wanne wanawake mama yao ni Sayyidatna Khadija.

Qaasim na Abdallah walifariki wakiwa wadogo, mtoto wa tatu wa kiume Ibrahim alizaliwa na kijakazi Bibi Maariya Al-Qibtiyya. Alizaliwa mwaka wa nane baada ya kuhama, na aliishi miezi 16 au 18 na kuzikwa Baqii.

Bibi Zaynab(ra) aliolewa na Bwana Abil-Aas bin Rabii. Bibi Ruqayya na Bibi Ummu Kulthuum(ra), wote wawili waliolewa na Sayyidna Uthman(ra) mmoja baada ya mmoja; na Bibi Fatma aliyeolewa na Sayyidna Aliy bin Abi Talib(ra).

Ifuatayo ni historia fupi ya mabinti zake ukiondoa ya Bibi Fatima ambayo inakuwa na tarjama inayojitegemea.

Bibi Zaynab(ra)

Bibi huyu ndiye mtoto wa kike mkubwa na aliolewa na Bwana Abil-Asi bin Rabii bin Abdil Uzza bin Abd Shams bin Abd Manaf. Mtume(saw) alipopewa Utume, watoto wa Abi Lahab walikuwa wamewaoa watoto wa Mtume(saw), Bibi Ruqayya na Bibi Ummu Kulthum(ra), ambao waliwaacha. Kisha wakamshawishi Abil-Aasi naye amwache mke wake ili wamkomoe Mtume(saw). Yeye akakataa. Bibi Zaynab(ra) alihama kwenda Madina kwa baba yake, na Abil-Aasi akabaki Makka bila kusilimu. Vilipopiganwa Vita vya Badr, Abil-Aasi alipigana dhidi ya Mtume(saw). Makafiri wakashindwa na yeye akawa ni miongoni mwa mateka wa Waislamu. Kisha akatolewa fidia na ndugu yake Amr bin Rabii kwa mali aliyopewa na Bibi Zaynab, ukiwemo mkufu wa Bibi Khadija ambao alipewa zawadi alipoolewa na Abil-Aasi. Mtume(saw) akasema, “Mukiona kuwa mumwachie huru na mumrudishie mali

aliyoitoa basi fanyeni hivyo". Hivyo Abul-Aasi akaachiwa huru na akarudi Makka.

Baadaye, kabla ya kutekwa Makka na waislamu, Abul-Aasi alitoka kwa ajili ya biashara akiwa na mali ya Makureshi akielekea Sham. Ulipokuwa ukirudi msafara wake, ukakutana na kikosi cha Sahaba Zayd bin Harith(ra) kilichotumwa na Mtume(saw). Wakawanyang'anya mali yao. Akaja Abul-Aasi usiku akaingia Madina na kuomba mke wake amhami. Mtume(saw) alipotoka kwa ajili ya swala ya Alfajiri, Bibi Zaynab(ra) akapiga ukelele, "Enyi watu hakika nimempa dhima Abal-Aasi bin Rabii." Mtume(saw) alipotoa salamu akasema, "Je, mumesikia niliyoyasikia mimi?" Wakajibu, "Ndiyo". Kisha Mtume(saw) akasema kwamba inaruhusiwa mwislamu yeyote hata akiwa wa hali ya chini kumwekea himaya mtu amtakaye. Kisha Mtume(saw) akaenda kwa binti yake Zaynab(ra) na kumwambia, "Ewe binti yangu! Mfanyie wema lakini si halali kwako (yaani kama mume)". Bibi Zainab(ra) akasema, "Hakika amekuja kufuata mali yake". Akatoka Mtume(saw) na kuwaita watu walioshiriki kwenye vita vile, akasema, "Hakika huyu mtu (Abal-Aasi) ni katika sisi, na kama munavyojua mumepata mali yake - ni ngawira ambayo Mwenyezi Mungu amekupeni. Na mimi napenda kuwa mumfanyie ihsani na mumrudishie mali yake. Mukikataa basi nyie muna haki zaidi (juu ya mali hiyo kwani imetekwa katika vita). Wakasema, "Bali tunamrudishia mali yake". Wakamrudishia mali yake. Alipofika Makka akampa kila mwenye mali yake ambayo alikuwa nayo. Kisha akasema, "Enyi Makureshi! Je, kuna mtu ambaye ana mali yake hajaichukua?" Wakajibu, "Mwenyezi Mungu akulipe kila la kheri, hakika umekuwa ni mwenye kutimiza ahadi na mkarimu". Akasema, "Hakika nashuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Wallahi hakukunizuia kusilimu ila kuhofia kuwa mutadhania nimekula mali yenu. Alipozifikisha Mwenyezi Mungu kwenu (mali zenu) nimesilimu". Kisha akatoka na kwenda kwa Mtume(saw) huku akiwa muislamu. Ukawa mzuri Uislamu wake na Mtume(saw) akamrudishia mke wake Zaynab.

Mtume(saw) alimshukuru kwa wema wake wa kutomwacha binti yake aliposhawishiwa na Makureshi. Pia aliusifia ukwe wake kwa kusema,

“Ameniambia, na alichoniambia kikawa kweli, na akanipa ahadi na akaitimiza ahadi yake”.

Bibi Zaynab alifariki katika uhai wa Mtume(saw), mwaka wa nane toka kuhamia Madina. Mtume(saw) alikaa kwenye kaburi lake, ukabadilika uso wake, kisha ukarudi kama kawaida. Akaulizwa na masahaba, akasema, “Nimemkumbuka binti yangu Zaynab na udhaifu wake na adhabu ya kaburi, nikamwomba Mwenyezi Mungu akamwondolea”.

Bibi Zaynab(ra) alipata mtoto wa kiume aliyekuwa akiitwa Aliy ambaye alifariki baada ya kubaleghe. Kijana huyu Aliy alipanda pamoja na Mtume(saw) juu ya ngamia katika Fat-hi Makka.

Vile vile Bibi Zainab(ra) alipata mtoto wa kike Umaama, ambaye Mtume(saw) alikuwa akimpenda sana na akimbeba kwenye swala mabegani kwake. Akirukuu humweka chini, kisha akisimama kutoka kwenye sijda humnyanyua tena. Imepokewa kutoka kwa Bibi Aisha, kwamba Mtume(saw) aliletewa zawadi ya mkufu wenye kito cha rangi. Akasema, “Nitampa ninayempenda zaidi katika ahli wangu”. Wakasema akina mama atapewa binti wa Abi Quhaafa (yaani Bi. Aisha). Mtume(saw) akamwita Umaama binti Abil-Aasi na akamvisha shingoni.

Bibi Umaama aliolewa na Sayyidna Aliy(ra) baada ya kufariki Bibi Fatima(ra) kwa wasia wake mwenyewe. Alipouawa Sayyidna Aliy akaolewa na Bwana Al-Mughiira bin Naufal bin Al-Harith bin Abdul-Muttalib kwa wasia wa Sayyidna Aliy.

Bibi Ruqayya(ra)

Baadhi ya riwaya zinasema kuwa yeye ni binti mkubwa, lakini riwaya iliyo sahihi ni kuwa Bibi Zaynab ndio mkubwa. Alizaliwa na Mtume(saw) akiwa na umri wa miaka 33. Alikuwa yeye na dada yake Ummu Kulthum wameolewa na watoto wa Abi Lahab. Ilipo shuka aya ya kuangamia kwa Abi Lahab, Abi Lahab akawaambia watoto wake, “Mimi kuonana na nyinyi ni haramu mpaka muwaache mabanati wa

Muhammad". Wakawapa talaka na hawakuwa wameingia nyumbani. Akaolewa Bibi Ruqayya na Sayyidna Uthman.

Bibi huyu alipewa uzuri wa kupindukia. Imepokewa kwamba Usama(ra) alitumwa kwake (akiwa kijana mdogo), akawa anawaangalia na anawashangaa wote wawili, Sayyidna Uthman na Sayyidatna Ruqayya(ra). Alipo rudi kwa Mtume(saw), akamwuliza, "Umeingia ndani?" Akajibu: "Ndio". Akasema, "Je, umewahi kuona mume/mke bora kuliko wao?" Akajibu, La, nilikuwa mara namtazama Uthman na kisha nageuka kumtizama Ruqayya.

Bibi Ruqayya(ra) alihama kwenda Habasha pamoja na Sayyidna Uthman na Mtume(saw) alipoambiwa kuwa walimwona Bibi Ruqayya akiwa amepanda punda na Uthman akiwa anamwelekeza, alisema, "Mwenyezi Mungu awe nao, Uthman ni wa mwanzo kuhama kuelekea kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka baada ya Luut".

Bibi Ruqayya alifariki wakati Waislamu walipoenda Badr baada ya kuumwa surua. Hii ndio sababu Sayyidna Uthman hakuhudhuria vita hivyo na Mtume(saw) alimpa sehemu yake ya ngawira. Mtume(saw) alipopewa pole kwa kufariki binti yake alisema: "Al-hamdu lillah! Kuzika mabinti ni katika matendo/mambo matukufu."

Bibi Ummu Kulthuum(ra)

Bibi huyu alijulikana kwa jina hili tu na wamekhitalifiana wanazuoni nani ni mkubwa kati yake na Bi. Ruqayya, ila yeye ni mkubwa kuliko Bi. Fatima.

Kama tulivyotangulia kusema kuwa aliolewa kwanza na mtoto wa Abi Lahab, Utayba. Alipokuja kumwacha kwa Mtume(saw) alisema, "Nimeikufuru dini yako na nimemwacha binti yako, sikupendi wala hunipendi". Kisha akapasua shati lake na alikuwa anatoka kuelekea Sham kwa ajili ya biashara. Akasema Mtume(saw), "Ama mimi namwomba Mwenyezi Mungu akutumie mbwa wake." Walipofika Zarqaa usiku, akaja simba akinusa, wote wakaogopa. Utayba akasema, "Ole wangu! Huyu simba atanila mimi kama alivyoniapiza Muhammad,

Ibn Abi Kabsha ataniua akiwa Makka na mimi niko Shaam?" Yule simba akamvamia baina ya watu na kumkata kichwa chake na kukitafuna.

Baada ya kufariki Bibi Ruqayya, Mtume(saw) alimwozesha Sayyidina Uthman(ra) Ummu Kulthuum(ra), na alipomwoza alimwambia, "Nakuoza kwa amri ya Mwenyezi Mungu aliyokuja nayo Jibriil kwa mahari ile ile ya Ruqayya".

Amefariki Bi. Ummu Kulthuum mwaka wa 9 tangu kuhamia Madina. Na alioshwa na Bi. Asmaa bint Umays na Bi. Safiyya bint Abdil Muttalib. Walifahamishwa jinsi ya kumwosha kama ilivyopokewa na maimamu Bukhariy na Muslim: "Mwosheni mara tatu, tano au saba au zaidi kama munavyo-ona, kwa maji na majani ya mkunazi na mara ya mwisho wekeni Kaafur, mukimaliza muniambie niingie". Tulipo maliza, tukamwambia. Akatutupia shanuo lake na akasema: "Sukeni kwalo nywele" Anasema (mpokezi), "Tukamfunga mafungu matatu na tukayatupia nyuma yake". Na imepokewa pia kwamba Mtume(saw) alisema, "Anzeni na pande zake za kulia na mwahala mwa kusujudia".

Aliswaliwa na Mtume(saw), kisha Mtume (saw) akakaa kwenye kaburi lake na kulia, kisha akauliza, "Nani kati yenu hajaonana na mke wake leo?" Akasema Abu Twalha, "Mimi". Mtume(saw) akamwambia, "Shuka kwenye kaburi lake". (Bukhariy)

Ammi zake Mtume(saw):

Mtume(saw) alikuwa na Ammi (baba wakubwa/wadogo) 12, na walio udiriki Uislamu ni wanne nao ni: Abi Talib, Abi Lahab, Hamza na Abbas. Waliothibiti uislamu wao ni Hamza na Abbas.

Sayyidna Hamza bin Abdil Muttalib.

Alikuwa ndugu wa Mtume(saw) katika kunyonya na mkubwa kuliko Mtume(saw) kwa miaka 4. Alikuwa akiitwa, "Asadullah wa Asadu Rasulihi" yaani, "Simba wa Mwenyezi Mungu na simba wa Mtume wake(saw)". Sababu ya kusilimu kwake ni kuwa Abu Jahal siku moja alimtukana Mtume(saw), kijakazi cha Abdallah bin Jad'an akamwona. Kisha akaja Hamza akiwa amerudi mawindoni amebeba mishale yake. Na alikuwa akirejea mawindoni harudi nyumbani ila baada ya kutufu Ka'aba. Akiwapitia Makureshi akisalimiana nao na kuzungumza nao. Na alikuwa ni kijana mtukufu miongoni mwa Makureishi na mwenye nguvu. Na alipompitia yule kijakazi na Mtume(saw) akiwa ameshaondoka kurudi nyumbani, akamwambia, "Ewe Aba Amaara lau ungeona yaliyompata mtoto wa ndugu yako kwa Abul-Hakam bin Hisham hapa, alimkuta hapa akamwudhi na kumtukana na kumfanyia anayoyachukia, kisha akaondoka na Muhammad hakumjibu kitu". Zikampanda ghadhabu Hamza na kwa ile hidaaya aliyoandikiwa na Mwenyezi Mungu, akatoka mbio asizungumze na mtu akiwa na hasira juu ya Abi Jahl ampige akikutana naye. Alipoingia msikitini akamwangalia akiwa amekaa na watu, akamwendea, akamsimamia kichwani kwake, akanyanyua upinde na kumpiga nao akamtia jeraha kubwa na kumwambia, "Unamtukana? Basi mimi niko juu ya dini yake, nasema anayosema, basi nijibu kama unaweza". Wakasimama Baniy Makhzuum kutaka kumnusuru. Abi Jahl akasema, "Mwacheni Abi Amaara kwani mimi nimemtukana vibaya mtoto wa ndugu yake". Kukatimia kusilimu kwa Hamza na kumfuata Mtume(saw). Na aliposilimu Hamza, walifahamu Makureshi kuwa Mtume(saw) amepata

utukufu na ulinzi na kwamba Hamza atamlinda, wakaacha baadhi ya maudhi kwa Mtume(saw).

Alisilimu Sayyidna Hamza(ra) mwaka wa pili baada ya Utume na siku 3 kabla ya kusilimu kwa Sayyidna Umar(ra).

Sayyidna Hamza ndiye aliyemuua Shayba bin Rabiah siku ya Badr, walipotoka mbele ndugu watatu wakasema, “Nani atapigana na sisi mmoja mmoja”. Wakatoka vijana wa kiansaar, wakasema, “Hatuwataki hawa, bali waje baniy ammi zetu”. Akasema Mtume(saw), “Simama ewe Aliy, simama ewe Hamza, simama Ewe Ubayda bin Harith”. Walipowakaribia, wakauliza, “Ni akina nani nyinyi?”. Wakawatajia, wakasema, “Naam, nyinyi ni watu walio sawa yetu”. Bwana Ubayda alikuwa mkubwa akapigana na Utbah, Bwana Hamza na Shayba, na Bwana Aliy na Waliid. Ama Bwana Hamza hakukaa ila muda mdogo akamwua Shayba, na Bwana Aliy akamwua Waliid, na Bwana Ubayda na Utbah kila mmoja alimpiga mwenzake pigo la kuumiza, akafa Utbah pale pale na Bwana Ubayda akafariki njiani walipokuwa wanarudi Madina.

Sayyidna Hamza pia ndiye wa kwanza kupewa bendera na Mtume(saw) katika vita. Hii ilikuwa baada ya Mtume(saw) kufika Madina akawatuma watu 30 katika Muhaajiriin kwenda *Sayfil-Bahr*.

Sayyidna Hamza aliuawa kwenye vita vya Uhud na aliyemwua alikuwa mtumwa aliyekuwa akiitwa Wahshiy. Mtumwa huyu aliahidiwa kuwa ataachwa huru na Bwana wake Jubayr bin Mut-im kama atamwua Hamza. Na huyu aliyemwua baadaye alisilimu, lakini Mtume(saw) alikuwa akimwambia, aweke mbali uso wake, kisha Wahshiyy alimwua Musaylamah (muovu aliyejitangazia Utume) na kusema huenda ikawa kafara ya kumwua Hamza.

Mtume(saw) alihuzunika na kulia sana alipomwona Ammi yake Hamza ameuawa na kukatwa katwa, akaapa kuwa na yeye atalipa kwa kuwafanyiwa hivyo watu 70, lakini ikashuka aya 126 katika Surat Nahl:

وَإِنۡ عَاقَبۡتُمۡ فَعَاقِبُواْ بِمِثۡلِ مَا عُوقِبۡتُم بِهِۦۖ وَلَئِن صَبَرۡتُمۡ لَهُوَ خَيۡرٞ لِّلصَّٰبِرِينَ

"**na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyo adhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanao subiri**".

Mtume(saw) akasubiri na kuvunja kiapo chake.

Sahaba Ibn Mas-uud(ra) amesema, "Hatukumwona Mtume(saw) akilia zaidi ya tulivyomwona akilia juu ya Hamza alivyouawa na aliuawa mwingine na kufanyiwa kama alivyofanyiwa (kukatwa katwa) katika Ansaar akiitwa Suhayl. Akaja (dada yake Bibi) Safiyya na nguo mbili kwa ajili ya sanda yake. Lakini Mtume(saw) alimkataza kumwona ndugu yake. Akarudi na akakabidhi zile nguo mbili. Ikapigwa kura baina ya wawili, nguo kubwa akaipata Suhayl na ndogo akapata Hamza, akifunikwa kichwani inaonekana miguu, ikifunikwa miguu unaonekana uso, Mtume(saw) akamfunika uso na kumwekea majani mabichi miguuni mwake. Kisha akaelekezwa Kibla akasimama Mtume(saw) juu ya jeneza lake, akalia na kutoa sauti huku akisema, "Ewe Hamza! Ewe Ammi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ewe simba wa Mwenyezi Mungu na simba wa Mtume wake! Ewe Hamza! Ewe mtenda wema! Ewe Hamza! Ewe mwenye kuondosha shida! Ewe Hamza! Ewe mwenye kuulinda uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu!", Akalia sana, kisha akaletwa mtu mmoja mmoja akimswalia mpaka wakamswalia swala 70 (idadi ya mashahidi) na Sayyidna Hamza yuko pale pale.

Sayyidna Abbas bin Abdil Muttalib

Alikuwa mkubwa kuliko Mtume(saw) kwa miaka mitatu. Imepokewa aliulizwa Sayyidina Abbas(ra), nani mkubwa Mtume(saw) au wewe? Akajibu yeye ni mkubwa na mimi nimezaliwa kabla yake.

Sayyidina Abbas(ra) alikuwa na Mtume(saw) siku ya kuahidiana na Ansaar na aliwaambia Ansaar kuwa kama wanaweza kumuhami na kuwa tayari kwa ajili ya vita basi wamchukue Mtume(saw) kwao (Madina), kama hawawezi basi wamwache. Wakatoa ahadi, pamoja na kusema kuwa wanao uwezo wa vita na wana asili ya kupigana vita. Mtume(saw) akafunga ahadi nao.

Alisilimu Abbas mwanzoni, lakini alikuwa akificha Uislamu wake, mpaka Mtume(saw) aliwaambia masahaba siku ya Badr, "Mwenye kukutana na Abbas asimwue kwani amelazimishwa kuja vitani". Akachukuliwa mateka, hata alipofungwa kama wanavyofungwa mateka wengine, Mtume(saw) hakupata usingizi kwa kusikia mguno wa Abbas. Mmoja wa masahaba akamwuliza nini kilichokufanya ukeshe, akasema kuguna kwa Abbas. Akaenda mtu mmoja na kulegeza kamba yake, usiku wa pili alipokuwa hakuusikia mguno wake, akauliza mbona sisikii kuguna kwa Abbas? Akasema mtu mmoja, "Nimeilegeza kamba yake". Mtume(saw) akasema, "Basi fanya hivyo kwa mateka wote". Kisha Abbas akajikomboa na kurudi Makka akiendelea kuwa jasusi wa Mtume(saw). Kabla kidogo ya Fat-hi Makka, Mtume(saw) alimpelekea khabari ahame aje Madina, ili aupate utukufu wa kuhama kwani hakuna kuhama baada ya kufunguliwa Makka.

Mtume(saw) alikuwa akimpenda sana Ammi yake na kusema, "Huyu ni ammi yangu, ndugu shakiki (baba mmoja mama mmoja) wa baba yangu". Ilikuwa Mtume(saw) anapokaa huzungukwa na Masahaba wake wakubwa, kulia kwake Sayyidina Abubakar(ra), kushoto kwake Sayyidina Umar(ra), na mbele yake Sayyidina Uthman(ra). Akitokea Sayyidina Abbas(ra) kuja kwa Mtume(saw), Sayyidna Abu Bakr akisogea ili akae karibu na Mtume(saw). Imepokewa na Imaam Tirmidhiy kwamba alikuja mara moja Sayyidina Abbas(ra) akalalamika kwa Mtume(saw) kuwa wana nini Makureshi, wakiwa wenyewe wanakuwa na furaha na wakikutana na sisi wanakuwa hawana hayo (yaani hawana bashasha wala furaha). Mtume(saw) akakasirika hadi uso wake ukawa mwekundu na akasema, "**Namwapia Mwenyezi Mungu haiingii imani moyoni mwa mtu mpaka akupendeni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume(saw) wake**". Kisha akasema, "**Enyi**

watu! Mwenye kumwudhi ammi yangu basi huyo ameniudhi mimi. Kwani ammi wa mtu ni ndugu wa baba yake". Imepokewa na Imaam Ahmad kuwa mmoja wa Ansaar alimtaja kwa ubaya baba yake Abbas katika zama za ujahiliya, Abbas akampiga kibao. Akaja kwa watu wake (na kuwaambia) wakavaa silaha zao na kusema: Wallahi tutampiga kama alivyompiga (mtu wetu). Mtume(saw) aliposikia akapanda mimbarini na kusema, "Ni mkazi gani wa ardhi mtukufu zaidi kwa Mwenyezi Mungu?" Wakajibu, "wewe". Akasema Mtume(saw), "**Basi Abbas anatokana na mimi na mimi ninatokana na yeye, musiwatukane maiti wetu mukawakasirisha walio hai kati yetu**". Wakaja (Ansaar) na kusema, "Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu na ghadhabu zako".

Imepokewa na Imaam Bukhariy kwamba Sayidna Umar katika ukhalifa wake alitawasali na Sayyidna Abbas ili wapate mvua, na wakakubaliwa dua yao.

Alifariki Sayyidna Abbas katika ukhalifa wa Sayyidna Uthman, akiwa na miaka 88 na akazikwa Baqii.

Shangazi zake:

Mtume(saw) alikuwa na mashangazi 6, nao ni: Aatika, Umayma, Baydhaa (au Ummu Hakiim), Barrah, Safiyya na Arwaa. Kumethibiti kusilimu kwa Bibi Safiyya na kuna khilafu kwa Aatika na Arwaa.

Sayyidatna Safiyya bint Abdil Muttalib

Aliolewa na Harth bin Harb, kisha akafariki na akaolewa na Awwaam bin Khuwaylid, ndugu wa Sayyidatna Khadija na kupata mtoto Zubayr na Saib.

Mtume(saw) alimpa fungu Sayyidatna Safiyya(ra) kwenye vita vya Khandaq kwa kuwa alimwua yahudi mmoja.

Alifariki katika ukhalifa wa Sayyidna Umar na kuzikwa Baqii.

Imepokewa hadithi moja kutoka kwake na Daaruqutniy na alitunga mashairi alipofariki Mtume(saw).

Sayyidatna Fatima.

Amezaliwa wakati Makureshi wakijenga Ka'aba, naye ni binti mdogo kabisa, bali anayependwa zaidi na Mtume(saw) kuliko wengine. Aliolewa na Sayyidna Aliy mwaka wa pili tangu kuhamia Madina.

Imepokewa kutoka kwa Anas-Mwenyezi Mungu amridhie amesema: Walikuja Abubakar na Umar kwa Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu-rehema na amani zimshukie-kumposa Fatima. Mtume(saw) akanyamaza asiwajibu kitu. Wakamuendea Aliy wakamuamrisha kwenda kuposa yeye. Aliy anasema: Wakanizindua kwa jambo hilo, basi nikainuka nikiburuza shuka langu mpaka nikafika kwa Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu-rehema na amani zimshukie-nikamwambia: Niozeshe Fatima. Akaniuliza: Unayo mahari? Nikajibu: Ninaye farasi wangu na ngamia wangu. Akasema: Ama farasi wako unamuhitajia (katika vita), muuze ngamia wako. Basi nikamuuza kwa dirham mia nne na themanini. Nikampelekea, akaziweka mapajani mwake na akatwaa kiasi, akasema: Ewe Bilali, katununulie manukato. Na akawaamrisha kumtayarisha bi harusi, akamtengenezea kitanda chenye tao na mto wa ngozi uliotiwa hasho la usumba. Na akamwambia Aliy: Akikujia, usizungumze nae lolote mpaka nije. Akaletwa na Ummu Ayman, akakaa katika pembe moja ya chumba nami nikiwa katika pembe nyingine. Akaja Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) akasema: Njoo hapa ndugu yangu. Ummu Ayman akasema: ndugu yako na ilhali umekwisha muozesha binti yako? Akajibu: Ndio. Mtume(saw) akaingia ndani na akamwambia Fatima: Niletee maji. Akaenda akachukua bilauri kubwa iliyo kuwemo ndani, akatekea humo maji. Mtume(saw) akayachukua, akatemea ndani yake, kisha akamwambia: Njoo. Akaja, akamnyunyuzia baina ya kifua chake na kichwani kwake na akasema: Ewe Mola wa haki! Mimi ninamlinda kwako na kizazi chake kutokana na shetani mrujumiwa. Halafu akasema: Geuka. Akageuka, akamwagia maji baina ya mabega yake na akasema: Ewe Mola wa haki! Mimi ninamlinda kwako na kizazi chake kutokana na shetani mrujumiwa. Mtume(saw) akasema: Nileteeni maji. Aliy anasema: Nikajua analo likusudia, basi nikainuka nikaijaza hero maji, nikamletea. Akayatwaa na kutemea ndani yake na akamfanyia Aliy kama alivyo mfanyia Fatima na akamuombea kama

alivyo muombea. Kisha akasema: ingia nyumbani kwa ahali yako kwa jina la Mwenyezi Mungu na baraka zake.

Imepokewa kuwa Mtume(saw) aliwaombea kwenye harusi yao kwa kusema: Mwenyezi Mungu ajaalie kutokana na wawili nyie watoto wengi walio wema na akubarikieni. Anasema Anas: Basi wallahi, kwa yakini Allah alitoa kutokana nao watoto wengi walio wema.

Sayyidatna Fatima alipata watoto watano, nao ni: Hasan, Husain, Muhsin, Zaynab na Ummu Kulthuum. Zaynab akaolewa na Abdallah bin Ja'afar akapata watoto Aliy, Ja'far, Awn, Abbaas na Ummu Kulthuum.
Ummu Kulthum akaolewa na Sayyidna Umar akapata mtoto Zayd. Muhsin alifariki mdogo na Hasan na Husain tutawaelezea kwa kirefu hapo mbele.

Sayyidna Aliy(ra) amesema, "Nimemwoa Fatima na sina mimi wala yeye chochote zaidi ya ngozi ya mbuzi, tunailalia usiku, na tunainyunyuzia maji juu yake mchana, na sina mtumishi zaidi yake". Ataa bin Rabaah amesema, "Alikuwa Fatima binti wa Mtume(saw) anakanda unga na kibanio chake cha nywele kikigusa ardhi na beseni."

Sayyidna Aliy(ra) alisema kumwambia mtu mmoja, "Ewe mtoto wa Abdillah! Je, nikwambie kuhusu Fatima? Alikuwa binti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw), ndiye mbora wa Ahli bayti wake kwake, na alikuwa mke wangu akiendesha jiwe la kusagia mpaka ikaathirika mikono yake kwa hilo jiwe. Na akiteka maji kwa kiriba mpaka kiriba kikaiathiri shingo (kikaacha alama) yake, na akisafisha nyumba mpaka ikatapakaa vumbi nguo yake, na akikoleza moto mpaka akazichafua nguo zake na akapata madhara kutokana na kazi hizo."

Sayyidina Aliy(ra) alimwambia Bibi Fatima(ra) siku moja, "Wallahi hakika nimeteka maji kisimani mpaka kifua changu kinaniuma na Mwenyezi Mungu amemletea baba yako mateka wa vita, basi nenda kamwambie atupatie mtumishi." Akasema Bibi Fatima(ra), "Na mimi Wallahi nimesaga mpaka imevimba malenge-lenge mikono yangu".

Akaenda kwa Mtume(saw) akamuuliza, “Nini kimekuleta ewe binti yangu!” Akajibu, “Nimekuja kukusalimia”. Aliona haya kumwomba na akarudi. Mumewe akamwuliza, “Imekuwaje?” Akamjibu, “Nimeona haya kumwomba”. Wakaenda wote wawili kwa Mtume(saw) na akasema Sayyidina Aliy(ra), “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wallahi hakika nimeteka maji kisimani mpaka nimeumwa na kifua”. Akasema Bibi Fatima(ra), “Na mimi nimesaga mpaka imevimba malenge lenge mikono yangu na Mwenyezi Mungu amekuletea mateka na ukunjufu wa hali, basi tupe mtumishi”. Akasema Mtume(saw), “Wallahi siwezi kukupeni nikawaacha watu wa Sufa [masikini waishio katika baraza ya msikiti wa Mtume(saw)] wakilala na njaa sina cha kuwapa. Lakini nitawauza na thamani yake nitawanunulia chakula”.

Wakarudi, kisha akawajia Mtume(saw) nao wameshajiingiza kwenye shuka yao. Shuka yenyewe ilikuwa ndogo kiasi kwamba wakifunika vichwa vyao inaonekana miguu yao, na wakifunika miguu yao vinaonekana vichwa vyao. Wakavumburuka kutaka kuinuka, akawaambia. Hapo hapo mulipo. Kisha akawaambia, “Je, nikwambieni bora kuliko muliyoniomba?” Wakasema, “Tuambie”. Mtume(saw) akasema, “Maneno aliyonifundisha Jibriil: mnaleta tasbihi (Subhaanallah) mara 10, mnaleta tahmidi (Al-hamdulillah) mara 10 na mnaleta takbira (Allaahu Akbar) mara 10 baada ya swala. Na mukifika sehemu ya kulala, munaleta tasbihi mara 33, tahmidi mara 33, na takbira mara 34.....hiyo ni bora kwenu kuliko mtumishi”. Sayyidina Aliy(ra) akasema, “Wallahi sikuwacha uradi huo tangu aliponifundisha Mtume(saw)”.

Na imepokewa na Sayyidatna Aisha kwamba, “Alikuja Fatima akitembea kama utembeaji wa Mtume(saw). Mtume(saw) akasema, ‘Karibu binti yangu!’ Akamkalisha pembezoni mwake, akamwambia kitu kwa siri na Fatma akalia. Nikamwambia, ‘Amekukhusisha Mwenyezi Mungu kwa kuzungumza na Mtume(saw) kisha unalia!’ Kisha Mtume(saw) akamwambia tena kwa siri na Fatima akacheka. Nikasema, ‘Sijaona siku ambayo furaha iko karibu na huzuni kama leo.’ Nikamwuliza Fatima alichosema [Mtume(saw)]. Akasema, ‘Mimi sio mwenye kutoa siri ya Mtume(saw). Alipofariki Mtume(saw),

nikamwuliza, akaniambia kwamba alimwambia, ‘Jibriil ananijia na Qur-ani kila mwaka mara moja na mwaka huu amenijia na Qur-ani mara mbili, na sioni ila ya kuwa ajali (mauti) yangu imekaribia, na wewe ni wa kwanza katika Ahli bayti wangu kunifuata. Na mimi ni mbora wa mwenye kutangulia kwa ajili yako’. Nikalia kwa hilo, kisha akaniambia, ‘Je, huridhii kuwa wewe ni bibi (kiongozi) wa akina mama wa umati huu? Au bibi wa kina mama waumini?’ Nikacheka kwa hilo. (Bukhari na Muslim)

Maimamu Bukhari na Muslim wamepokea Hadithi kwamba Mtume(saw) alisema akiwa juu ya mimbari, “Hakika Baniy Hisham bin Mughiira wameniomba ruhusa wamwoze binti yao Aliy bin Abi Talib. Sitoi ruhusa, kisha sitoi ruhusa, ila kama ibn Abi Talib amwache binti yangu na aoe binti yao, kwani yeye (Fatima) ni sehemu yangu, kinanipa taabu kinachompa taabu yeye na kinanikera kinachomkera yeye”. Huyu aliyeposwa na Sayyidna Aliy wakaja kumwomba ruhusa Mtume(saw), ni Juwayriya binti Abi Jahl bin Hisham bin Mughiira. Juwayriya alisilimu na akala kiapo cha utii na akaolewa na Itaab bin Asad, na kisha akaja kuolewa na Ibaan bin Saeed bin Al-Aas.

Alifariki Sayyidatna Fatima miezi sita baada ya Mtume(saw) naye akiwa na miaka 28, na alikoshwa na Sayyidna Aliy na kuswaliwa na kuzikwa usiku.

Sayyidna Aliy

Mama yake ni Bibi Fatima bint Asad bin Hashim. Kwa hiyo Sayyidna Aliy ni Hashimiy kwa pande zote mbili. Mama huyu alikuwa katika wa mwanzo kusilimu na kuhama kwenda Madina. Alikuwa na daraja ya mama kwa Mtume(saw). Alipofariki mama huyu, Mtume(saw) alimvisha nguo yake, akalala yeye Mtume(saw) kwenye mwanandani kabla ya kumlaza kwa mkono wake. Baada ya kuzikwa akaulizwa, akasema nimemvisha nguo yangu ili avishwe nguo za peponi na nimelala sehemu yake ya kuzikiwa ili apunguziwe kukandamizwa (kubanwa) na kaburi. Alikuwa ni mwema mno kwangu katika viumbe vya Mwenyezi Mungu baada ya Abi Talib, akalia na kusema, “Mwenyezi Mungu akulipe wema ewe Mama, ulikuwa mama bora kabisa”.

Kusilimu kwake

Alisilimu akiwa na miaka 10, kwani alilelewa na Mtume(saw). Amesema Bwana Mujaahid bin Jubayr kwamba katika jumla ya neema za Mwenyezi Mungu juu ya (Sayyidna) Aliy bin Abi Talib ni kwamba walipata shida (njaa) na (Bwana) Abi Talib alikuwa ana watoto wengi. Mtume(saw) akamshauri (Sayyidina) Abbas(ra) waende wakamsaidie kwa kumpunguzia mzigo wa watoto. (Sayyidina) Abbas(ra) akakubali. Shauri hili lilikubaliwa vile vile na (Bwana) Abi Talib ila alitaka aachiwe mtoto wake (Bwana) Aqiil. Hivyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) akamchukua (Sayyidina) Aliy(ra) na kumweka kwake, na (Sayyidina) Abbas(ra) akamchukua (Sayyidina) Ja'afar(ra) na kumweka kwake. (Sayyidina) Aliy akabaki na Mtume(saw) hadi alipopata Utume akamwamini na kumsadikisha na kumfuata.

Kujitoa muhanga kwa ajili ya Mtume(saw)

Sayyidna Aliy(ra) alijitoa muhanga kwa ajili ya Mtume(saw). Siku alipohama Mtume(saw) kwenda Madina, yeye alilala sehemu ya

Mtume(saw) ili kuwapoteza makureshi walioweka doria nje ya nyumba ya Mtume(saw). Sayyidina Aliy(ra) akarudisha amana za watu zilizokuwa zimewekwa kwa Mtume(saw) kama alivyoamrishwa, na kisha akahama na kukutana na Mtume(saw) akiwa Qubaa.

Kupanda mabegani mwa Mtume(saw)

Imepokewa na Imaam Ahmad, kwamba Sayyidna Aliy alisema, "Nilikwenda na Mtume(saw) mpaka tukafika kwenye Ka'aba. Akaniambia, 'kaa (chini)'. Akapanda mabegani kwangu. Nikataka kunyanyuka, nae akaona nina udhaifu (siwezi kunyanyuka huku nimembeba), akashuka. Akakaa kwa ajili yangu Nabii wa Mwenyezi Mungu(saw) akaniambia, 'Panda kwenye mabega yangu'. Akanyanyuka akiwa amenibeba, basi nilihisi kuwa kama ningetaka kugusa mbingu ningeweza. Nikapanda juu ya Ka'aba na juu yake kulikuwa na sanamu la dhahabu au risasi. Basi nikawa nalitingisha kulia na kushoto, mbele na nyuma mpaka nikaling'oa. Akaniambia 'Litupe'. Nikalitupa chini, likavunjika kama kinavyo vunjika kioo. Kisha nikashuka. Nikaondoka na Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) haraka mpaka tukafika kwenye nyumba kwa kuhofia kukutwa na mtu yeyote.

Kupendwa na Mwenyezi Mungu na Mtume(saw) wake na kila mwislamu

Imepokewa na Maimamu Bukhari, Muslim, na Ahmad kwamba Mtume(saw) alisema siku ya vita vya Khaybar, "Nitampa bendera kesho mtu ambaye Mwenyezi Mungu Atatupa ushindi kwa kupitia kwake, anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda". Wakawa watu wanaulizana nani atapewa. Walipopambazukiwa watu, wakaenda kwa Mtume(saw) kila mmoja akitarajia atapewa yeye. Mtume(saw) akauliza yuko wapi Aliy bin Abi Talib? Akaambiwa anaumwa macho. Mtume(saw) akasema, "Mleteni". Mtume(saw) akamtemea mate kwenye macho yake na akamwombea. Akapona kama hakuwa na machungu yoyote, kisha akampa bendera. Aliy(ra) akasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi

Mungu, nipigane nao mpaka wawe mfano wetu (Waislamu)?" Akasema Mtume(saw), "Nenda taratibu mpaka ufike kwenye uwanja (ardhi) wao kisha walinganie Uislamu, na uwaambie yaliyo lazima juu yao katika haki za Mwenyezi Mungu. Namwapia Mwenyezi Mungu, kama akimwongoa Mwenyezi Mungu mtu mmoja kwa ajili yako ni bora kuliko kuwa na ngamia wekundu".

Imepokewa na Sahaba Abi Raafi', huru wa Mtume(saw), "Tulitoka na Aliy alipotumwa na Mtume(saw) kuchukua bendera yake. Alipoikaribia ngome (ya adui) wakatoka walio kuwamo humo tukapigana nao. Yahudi mmoja akampiga (Sayyidina Aliy), ikaanguka ngao yake. Aliy akaubeba mlango uliokuweko kwenye ngome, akawa anautumia kama ngao yake. Haukuacha kuwa mkononi mwake mpaka Mwenyezi Mungu Mshindi, Mtukuka, Akaifungua ngome hiyo kupitia kwake. Kisha akautupa yalipoisha mapambano. Basi ungetuona nikiwa na watu saba nikiwa wa nane wao, tunajaribu kuugeuza ule mlango tusiweze kuugeuza. (Imepokewa na Imaam Ahmad.)

Imepokewa na Sayyidina Anas bin Malik(ra) kuwa Mtume(saw) aliletewa zawadi ya ndege, akapiga bismillah, akala tonge na kusema, "Ewe Mwenyezi Mungu niletee unayempenda zaidi katika viumbe na ninayempenda (zaidi)". Akaja Aliy akabisha hodi, nikamwuliza nani wewe, akasema Aliy, nikamwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko ameshughulika … kisha Mtume(saw) akala tonge na kusema kama mwanzo. Akabisha hodi (tena) Aliy, nikamwuliza nani wewe, akasema Aliy, nikamwambia Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu yuko ameshughulika… kisha Mtume(saw) akala tonge na kusema mfano wa hayo. Akabisha hodi Aliy kwa nguvu, Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu akasema, "Ewe Anas fungua mlango!" Akaingia, Mtume(saw) alipomwona akatabasamu na kusema, "Namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye aliyekujaalia wewe, kwani nimekuwa nikiomba katika kila tonge niletewe kipenzi zaidi kwake (Mwenyezi Mungu) na kwangu mimi, basi ukawa ni wewe". Akasema (Aliy), "Namwapia yule aliyekutuma nimekuwa nikibisha hodi mara tatu na Anas ananirudisha". Akauliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), "Kwa nini

hukumfungulia?" Nikajibu, "Nilikuwa nikitamani aje pamoja naye mtu katika Ansaar. Mtume(saw) akatabasamu na kusema, "Halaumiwi mtu kwa (kuwapenda) watu wake".

Imepokewa na Imaam Muslim kwamba alisema Aliy: "Namwapia yule ambaye aliyeipasua mbegu na akawaumba viumbe ya kwamba ni ahadi ya Nabii asiyesoma(saw) ya kwamba hanipendi mimi ila muumini na wala hanichukii ila mnafiki".

Imepokewa na Imaam Ahmad, amesema Mtume(saw), "Enyi watu! Nakuusieni kumpenda ndugu yangu na mtoto wa ammi yangu: Aliy bin Abi Talib, kwani hampendi ila muumini na hamchukii ila mnafiki". Na amesema Sahaba Jabir bin Abdallah(ra), "Hatukuwa tukiwajua wanafiki ila kwa kumchukia kwao Aliy. Imepokewa na Imaam Ahmad.

Ushujaa wake

Tumeshaona jinsi alivyopigana na Waliid katika vita vya Badr akammaliza. Na kwenye vita vya Khandaq alipigana na Amr bin Abdi Wudd ambaye alikuwa shujaa mashuhuri katika Waarabu; walimhesabu yeye mmoja kuwa tosha ya elfu. Masahaba wote wakakaa kimya. Akajitokeza Aliy mara mbili, kila mara Mtume(saw) akimrejesha na kumwambia ni Amr. Mara ya tatu akamruhusu apigane naye, akapigana naye na kumwua. Tumeona pia kwenye vita hivi jinsi alivyozifungua ngome zao na kupigana kishujaa na kubeba mlango kama ngao ambao ulikuja kuwashinda watu 8 kuugeuza. Sayyidna Aliy pia alikuwa mshika bendera wa Mtume(saw) katika vita vya Badr na vita vingine, na hapewi bendera ila aliyekuwa shujaa.

Alipouawa Sayyidina Aliy(ra), alikhutubu Sayyidna Hasan bin Aliy(ra), akasema: "amekuondokeeni mtu ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) alikuwa akimpa bendera; na hakurudi nyuma ila Mwenyezi Mungu humpa ushindi. Hakuacha cha njano (dhahabu) wala cheupe (fedha) ila dirham 700 alizoziweka kwa ajili ya mtumishi wake." (Imaam Ahmad)

Elimu yake

Imepokewa na Imaam Ahmad, alikuja mtu kumwuliza swali Muawiya, akamwambia mwulize Aliy kwani yeye ana elimu zaidi. Akasema (muulizaji), Ewe Amirul-Muuminina jawabu lako nalipenda zaidi kuliko jawabu la Aliy. Akamwambia, Uovu mno uliosema, umemchukia mtu ambaye Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu alikuwa akimkhusisha na elimu; na hakika alimwambia, "Wewe kwangu ni kama daraja aliyokuwa nayo Harun kwa Musa ila hakuna nabii baada yangu na alikuwa Umar akiwa na mushkil humrejea yeye."

Imepokewa na Imaam Muslim kwamba Sayyidatna Aisha aliulizwa kuhusu kupangusa khofu mbili akasema "nenda kwa Aliy ukamwulize." Imepokewa na Imaam Ahmad, kwamba Bwana Saeed bin Musayyib amesema, "Hakuna katika masahaba wa Mtume(saw) aliyekuwa akisema niulizeni ila Aliy."

Sayyidina Aliy(ra) alipopelekwa Yemen na Bwana Mtume(saw) akawe Kadhi, alisema, "Ewe Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu! Unanituma kwa watu ambao kutakuwa na matukio baina yao na mimi, sina elimu ya ukadhi (hukumu)? Akasema Mtume(saw), "Hakika Mwenyezi Mungu atauongoza ulimi wako na kuuthibitisha moyo wako". Akasema (Aliy), "Basi sikutetereka katika hukumu baina ya (mahasimu) wawili". (Imaam Ahmad)

Wakati wa Ukhalifa wake Sayyidina Aliy(ra) alikuwa akisema, "Tanabahini mimi si nabii wala sipati wahyi, lakini natumia kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume(saw) kiasi ninachoweza, basi nikikuamrisheni kitu katika twaa ya Mwenyezi Mungu, basi ni haki juu yenu (yaani lazima) kunitii kwa munayoyapenda na munayoyachukia. (Imaam Ahmad)

Udugu wake na Mtume(saw).

Katika vita vya Tabuk, Mtume(saw) alimwacha Sayyidina Aliy bin Abi Talib(ra) (hakumchukua kwenye vita). Sayyidina Ali(ra) akalalamika

kwa Mtume(saw) kwa kusema, “Ewe Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu! Unaniwacha pamoja na wanawake na watoto wadogo?” Akamwambia, Je, huridhii kuwa kwangu kama daraja aliyokuwa nayo Harun kwa Musa Isipokuwa kuwa hakuna nabii baada yangu? (Bukhari na Muslim)

Sahaba Abdulla ibn Umar amesema, “Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) alifungisha udugu baina ya masahaba wake. Akaja Aliy huku akilia, akasema, ‘Ewe Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu Umefungisha udugu baina ya masahaba wako na hukufungisha udugu baina yangu na yeyote?’ Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) akamwambia, ‘Wewe ni ndugu yangu duniani na akhera’”. (Tirmidhiy)

Mawla (Bwana) wa kila Muumini

Imepokewa na Imaam Ahmad, kuwa Sayyidna Aliy alisema alipo kuwa Rahba, alikuwa akiwaapia wajitokeze wale waliomshuhudia Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) siku ya Ghadiir Khum akisema aliyoyasema. Basi wakasimama watu 13, wakashuhudia kwamba wao walimsikia Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu akisema, “Ambaye mimi ni Bwana mtawali wake basi Aliy (pia) ni Bwana mtawali wake.”

Na asili ya kisa hiki ni hadithi iliyopokewa na Sahaba Barraa bin Azib Mwenyezi Mungu amridhie amesema, “Tulikuwa na Mtume(saw) safarini, tukashukia Ghadiir Khum, ikanadiwa swala ya jamaa na pakasafishwa chini ya mti kwa ajili ya Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw), akaswali Adhuhuri. Kisha akasema, ‘Si munatambua kuwa mimi nina haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao?’ Wakajibu, ‘Ndio’. Akachukua mkono wa Aliy, akasema, ‘Ewe Mwenyezi Mungu! Ambaye mimi ni Bwana mtawali wake basi Aliy pia ni Bwana mtawali wake. Ewe Mwenyezi Mungu! Mfanye rafiki kipenzi yule aliyekuwa rafiki kipenzi chake na mfanye adui yule aliyemfanyia uadui’. Baadaye (Aliy) akakutana na Umar, akamwambia, ‘Hongera Ewe mtoto wa Abi Talib, umepambazukiwa na umechwewa ukiwa Bwana mtawali wa kila muumini mwanaume na muumini mwanamke’. (Imaam Ahmad)

Ucha Mungu wake na kuipa nyongo dunia.

Imepokewa na Imaam Ahmad kwamba Baytil maal ilijaa mali; dhahabu na fedha, Sayyidina Aliy(ra) akaigawa yote isibakie dirham wala diinar, kisha akaamuru ikanyunyiziwa maji (baytul maal) na akaswali humo rakaa mbili.

Imepokewa kwamba Sayyidna Mua'wiya bin Abi Sufyan alimwambia Bwana Dhwiraar bin Dhamra, “Nitajie wasifu wa Aliy”. Akamwambia, “Nisamehe”. Akamwambia, “Bali nitajie wasifu wake”. Akajibu tena, “Nisamehe”. Akamwambia, “Sikusamehi”. Akasema, “Ama ikiwa hivyo, basi wallahi hakika yeye alikuwa na upeo wa mbali, mwenye nguvu, azungumzaye kwa kituo na akihukumu kwa uadilifu. Ikichimbuka elimu pembezoni mwake na akitamka kwa hekima kwa pande zake zote. Anaionea upweke dunia na mapambo yake na akiliwazika na usiku na kiza chake. Wallahi alikuwa ni mwingi mno wa machozi, mwenye fikra nyoofu, moyo wake uko mkononi mwake (ameumiliki) na akizungumza na nafsi yake. Yakimpendeza katika mavazi yale mazito na katika chakula kile kilicho kizito. Wallahi alikuwa kama mwenzetu yeyote, tukimuuliza hutujibu na hutuandiliza kwa salamu tunapomuendea na hutujia tunapo mualika. Na sisi wallahi, pamoja na ukaribu wake kwetu hatumsemeshi kwa haiba na wala hatumuanzi kwa maneno kwa ajili ya utukufu wake. Na akitabasamu, basi ni mithili ya lulu zilizo tungwa. Akiwaadhimisha wana dini, na akiwapenda masikini, na wala hampi matumaini mwenye nguvu katika kuendelea na batili yake, na wala hamkatishi tamaa mnyonge kutopata uadilifu wake. Na ninashuhudia kwa Allah, nilipata kumuona akiwa katika mojawapo ya hali zake, usiku ukiwa umeshusha pazia zake na kuzizamisha nyota zake, katika mihrabu yake amezishika ndevu zake zikiwa zimeroa machozi, na akilia kilio cha mtu mwenye huzuni na kama nilimsikia akisema, ‘Ewe Dunia! Ewe Dunia! Je, wewe ndio umenipa mgongo mimi au umenitaka mimi?’ Li mbali mno hilo! Li mbali mno hilo! Umghuri mwingine asiye mimi kwani mimi nimekwisha kutaliki talaka tatu zisizo na rejea, kwa sababu umri wako ni mfupi na maisha yako ni duni na hatari yako ni kubwa. Ehee najutia uchache wa masurufu na ilhali safari ni ya mbali na upweke wa njiani

(kuelekea kwa Mola wangu)'". Anasema (Dhwiraar): Basi yakambubujika machozi Muawiya mpaka zikalovywa ndevu zake, basi hakuweza kuzifuta kwa mkono wa kanzu yake. Na watu wote wakaangusha kilio, halafu Muawiya akasema. "Allah amrehemu babie Hasan, wallahi alikuwa hivyo, basi je ikoje huzuni yako juu yake ewe Dhiwraar?" Akajibu: (Huzuni yangu ni kama) huzuni ya mtu aliye chinjwa mwanawe mbele yake, basi yasikatike machozi yake na wala isipoe huzuni yake."

Imepokewa na Bwana Aliy bin Aqmar kutoka kwa baba yake, kwamba alimwona (Sayyidna) Aliy, Mwenyezi Mungu amridhie, akiuza upanga sokoni, naye akisema, "Nani ataununua upanga huu? Namwapia yule aliyeipasua mbegu (kutoka ardhini, upanga huu) umefanya kazi kubwa ya kuuondoshea shida (kuuhami) uso wa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) na kama ningekuwa na thamani ya saruni (shuka ya kuvaa) nisingeuuza".

Imepokewa na Bwana Mujaahid kwamba alisema (Sayyidna) Aliy, "Nilishikwa na njaa kali sana siku moja nikiwa Madina, basi nikatoka kutafuta kazi katika nyanda za juu za Madina. Tahamaki huyo ni mwanamke mbele yangu akiwa amekusanya ndoo, basi nikajua anataka kuteka maji, nikamuendea nikamtekea kila ndoo kwa ujira wa tende, basi nikateka ndoo kumi na sita mpaka mikono yangu ikafanya malenge lenge. Kisha nikaleta maji na kuyamimina. Halafu nikamuendea, nikamuashiria mikono yangu (kutaka ujira), basi akanihesabia tende kumi na sita. Kisha nikamuendea Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) nikampasha khabari, naye akazila pamoja nami".

Alimlaumu mtu juu ya mavazi yake, akasema Sayyidina Aliy(ra), "muna nini na mavazi yangu? (Haya) yako mbali na kiburi na yako karibu na kufuata mfano wangu kila mwislamu".

Kumshirikisha Mtume(saw) kwenye wanyama wake wa sadaka.

Amesimulia Bwana Jabir bin Abdallah katika hadithi ndefu inayotaja matendo ya ibada ya Hijja, ".....Akachinja Mtume(saw) ngamia 63 kwa mkono wake na akampa Aliy akawachinja waliobaki na akamshirikisha katika wanyama wake wa sadaka. Kisha akaamrisha kichukuliwe kipande katika kila ngamia kitiwe kwenye chungu vikapikwa, wakala (yeye na Aliy) sehemu ya nyama yake na wakanywa mchuzi wake". (Muslim).

Yaliyojiri baina ya masahaba.

Fahamu kuwa inatubidi tuyanyamazie yaliyojiri baina ya masahaba, kwani Mtume(saw) amesema, "Wakitajwa masahaba wangu basi jizuieni (kuwataja kwa ubaya)".

Masahaba walifanya matendo yao kwa jitihada zao, kuna aliyepata ujira mara mbili kwa kuwa alisibu (alipatia) haki na yule aliye kosea alipata ujira mmoja, hakuna aliyepata madhambi. Na wale walio kosea kumepokewa kutubia kwao na kukubali makosa yao kama historia inavyo thibitisha hayo na hatuna haja ya kurefusha tukatoka nje ya makusudio ya kitabu.

Hapa tutanukuu baadhi ya maneno ya wanazuoni, amesema Imamu Ghazaaliy: "Ni haramu kwa mwenye kutoa waadhi na wengineo kuzungumzia kuuawa kwa Husein na hikaya yake na yaliyopita baina ya masahaba miongoni mwa ugomvi na uhasama, kwani hayo yataamsha chuki kwa baadhi ya masahaba na kuwatia makosani. Na ilhali wao ni viongozi wa dini, maimamu wamepokea kutoka kwao kwa mapokezi yaliyoungana (***riwaya***) na sisi tumepokea kutoka kwa maimamu kwa kufundishwa (***diraaya***), basi mwenye kuwatia makosa anajitia mwenyewe makosani katika nafsi yake na kwenye dini yake."

Amesema Imamu Ibn Salaah na Imamu Nawawy: "Masahaba wote ni waadilifu. Mtume(saw) alikuwa na masahaba 124,000 alipofariki na

Qur-ani na hadithi zinaeleza wazi uadilifu wao na utukufu wao. Na yaliyojiri baina yao kitabu hiki hakihimili kuyataja.”

Aliulizwa mmoja wao akasema: “Masahaba wa Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu ni macho na jicho haliguswi (kwa ndani) na katika ubora wa mwislamu ni kuacha yasiyomkhusu.” Mwengine aliulizwa: Akasoma aya ya Mwenyezi Mungu hao ni umma ulio pita…… (Baqarah:134 na 141) hadi mwisho wa aya.

Aliulizwa Bwana Maymuun bin Mahraan juu ya watu wa Siffiin, akasema: “Hizo ni damu ambazo Mwenyezi Mungu amesafisha mikono yangu nazo, basi sitaki kuharibu ulimi wangu kwa kuzitaja.” Amesema Imaam Abu Zur'a ambaye ni katika walimu wa Imaam Muslim mpokezi wa Hadithi: “Ukimwona mtu anavunja hadhi ya sahaba yeyote katika masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) basi ujue kuwa yeye ni mzandiki kwani Mtume(saw) ni haki, Qur-ani ni haki na aliyokuja nayo (Mtume(saw)) ni haki. Na yote hayo yamefikishwa kwetu na masahaba na mwenye kuwatia jeraha hakika ametaka kubatilisha Qur-ani na Sunna, basi lile jeraha (kosa) linamganda yeye na kuhukumiwa kwa uzandiki na upotofu na uongo na ufisadi ndio unao mlaiki (stahiki) kwa hakika.”

Maneno ya Aali Ba Alawiy kuhusu yaliyojiri baina ya masahaba

Habiib Abdillah Haddaad-Mwenyezi Mungu amrehemu-aliwataja Makhalifa waongofu akawasifia sana, kisha akasema: “Mwenye kuangalia kwa makini hali ya makhalifa na akawa yeye ana muono wa mbali na maarifa kamili, ataona kuwa njia ya Sayyidna Abu Bakr na Sayyidna Uthmaan ni moja, kwani imewatawala haya na huruma. Na tariqa ya Sayyidna Umar na ya Sayyidna Aliy ni moja, na wao wako kinyume na hayo miongoni mwa kutumia nguvu na ukali. Na alipo tawalishwa ukhalifa Sayyidna Aliy watu wa Basrah walimwuliza Al-Hasan Al-Basriy kwani walidhania kuwa atamtaja kwa ubaya kutokana na kupigana kwake vita na watu wa Basrah siku ya Jamal, akamtaja kwa wema kinyume na matarajio yao. Na watu wakweli kawaida wakimzungumzia mtu wakati hayupo kisha akatokea, maneno yao

huzidi, hawarai (yaani akiweko wamzungumzie kwa ubaya kinyume na akiwa mbele yao) tofauti na wanaochanganya (mambo-wasio wakweli). Na inatakiwa mtu asiingie sana kwenye kutalii vitabu ambavyo vinataja yaliyojiri kwa Sayyidna Aliy miongoni mwa vita kama Jamal na Siffiin na yasiyo kuwa hayo, kwani hupandikiza chuki nyoyoni, na hakuna budi atakutana na uchache wa hayo kwenye vitabu. Na mwanachuoni akipata mtihani kwa hayo na akahitaji kuangalia tuliyo yataja, basi aende mwendo wa kati wala asizame. Na hakika si jengine hata sisi tuliangalia kwenye hayo walivofika Zaydiyya pande hizi, wakatuuliza baadhi ya vitu na tukawajibu, na muulizaji alikuwa na insafu hata alimili kwa tuliyo yasema, na akatamani kukaa kwetu na alikuwa ni mwenye cheo kwenye Zaydiyya, na alikuwa amejitolea kuamrisha na kukataza. Wakatuambia kwanini mumemtanguliza mwengine juu ya baba yenu Aliy bin Abi Talib, tukawaambia, yeye ndiye aliye mtanguliza na kumweka mbele kuliko nafsi yake, na sisi tukamtanguliza na tukampa utukufu kwa kufuata mwenendo wake. Wakasema hiyo ilikuwa *taqiyya* (kuruhusiwa kusema uongo kwa sababu maalum-katika misingi ya kishia), tukasema hakika sisi si mfano wake kwenye nguvu, ushujaa na mamlaka yake ikiwa amefanya yeye taqiyya, basi ni nani mwenye nguvu na ushujaa kuliko yeye au mfano wake? Na kama taqiyya ilivyo mpa wasaa yeye basi na sisi pia inatupa wasaa."

Habiib Abdillah Haddaad-Mwenyezi Mungu amrehemu-aliwataja Raafidhii (shia), akasema: "Wao ni watu wa baatili hawatajwi wala kutegemewa kwenye chochote, hata kama wana haki kidogo wameichanganya na batili kiasi ambacho (haki) ikawa haina mabaki. Ni kama aliyeiweka jibini (cheese) kwenye kinyesi, na inatakiwa mtu wa haki awaachilie mbali, na akiona wana chochote cha haki asikikatae, ili wasimtolee hoja kwa kukataa kwake ile haki, na pia wakachukua hiyo kuwa ni dalili (hoja) kuwa waliyo nayo yote ni haki na yeye anaikataa. Na itikadi yao kuwa Sayyidna Aliy anastahiki zaidi ukhalifa, kwani yeye angepata ukhalifa baada ya Mtume(saw) angeyapata yale yale yaliyo tokea kwenye ukhalifa wake (mfano wa kushindana naye, kutofautiana naye na mengine, kwa kuwa ameandikiwa hayo yatokee kwake na amesha hukumiwa na Mwenyezi Mungu tangu mwanzo).

Lakini Sayyidna Abu Bakr watu walimridhia na miongoni mwao akiwa Sayyidna Aliy, kwa kutangulia kwake na kupata aliyo yapata alipo kuwa ndani ya pango na Mtume(saw) na kwa kuwa yeye aliwaswalisha watu kwenye uhai wake (Mtume)-rehema na amani zimshukie. Na yeye kwa jitihada yake alimuusia Sayyidna Umar, na Sayyidna Umar akajaalia kwenye watu wa Shuura, wamchague katika watu sita na yeye Sayyidna Aliy alikuwa kati yao, na inatosha utukufu na sifa ya upekee pamoja na kuchelewa ukhalifa wake. Hiyo inakuwa kwake ni ziyada ya utukufu, alikuwa Mtume(saw) akimtuma kwenye vita, husema: **"Mola wangu Mlezi! Usiniache peke yangu".** (Anbiyaa:89) Na wanayoyataja Raafidhiiy kwa kumtusi kuwa amenyamazia baadhi ya vitu kwa ajili ya taqiyya, basi kunyamaza kwake hakukuwa kwa woga, bali ilikuwa kuwabakisha Waislamu na kuchukia kuwakata mapande Waislamu". Na akazungumza zaidi na kuwasema kwa ubaya pamoja na maibadhi, akasema: "Maibadhi na Naasibah tunawachukia zaidi kuliko mashia, kwani wao wanawachukia Ahlil bayti. Baadhi ya shia katika watu wa Madina walimuuliza sharifu mmoja wa Aali Ba Alawiy, unasemaje kuhusiana shia na maibadhi? Akasema: Ni kinyesi kilicho gawika sehemu mbili. Na tulimuona mwaka tulio hiji sharifu raafidhii akiwa amesimama kwa Mtume(saw) akipiga kelele na kusema: Ewe Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu! Wametudhulumu na wakatufanyia. Na akiomba insafu sana, kutahamaki anataja vitu ambavyo vimepita muda mkubwa (yaani ambavyo vimesha tokea miaka chungu nzima iliyo pita), kama yaliyo fanywa kwa Sayyidna Aliy na mtoto wake Husain. Tukamwonea ajabu. Na katika jumla ya tabia ya Raafidha ni wazimu, yanayo julishwa kwa kisa cha mtu kama huyu, hata wakasema baadhi ya wanavyuoni: "Lau Raafidha wangekuwa ndege wangekuwa tumbusi (ndege wala mizoga – vulture) na kama wangekuwa wanyama wangekuwa punda (wabeba mizigo)". Na akazungumza sana kwenye hayo.

Habiib Aliy Habashy anasema: "Mimi nataraji kila dhambi itasamehewa na Mwenyezi Mungu na kufutwa ila kuwatukana masahaba na kuwatukana mawalii."

Ilisomwa Sahiih Bukhariy kwenye msikiti wa Ba Alawiy na msimamizi alikuwa Habiib Abdul Rahman Mash-hoor, na katika walio hudhuria alikuwa Sayyid Hasan bin Alawiy bin Shihaabud-Diin, baadaye Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas akaalikwa chakula kwa Sayyid Hasan, akasema Sayyid Hasan kumwambia Habiib Ahmad: Ewe Sayyidiy Ahmad umewasikia hawa? – akimaanisha wanao soma Bukhariy – wanamfanya Sayyid Muawiya na wanamwombea radhi. Akasema Habiib Ahmad: Sote tunamfanya sayyid na tunamwombea radhi, je halijakufikia neno lake (Mtume(saw)): "Ewe Muawiya! Utatawala amri (uongozi) ya umma huu, basi uwafanyie huruma", na akamwombea kwa neno lake: "Ewe Mwenyezi Mungu! Mjaalie kuwa ni mwenye kuongoza na mwenye uongofu". Na akamwombea pia kwa neno lake: "Ewe Mwenyezi Mungu! Mfundishe kitabu (Qur-ani) na hesabu na umlinde na adhabu, na ummakinishe (umthibitishe) kwenye miji", akauliza Sayyid Hasan: Hizi hadithi zimethibiti kwenu? Akasema (Habiib Ahmad): Ndio. Akasema (Sayyid Hasan): Zikiwa zimethibiti kwenu na kwangu pia zimethibiti.”

Habiib Alawiy bin Shihaab amesema: “Msiba mkubwa ni mtu kuwazungumzia masahaba na kuwatia makosa masahaba wa Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu, nani wewe (wa kufanya hivyo), watu wamelelewa na Mtume(saw) mwenyewe (ama wewe umelelewa na nani?) Baadhi ya watu wanasema: Ammi Alawiy (yaani mwenyewe) anamwombea radhi Mua'wiya, vipi tusimwombee radhi na yeye amekaa mbele ya Muhammad bin Abdillah, na akaswali nyuma ya Muhammad, na yaliyo jiri baina yake na baba yetu Aliy inatuhusu nini? (kisha akanukuu ubeti wa Zubad):

Na yaliyo jiri baina ya masahaba tunanyamaza,
na ujira wa jitihada tunauthibitisha.

Mwenye kupatia ana ujira mara mbili na mwenye kukosea anapata ujira mmoja, (kisha akasoma aya): “**huo ni umma umepita utapata uliyo yachuma na nyie mutapata muliyo yachuma**”. Na ilikuwa amali ya wazee wetu na salaf wetu hawawasemi vibaya masahaba wa Mtume(saw) … lakini hii ni kutokana na ushakii (uovu wa nafsi na matendo) na kunyimwa kheri (kwa hao wanao watukana masahaba). Wamesema (yaani Salaf): Mwenye kuwazungumzia kwa ubaya

masahaba anafariki ugenini. Mwenyezi Mungu atuhifadhi, asije kufa mmoja wetu juu ya mwisho mbaya."

Amesema Sheikh Abubakr Al-Adany bin Abdallah Aydaroos, "Namwapia Mwenyezi Mungu Mtukufu, lau Mwenyezi Mungu angemhuisha baba yangu Sheikh Abdallah na mwalimu wangu Sheikh Sa'd wakanitajia kuwa Sayyidna Aliy ni bora kwa Mwenyezi Mungu kuliko Sayyidna Abubakr Mwenyezi Mungu awaridhie wote wawili, nisingerudi nyuma na kuacha itikadi ya Ahlil Sunna na Jamaa kwamba Abubakr, Umar na Uthman ni bora kuliko Aliy, Mwenyezi Mungu awaridhie wote"

Maneno ya Sayyidna Aliy kuhusu ukhalifa

Sayyidna Aliy(ra) alipofika Basra, walimwendea Abdallah bin Al-Karaai na Qabas bin Ubaad wakamwambia, "Je, unaweza kutufahamisha kuhusu mwendo wako unaoufuata?. Mtu anatawalia uongozi na ilhali watu wanapigana wao kwa wao. Je ni ahadi (wasiya) wa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) kwako, tuzungumzie, kwani wewe ni mkubaliwa na muaminiwa kwa uliyoyasikia." Akajibu Sayyidna Aliy, "Ama mimi kwamba nina usia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) katika hilo, hapana (sina). Wallahi, nijapokuwa mimi ni wa mwanzo aliyemsadiki, siwi wa mwanzo kumuongopea, ningelikuwa nina ahadi ya Mtume(saw) katika hilo, nisingeliwaacha ndugu wa Taim bin Murrah (yaani Abu Bakr) na Umar bin Khattaab, wasimame juu ya mimbari yake. Ningeliwapiga vita kwa mkono wangu hata kama sikupata (silaha) ila kishali changu hiki. Lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) hakuuawa na wala hakufa ghafla, aliugua kwa siku kadhaa; akijiwa na muadhini akimuadhinia swala, naye akimuamrisha Abubakr kuwaswalisha watu. (Akiyafanya yote hayo) naye akiiona (akiijua) daraja yangu. Mmoja kati ya wakeze alitaka kuiondosha nafasi hiyo kwa Abubakar, Mtume(saw) akakataa, akaghadhibika, na akasema, 'Hakika nyie ni (kama) watu wa Yusuf (mlio taka kumfitinisha)! Hebu muamrisheni Abubakar awaswalishe watu'. Mwenyezi Mungu alipomfisha Mtume wake(saw) tuliyaangalia mambo yetu (ya uongozi), basi tukamchagua kwa ajili ya (kutuongoza

katika) dunia yetu yule ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) alimridhia kwa (kutuongoza katika) dini yetu. Na swala ndio nembo kubwa ya Uislamu na ndio nguzo ya dini. Basi tukampa kiapo cha usikivu na utii Abubakar naye akawa ni mstahiki wa hilo. Hawakukhitalifiana juu yake watu wawili miongoni mwetu, na wala hatukushuhudiana wenyewe kwa wenyewe (kwenda kinyume naye), na wala hakumuondolea dhima yeyote. Basi na mimi nikamtekelezea Abubakar haki yake na nikaukiri utii wake na nikapigana jihadi pamoja nae nikiwa mmoja wa jeshi lake. Na nilikuwa nikitwaa pale anipapo (kitu katika Baytul-maal), na ninaenda vitani pale aniamrishapo, na ninapiga mbele yake haddi (adhabu ya makosa ya jinai) kwa bakora yangu. Alipofishwa, uongozi ukatwaliwa na Umar bin Al-Khattaab naye akafuata sera za mtangulizi wake na mwenendo wake aujuao. Basi tukampa kiapo cha utii na usikivu Umar na hapana yeyote ambaye hakula kiapo. Hawakukhitalifiana juu yake watu wawili miongoni mwetu na wala hatukushuhudiana wenyewe kwa wenyewe na wala hakumuondolea dhima yeyote. Basi na mimi nikamtekelezea Umar haki yake, na nikaukiri utii wake, na nikapigana jihadi pamoja nae nikiwa mmoja wa jeshi lake. Na nilikuwa nikitwaa pale anipapo (kitu katika Baytul-maal), na nikienda vitani pale aniamrishapo, na ninapiga mbele yake haddi (adhabu ya makosa ya jinai) kwa bakora yangu. Na alipofishwa, nikaukumbuka nafsini mwangu utangu wangu (katika Uislamu), udugu wangu kwa Mtume(saw), na ubora wangu. Nikadhania kwamba sitaukosa huo (ukhalifa). Lakini nilichelea Khalifa wa baada yake (Umar) asije kutenda dhambi akakutana nayo kaburini mwake, na akaitia mashakani nafsi yake na watoto wake kwa sababu ya (dhambi) hiyo. Na lau yangelikuwa ni mapenzi yake (Umar) basi angelimpendelea mwanawe. Lakini akajiweka mbali na hilo, na kuliweka mikononi mwa kikundi cha watu sita katika Makureishi nami nikiwa mmoja wao. Kilipokutana kikundi hicho, nikakumbuka nafsini mwangu udugu wangu kwa Mtume(saw) na utangu wangu (katika Uislamu), nami nikidhania kuwa hawatoniweka kando. Abdurahman bin Auf akaanza kuchukua ahadi zetu ya kwamba tutaitii na kuisikia amri ya yule ambaye Allah Atamtukuza na Atamtawalisha uongozi wetu. Kisha akapiga kwa mkono wake juu ya mkono wa Uthman akala kiapo cha utii kwake. Nami nikaangalia shauri langu. Tahamaki utii

wangu umekwisha kitangulia kiapo changu cha utii na ahadi yangu imekwisha twaliwa na mtu mwingine. Basi tukala kiapo cha usikivu na utii kwa Uthman. Basi na mimi nikamtekelezea Uthman haki yake na nikaukiri utii wake na nikapigana jihadi pamoja nae nikiwa mmoja wa jeshi lake. Nilikuwa nikitwaa pale anipapo (kitu katika Baytul-maal), na nikienda vitani pale aniamrishapo, na ninapiga mbele yake haddi (adhabu ya makosa ya jinai) kwa bakora yangu. Na alipofishwa Uthman, nikaangalia shauri langu, tahamaki wale makhalifa wawili walioutwaa ukhalifa kwa usia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) (kuwausia wao) kwa swala, wameshakwenda zao. Na huyu ambaye aliyepata ahadi yangu ya kweli naye amekwishapatwa (na mauti). Basi hapo ndipo wakanipa kiapo cha usikivu na utii watu wa Haramain (Makka na Madina) na watu wa miji miwili hii, (yaani Basrah na Koufa)". Imepokewa na Abu Ahmad Hamza bin Al-Haarith, Abul Fadhl bin Khairoon, Daaruqutniy, Ibn Asaakir, Dhahabiy na wengine, pia imepokewa na Ibn Al-Samaan kwenye *Muwaafaqah*.

Kuuawa kwake:

Sayyidna Aliy(ra) alikuwa akijua kuwa atauawa, kwani alishaambiwa na Mtume(saw) kuwa atauawa hadi damu za shingo yake zitaingia kwenye ndevu zake. Na katika baadhi ya riwaya mpaka akimjua nani atamwua.

Imepokewa kwamba alikuja mtu kutoka Muraad (mji aliotoka Ibn Muljim) akamwambia akiwa msikitini, "Jilinde, kwani kuna watu wa Muraad wanataka kukuua". Sayyidina Aliy(ra) akasema, "Kila mtu ana malaika wawili wanaomhifadhi kwa jambo ambalo halijakadiriwa kumfika. Basi ikija Qadari huacha baina ya yule mtu na Qadar. Hakika ajali ni ngome madhubuti".

Alipigwa panga na Ibn Muljim alipokuwa anatoka kwa ajili ya swala ya Alfajiri akiwa Kuufa, siku ya Ijumaa tarehe 17 Ramadhan mwaka wa 40 tangu Hijra. Akabakia Ijumaa na Jumamosi na kufariki Jumapili. Akaoshwa na watoto wake Bwana Hasan na Bwana Husain na Bwana

Abdallah bin Ja'afar, na akaswaliwa na Bwana Hasan. Alifariki Sayyidna Aliy akiwa na umri wa miaka 63.

Wasiya wake wa mwisho.

"Enyi wana wa Abdil-Mutwalib! Msizimwage bure damu za Waislamu, mkisema ameuawa Amirul-Muuminina. Ehee zindukeni! Msipigane, msipigane kwa ajili yangu ila na yule muuaji wangu tu! Angalieni, mimi nikifa kutokana na pigo lake hili, basi nanyi mpigeni pigo moja na wala msimkate-kate viungo vyake, kwani hakika mimi nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) akisema, "Jiepusheni na kukata-kata viungo ijapo kuwa ni vya mbwa kichaa".

Baadhi ya maneno yake ya Hikma.

Baadhi ya maneno yaliyochukuliwa kutoka katika mazungumzo na hotuba zake ni kama ifuatavyo:-

Imepokewa kutoka kwa Abdi kheir, kutoka kwa Imamu Aliy, "Si kheri kukithiri mali yako na watoto wako, lakini kheri ni kukithiri amali (matendo mema) yako na kuwa mkubwa upole wako. Na Dunia haina kheri ila ni kwa mmoja wa watu wawili: mtu aliye tenda dhambi naye akaidiriki dhambi hiyo kwa kuleta toba. Au mtu aliye yaendea haraka mambo ya kheri kuyatenda na wala hasemi ametenda katika ucha Mungu na ni vipi aseme ambalo halijapokelewa".

Na imepokewa kutoka kwa Muhajir bin Amir amesema, "Alisema Aliy bin Abi Talib, Hakika katika jumla ya mambo ninayoyachelea (kukufikeni) ni kufuata matamanio na mipango mingi. Basi kufuata matamanio kunazuia kuifuata haki, na ama mipango mingi, huko kunasahaulisha Akhera. Ehee zindukeni! Hakika Dunia imekwisha funga safari ikirudi nyuma. Ehee zindukeni! Na hakika Akhera imekwisha funga safari ikija; na kila mojawapo kati ya mbili hizo (Dunia na Akhera) ina watu wake. Basi nyinyi kuweni miongoni mwa watu wa Akhera na wala msiwe miongoni mwa watu wa Dunia".

Imepokewa kutoka kwa Hasan, kuwa Sayyidina Aliy(ra) amesema, “Kheri na furaha ni yake mja mwenye kujilaumu (kwa makosa yake), aliyewajua watu na watu wasimjue yeye. Hao ndio taa za uwongofu ambao Mwenyezi Mungu huwafichulia fitina zote zilizojificha, Mwenyezi Mungu atawaingiza kwenye rehema zake. Wao si wenye kufichua siri za watu na wala wenye nyoyo kukutavu, wafanyao riya”.

Na imepokewa kutoka kwa Aaswim bin Dhwamrah, kutoka kwa Aliy(ra), “Tanabahini! Faqihi (mwanachuoni wa kweli) ni yule ambaye hawakatishi watu tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu na wala hawapi rukhsa ya kufanya maasi ya Mwenyezi Mungu na wala haiachi Qur-ani kwa kuichukia na kufuata kisicho Qur-ani. Na wala hakuna kheri katika ibada isiyo na elimu (ya namna ya kuitenda) ndani yake; na wala hakuna kheri katika elimu isiyo na ufahamu ndani yake; na wala hakuna kheri katika kisomo kisicho na mazingatio ndani yake”.

Imepokewa kutoka kwa Sha’abiy ya kwamba Aliy(ra) alisema, “Enyi watu! Yatwaeni kutoka kwangu maneno haya, lau nyinyi mtawaendesha shoti wanyama kuyatafuta mpaka mkawachosha, hamtayapata maneno kama haya, ‘Mja asimtaraji na kumtegemea ila Mola Mlezi wake na wala asiichelee (asiigopee) ila dhambi yake. Na wala asione haya kujifunza kama hajui na wala asione haya atakapoulizwa asilolijua kusema sijui. Na jueni ya kwamba subira katika imani iko katika daraja ya kichwa kwenye mwili na wala hapana kheri kwa mwili usio na kichwa”.

Na imepokewa kutoka kwa Abdillah bin Abbas kwamba yeye amesema, “Sikupata kunufaika na maneno ya yeyote baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) kama kunufaika kwangu na waraka nilioandikiwa na Aliy bin Abi Twalib, kwani yeye aliniandikia, ‘Amma baad, hakika mja huchukizwa kupitwa na lile ambalo hakuwa alipate na kunamfurahisha kulipata lile ambalo halikuwa limpite. Basi na iwe furaha yako ni kwa lile ulilolipata katika mambo ya Akhera yako. Na iwe huzuni na majuto yako kwa lile lililokupita katika hayo. Na ulilolipata katika Dunia yako, basi usikithirishe mno kulifurahikia, na

ulilolikosa katika hiyo (Dunia), basi usilihuzunikie mno. Hima yako iwe ni (kuyahangaikia) yaliyo baada ya kufa".

"Elimu ni bora kuliko mali. Elimu inakulinda wewe na wewe unailinda mali. Elimu inakua kwa kuitumia, na mali inapungua kwa kuitumia. Elimu ni mtawala, na mali ni mtawaliwa. Sanaa ya mali huondoka kwa kuondoka kwake (hiyo mali). Mapenzi ya mwenye elimu ni deni linalolipwa na elimu inayomvika utii katika maisha yake, na utajo mwema baada ya kufa kwake. Wamekufa walimbikiza mali ilhali wangali hai; na wenye elimu ni wenye kusalia muda wa kusalia kwa ulimwengu, dhati zao tu ndizo hazipo lakini mifano yao imo mioyoni mwa watu".

"Elimu inakufa kwa kufa mchukuzi wake (mwanachuoni). Ewe Mola wa haki! Hapana, Dunia haitokosa kuwa na aliyesimama kwa niaba ya Mwenyezi Mungu kwa hoja ili zisibatilishwe hoja za Mwenyezi Mungu na maelezo yake ya wazi. (Watu wa namna hiyo) hao ni wachache kiidadi, watukufu mbele ya Mwenyezi Mungu. Kupitia kwao Mwenyezi Mungu huzihifadhi hoja zake mpaka wazifikishe kwa wenzao na wazipande nyoyoni mwa walio kama wao. Elimu ikawafunulia uhakika wa mambo. Basi wakawa laini pale walipokuwa wagumu watanuao katika maisha, na wakaliwazika na yale yawatiao upweke watu majaahili".

"Ama wale wenye kusimama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa kupitia hoja zake, hao ni makhalifa wa Mtume wake kwa umati wake. Kwani wao kutokana na ukamilifu na nguvu ya elimu yao, elimu hiyo imewapenyeza kwenye uhakika/uhalisia wa mambo, ikawafunulia, kwa ajili hiyo, wakaona kwa macho yao ya moyoni yale yaliyofichikana kwenye uoni wa watu majaahili. Na wakasuhubiana na Dunia kwa viwiliwili vyao. Roho zao zikijiangika na mahala patukufu mno pa juu kabisa. Kwa hivyo basi, wao wako pamoja na watu kwa viwiliwili vyao, ilhali roho zao zikiwa pamoja na Mola wao Mlezi zikimsabihi pembezoni mwa Arshi pamoja na zile roho tukufu za juu, kama alivyosema Bwana na Kiongozi wao, Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu-Rehema na Amani zimshukie, "Hakika mimi si kama nyinyi,

hakika mimi ninakesha nikiwa na Mlishaji anaye nilisha na Mnyweshaji anaye ninywesha".

Imepokewa kutoka kwa Abi Araakah amesema, "Niliswali swala ya Alfajiri pamoja na Aliy(ra) alipotoa salamu, alitema kuliani kwake kisha akakaa akiwa na huzuni hata jua lilipokipiga kiambaza cha msikiti kiasi cha ute wa fumo akageuza mkono wake na akasema, 'Hakika niliwaona masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) basi leo sioni kitu kinacho fanana nao. Hakika walikuwa wakipambazukiwa hali ya kuwa watim-tim wa nywele, pekupeku, wenye mavumbi machoni kwao, kukiwa na mfano wa kupiga magoti kwa mbuzi. Kwa yakini wamekesha wakimsujudia Allah na wakisimama wakikisoma kitabu cha Allah. Wakivipumzisha vipaji vya nyuso zao (kutokana na kusujudu sana) na miguu yao (kutokana na kusimama muda mrefu). Basi wanapopambazukiwa, wakamdhukuru Mwenyezi Mungu huyumba-yumba kama unavyo yumba-yumba mti katika siku yenye upepo mkali na macho yao yakafurika machozi furi furi mpaka zikalowa nguo zao. Wallah watu leo wamo mghafalani". Kisha akainuka, basi hakupata tena kuonekana akicheka kwa uwazi mpaka akapigwa na Ibn Muljim.

Sayyidna Hasan bin Aliy.

Alizaliwa katikati ya mwezi wa Ramadhan, mwaka wa tatu baada ya Hijra. Mtume(saw) alimwadhinia sikioni mwake na akamfanyia aqiqa kwa mbuzi mmoja; katika riwaya nyengine mbuzi wawili. Alimwamrisha Bibi Fatima apime uzani wa nywele za kichwa chake atoe sadaka ya fedha kwa uzani wa nywele hizo. Imepokewa katika Bukhari na Muslim kwamba Mtume(saw) alimbeba begani naye akisema, “Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nampenda basi na wewe mpende”.

Imepokewa na Imaam Bukhariy, kwamba Sahaba Uqbah bin Harith amesema, “Nilitoka na Abu Bakr kwa ajili ya swala ya Alasiri baada ya kufariki kwa Mtume(saw) kwa masiku na Aliy akiwa anatembea pembezoni mwake. Akamkuta Hasan bin Aliy akicheza na watoto wenzake, akambeba shingoni na huku akiwaambia, ‘Nakufidia kwa wazazi wangu. Hakika unafanana na Mtume(saw) na hufanani na Aliy’, huku Aliy(ra) akicheka”.

Imepokewa pia na Imaam Bukhariy, kwamba Sahaba Abu Bakrata amesema, “Nilimwona Mtume(saw) juu ya mimbari na Hasan bin Aliy akiwa pembezoni mwake, akiwaelekea watu na kisha akimwelekea yeye (Hasan) na huku akisema, ‘Hakika mtoto wangu huyu ni Sayyid, (Bwana) na nataraji Mwenyezi Mungu Mshindi Mtukuka atasuluhisha kwaye baina ya vikundi viwili vikubwa vya Waislamu’”.

Jambo hili lilitokea kama alivyolibashiri Mtume(saw). Alipouawa baba yake [yaani Sayyidna Aliy(ra)], alitoka na jeshi la watu 40,000 ambao walimpa ahadi ya utii kama walivyompa ahadi baba yake. Lilipo karibiana jeshi lake na jeshi la Bwana Muawiya(ra) katika sehemu inayoitwa Maskan, akaangalia Bwana Hasan kwa jicho la hekima na akaona kuwa vita havitakwisha ila watauawa Waislamu wengi. Yote hayo yatatokea kwa sababu yao wao wawili. Akamwandikia Bwana Mua'wiya(ra) kuwa anakubali suluhu ya kumwachia yeye utawala kwa sharti la kutomuadhibu yeyote aliyekuwa kinyume naye wakati wa baba yake miongoni mwa watu wa Iraq, Hijaz na Madina. Akakubali Bwana Mua'wiya ila watu 10. Sayyidina Hasan(ra) akamwambia asichukue

kisasi kwa yeyote, ama sivyo hatomwachia utawala. Bwana Mua'wiya(ra) akamtumia karatasi nyeupe na kumwambia aandike anachotaka. Wakakubaliana. Na Bwana Hasan akaachia ukhalifa kwa ajili ya kuhifadhi damu ya Waislamu isimwagike. Wakawa watu wake wanamtukana na kumwambia, “Ewe uliyewaaibisha Waislamu”. Naye akiwajibu, “Afadhali aibu kuliko moto”. Wengine wakimwambia, “Ewe uliyewadhalilisha Waislamu”. Naye akiwajibu, “Msiseme hayo, mimi sijawadhalilisha, lakini nimechukia kuwapiganisha vita kwa ajili ya kugombea ufalme”.

Imepokewa na Muhammad bin Aliy, kwamba Hasan amesema, “Mimi naona haya kukutana na Mwenyezi Mungu nikiwa sijatembea kwa miguu kwenda kwenye nyumba yake”. Na imepokewa kutoka kwa Aliy bin Zayd, “Alihiji Hasan hijja 15 kwa kutembea, na ngamia wakivutwa mbele yake. Alitoa mara mbili kwenye mali yake yote sadaka; na mara tatu aligawana na Mwenyezi Mungu kwa kutoa nusu ya mali yake, hata alikuwa akitoa pea za viatu na kubakia na pea moja.

Kufariki kwake.

Alikufa Sayyidina Hasan(ra) kwa kupewa sumu. Aliumwa siku arobaini (40). Katika maradhi ya kufa alisema, “Hakika nimepewa sumu mara nyingi, lakini sikupewa mfano wa mara hii”. Hata mdogo wake Sayyidina Husain(ra) alimwuliza, “Unamtuhumu nani?” Akamwambia, “Kwa nini unaniuliza? Unataka kumwua?” Akasema, “Ndio”. Akamwambia, “Akiwa ninaye mdhania, basi Mwenyezi Mungu ndiye Mkali mno wa kuadhibu na kutesa. Na akiwa siye, basi sitaki auawe mtu asiye na kosa kwa ajili yangu”. Kisha ikapita hukumu ya Mwenyezi Mungu, akafa. Sayyidina Hasan(ra) amefariki mwezi 5, mfunguo sita mwaka wa 50 na yasemekana ni mwaka wa 49 na akazikwa Baqii-Allah amuwiye radhi. Alifariki akiwa na miaka 47, alikaa na Mtume(saw) miaka 7, na alikaa na baba yake miaka 30. Aliendelea kuishi miaka kumi baada ya kufariki baba yake.

Wasiya wake kwa ndugu yake Bwana Husain.

Imepokewa na Abu Umar kwamba Sayyidina Hasan(ra) alipokaribia kufa alimwambia ndugu yake Husain, "Ewe ndugu yangu! Hakika alipofishwa Mtume(saw), baba yako aliutamani ukhalifa na akataraji awe khalifa wake. Mwenyezi Mungu akamuondoshea na akautawalia Abubakar. Kifo kilipo mjia Abubakar(ra) aliurondea pia, ukaondoshwa kwake akapewa Umar(ra). Umar(ra) alipofariki akauweka (ukhalifa) kuwa ni shura baina ya watu sita naye akiwa ni mmoja wao; na hakuwa na shaka yoyote kuwa ataukosa. Ukapelekwa kwa Uthman(ra). Alipokufa Uthman akapewa kiapo cha utii kwa huo (ukhalifa). Kisha akanyang'anywa mpaka akachomoa panga kuutafuta. Basi halikumuongokea lolote katika huo na hakika mimi wallah sioni kwamba Mwenyezi Mungu atatukusanyia pamoja sisi Ahlu Bayt utume na ukhalifa. Basi sijui ni kipi walichokughuri nacho watu masafihi wa Koufa mpaka wakaweza kukutoa."

Kizazi cha Sayyidna Hasan

Kizazi cha Sayyidna Hasan kiliendelezwa na watoto wake wawili, Bwana Zayd na Bwana Hasan Muthanna (yaani Hasan bin Hasan). Bwana Zayd bin Hasan alipata kizazi kikubwa, na katika kizazi chake ni wafalme wa Tabrastan.

Ama Bwana Hasan Muthanna, alipata mtoto akiitwa Abdallah Al-Mahdh aliyepata watoto watano walioenea sehemu mbali mbali za dunia, nao ni mabwana Muhammad Nafsul Zakiyya, Ibrahim, Idris, Yahya na Musa Al-Juuni.

Bwana Hasan Muthanna

Bwana huyu alikuwa ni msimamizi wa wasiya wa baba yake, na mwenye kusimamia sadaka za Sayyidna Aliy bin Abi Talib katika zama zake. Imepokewa na Al-Haafidh Ibn Mundhir kwamba Hasan (Muthanna) bin Al-Hasan (As-sibtw) bin Aliy bin Abi Taalib alimwambia mtu mmoja katika Maraafidha: "Wallah, lau Mwenyezi Mungu atatumakinisha (atatupa ushindi) juu yenu, basi bila ya shaka

tungeliikata mikono na miguu yenu, kisha tusingeli ikubali toba yenu". Mtu mmoja akasema, "Kwa nini hamtaikubali toba yao?" Akajibu, "Sisi tunawajua vizuri zaidi hawa kuliko nyinyi. Hakika hawa wakitaka watakuambieni kweli, na wakitaka watakuongopeeni, na watadai ya kwamba hilo linawaongokea katika taqiya. Ee ole wako! Hakika taqiya ni mlango wa rukhsa kwa muislamu pale anaposongeka kufanya hivyo na akauchelea uovu wa kiongozi. Hapo ndipo atampa kinyume na yaliyo ndani ya nafsi yake akiilinda dhima ya Mwenyezi Mungu na wala taqiya sio mlango wa fadhila. Hakika si vinginevyo, ubora katika kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu ni kusema kweli. Na namuapia Mwenyezi Mungu, taqiyya haikufikishwa kuwekwa mahala ambapo mja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu huwapotezea waja wa Mwenyezi Mungu"

Imenukuliwa kutoka kwa Al-Haafidh Ibn Asaakir kutoka kwa Al-Haafidh Al-Baihaqiy hadithi ya Fudhail bin Marzuuq ya kwamba Al-Hasan (Al-Muthanaa) bin Al-Hasan bin Aliy bin Abi Taalib, aliulizwa akaambiwa, "Hivi Mtume(saw) hakusema, **"Ambaye mimi ni Mtawala wake, basi na Aliy ni mtawala wake"?** Akajibu, "Ndivyo hivyo hivyo, lakini wallahi, Mtume(saw) hakukusudia kwa kauli yake hiyo uongozi na utawala. Na lau angeli-likusudia hilo, basi angeliwaambia wazi hilo, kwani Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu alikuwa ni mtoa nasaha mno kwa Waislamu. Na lau suala lingelikuwa kama lisemwavyo, basi Mtume(saw) angelisema, "Enyi watu! Huyu (Aliy) ndiye mtawala na msimamizi wa mambo yenu baada yangu, basi msikilizeni na mtiini". Wallahi, lau ingelikuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamemteua Aliy kwa jambo hili (la uongozi) na kumfanya kuwa ndiye msimamizi wa masuala ya waislamu baada yake, kisha Aliy akaiacha amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume(saw) wake, basi angelikuwa Aliy ndiye mtu wa mwanzo kuiacha amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume(saw)."

Bwana Abdallah Al-Mahdh:
Aliitwa Al-Mahdh na Al-Kaamil kwa sababu alikuwa ni wa mwanzo kukusanya nasabu zote mbili za Sayyidna Hasan na Sayyidna Husain.

Baba yake ni Sayyidina Hassan bin Hassan bin Aliy bin Abi Talib(ra), na mama yake ni Bibi Fatima bint Husain bin Aliy. Na alikuwa kiongozi wa Ahlil Bayti wakati wake.

Imepokewa kuwa Sayyidina Abdulla Al-Mahdh(ra) aliulizwa, "Je unapangusa khofu mbili?" Akajibu, "Napangusa juu yake kwani Umar alikuwa akipangusa". Yule muulizaji akasema, "Mimi nakuuliza wewe, unapangusa?" Akamwambia, "Hiyo ni ajizi kutoka kwako, nakwambia kuhusu Umar unaniuliza rai yangu? Basi Umar ni bora kuliko mimi na bora kuliko ujazo wa dunia wa walio kama mimi". Akaambiwa hii ni taqiyya. Akasema, "Sisi tuko baina ya kaburi la Mtume(saw) na mimbari (yake). Ewe Mwenyezi Mungu hili ndilo neno langu katika uficho na uwazi, basi nisisingiziwe baada yangu. Nani huyu mwenye kusema kuwa Aliy alikuwa amelazimishwa (na kuzidiwa nguvu)? Na kwamba Mtume(saw) alimwamrisha kitu asitekeleze? Hii inatosha kuwa ni uzushi na mapungufu".

Bwana Muhammad Nafsul Zakiyya

Huyu ni mtoto wa Sayyidina Abdalla Al-Mahdh(ra); yeye ni Muhammad bin Abdalla bin Hasan bin Hasan bin Aliy bin Abi Talib. Imepokewa na Imaam Daaruqutniy, kuwa aliulizwa Muhammad mwenye laqabu ya Nafsul Zakiyya juu ya Sheikhain (yaani Abu Bakr na Umar) akasema, "Kwangu mimi wao ni bora kuliko Aliy".

Bwana huyu alipewa kiapo cha utii na Ahlil bayti baada ya kukutana Madina na kumchagua awe Imamu baada ya kudhoofika utawala wa Bani Umayya; hata maimamu Abu Hanifa na Malik nao pia walimkubali, na ndiyo sababu ya wao kupata mitihani kwa mtawala wa wakati huo Abi Ja'afar Al-Mansur.

Bwana huyu alimpeleka Basrah ndugu yake Bwana Ibrahim, na Bwana Idriis akampeleka Maghrib. Bwana Ibrahim akauawa. Ama Bwana Idriis akakubaliwa na watu wa Maghrib na akatawala huko yeye na kizazi chake. Imepokewa kuwa sababu ya kuenea kwa madhehebu ya Imaam Malik Afrika Magharibi ilikuwa ni kuwa watawala wake, ambao

ni kizazi cha Bwana Idriis, waliitilia nguvu madhehebu yake. Na sababu yake ni kuwa alipodhihiri Bwana Muhammad Nafsul Zakiyya walikwenda watu kumwuliza Imaam Malik(ra) naye akawaashiria wampe kiapo cha utii. Wakasema shingoni mwao kuna utii kwa Abu Ja'afar Al-Mansur. Akawaambia, “Hakika mulitoa kiapo cha utii mukiwa mumelazimishwa”.

Mtoto mwengine wa Sayyidina Abdalla (Al-Mahdh) bin Hasan Muthanna, ni Bwana Musa Al-Juuni. Huyu aliitwa hivyo kwa sababu ya kukoza rangi yake. Yeye alijificha wakati wa vita dhidi ya kaka yake Bwana Muhammad Nafsul Zakiyya. Bwana Musa Al-Juuni ndiye babu wa Sheikh Abdul Kadir Jeilaniy.

Sayyidna Husain bin Aliy.

Alizaliwa tarehe 4 au 5 mwezi wa Shaabaan mwaka wa nne tangu kuhama.

Imepokewa kuwa Mtume(saw) alitoka nyumbani kwa Bibi Aisha, akapitia nyumba ya Bibi Fatima, akamsikia Husain akilia, akamwambia (Bibi Fatima): "Je, hujui kuwa kilio chake kinaniudhi?"

Na imepokewa pia kuwa Mtume(saw) alimbeba Husain bin Aliy begani kwake huku akisema, "Ewe Mwenyezi Mungu mimi nampenda na wewe mpende".

Imepokewa na Imaam Bukhariy, kuwa mtu mmoja alikuja kumwuliza Ibn Umar(ra)? unajisi wa damu ya mbu. Akamwuliza, “Unatokea wapi?” Akamjibu, “Iraq”. Akasema (Ibn Umar), “Mwangalieni huyu amekuja kuniuliza kuhusu damu ya mbu, na wamemwua mtoto wa Mtume(saw), na hakika nilimsikia Mtume(saw) akisema, “Hao ni maua mazuri yangu duniani”.

Imepokewa na Imaam Tirmidhiy kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) amesema, “Hasan na Husain ni mabwana wa vijana wa peponi”. Imepokewa pia, Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) amesema, “Hawa ni watoto wangu, mwenye kuwapenda, ndio amenipenda mimi”.

Imepokewa na Imaam Tirmidhiy kwamba Sayyidna Aliy(ra) amesema, “Hasan anafanana na Mtume(saw) wa Mwenyezi Mungu baina ya kifua na kichwa na Husain anafanana na Mtume(saw) chini ya hapo”.

Imepokewa na Bwana Abdallah bin Ubeid bin Umeir amesema, “Amehiji Husein bin Aliy hijja 25 akiwa anatembea kwa miguu na ngamia wake wakivutwa mbele yake”.

Imepokewa kwamba Bwana Amr bin Al-Aasi(ra) siku moja alikuwa kwa Bwana Muawiya(ra) na kilikuwepo hapo kikundi cha watu watukufu. Bwana Muawiya akauliza ni nani mtukufu zaidi kuliko watu

wote kwa baba na mama, babu na bibi, ami na shangazi, mjomba na khaloo. Nu'maan bin Ajlaan akajibu, “Ni Hasan na Husein, baba yao ni Aliy bin Abi Taalib, mama yao ni Fatima, babu yao ni Mtume(saw), na bibi yao ni Bi. Khadija, ami yao ni Ja’afar na shangazi yao ni Ummu Haaniy bint Abi Talib, na Mjomba wao ni Al-Qaasim na khaloo yao ni Zainab, Mwenyezi Mungu awawiye radhi wote”.

Aliuawa Bwana Husain siku ya Ashura mwaka wa 61 akiwa na miaka 58. Kwa hakika sote tunasikitika kwa kuuawa kwake, lakini ni kitu ambacho Mwenyezi Mungu amekiandika. Hatupati chochote kwa kukitaja zaidi ya maumivu. Imaam Ghazaaliy amesema kuelezea kuuawa kwake ni haramu. Kwa hakika masahaba Abdallah bin Umar, Abdallah bin Abbas na Abdallah bin Zubayr wote walimkataza asiende Iraq. Pamoja na hayo wasiya wa kaka yake ulimwashiria hivyo, lakini ilikuwa ni kitu ambacho kimeandikwa lazima kitokee - Mwenyezi Mungu amrehemu na atusamehe madhambi yetu.

Maneno ya Ba Alawiy kuhusu kueleza kisa cha Bwana Husain.

Amesema Habiib Abdillah Haddaad alipo ona kitabu cha Mashraa Rawiy ambacho kimejaa tarjama ya masharifu wa Ba Alawiy: "Lau kama asingetaja kisa cha kuuawa Husain."

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas, "Walikuwa Salaf-Mwenyezi Mungu awaridhie-wanakataza kuangalia (kwa kusoma) yaliyo jiri baina ya masahaba-Mwenyezi Mungu awaridhie-khasa baina ya Bani Umayya na Bani Hashim. Na imetufikia kuwa msomaji akifikia sehemu inayo taja baadhi ya hayo kwenye kitabu ambacho wanakisoma, humwambia: wacha hayo (usisome), jisomee mwenyewe. Na imetufikia kuwa Habiib Aliy bin Hasan Al-Attaas (wa Mash-had) alipo kuwa akisoma *Al-Fusuulul-Muhimma* ya Ibn Sabbaagh kwa babu yake Habiib Husain bin Umar Al-Attaas, akafikia kisa cha Sayyidna Husain, (babu yake) alimwambia jisomee mwenyewe."

HISTORIA YA BA ALAWIY

- ASILI YAO
- WAASISI WA BA ALAWIY
- BAADHI YA VIONGOZI
- AALI BA ALAWIY AFRIKA MASHARIKI

ASILI YAO

- Imaam Aliy Zainil Abidina
- Imaam Muhammad Baaqir
- Imaam Ja’far Saadik
- Imaam Aliy Ureidhiy
- Imaam Muhammad bin Aliy Ureidhiy
- Imaam Isa Naqiib bin Muhammad

Aali Ba Alawiy ni masharifu, yaani wajukuu wa Mtume(saw) kupitia kwa Sayyidna Husain bin Aliy bin Abi Talib. Asili ya kuitwa Ba Alawiy, yaani ukoo wa Alawiy ni kwa babu yao anaye itwa Alawiy bin Ubeidillah bin Ahmad (Al-Muhaajir) bin Isa (Naqiib) bin Muhammad bin Aliy Ureidhiy, bin Musa Al-Kaadhim bin Ja'afar Sadik bin Muhammad Baaqir bin Aliy (Zainil-Abidina) bin Husain bin Aliy bin Abi Talib. Na Husain pia ni mtoto wa Fatima bint Rasulillah Muhammad bin Abdillah (saw). Tutaanza kueleza tarjama yao fupi tukianzia kwa Sayyidna Aliy (Zainil Abidina) bin Husain-Mwenyezi Mungu awaridhie wote.

Imaam Aliy Zainil Abidina:

Alizaliwa tarehe 5 Shaaban siku ya Alkhamisi mwaka wa 37 au 38 tangu Hijra ya Mtume(saw). Alizaliwa Madina na akalelewa hapo. Alikuwa akiitwa Zainil Abidina kwa ajili ya ibada zake. Imepokewa kuwa alikuwa akiswali kila siku rakaa elfu moja. Pia alikuwa akiitwa Sajjaad kwa sababu ya kusujudu sana. Mama yake alikuwa binti wa mfalme Yazdajir wa Uajemi. Walipoleta Waislamu mateka kutoka Uajemi, kulikuwa na mabinti watatu wa mfalme, wakataka kuwauza, lakini kukatoka ushauri kuwa hawa ni mabinti wa mfalme, haitopendeza kuwauza, ila watatiwa thamani, anayeweza atawanunua na kuwaoa. Akawachukua Sayyidna Aliy(ra). Mmoja wao akampa Sayyidna Abdallah bin Umar, wa pili mtoto wake Sayyidna Husain, na wa tatu Sayyidna Muhammad bin Abu Bakr. Wakapata watoto Salim bin Abdallah, Aliy bin Husain, na Qasim bin Muhammad. Walikuwa watu wa Madina hawapendi masuria, lakini walipopata umashuhuri hawa watatu kwa elimu na ucha Mungu, wakaanza na wao kuoa masuria.

Sayyid Aliy (Zainil Abidina) bin Husain alikuwa akiitwa mabaki ya upanga, kwani ndugu zake wote waliuawa pamoja na baba yao Sayyidna Husain hapo Karbala.

Imehadithiwa na Sayyidna Jabir bin Abdillah(ra) kwamba Husain alikuwa amekaa kwenye mapaja ya Mtume(saw) akicheza naye. Bwana Mtume(saw) akamwambia Sayyidna Jabir(ra), “Huyu (Husain) atapata mtoto ataitwa Aliy, ikifika siku ya Kiyama patanadiwa asimame mbora (pambo) wa wenye kuabudu ***(Zainil Abidina),*** atasimama mtoto wake (huyu Husain). Na yeye (Aliy) atapata mtoto ataitwa Muhammad ukikutana naye mpe salamu zangu”.

Katika kisa kinachoonyesha utukufu wake, ni kuwa Hishaam bin Abdil Malik alipohiji, baada ya kutufu akajitahidi kulibusu jiwe jeusi asilifikie, wakamwekea mimbari akakaa akiwaangalia watu, akamuona Zainil Abidina naye ni katika wazuri mno wa watu kwa sura, watu wote wakampa nafasi hadi akaenda kulibusu jiwe jeusi. Mtu mmoja kutoka Shaam akauliza, “Nani huyu ambaye watu wote wanamhishimu na kumwogopa kiasi hiki?” Akajibu Hishaam, “Simjui”. Akasema Firazdaq, “Lakini mimi namjua”. Akamwuliza mtu wa Shaam, “Ni nani yeye ewe Abu Faris?” Akatamka shairi lake mashuhuri kumwelezea Zainil Abidina,

هذا الذي تعرف البطحاء وطأته		والبيت يعرفه والحل والحرم
هذا ابن خير عباد اللّٰه كُلِّهمُ		هذا التقي النقي الطاهرُ العلم
هذا ابن فاطمةٍ انْ كنت جاهله		بجده انبياء اللّٰه قد ختموا
وليس قولك : منْ هذا؟ بضائره		العرب تعرف من انكرت والعجمُ
كلتا يديه غياثٌ عمَّ نفعهما		يستوكفان ولا يعروهما عَدمُ
سهل الخليقة، لاتخشى بوادره		يزينه اثنان: حِسنُ الخلقِ والشيمُ
حمّال اثقال اقوامٍ اذا امتدحوا		حلو الشمائل، تحلو عنده نعمُ
ما قال: لاقط، الا في تشهده		لولا التشهّد كانت لاؤه نعم
عمَّ البرية بالاحسان، فانقشعت		عنها الغياهب والاملاق، والعدم
اذا رأته قريش قال قائلها :		الى مكارم هذا ينتهي الكرم
يُغضي حياءً، ويغض ى من مهابته		فما يكلَّم الا حين يبتسم

بكفّهِ خيزرانُ ريحها عبق		من كف اروع، في عرنينه شمم
يكاد يمسكه عرفان راحته		ركن الحطيم اذا ما جاء يستلم
اللّه شرّفه قدماً، وعظّمه		جرى بذاك له في لوحة القلم
ايُّ الخلائق ليست في رقابهمُ		لأوّليّه هذا، اوله نِعم
من يشكرِ اللّه يشكر اوّليّه ذا		فالدين من بيت هذا ناله الامم
ينمي الى ذروة الدين التي قصرت		عنها الاكف، وعن ادراكها القدم
من جده دان فضل الانبياء له		وفضل امته دانت له الأمم
مشتقة من رسول اللّه نبعته		طابت مغارسه والخيم والشيم
ينشق ثوب الدجى عن نور غرته		كالشمس تنجاب عن اشراقها الظلم
من معشرٍ حبهم دينٌ وبغضهم		كفرٌ وقربهم منجى ومعتصم
مقدّمٌ بعد ذكر اللّه ذكرهم		في كِلّ بدءٍ ومختوم به الكلم
إن عدَّ اهل التقى كانوا ائمتهم		او قيل من خير اهل الارض؟ قيل: هم
لا يستطيع جوادُ بعد جودهم		ولا يدانيهم قوم، وإن كرموا
هم الغيوث، اذا ما أزمة أزمت		والاسد اسدُ الشرى والبأس محتدم
لاينقص العسر بسطاً من اكفّهم		سيّان ذلك: إن اثروا وإن عدموا
يستدفع الشرُّ والبلوى بحبّهم		ويستربُّ به والاحسان والنعم

Kwa ufupi shairi hili linasema:

Anazijua tambarare za Makka nazo zinamjua, ni mtoto wa mbora wa viumbe, kwake yeye ndio inakomelea tabia njema, na kwa jinsi nyumba tukufu inavyompenda inakaribia kuugandisha mkono wake akija kubusu nguzo zake, yeye ni mtoto wa Fatima ikiwa humjui, na babu yake ndio mwisho wa Mitume. ...

Kwa ukweli linaeleza ubora wake juu ya watu wote wa zama zake, na ni fakhari kwa kila anaye nasibika kwake. Hishaam akakasirika na kumfunga jela Firazdaq. Zainil Abidina aliposikia alimzawadia dirham elfu kumi na mbili, pamoja na kumwambia, "Tusamehe, tungekuwa na zaidi tungekupa". Akajibu Firazdaq, "Sikusema niliyoyasema ila hasira iliyonipanda kwa sababu ya Mwenyezi Mungu Mshindi Mtukuka na Mtume wake(saw), na siwezi kuchukua kitu kama ujira wake. Zainil Abidina akamjibu, "Mwenyezi Mungu atakulipa kwa hayo, ila sisi Ahlil bayt tukitoa kitu haturejeshi". Akaikubali na kuipokea zawadi hiyo.

Alipokea elimu kutoka kwa baba yake na ammi yake Sayyidna Hasan, na masahaba Ibn Abbaas, Miswar bin Makhrama, na Abi Hurayra, na mamama wa waumini Safiyya, Aisha, na Ummu Salamah(ra). Vile vile alikuwa akienda kwenye baraza ya Bwana Zayd bin Aslam na akijitahidi kuwa karibu naye. Sayyid Zainil Abidina alikuwa akisema, "Elimu inabidi ifuatwe popote ilipo, na mtu anatakiwa akae kwa atakaye mnufaisha kwenye dini yake".

Amesema Bwana Yahya Al-Ansariy, "Yeye ni mbora wa Baniy Hashim niliyewahi kumwona". Imepokewa pia kutoka kwa Imaam Zuhriy, "Sijamdiriki Madina aliyekuwa bora kuliko yeye".

Alikuwa na khofu kubwa ya Mwenyezi Mungu, akitawadha hubadilika rangi hadi anakuwa wa njano. Wakimwuliza, "Kumetokea nini?" Huwaambia, "Je, munajua mbele ya nani nasimama?" Alipokwenda kuhiji akaleta Talbiyya, "*Labbayka Allahumma Labbayka....*" hakuwahi kuimaliza ila alizimia pale pale. Mara moja alikuwa akiswali ndani ya nyumba, ile nyumba ikaungua na yeye yumo ndani ya swala hana khabari, alipomaliza wakamwambia yaliyotokea. Akasema, "Ulinishughulisha moto mwengine". Hata akitawadha hapendi atawadhishwe na yeyote. Anakwenda kuchota maji yeye mwenyewe. Alikuwa hawachi kisimamo cha usiku, si safarini wala nyumbani.

Akisikia mtu anamsema kwa ubaya, humwambia, "Ikiwa unayosema ni kweli Mwenyezi Mungu anisamehe, na ikiwa unayo sema ni uongo Mwenyezi Mungu akusamehe". Mara moja alikutana na mtu akamtusi vibaya, yeye akamwambia, "Yaliyositirika kwako ni mengi zaidi kuliko yaliyodhihiri kwako, je unahitaji chochote tukusaidie?" Kisha

akamtolea nguo yake, akampa, pamoja nayo, dirham elfu moja. Yule mtu akaona haya akasema, "Nashuhudia kuwa wewe ni katika watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw)." Akiulizwa kwa nini humtukani anayekutukana, husema, "Yeye ameona mabaya yangu, lakini mimi sijaona kitu kibaya kwake hata nimtukane".

Alikuwa mkarimu sana. Alikuwa akibeba chakula mgongoni mwake usiku na kupeleka kwenye nyumba za wahitaji wa Madina bila ya wao kujua. Mara kwa mara alikuwa akisema kuwa sadaka ya siri inazima ghadhabu za Mola. Hata alipofariki ndio ikajulikana kuwa ni yeye ndiye aliyekuwa akipeleka chakula nyumba zaidi ya mia moja. Na alikuwa akikopesha au kumuazima mtu pesa husamehe. Kadhalika akimwombea mtu ikashindikana hutoa kwenye mali yake akamlipia au kumfidia. Pia alikuwa na huruma kwa wanyama na hampigi mnyama anayempanda kwenye safari yoyote.

Pamoja na elimu ya kupambanua mema na mabaya, Mwenyezi Mungu alimpa vile vile elimu ***ladunniy,*** yaani elimu isiyochumwa kwa kusoma, bali itolewayo hiba na Mwenyezi Mungu kumpa mja wake amtakaye. Elimu hii hawaipati ila wacha Mungu wa kweli. Sayyidina Zainil Abidin(ra) anasema kwa mashairi:



Hakika mimi naificha katika elimu yangu johari,

Ili mjinga asije kuiona hiyo haki akafitinika.

Na ametangulia kuyasema haya Abal Hasan,

Kumwambia Al-Husain, na ndio wasiya wa Al-Hasan baada yake.

Huenda johari moja tu ya elimu lau ningeitoa

ningeambiwa wewe ni katika waabudu masanamu,

Na waislamu wangehalalisha damu yangu

wakiona kuwa kibaya mno wanacho kifanya ni kizuri.

Na hii siyo ajabu kwani Bwana Mtume(saw) amesema kuwa yeye ni mji wa elimu na Sayyidna Aliy(ra) ni mlango wake, na bila ya shaka Imaam Aliy Zainil Abidina karithi kwa babu yake.

Hoja ya kuficha elimu za ndani limepokewa hata na Sahaba Abu Hurayra, kuwa alipewa viriba viwili vya elimu, kimoja amekitoa kwa watu, na kiriba cha pili kama angekitoa wangemkata shingo yake.

Sayyid Zainil Abidin(ra) alimdiriki babu yake, Sayyidina Aliy bin Abi Talib(kw) kwa miaka miwili, na ammi yake, Sayyidna Hasan(ra), kwa miaka 10, na baba yake, Sayyidna Husein(ra), kwa miaka 11. Aliweka darasa ndani ya msikiti wa Mtume(saw), na walichukua kwake elimu Tabiin wengi, miongoni mwao ni Bwana Said bin Musayyib, na Bwana Said bin Jubair.

Amefariki mwaka wa 92 (riwaya mbili nyengine zinasema 93 na 94), tangu Hijra ya Mtume(saw) na alizikwa Baqii karibu na Ammi yake Sayyidna Hasan. Na yeye ndiye aliyeendeleza kizazi cha Sayyidna Husain.

Imaam Muhammad Baaqir.

Alizaliwa Madina siku ya Ijumaa tarehe tatu Safar mwaka wa 57. Aliitwa Baaqir kwa sababu alitoboa elimu, yaani alikuwa amezama na kupata sehemu kubwa ya elimu. Amepokea hadithi kwa babu zake Hasan na Husain, Bibi Aisha, Bibi Ummu Salamah, na masahaba Ibn Abbas, Ibn Umar, Abi Said, Jabir bin Abdallah, Samurah bin Jundub, Abdallah bin Ja'afar, baba yake, Bwana Sae'ed bin Musayyib na wengineo(ra).

Katika wanafunzi wake ni pamoja na mtoto wake Ja'afar, ndugu yake Zayd, Ibrahim bin Ad-ham, Amru bin Diinar, Al-a'mash, Rabia' Rayi, Ibn Jurayj, Awzaai' na wengineo. Imaam Nasaai amemuhesabu Sayyid Muhammad Baaqir katika Mafuqahaa (wataalamu wa fani ya Fiq-hi) wa kitabiin. Imepokewa kuwa Khalifa Umar bin Abdul Aziz alipopewa uliwali wa Madina, alikuja kwake msikitini (kwani alikuwa na darasa), na kumwambia, "Nilikuwa nikijua kuwa uko sehemu hii wakati kama huu, na ilikuwa ni wajibu wangu kuja nyumbani kwako, isipokuwa ni pupa na shauku yangu kukutana na wewe na kusikiliza maneno yako". Na alipoamrisha Khalifa Umar bin Abdul Aziz kuupanua msikiti, aliwafahamisha watu wake wafanye kazi kwa njia ambayo haitovunja darasa za Imaam Baaqir.

Inatosha kuwa ni fakhari kwake kuwa Mtume(saw) amemtaja kama tulivyoona katika hadithi iliyopokewa na Sayyidna Jabir(ra). Na Sayyidna Jabir(ra) amesema, "Mwenyezi Mungu akanipa umri mrefu mpaka nikafikisha salamu za Mtume(saw) kwa Muhammad Baaqir kutoka kwa babu yake".

Sayyid Muhammad Baaqir alikuwa akiwapa chakula na mavazi ya kifakhari ndugu zake na watu wake. Na alikuwa akisema, "Hakuna jema duniani kama kuwaunga ndugu". Alikuwa akitoa sadaka sana pamoja na kuwa na familia kubwa na hali yake ya wastani.

Alikuwa akimpenda Sayyidna Abubakr Siddiik(ra), na akimsifia sana. Alikuwa akisema, "Asiye mtaja kuwa ni siddik basi Mwenyezi Mungu

hawezi kusadikisha maneno yake". Na alikuwa akisema, "Mimi niko mbali mno na mwenye kuwachukia masheikh wawili: Abu Bakr na Umar, na lau ningepata uongozi ningejikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa damu za wanaowachukia (yaani kuwaua). Wallahi nawatanguliza na nawaombea maghfira. Sikumdiriki yeyote katika Ahlil bayt ila anawatanguliza". Amesema Ibn Fudhayl, Imepokewa kutoka kwa Salim bin Abi Hafsa, "Nilimwuliza baba Ja'afar (yaani Muhammad Baqir) na mtoto wake, juu ya AbuBakr na Umar, akasema, "Ewe Salim! Watangulize na ukae mbali na adui zao, kwani walikuwa ni maimamu waongofu". Amesema Al-Hafidh Dhahabi, "Isnadi ya maneno haya ni sahihi. Na Ibn Fudhayl na Salim ni mashia lakini ni wenye kuaminika".

Kuna khitilafu ya mwaka aliofariki kwa riwaya tatu, 114, 117 na 118H. Amezikwa Baqii kwa baba yake. Aliusia akafiniwe kwenye nguo aliyokuwa akiisalia.

Imaam Jaafar Saadik:

Mashuhuri kama Al-Saadik, yaani mkweli. Alizaliwa Madina, siku ya Jumatatu, 10 Rabiul-Awwal mwaka wa 80 (na riwaya nyengine 83) na akalelewa hapo. Mama yake ni Bibi Farwah bint Qasim bin Muhammad bin Abubakar Siddiik(ra). Na mama wa Farwah ni Bibi Asmaa bint Abdulrahman bin Abubakar Siddiik(ra). Hii ndiyo sababu alikuwa akisema amenizaa Siddiik mara mbili.

Amepokea elimu kwa ammi yake Bwana Zayd, na babu yake kwa upande wa mama Bwana Qasim bin Muhammad, Bwana Urwah bin Zubayr, na maimamu Ataa, Naafi', Zuhriy na wengineo. Na wamepokea kwake watoto wake Musa Al-Kaadhim, Aliy Uraydhiy, na maimamu Malik, Abi Hanifa, na Sufyani wawili (Sufyaan bin Uyayna na Sufyaan Thawry) na wengineo wengi. Amesema Imaam Abu Hanifa(ra), "Sijamuona mwenye Fiq-hi kuliko yeye". Alitumwa Imaam Abu Hanifa na Mfalme Mansur amwandikie maswali magumu kabisa kwani watu wamefitinika naye. Akamwandikia maswali 40, akajibu kila swali kwa kusema nyie munasema hivi, watu wa Madina wanasema hivi na sisi tunasema hivi, mpaka akayamaliza maswali yote kwenye majlis moja. Aliwahi kumkataza Imaam Abi Hanifa na kufanya *Qiyaas*[1] na kumwambia wa kwanza aliye fanya *Qiyaas* ni Iblis. Akamjibu Imaam Abu Hanifa kwamba nafanya *Qiyaas* kwenye mas-ala yasiyo na *nassi* (ya Qur-ani au Hadithi). Akamwambia: Kama ni hivyo basi hamna tatizo (si vibaya).

Imepokewa kwake Imam Jaafar Saadik kuwa amesema, "Ewe Salim! Mtu anamtukana babu yake? Abubakar(ra) ni babu yangu, na sitegemei shafaa (maombezi) ya Aliy(ra) ila nataraji mfano wake kwenye shafaa ya Abubakar(ra)". Imepokewa pia kuwa alipotaka kuondoka Abbas Al-Hamadaani kutoka Madina, alimzuru Ja'afar bin Muhammad, (Ja'afar) akamwambia, "Nategemea kuwa wewe ni katika watu wema wa mji

[1] huu ni msingi miongoni mwa misingi ya elimu ya Fiq-hi, ambao ni mizani ya kulipima jambo au suala ambalo halina ufafanuzi ndani ya Qur-ani au hadithi na jambo au suala lililo tajwa ndani ya Qur-ani au Hadithi, kwa kulingana sababu

wenu, basi wafikishie haya, kuwa mwenye kudai kuwa mimi ni Imaam ambaye ni lazima kufuatwa kwa kutiiwa basi mimi niko mbali na yeye, na mwenye kudai kuwa mimi ninajiweka mbali na Abubakar na Umar basi mimi ni mbali mno na yeye".

Alifariki siku ya Jumatatu kati kati ya Rajab mwaka 148 na akazikwa Baqii alipozikwa baba yake, babu yake na Sayyidna Hasan.

Imaam Aliy Ureidhy:

Alizaliwa Madina na kukulia hapo, na akasuhubiana na baba yake mpaka alipofariki akahamia Ureidh, maili 4 kutoka Madina na kufariki hapo, na kaburi lake ni mashuhuri.

Ametajwa na Haafidh Dhahaby na Haafidh Ibn Hajar Asqalani na wengine. Amepokea kwa baba yake Ja'afar Saadik na ndugu yake Musa Al-Kaadhim, na Sufyaan Thawri na wengine. Wanafunzi wake ni pamoja na watoto wake Muhammad na Ahmad, Imaam Ahmad Al-Bazziy mwenye *Qiraa*, Salamah bin Shabiib, na Nasr bin Aliy Jahdhamiy na wengine wengi. Alipata umri mrefu mpaka wajukuu wakasoma kutoka kwa babu. Yeye ndiye mtoto wa mwisho wa baba yake na mwenye umri mrefu.

Amefariki mwaka 220H.

Imaam Muhammad bin Aliy:

Alizaliwa Madina na akalelewa na baba yake na akakaa naye mpaka alipofariki ndipo akahamia Basra. Walimpenda watu wa Basra kutokana na tabia zake njema kabisa. Alikuwa mcha Mungu na karimu khasa kwenye kulisha chakula, mwenye kujitolea kwa aliye muhusu na asiye muhusu. Jambo jengine muhimu ni kuwa alikuwa mwenye kukubaliwa shafaa akimwombea mtu.

Imaam Isa Naqiib:

Alisoma Fiq-hi na elimu nyengine za dini, na alikuwa mwenye ufasaha na mwenye kukubaliwa kwa watu mpaka wafalme. Alikuwa akiitwa macho bluu kwa sababu ya umanjano kwenye macho yake, na akiitwa pia Mrumi. Ama kuitwa Naqiib, ni kwa sababu alikuwa ni mdhamini, mwangalizi na kiongozi wa masharifu. Alikuwa akifuata madhehebu ya Sunni, na aqida yake ilikuwa ni ya kisunni.

Amemtaja Bwana Ibn Uqbah kwenye kitabu chake *Umdatul-Taalib*.

Amefariki Basra.

WAASISI WA BA ALAWIY

- Imaam Al-Muhaajir Ahmad bin Isa
- Imaam Abdallah bin Ahmad bin Isa
- Imaam Aliy bin Alawiy Khaali Qasam
- Imaam Muhammad bin Aliy Saahib Mirbaat
- Al-Faqiih Al-Muqaddam
- Tasawwuf
- Tariqa ya Aali Ba Alawiy

Imaam Ahmad Al-Muhaajir ila Allah:

Huyu ni Imamu mwenye kutegemewa, asiye na tamaa na ulimwengu na mwenye kudumu juu ya ibada. Alikuwa pia mtoaji waadhi na mwenye ulimi wa ufasaha. Hata alipotawala ndugu yake Bwana Muhammad bin Isa baadhi ya vitongoji vya Iraq alikuja akampa mawaidha makubwa, hakuwacha kumpa waadhi hadi akaacha utawala. Imaam Ahmad bin Isa alikuwa na cheo kikubwa na mali nyingi Iraq, lakini haikumshughulisha na ibada na kuwaongoza walio potea.

Kuhamia kwao Hadhramout:

Mtu wa kwanza kuhamia Hadhramout alikuwa ni Imaam Ahmad bin Isa na hapa tutaeleza sababu ya kuhamia Hadhramout.

Iraq ilikuwa ni nchi ambayo imeendelea kielimu, si elimu tu za dini, bali lugha, falsafa, unajimu, hisabati na nyenginezo. Pamoja na kuendelea kielimu ilikuwa pia ni sehemu ambayo imejaa fitna, vita kila kukicha, na ugomvi wa kiitikadi na kifikra.

Kilichozidisha zaidi ni kudhoofika kwa wafalme na kuzama kwao kwenye matamanio na kutojishughulisha na raia, hata vikadhihiri baadhi ya vikundi vya watu weusi ambavyo vilieneza ufisadi wa kila aina na kuwaua watu, kuwateka na kuwauza wanawake wa kiislamu kwa dirham mbili, wakavunja misikiti na wakachoma moto mji. Wakatawala Basra na baadhi ya miji iliyo karibu nayo. Mwaka wa 307 kikadhihiri kikundi kibaya zaidi *Qaraamita.* Wakaingia Basra, wakaua, wakateka, wakaiba na wakahalalisha yaliyo haramu, hata baadhi ya wakazi walijitupa kwenye mito wakafa wengi. Na hawa walikuwa ni mabaki ya kikundi cha mwanzo, kwani waliposhindwa vita na watawala wa kibani Abbas, wakajikusanya chini ya uongozi mpya wa *Qarmatiy*, na asili yao ni Bahrain na fitna yao ilianza tangu mwaka 286.

Hapa Imaam Ahmad bin Isa akaangalia kwa jicho la hekima, na kuona ni lazima kuhama kutoka Iraq, akitekeleza amri ya Mwenyezi Mungu inayosema:

فَفِرُّوٓاْ إِلَى ٱللَّهِۖ

"**Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu"** (Dhaariyaat:50)

akawakusanya jamaa zake na ndugu zake, akawatolea waadhi na kuwafahamisha uharaka wa kuondoka duniani, na akawatia mapenzi ya kuitamani akhera na neema yake itakayo dumu. Na akawanasihi kuhama Iraq kutokana na fitina zilizodhihiri na akawaambia, ni lazima kuhama kutoka miji hii kwa sababu ya kuzuka humo bidaa na watu waovu. Wakaikubali ishara yake walioandikiwa uongofu, na wakajitayarisha na safari. Alimwacha mtoto wake Bwana Muhammad kusimamia mali zake naye alibaki hapo hapo Basra hadi akafariki na kizazi chake kiko huko.

Imamu Al-Muhaajir akaanza safari yake mwaka wa 317 akiwa na watu kama 70. Katika waliohama pamoja naye ni mtoto wake Bwana Abdallah, watoto wawili wa ammi zake Bwana Muhammad bin Sulayman, babu wa masharifu wa kiahdal, na wa pili Bwana Ahmad Qudemi; babu wa masharifu wa Qudemi. Pia walitoka pamoja naye mtumishi wake Mukhaddam na huru wake wawili: Mukhtar na Shawiyh. Wakaelekea Madina, wakakaa huko mwaka mzima. Na mwaka huu yaani 317, *Qaraamita* walifika Makka na kueneza fitna yao.

Katika mabaya waliyoyafanya *Qaraamita* ni kuvunja heshima ya Haramain, wakawaua mahujaji na wakawatupa kwenye kisima cha Zamzam; wakavunja majumba ya watu, wakaiba, na kuwateka wanawake na watoto, na wakachukua vilivyomo ndani ya Ka'aba miongoni mwa makandili, nguo na milango. Na kubwa zaidi wakalitoa jiwe jeusi na kuondoka nalo kwenda kwenye mji wao, wakitegemea kuwa watahamishia Hijja huko. Walijaribu kutoa miizab wasiweze. Na hawakusimama Arafa mwaka huo ila watu kidogo, na wengi walijificha

kwenye majabali. Kisha mkubwa wao akapata ugonjwa mbaya, mpaka viungo vyake vikapuputika na akafa. Baada ya miaka 20 lile jiwe likarudishwa walipoona hawana njia ya kuhamisha Hijja iwe kwao.

Tukirudi kwa Al-Muhaajir na watu wake, walihiji mwaka 318, pamoja na kukosa kuligusa Jiwe Jeusi, na wakaona hawawezi kukaa Haramain. Wakawa daima wanamwomba Mwenyezi Mungu awaonyeshe panapofaa kuishi katika miji. Kisha Mwenyezi Mungu akawapa maono ya moyo (***ilhaam***) kuwa Yemen ndio sehemu inayo faa, kwa kuwa ipo mbali na fitina na mitihani, pamoja na hadithi zilizo pokewa kutoka kwa Mtume(saw). Miongoni mwa hadithi hizo ni hizi zifuatazo:

1. Zikizidi fitina basi juu yenu (kuhamia) Yaman.
2. Juu yenu (kuhamia) Yaman zikizidi fitina, kwani watu wake ni marahimu na ardhi yake imebarikiwa na ibada ndani yake ina ujira mkubwa.
3. Ewe Mwenyezi Mungu tubarikie kwenye Shaam yetu! Ewe Mwenyezi Mungu tubarikie kwenye Yaman yetu! Wakamwambia na Najd je? Mtume(saw) akarudia: Ewe Mwenyezi Mungu tubarikie kwenye Shaam yetu! Ewe Mwenyezi Mungu tubarikie kwenye Yaman yetu! Wakamwambia tena na Najd je? Akasema, “Huko kutakuwa na mitetemeko na fitina”. (Bukhari)
4. Na imepokewa katika Sahiihain, kwamba Mtume(saw) aliashiria Yaman, na kusema Imani ipo hapa kwa sasa.
5. Wamekuja watu wa Yaman wana mioyo safi, wana twaa (kutii) bora, Imani ina asili ya Yaman, fiq-hi ina asili ya Yaman, na hekima ina asili ya Yaman. (Bukhari na Muslim)
6. Katika Bukhariy: Wamekujieni watu wa Yaman wenye vifua laini na nyoyo laini, Imani ina asili ya Yaman na hekima ina asili ya Yaman, na ufakhari na kiburi kiko kwa watu wa ngamia, na utulivu na heshima viko kwa watu wa mbuzi.
7. Imani iko hapa, na akaashiria Yaman, na ukukutavu (uzito wa mioyo) uko kwa wapiga mbinja machungani na mashambani,

kwenye asili ya mikia ya ngamia ambapo patakapo chomoza pembe za Sheitani wa Rabia na Mudhar. (Bukhari)

Na hadithi nyengine nyingi zisizo kuwa hizi. Kuna vitabu vilivyo kusanya fadhila za Yemen, kama kitabu "*Bahjatul-Zaman fi akhbaaril-Yaman*", na "*Qurratil-Uyuun fi akhbaaril-Yaman al-Maymun*".

Wakatoka Imaam Al-Muhaajir na watu wake kuelekea Yemen, Babu wa Ahdal akatua Waadiy Sihaam, na Babu wa Qudemi akatua Waadiy Surdud. Ama Imaam Al-Muhaajir akaendelea na safari na mtoto wake na watumishi wake wakihama mji hadi mji, hadi akafika Hadhramout. Mji wa kwanza alioshukia ulikuwa Hijrain. Hapo akatulia kidogo, akanunua ardhi, akanunua mitende. Baadaye akaamua kuhama na kumwachia huru wake Shawiyh, akafikia kitongoji cha Bani Jushayr. Hapo hakukaa sana, akaendelea hadi akafikia Waadiy Husayyisa na kufanya hapo kuwa makazi yake. Akanunua sehemu kubwa ya ardhi, akaishi hapo hadi kufariki na kuzikwa hapo. Hivi sasa sehemu hii inaitwa Shiib Ahmad, kwa jina lake Imaam Ahmad bin Isa.

Hadhramout wakati alipokuja ilikuwa na masunni na maibadhi, ila maibadhi ndio walio kuwa na nguvu. Baadaye maibadhi walihama mji na kuelekea Oman. Yakaenea Hadhramout madhehebu ya Imaam Shafiy, na Aqida ya Sunna na Jamaa. Mabadiliko hayo yalitokea kutokana na kukubaliwa kwake na wakaazi wa sehemu hizo. Mwenyezi Mungu akajaalia kizazi chake kikasalimika na fitina za Iraq, za kuafikiana na mashia katika itikadi zao potofu. Wakawa watoto wake na kizazi chake ndio viongozi wa dini na nguzo za Hadhramout. Katika waliofanya kazi kubwa ya kuendeleza aqida ya Sunna ni Sheikh Salim Ba fadhl. Na baada yake akaendeleza harakati hizo Al-Faqiih Al-Muqaddam.

Amefariki Imaam Ahmad bin Isa Al-Muhaajir mwaka 345 Hijriy, na kuzikwa Husayyisa, na kaburi lake ni maarufu na linakusudiwa kwa ziyara.

Maneno ya baadhi ya Ba Alawy kuhusu Al-Muhaajir.

Habiib Abdillah Haddad: “Watu wawili wana hisani kubwa juu ya Aali Ba Alawiy: Sheikh Ahmad bin Isa kwa kuwatoa kwenye bid-a na fitna, na Al-Faqiih Al-Muqaddam akawahifadhi na kubeba silaha na Ukabaila (***U’muumiyya***)”.

Habiib Abdallah bin Umar bin Yahya: “Yeye ni mbora wa wote waliokuweko kwenye bonde (la Hadhramout) kwa elimu, matendo na ukaribu kwa Mtume(saw). Hakika himma ya Sayyid Ahmad bin Isa ni kuwa asirudi yeyote katika kizazi chake Iraq, na kama yupo basi hakudumu muda mrefu”.

Ametaja pia Habiib Abdallah bin Umar bin Yahya kwamba Sayyid Ahmad bin Issa alikuwa na maisha ya raha na ufakhari hata akitaka mmoja wao kwenda kujisaidia, hukaa vijakazi wakimsubiri na vyetezo vilivyojaa udi na sandal na (manukato) mengine, yenye kima (thamani) ya diinar chungu nzima na hayo ni kwa mara moja tu.

Imaam Abdallah bin Ahmad bin Isa.

Huyu ndiye mtoto wa Al-Muhaajir aliyeendeleza kizazi chake katika miji ya Hadhramout.

Alizaliwa Basra, na alisafiri na baba yake kuja Hadhramout. Akachukua elimu kwa baba yake na maulamaa walio kuweko wakati huo. Alipohiji akakutana na Sheikh Abu Talib Al-Makkiy mwandishi wa *Quut al-Quluub*, na akasoma kwake na kupata faida kubwa kielimu.

Imaam Abdallah alikuwa ni mtu mwenye unyenyekevu mkubwa, hata alibadili jina lake na kujiita Ubaidillah (kijimja cha Allah) na likawa mashuhuri kwake kuliko la mwanzo.

Baada ya kufariki baba yake alihamia Sumal, akaowa huko na kupata mtoto akamwita Jadiid. Na alikuwa na watoto wawili kabla wa mama mmoja, Basriy aliyezaliwa Basra, na Alawiy ambaye ndiye aliye-endeleza kizazi chake. Kizazi cha Bani Basriy na Bani Jadiid kilikatika wakati wa Al-Faqiih Al-Muqaddam pamoja na kuwa walitoka wanachuoni na wachamungu wengi sana katika kizazi chao.

Watoto wake walikaa kidogo Sumal kisha wakahamia Bayt Jubayr na wakajenga msikiti wa Taqwa hapo, na walikuwa na kitongoji, sehemu inayoitwa Alawiyya. Masharifu hawa, pamoja na watoto wao na wajukuu wao, wakati wakikaa Bayt Jubayr, walikuwa wakiingia na kutoka mji wa Tariim. Walipendezewa na hali ya hewa ya mji wa Tarim, pamoja na ardhi yake na maji yake. Walivutiwa zaidi na kuona watu wa Tarim wameshughulika na kutafuta elimu na wenye fahamu nzuri. Hivyo wakaanza kuweka mahema yao na hatimaye kuhamia hapo. Mwanzo wa kuishi kwao Tariim ilikuwa mwaka 521. Wa mwanzo kuishi hapo ni Imaam Ali (Khaali Qasam) bin Alawiy bin Muhammad bin Alawiy bin Ubeydillah bin Ahmad bin Isa, pamoja na ndugu zake na jamaa zake kutoka Bani Basry na Bani Jadiid.

Mji wa Tariim ulipata dua za Sayyidna Abu Bakr(ra). Baada ya kufariki kwa Mtume(saw), iliritadi miji mingi katika Bara Arabu. Miongoni mwa miji kidogo sana ambayo ilibaki juu ya Uislamu ni mji wa Tariim.

Sayyidna Abubakar(ra) akauombea dua tatu: waongezeke watu wema ndani ya mji huo, Mwenyezi Mungu atie baraka kwenye maji yake, na usizimike moto wake hadi siku ya Kiyama. Moto uliokusudiwa hapa usizimike ni moto wa imani katika nyoyo za watu wa Tarim, kwamba imani zao zisiharibike hadi siku ya Kiama. Na dalili za qabuli ya dua yake iko wazi kwa kila mwenye imani na mapenzi ya kweli ya dini yake.

Kuthibitishwa nasabu yao.

Baada ya wajukuu wa Imaam Ahmad bin Isa kufanya maskani yao Hadhramout na kudhihiri kwa usharifu wao, baadhi ya watu wa Hadhramout walitaka wathibitishiwe nasabu yao kwa hoja za kisheria na dalili zilizoridhiwa. Akasafiri Imaam Ali bin Muhammad bin Jadiid, mwanachuoni mkubwa wa wakati huo na pia mjukuu wa Imaam Al-Muhaajir, kuelekea Iraq, akathibitisha nasabu yao na akachukua ushahidi wa watu 100 waadilifu waliokusudia kwenda Hijja mwaka ule. Kisha akaenda Makka na kuwashuhudisha watu wa Hadhramout waliokuja kuhiji mwaka huo. Mahujaji hawa waliporudi Hadhramout wakatoa ushahidi wao juu ya kuthibiti kwa nasabu ya Bani Ahmad na silsila yao kwa Mtume Muhammad(saw).

Imaam Aliy bin Alawiy (Khaali Qasam).

Kama tulivyotangulia kusema huyu ndiye wa kwanza katika Bani Alawy kuhamia Tariim. Alihamia mwaka 521 pamoja na ndugu zake na watoto wa ammi zake.

Sababu ya kuitwa *Khaali Qasam* ni kuwa alinunua ardhi, akaotesha mitende mingi kwenye ardhi hiyo, na akaiita Qasam. Jina hili lilitokana na jina la ardhi yao iliyoko Basra. Akaotesha mitende, watu wakaanza kukaa na ukawa mji, alikuwa akienda Qasam wakati wa mavuno ya tende.

Khaali Qasam alikuwa mwenye tabia njema kabisa, na mkarimu sana, khasa kwa aliyetoka nje ya mji kumkusudia yeye. Alikuwa pia mnyenyekevu wa kauli, matendo na mavazi; hajioni kuwa ana fadhila juu ya yeyote; na akikaa na watu hajulikani kama ni mwanachuoni ila akiingia kwenye utafiti wa mas-ala ya kielimu.

Alifariki mwaka wa 527 na akazikwa Zanbal, makaburi ya masharifu hapo Tariim.

Imaam Muhammad bin Aliy (Saahib Mirbaat).

Huyu ni mtoto wa Imaam Aliy (Khaali Qasam), mashuhuri amejulikana kwa jina la Saahib Mirbaat. Mirbaat ni mji wa zamani wa dhafaar ambao yeye ndiye aliyeuamirisha, kuuendeleza na kueneza elimu. Alilelewa na baba yake, na alijitahidi kutafuta elimu hata akawa katika wanachuoni mashuhuri. Miongoni mwa wanafunzi wake ni watoto wake wanne, pamoja na Sheikh Salim bin Fadhl, Sheikh Ali bin Ahmed Ba Marwan, Qadhi Ahmad bin Muhammad Ba Isa, Sheikh Aliy bin Muhammad Al-Khatiib (Sahibul Wiil), Sheikh Ali bin Abdallah Al-Dhafaariy na Sheikh Sa'ad Diin Al-Dhafaariy. Baadhi ya hawa wanafunzi wa Saahib Mirbaat ndio waliokuja kuwa masheikh wa Al-Faqiih Al-Muqaddam kama tutakavyo kuja kuona.

Saahib Mirbaat alikuwa mkarimu sana kwa ndugu zake, jamaa zake na wengine, hata walihesabu nyumba ambazo alikuwa akizitolea nafaka zikafika 120. Alikuwa akifikiwa na mgeni hujitahidi mno kumkirimu. Imepokewa kwamba alifikiwa na mgeni, na hakuwa na kitu, akaomba kwenye nyumba ambazo alikuwa akiwasaidia. Kikakusanyika maradufu ya alichokuwa akiwapa. Sehemu kubwa ya mali yake ilikuwa ni mitende iliyopo Bayt Jubayr. Mavuno yakizidi mahitaji yake hutoa sadaka. Imaam Muhammad bin Aliy alikuwa mtu mwenye kusafiri sana. Hakufika katika mji, ila waliukiri utukufu wake na walimkirimu kadiri walivyoweza. Alipofika katika mji wa Mirbaat akatua hapo, ikawa ndio sababu ya kuendelea kwa mji huo. Watu wa Mirbaat walipata faida nyingi za kielimu na maarifa kutoka kwake. Jina la Saahib Mirbaat amelipata kutokana na kazi yake aliyoifanya katika mji huo. Alifariki mwaka 561 na kuzikwa huko, na kaburi lake ni maarufu na linazuriwa hadi sasa.

Saahib Mirbaat alipata watoto wanne: mabwana Alawiy, Aliy, Ahmad na Abdallah. Bwana Aliy akamzaa Al-Faqiih Al-Muqaddam. Kati ya hawa watoto wanne Bwana Aliy na Bwana Alawiy (mashuhuri kama Ammil-Faqiih) ndio walioendeleza kizazi cha Ba Alawiy, kwa hiyo sharifu yeyote wa Ba Alawiy aliyepo sasa ima ananasibika kwa Al-Faqiih Al-Muqaddam au Ammil Faqiih (Bwana Alawiy).

Muhammad bin Aliy Ba Alawiy (Al-Faqiih Al-Muqaddam)

Jina lake kamili ni Al-Faqiih Al-Muqaddam Muhammad bin Aliy bin Muhammad (Sahib Mirbaat) bin Aliy (Khaali Qasam) bin Alawiy bin Muhammad bin Alawiy bin Ubeydillah bin Ahmad (Al-Muhaajir) bin Isa bin Muhammad bin Aliy (Ureidhiy) bin Ja'afar (Saadik) bin Muhammad (Baaqir) bin Aliy (Zainil-Abidina) bin Husain bin Aliy bin Abi Talib(ra). Na Sayyidna Husain ni mtoto wa Sayyidatna Fatima bint Rasulillah Muhammad(saw).

Alizaliwa Tariim mwaka 574H, akakulia hapo, akahifadhi Qur-ani na kusoma elimu kwa jitihada kubwa. Miongoni mwa masheikh zake ni Sheikh Abdallah bin AbdulRahman Ba-Ubaid, mwanachuoni mashuhuri na mwandishi wa kitabu *Al-Ikmaal*. Bwana huyu alikuwa haanzi darsa mpaka Al-Faqiih ahudhurie. Masheikh wake wengine ni Qadhi Ahmad bin Muhammad Ba-Isa, Sheikh Aliy bin Ahmad Ba-Marwan, Sheikh Muhammad bin Ahmad bin Abil-Hubb, Sayyid Aliy bin Muhammad Ba-Jadiid, Sayyid Salim bin Basriy bin Abdallah bin Basry bin Ubeidillah, Sheikh Muhammad bin Aliy Al-Khatib na ammi yake Sayyid Alawiy bin Muhammad Sahib Mirbaat. Pia alichukua elimu kwa Sheikh Sufyaan Al-Yamaniy, mwanachuoni mashuhuri alipozuru Tariim. Al-Faqiih alikuwa hodari sana, hata imepokewa sheikh wake Bwana Ba-Marwan alimwambia kuwa amefuzu shuruti zote za kuwa Imamu Mkuu. Aliwahi kuulizwa masuala 300 katika elimu tofauti akayajibu yote kwa jawabu bora kabisa na kuondoa mushkil wote. Nyumba yake ilikuwa wazi kwa mayatima, mafakiri na wajane, hata mkewe Bibi Zaynab akiitwa Ummul-Fuqaraa. Al-Faqiih akijiwa na mgeni humsogezea chakula kingi, na yeye akichukua baraka ya kile kinachobaki kwa kukila yeye.

Al-Faqiih Al-Muqaddam ndiye marejeo ya Alawiyyin wote kwenye Tariqa. Yeye amepokea kwa Sheikh Abu Madyan Al-Tilmisaani kwa kupitia Sheikh AbdulRahman Muq-a'd na Sheikh Abdallah Saleh Maghribiy. Baada ya kuingia kwenye tariqa na kubadilisha mavazi yake, sheikh wake Ba Marwan alikasirika sana, akasema tulitarajia

utakuwa kama Ibn Furik (Mwanachuoni maarufu katika Fiq-hi), ukachagua njia ya tasawwuf na ufakiri. Al-Faqiih akajibu: "Huo ufakiri ndio fakhari yangu na ndio ninao tumia kumshinda shetani na nafsi, na wala sitokaa mbali na nyie kwa kukupeni mgongo, wala sijapata badala yenu."

Wakati huo watu wa Hadhramout walikuwa wameshughulika zaidi na elimu za fiq-hi na hadithi za Mtume(saw), na hawakuwa wakijua tariqa za kisufi wala mwenye kueleza istilahi zao, na Al-Faqiih ndio akawa wa mwanzo kueneza katika pande hizo. Kutoka kwake wamepokea watu wengi. Waliokuwa mashuhuri kati yao ni Sheikh Abdallah bin Muhammad Ba-Abbaad na ndugu yake Abdul Rahman, Sheikh Abdallah bin Ibrahim Ba-Qushair, Sheikh Said bin Umar Bal-Haaf, Sheikh Ibrahim bin Yahya Ba-Fadhl, Sheikh Aliy bin Muhammad Al-Khatib na ndugu yake Ahmad, Sheikh Sa'ad bin Abdallah Akdar na watoto wake mwenyewe mabwana Alawiy, Abdallah, na Ahmad, na watoto wa Bwana Alawiy ambao ni mabwana Abdallah na Aliy na Sheikh Abubakar bin Ahmad.

Amesema Imaam Sufyan Thawriy: Mwenye kupata sifa mbili tu katika hizi, kutakuwa hakuna bora kuliko yeye katika watu wa zama zake: Sharifu wa ki-Sunni, Faqih wa ki-Sufiy, na mwanachuoni ***Zaahid*** (mwenye kuupa nyongo/mgongo ulimwengu/asiye na tamaa na ulimwengu), Tajiri mwenye kunyenyekea, na Fakiri mwenye kushukuru. Na si tu sifa mbili bali zote amezipata Al-Faqiih Al-Muqaddam kama wanavyosema wanavyuoni waliomshuhudia.

Na walikuwa masharifu wa wakati huo wanakuwa na silaha popote wanapokuwa kama walivyokuwa watu wengine wa sehemu hizo, Al-Faqiih akavunja tabia hiyo, akatupilia mbali upanga, na kizazi chake wakamfuata katika hilo. Kisa chake ni kama kifuatavyo:

Kilipungua sana kizazi cha Al-Muhaajir wakati wake Al-Faqiih, hata hakubakia ila yeye Al-Faqiih, watoto wake na watoto wa ammi yake Alawiy. Idadi ya hawa wote haikuzidi hata kumi na kitu. Al-Faqiih na watu wake walikuwa wakibeba silaha kama ambavyo wanafanya watu wa sehemu hizo kwa ajili ya kujihami, na walikuwa wanakubaliwa kwa elimu, utajiri, uongozi na kusikika kwa maneno yao. Wakatia fitna

baadhi ya watu kwa wafalme kuwa Alawiyyin wanataka kusimamisha dola yao kwani Tariim ilikuwa ni mji mkuu wa Hadhramout. Akaamua Al-Faqiih kuvunja tuhuma hiyo, na kwamba hawakuwa na haja ya kusimamisha dola yao tangu walipohamia Hadhramout, na haya yalitokea baada ya kufariki kwa Imaam Alawiy, ammi yake. Hivyo Al-Faqiih Al-Muqaddam akawaita viongozi wa mji na akasimama akatoa khutba na kuuliza, "Je dola inasimamishwa kwa nini?" Wakasema, "kwa upanga". Naye akasema, "Mimi hapa nauweka chini upanga wangu (sitautumia tena) kuvunja hizi khabari za uongo". Katika mahafali hii alihudhuria Sheikh Said Al-Amuudy. Al-Faqiih akampa upanga ule ukabakia kwake hadi akafariki. Kwenye riwaya nyengine kuwa alivunja upanga wake na kumwachia Sheikh Said.

Fitna hii ilitokana na kuwa watoto wa Al-Muhaajir walikuwa wakikubaliwa na watu kwa wanayoyasema. Watawala wakawa wanaogopa wasije wakawapindua. Imepokewa kuwa ammi yake Al-Faqiih alikuwa akikubaliwa na watu kiasi ambacho angewaambia watu wampindue mfalme wangefanya hayo. Na mfalme alikuwa akijua hayo hata akapanga njama ya kumpa sumu.

Amesema Al-Habiib Aliy bin Husain Al-Attaas katika kitabu chake *Taajul-Aaraas*: Kwa kuvunja upanga, Al-Faqiih amejiweka mbali, yeye na kizazi chake, na fitina ambazo Mtume(saw) alishazibashiria kwa Hadithi yake iliyopokelewa na Imam Muslim kama ifuatavyo: "Zitatokea fitina (kubwa), atakayekaa ni bora kuliko atakayesimama, na mwenye kusimama ni bora kuliko mwenye kwenda, na mwenye kwenda ni bora kuliko mwenye kukimbia, na mwenye kuirondea ataipata, na atakayeweza kuwa mbali nayo na ajilinde". Kwenye riwaya nyengine: "Mwenye kulala ni bora kuliko aliyemacho, na aliye macho ni bora kuliko mwenye kusimama". Akaendelea hadi akasema: "Atachukua upanga na kuvunja makali yake kwa jiwe". Amesema Imaam Nawawiy kwenye sherehe ya Sahiih Muslim: "Ama neno lake Mtume(saw), "atakaye pata njia ya kuwa mbali nayo", maana yake atakayeweza kupata sehemu akakaa mbali nayo (fitna hiyo) basi akae mbali nayo. Ama neno lake "mwenye kukaa ni bora kuliko aliyesimama", linaonyesha hatari yake na umuhimu wa kukaa mbali nayo na kuikimbia, wala asijiingize kwa lolote, kwani shari yake na

fitina yake itakuwa kwa kiasi cha kujiingiza ndani yake. Na ama neno lake “atachukua upanga wake na kuvunja makali yake kwa jiwe”, muradi wake ni kuvunja upanga kwa hakika hasa kwa maana ya dhaahiri ya hadithi, ili ajifungie mlango kwenye vita hivi, na imesemwa pia kuwa maana yake ni kuacha kupigana, na kauli ya mwanzo ndiyo sahihi zaidi.

Al-Faqiih alikuwa mkarimu sana, alikuwa na mitende, na alikuwa akiweka mavuno yake yaliyo bora baada ya kutoa mahitaji yake kwenye mapipa makubwa 360 kwa ajili ya kutoa sadaka kila siku kwa mafakiri na wahitaji. Alikuwa pia mwenye jitihada sana kwenye ibada, akifunga mchana na kusimama usiku katika shiib Nueir, akisoma Qur-ani sana, kila akimaliza khitma huanza nyengine.

Pamoja na utukufu wake, Al-Faqiih alikuwa mnyenyekevu sana, hata alikuwa akinunua samaki sokoni akimbeba mfukoni hadi nyumbani kwake. Alikuwa akijitahidi kila anachokifanya kiwe ni kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna. Wala hakuweka alama fulani wala kuweka sharti maalum kwenye tariqa yake litakayoinasibisha na umashuhuri. Bali tariqa yake ilikuwa ni ufakiri wa uhakika na kudhalilika moja kwa moja kwa Mwenyezi Mungu.

Na Al-Faqiih Al-Muqaddam amekiombea kizazi chake kwa dua tatu: Ya kwanza kuwa na mwendo mwema; ya pili Mwenyezi Mungu asiwatawalishie dhalimu juu yao atakayewaudhi; na ya tatu asife mmoja wao ila amesitirika.

Amefariki Al-Faqiih Al-Muqaddam siku ya Ijumaa mwisho wa mwezi Muharram 653 H, akiwa na umri wa miaka 79, na kuzikwa Zanbal. Kaburi lake ni mashuhuri.

Maneno ya Ba Alawiy kuhusu Al-Faqiih Al-Muqaddam.

Amesema Sayyidna Abdul Rahman bin Muhammad Al-Saggaaf, *“*Hatumfadhilishi (Hatumtangulizi au hatumfanyi kuwa bora) yeyote juu ya Al-Faqiih Al-Muqaddam baada ya masahaba ila ambaye imepokewa nassi ya kufadhilishwa kwake, kama Uways Al-Qaraniy

Mwenyezi Mungu awaridhie wote, na sisi pia aturidhie na atupe baraka zao” .

Amesema Habiib Abdallah bin Umar bin Yahya, “Hakika Saada (mabwana viongozi) wetu wa Aali Ba Alawiy kabla ya Sayyidna Al-Faqiih Al-Muqaddam walikuwa wamejisitiri kwa kubeba silaha kwa mwendo wa masahaba(ra) kwa elimu na amali. Hawakudhihiri kwa kufuata umashuhuri, karama na kufuata tariqa ya kisufi ila wakati wa Sayyidna Al-Faqiih Al-Muqaddam na baada yake”.

Tasawwuf:

Amesema mwenye *Mashra'*: "Hakika tariqa ya kufuata Sunna ndio njia iliyo nyooka na mfumo/taratibu iliyo simama sawasawa, na walikuwa Waislamu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu-rehema na amani zimshukie-wakiwaita walio wabora miongoni mwao katika enzi zao kwa sifa ya usahaba, kwa sababu ya utukufu wake juu ya kila sifa na nasabu. Kisha wakawaita wale walio wadiriki hao kwa jina la Taabiin, kisha zilipo pita (zama) zilizo kuwa mbali na zama za utume na ukapita muda mkubwa (kitambo kirefu) na zikakhitalifiana rai, walipwekeka watu makhsusi katika Ahlil-sunna kwa matendo mema na hali njema na wakatangaa kwa jina la Suufiya na hiyo ndio ikawa nembo iendeleayo na khabari yakini. Na zimetofautiana ibara za Wanazuoni katika kuelezea ujuvyo (fasiri) wake (hiyo Tasawwuf) na kuondokea hapo ndio alisema Sheikh Abu Muhammad Al-Juwainiy: "Hakuswihi kuelezea juu ya sufiyya kwa sababu wao hawana mpaka maarufu" na ilivyo sahihi ni kuswihi kwake. Na maneno yaliyo mazuri mno katika kuizungumzia Tasawwuf ni yale yaliyo nenwa na Imaam Ghazaaliy-Mwenyezi Mungu amuwiye radhi: "Hiyo (Tasawwuf) ni kumuweka Mwenyezi Mungu moyoni peke yake na kukiona duni kila kisicho Yeye. Na ama fasiri yake kwa maana ya elimu, basi hiyo (Tasawwuf) ni elimu ya usuuli (misingi) ambayo kwayo hujulikanwa utengevu wa moyo na viungo vingine." Na baadhi ya wahakiki mambo wamesema: Sufiy (Mwana Tasawwuf), ni mwanachuoni mtendea elimu yake kwa njia ya Ikhlaasi (kumtakasia matendo Mwenyezi Mungu) na wala hakuswihi mtu kwenda juu zaidi ya ujuvyo huu. Na amesema Al-Hafidh Suyuuty: "Na watu wengi wanadhania ya kwamba atakaye viendea vitabu vya usufi na akasoma kitu katika vitabu hivyo na akaandika na akasherehesha, huyo huitwa Sufiy (mwana Tasawwuf) na ilhali si hivyo. Hakika si vinginevyo, Tasawwuf ni elimu ya hali na wala si elimu ya maneno, nayo ni mtu kujipamba na tabia njema zilizo pokewa katika Sunna ya Mtume na ni kwa ajili hiyo ndio Wanazuoni wakasema: Tasawwuf ni elimu iliyo fungamanishwa na Hadithi na misingi ya dini, basi atakaye ishiba na akakitendea kile alicho kijua na itikadi yake ikawa ni sahihi, huyo ndio huwa Sufiy. Hivi huoni kwamba mmoja wao aliacha kula tikiti kwa tende kwa sababu tu haikuthibiti

mbele yake namna ambavyo Mtume wa Mwenyezi Mungu alivyo lila, ijapo thibiti asili ya kuliwa kwake."

Maneno ya wanavyuoni juu ya Tasawwuf

Sheikh Abul Qasim Al-Qushairiy(ra) amesema katika kitabu chake *Ar-risaalatu Al-Qushairiyyah,*

"Fahamuni - Mwenyezi Mungu akurehemuni - ya kwamba Waislamu baada ya kifo cha Mtume(saw) hawakuunasibisha ubora wao katika zama zao na elimu zao, bali kwa usuhuba wao na Mtume wa Allah(saw). Kwani hakuna jina lililo bora zaidi ya hilo, ndiyo wakaitwa "Maswahaba". Na wale walioishi zama za pili, wakasuhubiana na maswahaba wakaitwa kwa jina la "Taabiina", nao wakaliona kuwa hilo ndilo jina tukufu mno; kisha wakaitwa wale waliokuja baada yao Wafuasi wa Taabiina – yaani "Taabii taabiina". Baada ya hapo, watu wakakhitalifiana, na daraja zikatofautiana. Wale waliojishughulisha mno na dini wakaitwa "*Zuhaadi*" – yaani wapa nyongo Dunia, na "Ubbaad" – yaani wenye kuabudu sana. Kisha zikadhihiri bidaa na yakapatikana madai, na kila kikundi kikadai ya kwamba miongoni mwao wamo ma-Zuhaad. Hapo *khawaasu* katika Ahli Sunna, wale wenye kuzichunga nafsi zao wakazihifadhi nyoyo zao na vizuka vya mghafala, wakajitenga kwa jina la masufiy. Jina hilo likatangaa kwa mabwana wakubwa baada ya miaka mia mbili tangu Hijra."

Ibn Khaldun amesema, "Elimu hii – yaani Tasawwuf – ni miongoni mwa elimu za sheria zilizozuka katika Uislamu. Asili yake ni Salaf wa Umma ambao ni miongoni mwa maswahaba na Taabiina na waliokuja baada yao. Hii ni tariqa ya haki na uongofu**.** Msingi wake ni kushikilia ibada na kujitoa kabisa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujiepusha na starehe na mapambo ya Dunia. Hii maana yake ni kuvipa nyongo vile vinavyoendewa na watu walio wengi, yaani mali na vyeo; pia kujitenga na viumbe na kukaa faragha kwa ajili ya ibada.

Mwenendo huu ulikuwa umeenea miongoni mwa maswahaba na Salaf. Katika karne ya pili watu walipoelemea sana katika kuitumikia dunia wengine wakajitenga na kuipa nyongo dunia; hawa wakaitwa Suufiya na Mutasawwifa."

Maruuf Al-Karkhy amesema, "Tassawuf ni kuzishika (kuzifuata) "hakika" (ni neno katika Istilahi za Tassawuf lenye maana ya kufunuliwa kuona uhakika wa mambo na hayo hupatikana baada ya kudumu juu ya ibada kwa muda mrefu) na kukupukwa na vile vilivyomo mikononi mwa viumbe. Sheikh Zakariya Al-Answaariy-Mwenyezi Mungu atunufaishe naye-amesema katika (*Sherehe ya Risaalah)*: "Kwa sababu yule aliye mtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu na akajua ya kwamba hakuna awezaye kudhuru wala kunufaisha, hakuna anaye weza kutoa au kuzuia asiye Yeye, na akajishughulisha na yale yanayo mkurubisha kwenye hakika (mambokweli), basi huko kunapelekea kukupukwa na vile vilivyomo mikononi mwa viumbe mpaka asimtegemee ila Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Imaam Juneid Al-Baghdaadi

"Hatukuitwaa Tassawuf kwa maneno matupu, lakini tumeipata kwa njaa, kukesha, kuiacha Dunia na kukata tulivyo vizoea na vizuri vipendwavyo".

Imaam Ghazaaliy

"Jua ya kwamba Tassawuf ina mambo mawili; Kuwa na msimamo kwa Mwenyezi Mungu na kuwa mtulivu kwa viumbe, basi yule atakaye kuwa na msimamo kwa Mwenyezi Mungu na akawa na tabia njema kwa watu na akaamiliana nao kwa upole, huyo ndiye Sufiy. Na kuwa na msimamo kwa Mwenyezi Mungu: Ni mtu kulitoa fidia fungu la nafsi yake kwa ajili ya mtu mwingine. Na tabia njema: Ni kutowatendea kwa

mapendeleo (matashi) ya nafsi yako bali huipeleka nafsi yako kulingana na mapendeleo yao maadam hayakhalifiani na sheria."

Sheikh Umar Sahrawardiy

“Mwanzo wa Tassawuf ni elimu, katikati yake ni amali na mwisho wake ni kipawa. Basi elimu hiyo ndio ifichuayo muradi (makusudio), na amali husaidia katika kutafuta na kipawa hufikisha kwenye lengo la mwisho.”

Maneno ya Aali Ba Alawiy kuhusu Tasawwuf

Aliulizwa Habiib Abdillah Haddaad – Mwenyezi Mungu amrehemu – kuhusu maana ya Suufi na Tasawwuf na nini akikifanya mtu huwa ni Suufi (Mwana Tasawwuf)? Akajibu: “Ama Sufiy ni kama walivyo sema baadhi ya wenye kumjua Mwenyezi Mungu(***Aarifiina Billah***): (Kwamba) Sufiy ni yule aliye takasika na vunju (***kadar***-taka) na akajaa mazingatio na akajitoshea na viumbe kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na zikawa sawa mbele yake dhahabu na dongo la mfinyanzi**.**

Na ama tassawuf nayo ni kama walivyo sema baadhi yao (hao wamjuao Mwenyezi Mungu): (ya kwamba) Tassawuf ni kujitoa kwenye kila tabia duni na kujiingiza kwenye kila tabia nzuri.

Na imepatikana khilafu nyingi baina ya wana tariqa katika kuielezea Tassawuf ni nini na Sufiy ni nani. Na haya tuliyo yataja ndio katika maana bora na jumuishi mno.

Basi yule ambaye yatakayo takasika matendo yake, kauli zake, nia zake na tabia zake, kutokana na taka za riyaa na akayasafisha na kila kitu kinacho mkasirisha Mola na akaenda kwa baatini na dhaahiri yake kwa Mwenyezi Mungu na kwenye twaa yake. (Akafanya hivyo) pamoja na kuvipa mgongo vyote visivyo Yeye na akayakata mambo yatakayo mshughulisha na kumkosesha faragha na jambo hili katika ahali, mali, matamanio, cheo na matamanio ya nafsi, na yote hayo yakakutanishwa na elimu (ujuzi) na kukifuata Kitabu (Qur-ani) na Sunna (Hadithi) na

muongozo wa Salaf wema, basi huyo ndiye Sufiy aliye kamilika. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Mjuzi mno.” *Mwisho wa kunukuu*

Amesema Habiib Aliy bin Hasan Al-Attaas wa Mash-had

“Na hakika yake (Tassawuf) iko katika mambo mawili, nayo ni: Salama ya moyo na ukarimu wa nafsi. Mawalii hawakupata daraja walizo zipata kwa sababu ya swala wala swaumu nyingi, na hakika si vinginevyo waliyapata waliyo yapata kwa sababu ya salama ya nyoyo na ukarimu wa nafsi.

Na muhimili wake – yaani Tassawuf – uko katika jambo moja, nalo ni tabia njema. Na wamesema: Tassawuf yote ni tabia njema, basi yule atakaye zidi kwako katika mizani ya tabia njema, huwa amezidi kwako katika Tassawuf. Na tabia njema imekusanywa katika mambo matatu, nayo ni: Kuzuia adha (maudhi), ukarimu wa kutoa na ukunjufu wa uso."

Mwisho wa kunukuu

Amesema Habiib Abdillah Haddaad-Mwenyezi Mungu amrehemu:

“Tariqa za Tassawuf zijapo kuwa nyingi, zote hizo ni tariqa moja tu, nayo ni kupambana na nafsi na kujinasua na kila inacho kilingania (katika maovu, maasi na matamanio ya nafsi), na hilo ni jambo gumu”.

Mwisho wa kunukuu

Tariqa ya Aali Ba Alawiy:

Katika kuzungumzia Tariqa ya Aali Ba Alawiy, Habiib Abdillah Al-Haddaad amesema, “Ama Tarika yetu kwa ujumla, haihitaji sherehe, kwani iko ndani ya Qur-ani na Sunna na kufuata waja wema walio tangulia, hakuna zaidi”.

Habiib Abdul Rahman bin Abdallah Balfaqiih pale alipo ulizwa kuhusu wasifu wa Tariqa ya Aali Ba Alawiy, akasema: “Tariqa ya Aali Ba Alawiy ni katika tariqa za kisufi, na misingi yake ni kufuata Qur-ani na Sunna”. Mahala pengine alisema: “Maana yake ya dhaahiri, ni kujua na kutenda kwa mujibu wa elimu, na maana yake ya ndani ni kuelekea kwa Mwenyezi Mungu kwa ukweli kwa kutenda anayo yaridhia. Basi (Tariqa hii) imekusanya kila tabia njema, na kujizuia na kila sifa mbaya, na lengo lake ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kupata kufunguliwa kwa njia bora."

Anamalizia kwa kusema: “Hakika wamekubaliana kumzuia muridi wakati anapo anza kutafuta kuhama tariqa moja hadi nyengine, na kutoka kwa sheikh mmoja hadi mwengine, kwani hilo linamdhuru kwa kutawanya himma yake na kuyatapanya yale aliyo yakusanya. Kwani moyo wake anapo anza ni sawa na jeraha, linadhurika kwa kuchanganya (madawa) na upepo, mpaka lipone na kukauka kwa mkono wa tabibu ambaye ameshikamana naye, na mwenye kumponyesha ambaye anaelewa dawa yake na uhakika wake”.

Amesema Habiib Abdallah bin Umar bin Yahya: “Ufupi wa maneno katika kuielezea Tariqa hii, ni kwamba hiyo ni kuzigawa nyakati kwa kutenda amali njema, pamoja na ukamilifu wa kumfuata katika matendo hayo Bwana wa mabwana (Mtume (saw)). Na kuzifanya ziwe sawa kwa kuzitakasa na taka na maafa (yanayo weza kuzibatilisha) na kuutwahirisha moyo kutokana na kila tabia duni (mbaya) na kuupamba na kila tabia njema. Na kuwaonea huruma na sikitiko waja wa Mwenyezi Mungu, na kutoa upeo wa juhudi katika kuwafundisha na kuwaongoza kwenye yale ambayo umo ndani yake uokovu. Na kujiepusha na haramu na shubuhaati (mambo tatizi) na kufanya uchache

wa yaliyo halali na matamanio na kuupatia faida muda wa umri kwa kujitenga (kwa ajili ya ibada)...Kwa hivyo basi, wasichanganyike na watu ila kwa ajili ya kujifunza na kufunza, na kwa ajili ya kuhudhuria swala za jamaa na Ijumaa na kumzuru kila aliye kipenzi na kuziamirisha ziara hizo kwa kudurusi elimu mbali mbali. Na kuwaunga jamaa na ndugu na kumtendea wema kila mtu na kuwa na tangamano jema. Na kuamrisha mema na kukataza maovu na kumsaidia mwenye shida, pamoja na kujilinda, kujiepusha na haramu, kuwa mnyenyekevu na kumuangalia Mzumbuzi (Mwenyezi Mungu Muumba pasina mithali) na kutekeleza ahadi, kuipa mgongo Dunia na kumtegemea Mwenyezi Mungu".

Habiib Aliy Habashy amesema kwenye moja ya kasida zake ambazo kuna wasiya kwa wote wanao mfuata:

وها هي أعمال خلت عن شوائب وعلم وأخلاق وكثرة أوراد

Na hiyo (tariqa) ni matendo yasiyo na taka

na ni elimu, tabia (njema) na nyiradi nyingi.

Habiib Ahmad bin Hasan Attas alipo ulizwa kuhusu Tariqa ya Alawiyya, alisema: "Ionekanavyo kwa nje ni Ghazaaliyya na undani wake ni Shaadhiliyya, yaani dhahiri yake (upande wa nje) ni kujivua na tabia mbaya na kujipamba na tabia njema, na batini yake (upande wa ndani) ni kushuhudia fadhila za Mwenyezi Mungu tangu khatua ya mwanzo". Hii ina maana kwamba wanajitahidi kufanya amali za kheri, lakini hawazitegemei hizo amali, bali wanategemea fadhila za Mwenyezi Mungu. Na akasema tena: "(Tariqa hii) imefungika kwenye ubeti mmoja katika maneno ya Habiib Abdillah Haddaad:

والزم كتاب اللّٰه واتبع سنة واقتد هداك اللّٰه بالأسلاف

Na lazimiana na kitabu cha Mwenyezi Mungu na fuata sunna

Na uwafuate Salaf, Mwenyezi Mungu akuongoze.

Amesema Habiib Ahmad bin Abi bakr bin Sumeit: “Hakika tariqa ya Alawiyya imekusanya siri za tariqa zote za kiislamu, na imejitambulisha kwa sifa bora, kwani imejengwa kwa mapito ya shadhiliyya na walio enda mfano wa mwendo wao kwa uhakika wa kumtegemea Mwenyezi Mungu na kumpwekesha. Na mwenendo wa Ghazaaliy katika jitihada za kufanya ibada, na hakikuingia kitu cha kuibadilisha, bali watu wake (wanao ifuata) wamedumu juu yake pamoja na kupita zama, wakirithishana tabaka hadi tabaka mpaka ikafikia zama zetu”.

Maana ya kuwa Dhahir ni Ghazaaliya na Batin ni Shadhiliyya

Maana yake sio kwamba tariqa yao imenukulu tu mpangilio wa Imaam Ghazaliy au mpangilio wa Sayyid Abul Hasan, kwani Aali Ba Alawiy walikuwa na sifa hizi hata kabla ya kudhihiri maimamu hawa, ila ina maana ifuatayo:

Dhahir ni Ghazaaliyya: Maana ni kuwa wanajitahidi kufanya amali za kheri kiasi cha uwezo wao kama ambavyo Imaam Ghazaliy alivyo eleza kwenye vitabu vyake khasa Ihyaa Uluumul-Din.

Batin ni Shadhiliyya: Pamoja na jitihada wanazo fanya, hawategemei kuwa matendo ya kheri ndio yatawanyanyua daraja kwa Mwenyezi Mungu, bali ni fadhila zake Mwenyezi Mungu, na huo ndio msingi wa shadhiliyya kutokutegemea amali.

Amesema Habiib Alawiy bin Tahir Al-Haddaad kwenye *Uquudul-Al-almaas*: “Fahamu kwamba uzuri mno wa tariqa ya shadhiliyya uko kwenye neno lao, kuona fadhila zote zinatoka kwa Mwenyezi Mungu, kulazimikiana na kushukuru na kuwa na ukweli kwenye utumwa (wa Mwenyezi Mungu). Kuepukana na vyeo vyote (vya kidunia), na kujijua kwa ajizi (ushindwa) na kutokutekeleza amri kwa jinsi inavyo takiwa, hii ndio jumla ya misingi yake.”

Maneno ya Sheikh Yusuf Ismail Nabahaniy:

Amesema Sheikh Yusuf bin Ismail Nabahaniy katika kitabu (*Riyaadhul Jannah fi Adhkaaril-Kitaab wal-Sunna*) baada ya kumtaja Habiib Zaynil Abidina Jamalillayl; mkazi wa Madina Munawwara: "Hakika mabwana wetu wa Aali Ba Alawiy ambaye huyu mtukufu ni katika wao-Mwenyezi Mungu awaridhie-wamekongamana umma Muhammadiyya katika zama tofauti na miji tofauti kuwa ndio walio sahihi mno katika Ahlil bayt wa Mtume, kwa nasabu na wenye kuthibitika kwa asili sharifu (tukufu) na wenye elimu zaidi na wenye matendo (mema) zaidi, na wenye utukufu zaidi na wenye tabia njema zaidi. Na wote ni katika Ahlil Sunna na Jamaa juu ya madhehebu ya Imaam wetu Shafii-Mwenyezi Mungu amridhie, pamoja na wingi wao hawapungui watu laki moja, na pamoja na kuwa jirani kwenye mji wao, nao ni mji wa Hadhramout na Zaydiyya na Rawaafidh waliovuka mipaka katika Yaman. Na pamoja na kutawanyika kwao kwenye miji mingine, khasa India na wingi wa Shia miongoni mwao, hatujasikia kuwa mmoja wao ameacha madhehebu yake ya Ahlil Sunna na Jamaa, wakiwa na hifadhi ya Mwenyezi Mungu. Ama wanachuoni wao wakubwa na mawalii wao wema wenye siri na nuru katika zama hizi na zama zilizo tangulia ni wengi sana, na wenye nuru zaidi ya nyota za mbinguni kwa kila mwenye kuwafuata kwa uongofu, na hakuna mwenye shaka ya nasabu yao na wingi wa fadhila zao na yanayo watofautisha na wengine katika watu kwa baraka ya babu yao (Mtume)-juu yake rehema na amani, (hakuna mwenye shaka) ila yule ambaye ana sehemu ndogo katika Uislamu. Na hakika nimepitia baadhi ya vitabu vyao nikaona vyote ni uongofu, vinaondoa uchafu juu ya moyo. Na nimekutana na baadhi yao, nikakuta wana fadhila na tabia njema ambazo zinajulisha asili njema ziyada kwa waliyo nayo katika asili/nasabu tukufu na yanayo tuliza macho na kufurahisha moyo. Na nimeandikiana barua na baadhi yao nikaona katika ibara zao miongoni mwa upole na unyenyekevu na ubora wa kuandika na kuathirika ambayo haiwezekani muumini yeyote akayaona kisha asimpende mwenye kuyaandika, mapenzi ya ndani. Na chochote utakacho kitaja katika khabari zao, miongoni mwa sifa njema na maneno mazuri basi ni kidogo kuliko yaliyo beba moyo wangu kwa kuwatawalisha kwa wema

na kuitakidi ukamilifu wao-Mwenyezi Mungu awaridhie na baki ya mabwana zetu wengine watukufu katika Ahlil-bayt. Na awafikishe wote katika wanayo yataraji katika kheri za duniani na akhera kwa jaha ya babu yao mbora wa viumbe-juu yake yeye na wao rehema na amani. Na aniruzuku fadhila zao kwa kupata radhi, kukubaliwa (na Mwenyezi Mungu amali njema nilizo tenda) na dua njema yenye kukubaliwa na ikikhitimishwa na Suratil-Faatiha basi ndio mwisho wa matarajio".

Maneno ya Sheikh Muhammad bin Ahmad Ba Jarfiil

Alipo ulizwa kuhusu Sheikh Abu Bakr Al-Adaniy, alisema: "Hakika Ahlil bayt ni bora ya watu, na Aali Ba Alawiy ni bora ya Ahlil-bayt kwa kufuata kwao Sunna na kwa yale yaliyo kuwa mashuhuri kwao katika ibada, kuupa mgongo Dunia, ukarimu, na tabia njema. Na Sheikh Abu Bakr ni mbora wa Aali Ba Alawiy kwa kongamano la Wanazuoni basi yeye ndiye mbora wa watu wa zama zake."

Maneno ya Sheikh Ahmad (Shahiid) bin Abdallah Bafadhl

Amesema Sheikh Ahmad (Shahiid) bin Abdallah bin Abdul Rahman Balhaaj Bafadhl-Mwenyezi Mungu amrehemu: "Hakika nimetembea miji mingi kama Makka ulio tukuzwa (na Mwenyezi Mungu), na Madina ulio pata sharafu (ya Mtume), na Yaman yenye utulivu na miji mengine. Na nimewaangalia mahujaji wengi ambao wanao kuja kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu tukufu kutoka pembe mbalimbali za miji na pande nyingine za mbali na nimemwuliza zaidi ya mmoja katika wanao tegemewa, sikukuta wala sikutajiwa katika masharifu mfano wa Aali Ba Alawiy, na tariqa yao kwenye istiqama, na kufuata Qur-ani na Sunna".

BAADHI YA VIONGOZI WA AALI BA ALAWIY

- Sheikh Abdallah Ba Alawiy
- Sheikh Abdul Rahman Saggaaf
- Sheikh Umar Mihdhaar
- Sheikh Abdallah Aydaroos
- Sheikh Abu Bakr Al-Adaniy
- Sheikh Abu Bakr bin Salim
- Al-Habiib Umar bin Abdul Rahman Al-Attaas
- Al-Habiib Abdillah bin Alawiy Al-Haddaad
- Al-Habiib Ahmad bin Zayn Al-Habashy
- Al-Habiib Umar bin Saggaaf Al-Saafiy
- Al-Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit
- Al-Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy
- Al-Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy
- Al-Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas
- Al-Habiib Abdallah bin Umar Al-Shatiry

Sheikh Abdallah bin As-a'd Al-Yaafi alipo andika kitabu chake *Rawdhul Rayyaahiin* katika kuelezea karama za mawalii na watu wema, akaulizwa mbona hujawataja watu wa Hadhramout, akasema: "Sikuwataja kutokana na wingi wao." Na alimtuma mtoto wake Bwana Abdul-Rahman akawazuru, akawazuru mara ya kwanza na ya pili na alipo ulizwa alijibu kwa beti hizi mbili:

مررت بوادي حضرموت مسلّما فألفيته بالبِشر مبتسما رحبا

وألفيت فيه من جهابذة العلى أكابر لا يلقون شرقا ولا غربا

Nimelipitia wangwa la hadhramout hali ya kuutolea salamu,

Nikaulaki kwa bashasha, hali ya kutabasamu na ukunjufu wa kifua,

Na nikakutana ndani yake na Wanachuoni wakubwa watukufu

Wakubwa (Watukufu) ambao hakuna mfano wao si Mashariki wala Magharibi.

Na kila akiulizwa, husema: "Nimewaona hawahesabiki kwa wingi na nuru zao zikiangaza."

Na huu ni uhakika hasa, na kwa nini wasiwe hivyo na wao wameombewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu siku ya ndoa ya Sayyidatna Fatma kwa dua ya kuwa wawe wengi na wema ? Amesema Habiib Abdillah Haddaad:

فهم الكثير الطيب المدعو لهم من جدهم حين الزفاف ألا تعي

Basi wao ni wengi wazuri walio ombewa

na babu yao siku ya ndoa, basi zingatia.

Na utawaona kila mtoto ameshikamana na tabia njema za baba yake na ana siri zake, na kila binti ameshikamana na tabia njema za mama yake na siri zake, basi vipi utaweza kuwahesabu na kuwajua, pamoja na tabia yao ya asili ya kujificha na kuwa na unyenyekevu mno ambayo inawafanya wasijulikane zaidi.

Na wameelezwa baadhi yao katika vitabu vinavyo taja tarjama zao, kama *Ghurar*, *Mashra'* na vingine, hata amesema mwandishi maarufu

Al-Amiir Shakiib Arsalan baada ya kukiona kitabu cha *Mashra'* ambacho wengi wa walio fanyiwa tarjama wameanziwa na "amezaliwa Tariim na kuhifadhi Qur-ani Tukufu", lau ningepata muda ningeandika kitabu nikakiita *Al-Hijrul Kariim fii man wulida bitariim wa hafidhal Qur-ani Kariim*".

Basi hatuna uwezo wa kuwataja ila baadhi yao ambao wamefanya kazi kubwa katika kueneza elimu na kufanya da'awa na athari yao katika Hadhramout na miji mingine ambapo Alawiyyin wamehamia na kufanya makazi yao ni kubwa.

Sheikh Abdallah bin Alawiy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam:

Amezaliwa mwaka 638 H, maarufu kama Sheikh Abdallah Ba Alawiy. Yeye ni wa mwanzo katika Aali Ba Alawiy kuitwa Sheikh.

Alimdiriki babu yake Al-Faqiih Al-Muqaddam katika utoto wake, na akapata kuangaliwa na kulelewa naye. Alisoma Fiq-hi kwa Faqiih Ahmad bin Abdul-Rahman bin Alawiy (Ammil Faqiih) bin Muhammad Sahib Mirbat, Sheikh Abdallah bin Ibrahim Ba Qushair. Alisoma Tafsiri, Hadithi, Fiq-hi na Tasawwuf kwa babu yake Al-Faqiih na baba yake, na alijitahidi kwenye elimu za lugha. Kisha akaenda mji wa Ahwar na kuchukua elimu kwa Sheikh Umar bin Maymun ambaye ni mwanafunzi wa Sheikh Ahmad bin Al-Ja'ad.

Alienda kuhiji mwaka 670 akiwa ana miaka 32, kisha akaenda Madina kumzuru babu yake na akakaa huko mwaka mmoja. Kisha akarudi Makka na kukaa miaka 8. Ikaenea baraka kwa watu wa Makka, hata walimwomba awaombee mvua, akawaombea na wakapata mvua na ukame na njaa vikaondoka. Sheikh Abdalla Ba Alawy alikuwa mashuhuri kwa kukubaliwa maombezi yake ya mvua tangu utotoni. Huko Makka alijitahidi kutafuta elimu hata akakusanya iliyo tawanyika kwa wengine. Jumla ya masheikh zake wanazidi elfu moja, na walimpa ruhusa ya kutoa fatwa na kusomesha (ijaaza). Kisha akazuru tena Madina na kukaa huko muda mrefu, baadaye akarudi Makka. Kwa mara nyengine tena walimwomba awaombee mvua, akawaombea na wakapata kwa baraka zake. Ukatangaa utajo wake kwenye miji na akatungiwa mashairi mengi ya kumsifia, na watu wa Haramain wakapata kusoma kwake, walio wakazi na wasio wakazi, khasa katika Tasawwuf na Usuul mbili. Alikuwa muda mwingi akiutumia alipokuwa Makka kwa ibada; usiku halali ila muda mdogo.

Alipofariki ndugu yake Sheikh Aliy bin Alawiy huko Tariim, walimwandikia barua ya *taaziya* (wakimpa pole), na wakimhimiza arudi kwa kuwa anahitajika nyumbani kwao. Akaondoka Makka, na kupitia Zabiid, wakati huo ikiwa imesheheni wanachuoni, akachukua

elimu kwa wanachuoni pamoja na watu kuchukua kwake. Kisha akaingia mji wa Taizz, akachukua kwa maulamaa wake na pia wakachukua kwake. Akatoa ijaza za Tariqa pamoja na yeye kuchukua kwao.

Kisha akaenda mji wa Ahwar akakuta Sheikh wake Umar bin Maymun amefariki, na wameshamwosha na kumkafini, wanasubiri kumswalia. Alipofika yeye wakamtanguliza kuswalisha. Kabla ya kufa, alipoulizwa nani atashika nafasi yake Sheikh Umar aliwacha wasia kwamba, "Baada ya kuniosha na kunikafini, atakuja mtu mwenye sifa kadhaa, mtangulizeni kuswalisha, na yeye ndio atashika nafasi yangu". Alipokuja Sheikh Abdallah Ba Alawiy na zile sifa zote wakamtanguliza, na baadaye wakataka akae kwao na ashike nafasi ya Sheikh. Yeye akatoa udhuru ila akapendekeza mtoto wa Sheikh Umar anafaa kushika nafasi ile. Akamtawalisha ile nafasi na kumwambia, "Jikaze vizuri kwani nimeamrishwa nikutawalishe nafasi hii".

Kisha akaelekea mji wa Tarim. Wakazi wa Tarim wakamkaribisha wakiwa na furaha kubwa na mji mzima ukachangamka kwa kurudi kwake. Akasomesha sheria na tasawwuf. Watu kutoka kila pembe wakaja kwake kusoma, na tabia zake zikawavutia waliokaribu na walio mbali. Akanyanyua cheo cha masheikh na wakakaa mbele yake watu wengi kwa ajili ya kuchukua elimu. Na hakuna uwezekano wa kuwahesabu kwa idadi ilivyo kubwa, lakini hapa tutawataja walio mashuhuri, miongoni mwao ni watoto wake watatu, mabwana Aliy, Muhammad na Ahmad, mtoto wa ndugu yake Sayyid Muhammad Mawla Dawila bin Aliy, mabwana Abu bakr na Alawiy watoto wa ami yake Ahmad, na Sayyid Muhammad mtoto wa Alawiy tuliye mtaja hivi punde, Sheikh Abdallah mtoto wa Sheikh wake Ahmad bin Abdul-Rahman, Sheikh Aliy bin Silm, Sheikh Fadhl bin Muhammad Ba Fadhl, Sheikh Abdallah bin Faqiih Fadhl, Sheikh Muhammad bin Abu Bakr Ba Abbaad, Sheikh Muhammad bin Aliy Ba Shuayb Al-Ansary, Sheikh Muhammad bin Aliy Al-Khatib, Sheikh Ahmad bin Aliy Al-Khatib, Sheikh Abdul-Rahman bin Muhammad Al-Khatib, Sheikh Umar Bawazir, Sheikh Muflih bin Abdallah bin Fahd, mtoto wa Sheikh wake Umar bin Maymun wa Ahwar, na Sheikh Ba Hamran.

Sheikh Abdalla Ba Alawiy alikuwa mnyenyekevu sana, hata akichukia kuitwa Sheikh, pamoja na kwamba yeye ndiye wa kwanza kuitwa kwa jina hilo katika masharifu wa Ba Alawiy, kwani akijiona kuwa hajafikia daraja ya kuitwa hivyo. Alikuwa na watumwa na watumishi, wala hajikwezi juu yao, hula nao pamoja na baadhi ya wakati hata hula nao katika sahani moja akifuata mwenendo wa babu yake Mtume(saw).

Ama kuupa kwake nyongo ulimwengu, basi ukarimu wake unatosha kuthibitisha hayo. Hata alikuwa na kitabu chenye majina ya watu ambao alikuwa anawagawiya nafaka miongoni mwa mafakiri na wapita njia. Pia alikuwa akiwapa masharifu wote walioko Tariim kwa kilicho bora kabisa. Walikuwa majirani zake wote wako chini ya hisani yake na wanaishi kwa ukarimu wake. Jirani mmoja alikoka moto kwa ajili ya kutengeneza mkate nao hawana unga, ila wamefanya tu makusudi kwa kuona haya na wingi wa hisani yake. Alipojua akawasema sana na kuwalaumu, hata akawa na tabia ya kuwauliza watoto wao. Walikuwa mafakiri na masikini wamefunga mahema nje ya nyumba yake, na wageni wakiwa ndani ya nyumba yake wameshukia. Imepokewa kwamba alishawahi kutoa mali yake yote ila kidogo tu kwa ajili ya familia yake. Walikuwa watu wa Tariim inawajia nafaka yao bila ya kujua nani anawaletea, mpaka alipokufa ndio ikajulikana kuwa ni yeye. Pia aliweka wakfu kwa ajili ya msikiti wa Ba Alawiy, mitende na ardhi, visima na chemchem. Kwa ajili ya wageni wanaoshukia msikitini hapo aliweka kiasi cha dinar 90,000. Vile vile akaweka wakfu ardhi na mitende kwa wanaochimba makaburi na kuwazika maiti.

Sheikh Abdalla Ba Alawiy alimpa mwanafunzi wake Sheikh Muhammad bin Aliy Ba Shuayb Al-Ansariy ardhi kubwa akaotesha Sheikh Muhammad mitende mingi na hiyo sehemu ikaitwa Ba Shuayb. Utoaji wake ulikuwa ni mkubwa hawauwezi hata wafalme na akiwatanguliza wale anaowapa juu ya nafsi yake. Anasema mwanafunzi wake Sheikh Aliy bin Salim: Alijiwa Sheikh Abdallah Ba Alawiy na dinar 500 akazitoa zote na asibakize chochote kwa ajili ya familia yake. Kwa uhakika ukarimu wake ulikuwa wa kupigiwa mfano.

Ama jitihada zake kwenye ibada wamesema hakutokea baada yake aliyekuwa na jitihada kama za kwake, ikiwa ni urithi kutoka kwa baba

yake na babu yake. Alikuwa akienda kwenye majabali na mawandani, akiilazimisha nafsi yake ibada zilizo ngumu. Usiku alikuwa akizuru makaburi na misikiti, na alikuwa ni mwenye kulia na kusoma sana Qur-ani; vile vile alikuwa akiamrisha watoto wake na watu wake kusoma sana. Baadhi ya wacha Mungu wamesema, kuwa wengi katika kizazi chake wanafunguliwa kwenye kusoma Qur-ani, na kizazi cha ndugu yake Aliy bin Alawiy wanafunguliwa kwenye dhikri. Alikuwa mwenye kulia sana wakati wa kusoma Qur-ani, hata akapofuka macho, na huenda ukapita usiku mzima na yeye akilia. Na ilikuwa inapita siku yake nzima akiwa kwenye ibada, tangu wakati wa kula daku hadi baada ya Ishaa, halali ila kwa wa usingizi kidogo wa mchana. Amesema mtoto wa ndugu yake; Sheikh Mawla Dawila: "Sijaona kwenye safari zangu na kukaa kwangu mjini mfano wa ammi yangu Abdallah."

Ama karama zake, basi zilikuwa ni nyingi sana, pamoja na kwamba alikuwa akizificha kiasi anachoweza na akichukia kunasibishwa karama yoyote kwake yeye.

Na alikuwa akipenda kazi ya kulima na akiifanya sana pamoja na kuhimiza watu wake, na kuwaambia kuwa kilimo ndio chumo bora. Maneno haya yameafikiwa na wanavyuoni wengi kuwa kilimo ni bora kuliko biashara kama yalivyo elezwa hayo kwenye *Rawdha* na *Majmuu*. Na katika hadithi iliyo pokewa na Muslim: **"Hakuna mwislamu yeyote aliyeotesha chenye kuota ila huwa kwa kila mwenye kula ni sadaka kwake, na mwenye kunywa sadaka kwake, wala hakipungui kitu ila huwa ni sadaka kwake".** Na katika riwaya nyengine ya Muslim: **"Haoteshi mwislamu chenye kuota, wala halimi chenye kulimwa akala mtu yeyote au mnyama au ndege ila huwa ni sadaka kwake hadi siku ya kiyama".**

Alifariki siku ya Jumatano katikati ya Jamadil Uula mwaka wa 731 H, umri wake ukiwa 91 au 93.

Sheikh Abdul-Rahman Saggaaf.

Jina lake: Sheikh Abdul-Rahman Saggaaf bin Muhammad Mawla Dawila bin Aliy bin Alawiy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam.

Alizaliwa mwaka 739 Tariim, akahifadhi Qur-ani kwa Sheikh Ahmad bin Muhammad Al-Khatiib na akazifahamu vizuri elimu za Tajwiid na Qira-aat, kisha akashughulika na elimu zengine kwa himma kubwa; akasoma fiq-hi kwa maulamaa wengi; alishikamana na vitabu vya Imaam Ghazaliy na Imaam Abi Is-haaq Al-Shirazy, na akasoma sana *Wajiiz* na *Muhadhab* hata alikaribia kuvihifadhi, na alivisoma vitabu hivi kwa mwanachuoni bahari: Sheikh Muhammad bin Alawiy bin Ahmad bin Al-Faqiih. Kisha akaenda Ghayl akasoma kwa Faqiih Muhammad bin Sa'ad Ba Shkeil *Ihyaa*, *Risaala* (*Qushairiyya*), *Awaarif* na vingine, na akaenda kwa Sheikh Al-Islam Muhammad bin Abibakr Ba A'bbaad na kulazimiana naye, na yeye ndiye aliye nufaika naye zaidi.

Alipewa ruhusa na masheikh zake kufundisha na kutoa ijaza, akawa anafundisha Hadithi, Fiq-hi katika misingi na matawi yake. Akajiwa na wanafunzi kutoka Mashariki na Magharibi, na akawa analetewa mas-ala ya fatwa kutoka baharini na nchi kavu na wakapata watu wengi sana faida za kielimu kutoka kwake. Wanafunzi wake ni wengi mno, lakini hapa tutawataja baadhi tu, miongoni mwao ni watoto wake, watoto wa ndugu yake mabwana Abuud na Hasan, mabwana Abu bakr na Muhammad watoto wa Alawiy Al-Sheibah, Sheikh Muhammad bin Hasan Jamalil-Layl, Sheikh Muhammad bin Aliy Mawla Aideed, Sheikh Ahmad bin Umar, Sheikh Sa'ad bin Aliy Mad-haj, Sheikh Muhammad bin Abdul-Rahman Al-Khatib na mtoto wake Abdul-Rahman, Sheikh Abdul-Rahim bin Aliy Al-Khatib, Sheikh Aliy bin Muhammad Al-Khatib, Sheikh Shuayb bin Abdallah Al-Khatib, Sheikh Ahmad bin Abi Bakr Ba Hirmiy, Sheikh Abdallah bin Faqiih Ibrahim Ba Hirmiy, Sheikh Abdallah bin Ahmad Al-Amoody, Sheikh Aliy bin Ahmad bin Aliy bin Muslim, Sheikh Abdallah bin Muhammad Ba Shuraahiil, Sheikh Muhammad bin Mua'fiy, Sheikh Abdallah bin Naafi Ba Mundhir, Sheikh Isa bin Umar bin Bahlul, Sheikh Ahmad bin Aliy Al-Hibaaniy, Sheikh Sa'ad bin Abdallah Ba Antar, Sheikh Muhammad

bin Said Al-Maghribi, Sheikh Muhammad bin Ahmad Al-Umariy na wengine wengi. Darsa zake nyingi zilikuwa kwenye vitabu: *Basit*, *Wasiit*, *Muhadhab* na *Muharrar*, na wakati mwengine *Wajiiz* pia, na akimfundisha kila mwanafunzi kitu kinachomfaa. Alikuwa akiwahimiza sana wanafunzi wake kujitahidi kwenye matendo ya moyo, na alitaja siku moja ubora wa Fiq-hi, akaazimia mtoto wake Sheikh Umar Mihdhaar amalize umri wake kwenye Fiq-hi na awache elimu nyengine. Ilipo malizika darasa alimwita: "Ewe Umar! Jitahidi kwenye amali za moyo, mafaqihi wana kijinga cha moto na masufi (watu wa tasawwuf) wana kaa la moto na wakia moja ya amali ya ndani inalingana na ***buhaar*** (uzito mkubwa uliokuwa ukitumiwa zamani zaidi ya kilogramu 200) ya amali za nje."

Ama jitihada zake kwenye ibada, alikuwa akitoka thuluthi ya tatu ya mwisho ya usiku akienda kwenye Shiib Nueir na kusoma Qur-ani, na akizuru makaburi na kuswali kwenye misikiti yote ya Tariim kila usiku. Akiswali utadhani ni nguzo kwa urefu wa kisimamo chake, na hakikupungua kitu katika jitihada zake hata siku yake ya harusi. Vile vile alikuwa akienda kuzuru ziara ya Nabii Huud na kukaa huko karibu mwezi na kula chakula kidogo sana.

Ama ukarimu wake, alikuwa akitoa sadaka kwa maelfu na maelfu. Aliotesha mitende mingi sana, na akisoma Sura ya Yasin kwenye kila mtende, na alipootesha mitende sehemu kubwa inayoitwa Ba Hubaishy aliwapa watoto wake (na wakati huo alikuwa na watoto 8 wa kiume, na 6 wa kike) kwa sharti ya kusoma nyiradi na kumpelekea yeye thawabu baada ya kufa kwake. Alijenga misikiti kumi na akaiwekea idara ya wakfu, na akisema mitende hii yote haina sehemu kwenye moyo wangu, hata nikiambiwa kuwa haijatoa matunda yoyote nisinge huzunika.

Na walimwita wanavyuoni Saggaaf, na wamesema kuwa ni kwa sababu ya kusitiri hali yake wasiijue watu kwani hakuwahi kudai *hali* wala *maqamu* yoyote, wala hakujinasibisha kwa elimu wala amali, na akichukia umashuhuri sana. Sababu nyengine ni kuwa amekuwa sakafu kwa mawalii wote katika zama zake, yaani yuko juu yao na yeye ndiye mkubwa wao.

Katika maneno yake ya Hikma ni: “Asiye na uradi ni kama ngedere”, “Asiye talii (durusi) *Adhkaar* (kitabu cha Imaam Nawawiy) basi yeye si *dhakar* (mwanaume wa kweli)”, “Asiye soma *Ihyaa* hana haya”, “Asiye soma *Muhadhab* basi hakufahamu kanuni za madh-hab”, “Asiye na adabu basi yeye ni dubu”. Pia katika jumla ya maneno yake: “Watu wote ni mafakiri (wahitaji) wa elimu, na elimu inahitajia amali (matendo) na amali inahitajia akili na akili inahitajia *tawfiiq* (kuwezeshwa na Mwenyezi Mungu). Na kila elimu bila ya amali ni batili, na kila elimu na amali bila ya nia inapotea bure, na kila elimu, amali na nia bila ya sunna inarudishwa (haikubaliwi). Na kila elimu, amali, nia na sunna bila ya ucha Mungu ni hasara”. Na pia katika maneno yake: “Kuwa mtu wa zama zako, ukiona watu wake ni mbwa mwitu basi usiwe mbuzi watakutafuna, na ukiwaona mbuzi usiwe mbwa mwitu ukawa unawatafuna”.

Na alikuwa na harufu nzuri, akiingia kwenye nyumba au akipita njiani hujulikana kuwa amepita yeye kwa harufu yake. Alipodhoofika mwisho wa umri wake alikuwa akimweka mtu akisoma Qur-ani na yeye husikiliza, na wakati mwengine husoma naye pamoja. Pamoja na hayo haimkuti swala ila yuko msikitini akiwa tayari na twahara yake. Na alikuwa daima anasikika akimtaja Mwenyezi Mungu kwa ulimi wake, na pia akimtaja kwa moyo wake, na kilikuwa kifua chake kinatoa sauti kwa kumtaja Mwenyezi Mungu na kuleta *istighfaar*.

Alikuwa mashuhuri sana kwa karama, pamoja na kwamba zilikuwa hazimshughulishi na kufanya jitihada na kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kila hali.

Alifariki siku ya Alkhamisi zikiwa zimebakia siku saba kabla ya kumalizika kwa mwezi wa Sha’abani mwaka wa 819 H. Aliwacha watoto wa kiume 13 wote wakiwa mashuhuri kwa ucha Mungu.

Sheikh Umar Mihdhaar bin Abdul Rahman Saggaaf

Alizaliwa Tarim, na kulelewa na baba yake. Alianza kwa kuhifadhi Qur-ani, kisha akahifadhi *Minhaaj Talibin* na kuisoma kwa baba yake na wengine katika wanachuoni. Alikuwa na uwezo mkubwa sana wa kuhifadhi vitabu alivyovisoma. Alisoma Fiq-hi kwa Sheikh Abu Bakr bin Muhammad Balhaaj Ba Fadhl, na baadhi ya wacha Mungu wengine. Kisha akaenda Shihr, Yemen na Haramain na huko nako akasoma na kusuhubiana na wanachuoni wengi. Alishikamana sana na *Minhaaji, Tanbiih, Ihyaa* na *Tafsir Sullamiy* ambayo alikaribia kuihifadhi.

Walisoma kwake watu wengi sana, walio mashuhuri ni mtoto wa ndugu yake Sheikh Abdallah Aydaroos na ndugu zake Sheikh Aliy na Sheikh Ahmad, Sheikh Ahmad bin Umar bin Aliy bin Umar bin Ahmad bin Al-Faqiih, Sheikh Husayn bin Faqiih Ahmad bin Alawiy. Sheikh Muhammad bin Abdallah bin Aliy, Sheikh Muhammad bin Aliy Ba Zughayfaan, Sheikh Ahmad bin Muhammad Ba A'bbaad, Sheikh Said bin Ahmad Ba Ghariib Al-Shihriy, Sheikh Abdallah bin Faqiih Aliy Ba Hirmiy na Sheikh Abu Bakr bin Abi Qubayl. Katika waliosoma kwake pia ni ndugu zake wadogo.

Alikuwa na jitihada kubwa kwenye ibada, alikuwa akisubiri bila ya chakula siku nyingi na aliacha kula tende; akiulizwa anasema kuwa tende ni katika matamanio yake na ameiacha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Chakula chake mara nyingi kilikuwa ni maziwa.

Alikuwa mkarimu sana, akiwapa mahitaji nyumba nyingi sana za masharifu na akiwatanguliza kwa vyakula vizuri, hata walimlaumu baadhi ya watu kutokana na kutoa kwake sana, akasema (nayo ni aya ya Qur-ani), **"Mlivyo navyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyo bakia".** (Nahl:96).

Alikuwa pia mwenye kukubaliwa dua yake, alikuja mtu mmoja akiwa mgonjwa sana, akamwombea akapona pale pale. Alikuja mwanamke mwengine akiumwa na kichwa ambacho walishindwa madaktari kukiponyesha, akamwombea apate afya akapona.

Alikuwa Sheikh Mihdhaar mwenye khofu kubwa ya Mwenyezi Mungu, alikuwa akisema: “Laiti ningelikuwa mbuzi kisha nikachinjwa na kuliwa, au nikawa mbwa nikafa na kugeuka kuwa mchanga”. Na katika maneno yake: “Nikivuta pumzi naogopa nisiweze kuchukua inayofuata, na nakula tonge nikihisi huenda nisiweze kulimeza (kabla ya kufikwa na mauti)”. Alikuwa pia akisema: “Lau ningejua kuwa Mwenyezi Mungu amekubali tasbiih yangu moja, ningewalisha wakazi wa Tariim ngano na nyama”.

Alikuwa Sheikh Mihdhaar ni kiongozi wa Alawiyyiin wakati wake, na mtu mwenye akili na kupangilia mambo yake vizuri. Aliweka mpangilio wa kutengeneza sehemu ya mapitio ya maji, na ada nyengine za maisha, na hayo si Tariim tu, bali hata miji ya pwani ambapo alikuwa akienda kama Shihr, Mukalla na Ghayl. Bali yeye mwenyewe alimiliki mashamba na maboti kwa ajili ya kuvua samaki, na faida yake ikawa inatumika kwa ajili ya maslahi ya elimu na da’awa, na kuwasaidia masikini na wasio na uwezo. Na aliweka hati/waraka ambao Aali Ba Alawiy walikubaliana kusimama juu ya haki, kuamrisha mema na kukataza mabaya, kumnusuru aliye dhulumiwa na kusimamia mali za wakfu za wazee wao na kuzitumia kwa njia inayotakiwa na kumkubali Sheikh Umar Mihdhaar kuwa kiongozi wao. Na hati/waraka huu ulitambuliwa hata na viongozi wa dola wa wakati huo.

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas(ra), “Alipokuwa Sheikh Umar Al-Mihdhaar kiongozi wa masharifu wa Alawiyyiin aliwakusanya na kuwaambia, “Nakutakeni mufanye mambo matatu, la kwanza, mwenye kutaka kulima au kupanda awe na wanyama wawili, mmoja akifanya kazi mwengine anapumzika. La pili, mabinti wa matajiri wenu waolewe na watoto wa masikini wenu, na mabinti wa masikini wenu waolewe na watoto wa matajiri wenu. La tatu, mupunguze mahari yenu, iwe ni wakiya tano ya fedha iliyotakata”. Wakamwambia, “Hakika mahari ya Ahlil bayti ni dirhamu 500”. Na Sheikh Umar al-Mihdhaar akawajibu, “Ama sasa nataka muipunguze iwe kama ninavyokuambieni, na nakufahamisheni kuwa Bwana wa viumbe(saw) siku alipoenda Israi alifaradhiwa swala 50, hakuacha kurudi kwa Mola wake (akimwomba takhfifu) hadi akazifanya kuwa 5. Na mimi nakuombeni kupunguza mahari kutoka dirhamu 500 (ambayo

kwa hisabu ya Hadhramout ni sawa na wakiya 500) yawe wakiya 5 (sawa na dirham 5)". Wakamwambia, "Tumekubali hayo". Akawaombea waliotekeleza ahadi yao katika Alawiyyiin kuwa na kizazi kikubwa."

Alifariki siku ya Jumatatu tarehe 2, Dhul Qa'ada, mwaka 833 H, naye akiwa amesujudu kwenye swala ya Adhuhuri.

Sheikh Abdallah Aydaroos bin Abi Bakr bin Abdul Rahman Saggaaf

Yeye ndiye wa kwanza kuitwa Aydaroos, alizaliwa katika kumi la mwanzo la Dhul-Hijja, mwaka 811 H. Alizaliwa na kukulia katika mji wa Tariim. Alimuwahi babu yake Sheikh AbdulRahman Saggaaf. Alipofariki babu yake yeye Sheikh Abdulla Aydaroos alikuwa mtoto wa miaka 8. Alipofika umri wa miaka 10 alipata msiba mwengine wa kufiliwa na baba yake. Hapo akachukuliwa na kulelewa na ammi yake Sheikh Umar Mihdhaar na ambaye alimwozesha binti yake.

Alipata elimu nyingi sana kwa ammi yake. Pia alisoma Fiq-hi kwa Sheikh Sa'ad bin Abdallah Ba Ubeid, Sheikh Abdallah Ba Harawah, Sheikh Ibrahim bin Muhammad Ba Hurmuz, na Sheikh Abdallah Ba Ghusheir. Alisoma Hadithi kutoka kwa masheikh mbali mbali wa Hadhramout. Vile vile alisoma Tasawwuf kwa Sheikh Muhammad bin Hasan Jamalillayl na kutoka kwa ammi zake mabwana Ahmad, Sheikh, Muhammad na Hasan. Alisoma elimu ya Kiarabu kwa Sheikh Ahmad bin Muhammad bin Abdallah Ba Fadhl, na elimu za Nahau na Sarufi kwa Sheikh Muhammad bin Aliy Ba Ammar na masheikh wengine. Sheikh Abdalla Aydaroos alionyesha uhodari mkubwa kwenye elimu tatu za sheria: Tafsiri, Hadithi na Fiq-hi. Katika jitihada zake alishikamana sana na vitabu: *Tanbiih*, *Khulasah* na *Minhaj*. Vitabu hivi alivisoma mara nyingi kisomo cha kutafuta undani na kuhakiki.

Kuhusu jitihada zake kwenye ibada, mwenyewe amesema, "Nilikuwa nikisoma vitabu vya Tasawwuf na ninajijaribu kwa kutekeleza jitihada zao. Nilikuwa ninakaa na njaa sana". Alikuwa akifunga sana na akifuturu kwa kula tende kidogo tu, hali chochote kingine.

Alipofariki ammi yake Sheikh Umar Mihdhaar ambaye alikuwa kiongozi wa Aali Ba Alawiy, yeye alikuwa ana umri wa miaka 25. Masharifu wakaenda kwa Sheikh Muhammad bin Hasan Jamalillayl, aliyekuwa akiishi Rogha, kumuomba achukue nafasi ya Sheikh Umar Mihdhaar lakini akatoa udhuru. Wakamtaka awachagulie anayeona anafaa. Yeye akaswali swala ya Istikhara na akaona wa kutangulizwa ni Sheikh Abdallah Aydaroos. Sheikh Aydaroos akatoa udhuru kuwa yeye

ni mdogo kwa umri na wako ammi zake. Lakini ammi zake wote wakasimama na kumhimiza ashike hiyo nafasi, na wakakubaliana kumfanya kiongozi wao.

Hivyo akaanza kusomesha fani za Tafsiri, Hadithi, Fiq-hi na Tasawwuf. Miongoni mwa wanafunzi wake ni ndugu yake Sheikh Aliy, Sheikh Umar bin Abdul-Rahman Sahib Hamraa, Sheikh Abdallah bin Ahmad Ba Kathir, Sheikh Ahmad Qasam bin Alawiy Al-Shaiba, na Sheikh Muhammad bin Aliy Al-Afiif Al-Hijraaniy. Wengine ni watoto wake mabwana Abubakr, Husain, na Sheikh. Vile vile miongoni mwa masheikh wakubwa wa wakati huo, Sheikh Muhammad Aideed, Sheikh Sa'ad bin Aliy na Sheikh Abdallah bin Abdul-Rahman Ba Wazir, pamoja na utukufu wao, walikuwa ni wenye kuchukua elimu kutoka kwake.

Katika jitihada zake Sheikh Abdalla Aydaroos alilazimiana sana na kusoma *Ihyaa Uluumul-Din* na kuitalii (kuidurusi) mpaka alikaribia kuihifadhi. Na aliwahimiza watu wake kuisoma, kuiandika na kuitalii. Katika jumla ya maneno yake, alikuwa akisema, "Waba'adu hatuna njia (ya kufuata) wala mfumo usiyokuwa Qur-ani na Sunna. Na hakika amesherehesha hayo yote kiongozi wa waandishi na baki ya *Mujtahidiin Hujjatil-Islam* Al-Ghazaliy, katika kitabu chake ambacho ni ajabu ya zama hizi, chenye utukufu mkubwa, chenye kuitwa *Ihyaa Uluumul-Din*, ambayo ni ibara (maelezo) ya Qur-ani na Sunna, na Tariqa na Hakika (kweli halisia)". Katika maneno yake pia, alisema, "Juu yenu kushikamana na Qur-ani na Sunna mwanzoni na mwishoni, kwa dhaahiri (muonekanavyo na watu) na kwa siri (muonekanavyo na Mwenyezi Mungu), kwa kuizingatia na kuiitakidi. Na sherehe (ufafanuzi) ya Qur-ani na Sunna imeelezwa kwa ukamilifu kwenye kitabu cha *Ihyaa Uluumul-Din*". Vile vile alisema, "Lau Mwenyezi Mungu angewafufua maiti wasingeliwausia walio hai ila kwa yaliyomo ndani ya *Ihyaa*". "Ninashuhudia kwa uficho na kwa wazi kuwa mwenye kutalii *Ihyaa* atakuwa katika *Mujtahidiin*".

Ama ukarimu wake alikuwa akitoa utoaji wa Wafalme na akinyenyekea unyenyekevu wa mtu asiye na kitu. Alikuwa akikaa na watu kwa kinachoafikiana nao, akikaa na mafakiri kwa kinachonasibiana nao, na

akizungumza na wenye elimu kitaaluma. Alikuwa na tabia ya kumsikiliza anayezungumza naye, na akikabiliana naye mpaka kila mmoja akihisi kuwa yeye yuko karibu zaidi kwake. Walikuwa wafalme wakimwogopa kwa haiba yake na wananyenyekea kwake. Lakini pamoja na hayo alikuwa huwarai, akizungumza nao kwa upole, na hata akiwatukuza kwa ajili ya kukidhi haja za Waislamu na kupatanisha wagomvi. Pamoja na hayo alikuwa akiwatahadharisha watu wake wasimfuate katika suala la kuingiliana na watawala, bali hata kupita kwenye viwanja vyao.

Sheikh Abdalla Aydaroos alifariki tarehe 12 Ramadhan 865 H akiwa na umri wa miaka 54 na alizikwa Zanbal, na kaburi lake ni maarufu.

Sheikh Abubakar Al-Adany bin Abdallah Aydaroos

Alizaliwa mwaka 851 H, na akalelewa na baba yake mpaka kufikia umri wa miaka 14 alipofariki baba yake. Alihifadhi Qur-ani kwa Sheikh Muhammad bin Aliy Ba Jahdab na Muallim Salim bin Nimeiriy. Ama Tasawwuf alichukua kwa baba yake na ammi zake Sheikh Aliy na Sheikh Ahmad na Sheikh wake Sa'ad bin Aliy Ba Mad-haj. Alisoma Fiq-hi kwa Sheikh Abdallah bin Abdul-Rahman Balhaaj Ba Fadhl na Sheikh Muhammad bin Abdul-Rahman Balfaqiih. Na alisoma fani nyingi zaidi kwa ammi yake Sheikh Aliy.

Alikuwa akipenda sana kusoma *Bidaayatul-Hidaaya*, *Minhaaj Al-Abidiin*, *Minhaaj Al-Talibin*, *Khulaasa* na *Umdah* ya Ibn Naqiib na akiwahimiza watu wake kuvisoma vitabu hivi. Ama *Ihyaa Uluumul-din* alikuwa mwenye kuzama katika kukipenda, kukisoma, kukisikiliza na kukitalii, hata alijilazimisha kwa nadhiri kusoma kitu (katika *Ihyaa*) kila siku na alikusanya nakala nyingi za *Ihyaa*.

Ama jitihada zake kwenye ibada, zilikuwa ni kubwa mno. Alikuwa akitoka usiku yeye na mtoto wa ammi yake Sheikh Abdul-Rahman bin Aliy kwenda kwenye boma la *Nueir*, kisha kila mmoja husoma juzuu kumi kwenye swala, na kurudi kabla ya alfajiri. Pia alijilazimisha kukaa macho usiku tangu utotoni mpaka ikawa tabia yake bila ya taklifu. Amesema mmoja katika watu wanaoaminiwa, "Nimemtumikia miaka 30, sijawahi kumwona akilala zaidi ya masaa 3". Hii peke yake ni karama kubwa, kwani alikuwa akila vyakula vizuri, akinywa maji sana, na akilalia kitanda cha kifakhari; aghalabu mwenye kuwa na tabia kama za kwake huwa ni mwenye kulala sana, lakini yeye hakuwa hivyo, bali alikikesha sana akidumu juu ya ibada.

Sheikh Abubakar Al-Adany alikuwa ni mwenye kusafiri sana kwenda Shihr. Pia alikuwa akizuru kaburi la Nabii Huud(as) na akiwazuru wacha Mungu wengine kama Sheikh Said Al-Amoody, Sheikh Abdallah bin Muhammad Ba A'bbaad, Sheikh Abdallah Ba Qushair, Sheikh Muhammad bin Aliy Ba Shuayb na wengine.

Alienda Haramain, na akaingia Aden na kuchukua elimu kwa Sheikh Abdallah bin Ahmad Ba Makhramah, na Sheikh Muhammad bin

Ahmad Ba Fadhl. Pia alienda Zabiid na kuchukua kwa Sheikh Al-Islaam Ahmad bin Umar Al-Mazjad, na Sheikh Yahya bin Abi Bakr Al-Amiriy mtunzi wa kitabu *Bahjatil-Mahaafil*. Alipokwenda Hijja mwaka 880 alichukua elimu kwa Al-Haafidh Muhammad bin Abdul-Rahman Sakhawiy. Wengi katika masheikh zake walimpa ijaza ya vitabu vyao na riwaya zao, na ruhusa ya kutoa fatwa na kufundisha. Na alikuwa na akili safi na utambuzi mzuri, na kusibu yaliyokuwa sawa, na muono wa ukweli ambao uliwashangaza sana masheikh zake. Na hayo yameshuhudiwa kwenye uzuri wa rai zake, maneno yake na matendo yake pamoja na umri wake mdogo.

Aliporudi Tariim alikaa kwa ajili ya kufundisha na kutoa manufaa kwa watu. Wakasoma kwake watu wengi, miongoni mwao ni ndugu yake Sheikh Husain, mtoto wa ndugu yake Sheikh Abdallah bin Sheikh, Sheikh Abdallah bin Muhammad Ba Qushair, na wengine wengi katika makabila ya Aali Ba Fadhl, Aali Ba Hirmiy, Aali Khatib na Aali Ba Abbaad. Na katika waliosoma kwake ni pamoja na Al-Haafidh Jarullah bin Fahd, Sheikh Husain bin Siddiik Al-Ahdal, Sheikh Muhammad bin Ahmad Ba Jarfiil, na Sheikh Muhammad bin Umar Bahraq wa Aden.

Sheikh Abubakar Al-Adany alikuwa mwenye kupitia vitabu vingi katika fani tofauti, na mwenye kutalii sana khasa vitabu vya Imaam Ghazaliy. Alikuwa pia hodari wa kusahilisha (kuwepesisha) ibara, akiulizwa suala gumu, hulieleza kwa njia bora hadi huondoka mushkili wake.

Kitabia alikuwa ni mtu mwenye kutabasamu, akizungumza na watu kwa bashasha, na akipenda kuwalisha watu. Anapokula na watu alikuwa ni mwenye kuwasogezea vyakula vitamu na matunda mazuri mbele yao. Alikuwa ni mwenye huruma na mpole kwa mafakiri, mayatima na wajane na akiwaunga kwa kuwaneemesha kwa siri na dhahiri. Alikuwa pia ni mwenye kula vyakula vizuri na kuvaa mavazi ya thamani, akidhihirisha neema ya Mwenyezi Mungu na kutaraji kupewa ziada. Akifanya hivyo kwa kuyafanyia kazi maneno ya Mwenyezi Mungu,

“Sema: Ni nani aliyeharimisha pambo la Mwenyezi Mungu alilowatolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki”. (Araaf:32).

Na neno Lake,

“Enyi mlio amini! Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu”. (Baqarah:172)

Na maneno ya Mtume(saw),

“Hakika Mwenyezi Mungu anapenda kuona athari ya neema yake juu ya mja wake”. (Tirmidhiy, Ahmad)

Na neno lake(saw),

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mzuri anapenda uzuri”. (Muslim).

Mwaka 888 alitoka tena kwenda kuhiji na kumzuru babu yake(saw), na alitembelea baadhi ya miji ya Yemen, kuzuru wacha Mungu na kuwanufaisha madhaifu (wanyonge). Kisha akaenda Aden akiwa njiani kuelekea Shihr, na ikawa kumekutana kuingia kwake na kufariki kwa Sheikh Umar bin Abdul-Rahman Sahibul Hamraa Taizz mwaka 889. Watu wakamkusudia kwa ajili ya kumpa pole na pia kumwomba akae kwao ili wapate manufaa kutoka kwake. Sheikh Abubakar Al-Adany alishabashiriwa kabla kuwa ataishi Aden. Hivyo yakawa aliyobashiriwa, yaani kuishi mji wa Aden. Alipokuwa Aden akawa ni mwenye kukusudiwa na wageni na wenyeji, ukatangaa umashuhuri wake na kuenea utajo wake. Pamoja na hayo hakuwa mwenye tamaa ya cheo. Alikuwa akisema, “Hatuna makusudio kwenye kudhihiri kwa watu lakini tumepewa haya kwa ajili ya kuwanufaisha (watu)”. Alikuwa pia akisema, “Mwenye kunibusu mkono huwa kama amenipiga kibao, na mwenye kunibusu mguu huwa kama amenitoa jicho”. Na katika maneno yake mengine akisema, “Laiti asingetujua mtu, wala tusingemjua mtu, laiti tusingezaliwa”.

Alikuwa na cheo kikubwa na utukufu baina ya watu, na mwenye uwezo wa kutekeleza anacho kikusudia, mwenye elimu na mwenye kutenda kwa elimu yake, mkweli kwenye usemi, mwenye uangalifu katika upokezi wa riwaya. Mwenyezi Mungu alimkusanyia aina tofauti za elimu. Alikuwa mwenye kutenda kwa elimu yake, mkweli katika kauli zake, na mwenye uangalifu katika upokezi wa riwaya. Pia Mwenyezi Mungu alimpa haiba na kuheshimiwa na watu, akiogopewa na wafalme

na viongozi hata wakawa wananyenyekea mbele yake na wakiwa tayari kutekeleza amri zake. Pamoja na hayo alikuwa mnyenyekevu, mwenye tabia njema kabisa na kupendwa na watu. Alikuwa akiuliza hali za watu wake, akienzi mapenzi yao, akimsamehe mwenye kukosea, na kuficha ghadhabu zake. Alikuwa akikidhi haja za watu, na kuzungumza nao kwa bashasha hata kila mmoja anahisi kuwa yuko karibu zaidi kwake kama ilivyo pokewa kwa Mtume(saw). Alikuwa pia mkarimu sana hasa kwenye kulisha chakula, na alikuwa akichinja kila siku kondoo 30 katika mwezi wa Ramadhani kwa ajili ya karamu. Na siku ya Idi akiwavisha watumishi na watu wake mavazi ya fakhari, na kutoa mali nyingi kama sadaka.

Vile vile alikuwa ni mwenye huruma kwa wenye kumkosea Mwenyezi Mungu na kuvunjika moyo, akiwatuliza na kuwafungulia mlango wa kumtarajia Mwenyezi Mungu kwa Msamaha Wake na ndio maana maneno yake mengi yako kwenye kuraghibisha (kuwavutia na kuwapendezeshea watu) na sio kutisha. Hata watu wake wakikosea kitu hawaambii kwa hasira bali kwa upole na kuwatoa kwenye mikono ya shetani kadri inavyomkinika. Alikuwa akiwavuta watu kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, akiyafanyia kazi maneno ya Mtume(saw),

“Fanyeni wepesi na musifanye uzito, na toeni bishara wala musiwakimbize (watu)”. (Muslim)

Sheikh Abubakar Al-Adany alikuwa akisema, “Mioyo ikishatawaliwa na matamanio, kutisha hakuizidishii ila kuiweka mbali, basi kuivuta mioyo ni kwa kuwafungulia milango ya matarajio (ya Mwenyezi Mungu) na ndiko kutakakowavuta kusikiliza mawaidha”. Alikuwa pia akisema: “Nikimwona muumini amewafikishwa na Mwenyezi Mungu kutekeleza faradhi na kuacha maasi makubwa, huupa uhuru moyo wangu na yeye kwani amekuwa akitembea pamoja na msafara na miguu yake. Ama himma yangu iko kwenye kumtoa yule aliyezama kwenye maasi na mwenye kuingia katika kamba za shetani”. Na alikuwa akiwapa mazoezi ya kukaa macho usiku wafuasi wake na vijana ili kuwahifadhi na maasi akiwaambia kuwa yeye anapata kuliwazwa kwa kukaa nao. Na akawa akiwapa malipo kwa kukaa naye kila kukicha, na kumpa zaidi yule anayemkhofia zaidi kuzama kwenye maasi. Na

alikuwa akiusia sana kuwa na dhana nzuri, kwani kunaonyesha kufaulu kwa mja, na kwamba mwenye dhana nzuri hutegemewa kuwa na mwisho mwema, na mwenye dhana nzuri hawezi kupata hasara hata kama akikosea. Na katika maneno yake alikuwa akisema, “Hawezi kujua kima cha johari ila mwenye kufanya kazi ya johari, na hawezi kumjua walii ila aliye walii, na vipi utamjua mtu ambaye anaghadhibika kama unavyoghadhibika na anakula kama unavyokula?'

Alifariki siku ya Jumanne, 14 Shawwaal mwaka 914 H Aden na kaburi lake ni mashuhuri.

Sheikh Abu bakr bin Salim.

Jina lake: Sheikh Abu Bakr bin Salim bin Abdallah bin Abdul-Rahman bin Abdallah bin Abdul-Rahman Saggaaf mpaka kwa Mtume(saw).

Alizaliwa siku ya Jumamosi 13 Jumadal Thani, mwaka 919 H Tariim, na alijitahidi sana katika suala zima la kutafuta elimu. Alisoma kwa Sheikh Umar bin Muhammad bin Ahmad Ba Sheiban, Sheikh Abdallah bin Muhammad bin Sahl Ba Qushair, Sheikh Umar bin Abdallah Ba Makhramah na Sheikh Ahmad bin Alawiy Ba Jahdab. Kisha akaenda Shibam na kulazimiana na Sheikh Ma'aruf Ba Jammaal na ndiye mwalimu wake mkubwa.

Kisha akahamia Lasik, akafanya jitihada kubwa kwenye ibada na kuizoeza nafsi yake kwa kuswali usiku, kufunga, kutoa sadaka na unyenyekevu hadi akafunguliwa na Mwenyezi Mungu.

Hapo tena akatoka na kuenda kuishi Inaat, na ndipo alipopata umashuhuri. Watu wengi kutoka sehemu mbali mbali walikuwa wanakuja Inaat kwa kumkusudia yeye. Hata imepokewa kuwa Inaat haikuwa mashuhuri kwa elimu, bali ilikuwa imejaa fitina na ugomvi baina ya makabila, mpaka alipohamia yeye mji wote ukabadilika. Mwenyezi Mungu akausafisha na fitina na ukapata heshima na umashuhuri kuliko miji mengine.

Alipokuwa Inaat alikaa kusomesha na wakachukua elimu kwake watu wasio na hesabu, miongoni mwao ni watoto wake na Al-Habiib Ahmad bin Muhammad Al-Habashy Sahib Shiib, Al-Habiib Abdul-Rahman Jufriy wa Tariis, Habiib Muhammad bin Alawiy wa Mukayrubaat, Al-Habiib Abdul-Rahman Al-Biidh wa Shihr, Sayyid Yusuf Al-Faasy, Sheikh Hasan Ba Shuayb, Sheikh Muhammad bin Siraj diin. Aliandika pia vitabu zaidi ya vinne katika Tasawwuf.

Alikuwa mkarimu sana, hata mali zake karibu zote zilitumika kwa ajili ya wahitaji, madhaifu na wageni. Wakawa wageni wanajaa kwake kutokana na ukarimu wake. Imepokewa kuwa ilikuwa ikitengenezwa kwake mikate 500 mchana na mfano wake usiku kwa wingi wa wanao kula kwake. Bali nyumbani kwake kulikuwa kukipikwa mara 3 kwa

siku. Alikuwa akisema, “Anaye kuja Inaat ni mgeni wangu”. Na alikuwa hakerwi na mabedui wa Kiarabu bali huzungumza nao kwa upole na huwalingania kwa upole kuelekea kwenye haki. Akizungumza kwa uzuri na watu wake, hadi kila mmoja huhisi yuko karibu zaidi kwake.

Alikuwa anajihadhari sana na kudhihirisha karama, pamoja na kwamba zilidhihiri sana kwake, lakini hakuwa mwenye kuzitegemea. Hii ni kwa sababu wacha Mungu wanaona kuwa *Istiqaama* (kusimama thabit katika haki) ndio karama kubwa kuliko zote.

Alifariki siku ya Jumapili, siku tatu kabla ya kumalizika kwa mwezi wa Dhul-Hijja, mwaka 992H na kuzikwa Inaat.

Al-Habiib Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas:

Jina lake kamili ni Al-Habiib Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas bin Aqiil bin Salim bin Abdallah bin Abdul-Rahman bin Abdallah bin Abdul-Rahman Saggaaf mpaka kwa Mtume(saw).

Alizaliwa mwanzoni mwa karne ya 11. Alipata upofu wa macho akiwa na umri mdogo. Mama yake akamchukua kwa mmoja wa wacha Mungu, naye akamwambia asihofu kwani mwanawe atakuwa na utukufu na umashuhuri mkubwa, na kizazi chake kitaongezeka na watapanda farasi kama Aali fulani.

Alikuwa akija Tariim kutoka mjini kwake Lasik nyakati za usiku, akiswali katika kila msikiti rakaa mbili, na akijaza maji mahodhi ya misikiti. Alichukua elimu kwa Al-Habiib Muhammad bin Abdul-Rahman Al-Haadiy, Sheikh Umar bin Isa Ba Rakwah wa Ghurfa. Sheikh wake aliyepata kwake manufaa zaidi ni Sheikh Husain bin Abi Bakr bin Salim. Pia alisoma kwa ndugu yake Sheikh Al-Haamid bin Abi Bakr bin Salim.

Kisha akahamia Huraydha na familia yake kwa ishara ya Sheikh wake Sheikh Husain. Baba yake akamfuata na kukaa naye. Alifariki baba yake baada ya siku chache na kuzikwa Huraydha. Habiib Umar Al-Attaas alikuwa akisita kwenda Huraydha kutokana na watu wake kuwa ni wagumu wa mioyo, lakini Sheikh wake akamhimiza kwenda, kwani makusudio yalikuwa ni mlingano wa Mwenyezi Mungu. Akaifanya kazi hiyo ya da'awa, na kuieneza Huraydha na kwenye vitongoji vilivyo karibu yake, akitoa mawaidha na kuwafundisha wakaazi wake elimu za dini.

Alikuwa Habiib Umar ni mwenye unyenyekevu mkubwa, hata Habiib Abdillah Haddad, mwanafunzi wake, alikuwa akiomba Mwenyezi Mungu ampe unyenyekevu kama wake. Katika maneno mengine ya Habiib Abdillah Haddaad, "Huyu Sayyid (Umar) ni hoja tosha katika *Istiqaama* na kumtumikia Mwenyezi Mungu kwa ukweli, na kujiweka chini na unyenyekevu wa hali ya juu, lakini si kila mtu anayemjua". Amesema tena Habiib Abdillah Haddaad(ra), "Hakika Umar bin Abdul

Rahman Al-Attaas ameotesha mti wake juu ya unyenyekevu, yakaja matawi yake pia vivyo hivyo (akimaanisha watoto wake)".

Habiib Umar Al-Attaas alikuwa pia mwenye ukarimu sana kwa mafakiri na masikini, hana tamaa ya Dunia pamoja na cheo na umashuhuri alioupata.

Katika wanafunzi wake ni Sheikh Ali bin Abdillah Ba Raas ambaye alianza kama mtumishi akichunga mbuzi, kisha akamsomesha hadi akafikia daraja kubwa ya elimu na akawa analingania da'awa na kusomesha fani chungu nzima. Wengine ni Habiib Abdillah Haddaad, Habiib Ahmad bin Hashim Al-Habashy, Habiib Isa bin Muhammad Al-Habashiy, Sheikh Abdallah bin Umar Ba Abbaad, na Sheikh Muhammad bin Ahmad Ba Shumuus wa Doan.

Katika jumla ya maneno yake ya Hikma, "Angalia hali unayopenda mauti yakujie ukiwa juu yake, ulazimiane nayo, na hali ambayo unachukia mauti yasikufikie ukiwa juu yake, ujiepushe nayo". Vile vile amesema, "Mwenye kumwombea kheri dhaalimu huaminika na shari yake". Na, "Kufanya twaa pamoja na kula haramu ni sawa na kuteka maji kwa kutumia kapu". Kadhalika amesema, "Uchache unao takiwa ni kusimamisha dhaahiri, na Mwenyezi Mungu ndiye anaye tawalia siri".

Kuhusu mji unaofaa mtu kukaa, amesema Habiib Umar bin Abdul Rahman Al-Attaas, "Mwenye kutaka ukaazi wa mji, basi asifanye makaazi yake ila kukiwa na vitu vitatu: iwe Sala za jamaa na Ijumaa zinaamirishwa katika misikiti yake, na iwe mikondo na mapitio ya maji yake ni yenye kuamirishwa, na wawe watoto wake (wa mji ule) wanajifunza Qur-ani na dini. Yakipatikana haya matatu kwenye mji, basi akae kwani kheri itaongezeka ndani yake".

Alifariki Habiib Umar Attaas siku ya Al-khamisi tarehe 23 Rabiul Thani, mwaka 1072H, na kuzikwa Huraydha.

Al-Habiib Abdillah Al-Haddaad:

Jina lake kamili ni: Al-Habiib Abdillah bin Alawiy bin Muhammad bin Ahmad bin Abdallah bin Muhammad Al-Haddaad bin Alawiy bin Ahmad bin Abi Bakr bin Ahmad Masrafah bin Muhammad bin Abdallah bin Faqiih Ahmad bin Abdul-Rahman bin Alawiy (Ammil Faqiih) bin Muhammad Sahib Mirbaat mpaka kwa Mtume(saw). Alizaliwa Tariim siku ya Jumatatu, tarehe 5 Safar mwaka, 1044H. Alikosa macho yake akiwa na miaka minne baada ya kupata ugonjwa wa ndui *(small pox).*

Alianza kwa kuhifadhi Qur-ani kwa Sheikh Ahmad bin Muhammad Balhaaj. Kisha baba yake akamhimiza kuhifadhi Irshaad. Akawa Habiib Haddaad akimsikia Sayyid Sahl Al-Kabsh akiitaja Fiq-hi kwa ubaya, akasema kumwambia, "Sitaki kusoma Fiq-hi, ila nataka kusoma *Bidaaya*. Baba yake akamkubalia na akahifadhi kwa baba yake kwenye utangulizi mpaka pale anaposema Imaam Ghazaliy, "***Wahaa Anaa ushiiru ilayka"*** (Na mimi ninakudokezea) ... Kisha akaenda kusoma kwa Faqiih Ba Jubair aliyekuwa akiwafundisha baadhi ya masharifu, akamwambia anataka kuhifadhi *Bidaaya.* Naye akamwambia, "Kuhifadhi *Bidaaya* ni ngumu, lakini kuna watu wanasoma *Bidaaya*, ukae uwasikilize, na uhifadhi *Irshaad".* Anasema Habiib Haddaad, "Rai yake ikawafikiana na rai ya baba yangu". Akasema Habiib Haddaad kumwambia Faqiih, "Kuhifadhi *Irshaad* ni ngumu". Akamwambia, "Tutakuwekea mtu atakuwa anakuhifadhisha na anakusikiliza". Akamkubalia kwa hilo. Habiib Abdillah Haddaad anasema baina yake na Imaam Ibn Hajar kuna watu wawili tu kwa kupitia sheikh huyu. Katika mambo ambayo yanashuhudia utukufu wake, na kuwa alikuja kuwa zaidi ya walimu wake, ni kwamba sheikh wake huyu, alisafiri na kwenda India. Aliporudi, ikiwa baada ya miaka kadhaa, akamwona Habiib Abdillah Haddaad amejaa kwa kila elimu, akaja kwake kumwomba asome kwake *Ihyaa*, na akamkubalia.

Habiib Abdillah Haddaad alisoma kwa masheikh wengi sana wanao zidi mia, tutawataja hapa walio mashuhuri, nao ni Habiib Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas, Habiib Abdul-Rahman bin Sheikh Mawla Aideed, Habiib Sahl bin Muhammad Ba Hasan, na Habiib Aqil bin

Abdul-Rahman bin Muhammad bin Aqil Al-Saggaaf. Na katika masheikh zake wa kuandikiana ni Habiib Muhammad bin Alawiy Saggaaf wa Makka.

Kadhalika alikuwa ana marafiki wengi aliosoma nao, baadhi yao ni:

- Habiib Abdallah bin Ahmad Balfaqiih, alikuwa akisoma naye Qur-ani. Wakisoma robo ya Qur-ani na kisha kuihifadhi. Na wakimaliza kusoma Qur-ani wakati wa Dhuhaa wanaingia baadhi ya misikiti na kuswali rakaa 200. Amesema Habiib Abdallah Balfaqiih, tulikuwa pamoja lakini Imaam Abdillah ametutangulia.

- Habiib Ahmad bin Umar Al-Hindawaan, ambaye anamtaja Habiib Abdillah Haddaad kuwa walikuwa pamoja na kulazimiana, kila mmoja akimliwaza mwenziwe wakati wameshughulika kutafuta elimu kwa Sayyid Al-Faqiih Abdul-Rahman Baharun. Amesema Habiib Ahmad, kuwa yeye (Haddaad) amefikia daraja ya Ijtihaad na si mfuasi tu. Walipokutana kwenye ziyara ya Nabii Huud, Habiib Abdillah Haddaad alimwambia, "Tunategemea dua zako kwani wewe ndio upanga (***Hindawaan***)". Akasema Habiib Ahmad bin Umar, "Wewe ndio tunategemea dua zako, hausilihi Upanga ila kwa muhunzi (***Haddaad***)."

- Habiib Ahmad bin Hashim, ambaye anasema walikuwa kitu kimoja kwa hali ya juu hapo mwanzoni katika kutafuta elimu, na pia wakati wa kukusanyika (pamoja tukitafuta elimu) kwa Sayyid Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas. Na katika maneno mengine anasema, "Wakati tukishughulika (kutafuta elimu) kwa Sayyid Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas alifunguliwa Sayyidiy Abdillah kabla yangu".

- Habiib Aliy bin Abdallah Al-Aydaroos wa India alisoma na Habiib Abdillah Haddaad alipokuwa Tariim na alifunga naye udugu wa kidini. Wakisoma vitabu vya dini sehemu kubwa ya usiku. Hata Habiib Aliy bin Abdallah Aydaroos anasema: "Enyi watu! Mukiridhia au mukikasirika, ametutangulia Sayyid

Abdillah Haddaad".

Habiib Abdillah Haddaad alikuwa akihimiza kusoma vitabu vyenye manufaa. Na katika maneno yake: "Nguzo za dini kwetu na misingi yake ni minne: *Bukhariy* kwa upande wa Hadithi, *Baghawiy* kwenye Tafsiri, *Minhaaj* kwenye Fiq-hi; na katika vitabu ambavyo vimekusanya ni *Ihyaa Uluumul-din"*. Na hivi ndivyo vitabu vilivyo kuwa vikisomwa sana kwake khasa *Ihyaa*; vingine ni *Minhaaj Al-Aabidiin*, *Arbain Al-asl* vyote vya Imaam Ghazaliy, *Risaala Qushairiyya*, na Sherhe ya *Hikam* ya Ibn Abbaad. Katika maneno yake, "Kwanza mtu afahamu lafdhi, kisha maana, kisha atende (kwa ile elimu)". Alimwambia mtu aliyekuwa akisoma *Minhaaj Al-Abidiin*, "Vitu hivi havidhihiri ila kwa kukariri na kuzingatia, kisha kuvitumia, basi utalii mara moja, mara mbili au zaidi, kisha zingatia, kisha utende, ukiwa hufanyi hivyo itakuwa sawasawa na mtu ambaye anajua dawa na yeye ni mgonjwa lakini haitumii". Na alikuwa Habiib Haddaad akitalii sana vitabu. Alikuwa akisema, "Umri wetu wote umeisha katika kusikiliza vitabu, na haikumalizika kiu yetu (kwenye vitabu) kama vile hatujawahi kuvisikia".

Amesema Habiib Ahmad bin Zayn: "Sikuona wala kusikia kitabu chochote katika fani yoyote na nikampelekea au nikamtajia (Habiib Haddaad) ila nilimkuta kuwa ana khabari nacho au keshawahi kukisikia kwa jitihada yake ya kutafuta vitabu na kuvipitia". Amesema Habiib Haddaad, "Sisi hatukuwa na tamaa ya kufundisha lakini alikuja mtu mmoja kutoka katika Aali Ba Fadhl akasema nataka baraka zako kwa kusoma kwako *Riyaadh Saalihiin*, kisha akaja Sayyid Hasan Al-Jufriy akasema nataka kusoma *Awaarif*, akataka Faqiih Bajubair kusoma kwenye *Hizbul Barr*, kisha kisomo kikaendelea. Tulipoona watu wamekuwa wengi tukawapangia muda." Ama wanafunzi wake ni wengi mno; miongoni mwao ni watoto wake, Habiib Ahmad bin Zayn Al-Habashy, Habiib Muhammad bin Zayn bin Sumeit, Habiib Umar bin Abdul-Rahman Al-Baar (wa kwanza), mwanachuoni mkubwa Habiib Abdul-Rahman bin Abdallah Bal Faqiih, na Habiib Muhammad bin Umar bin Taha Al-Saggaaf.

Ama Jitihada zake kwenye ibada, tumeshaona kuwa alikuwa akiswali raka 200 baada ya kutoka darasani. Na hizi jitihada alizianza tangu utotoni. Bibi yake mzaa baba Bibi Salmaa bint Umar bin Ahmad, alikuwa akimwambia ajihurumie kwa kumwona akifanya jitihada sana kwenye ibada. Na wazazi wake pia walikuwa wakimwambia hayo hayo. Katika baadhi ya maneno yake, anasema, "Nilikuwa nikiwacha baadhi ya jitihada wakati wangu wa mwanzo kwa sababu ya wazee wangu nilipokuwa naona huruma yao juu yangu".

Habiib Haddaad pia anasema, "Mwanzoni tulikuwa tunaenda kwenye miji kuzuru waja wema na kuzuru waliokwisha kufa. Tulikuwa tukizuru Shiib Mukhaddam ambamo wako maimamu wawili Ahmad bin Isa na Ahmad bin Muhammad Al-Habashy. Na huenda ziyara ikawa kwa miguu na pia tukiwa tumefunga swaumu". Alikuwa pia usiku akitembelea misikiti yote ya Tariim na kuswali ndani yake. Mtumishi wake anasema hata baadhi ya misikiti ambayo ilikuwa haiswaliwi tukienda, na alikuwa akinipanda begani ili aruke ukuta aende kuswali ndani. Kuna baadhi ya misikiti akienda kuswali ambayo ni ya udongo na hata watu hawajui kuwa ni msikiti. Habiib Haddaad mwanzoni alikuwa akijifungia katika Zawiya ya Msikiti wa Hujayra (msikiti uliokuwa chini ya uangalizi wa wazee wake, ambao uko nyuma ya msikiti wa Mihdhaar), akifanya ibada sana, na hata akigongewa mlango na mtu hafungui.

Habiib Abdillah alijenga sehemu yake ya Al-Haawiy mwaka 1074 na kuhamia 1099, na ikawa ndio makazi yake na makazi ya watoto wake na watu wake. Wakawa watu wanakuja kwake kusoma, kuchukua kwake faida za kidini na kuhudhuria vikao vyake. Amesema Habiib Muhammad bin Sumeit, "Baina ya kujenga Hawi na kufariki Habiib Haddaad ni kama miaka 48".

Mwaka 1079 alitoka Habiib Abdillah Haddaad kwa ajili ya Hijja, wakampokea watu wa Haramain mapokezi makubwa, na ikasadifu Arafa kuwa Ijumaa. Pia Habiib Abdillah Haddaad aliswalisha ndani ya Haram ya Makka, mwezi wa Muharram mwaka 1080 na kusoma Sura ya *Sajda* na *Insaan*. Kisha akaenda kumzuru Mtume(saw). Huko

Madina hakuweza kulala kwa sababu ya shauku ya Mtume(saw). Qasida yake maarufu imeandikwa ndani ya chumba cha Mtume(saw).

Mwenyezi Mungu amemjaalia Habiib Abdillah kuwa ni zawadi kwa watu wa zama zake na watakao kuja baada yake, kwani alikuja na njia ya kulingania iliyo nyepesi kabisa. Vile vile ameandika vitabu vilivyopata umashuhuri. Akalingania kwa ulimi wake, matendo yake, na kalamu yake. Alikubalika sana hapa duniani; na alikuwa mashuhuri kwenye maisha yake na baada ya kufa kwake kama kiongozi wa wenye kulingania na kutoa mwongozo. Miongoni mwa vitabu vyake ni: *Nasaaih Diiniya, Risaalatul-Muawana, Da'watul-Taammah, Risaalatul-Mudhaakara* na *Sabiilul-Iddikaar*. Katika jumla ya maneno yake, ni kauli yake, "Hakuna kitu anachohitajia mwenye kutafuta njia (ya kumfikia Mwenyezi Mungu) ila tumekiweka kwenye vitabu vyetu. Anayehitaji kitu katika hayo atakikuta ndani yake". Habiib Abdallah bin Umar bin Yahya amesema, "Mwenye kutaka kuijua tariqa ya Saada wetu Aali Ba Alawiy basi atalii vitabu vya Sayyidna Habiib Abdillah Haddaad Ba Alawiy, kwani tariqa yao ni Qur-ani na Sunna na ukamilifu wa kumfuata Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) katika maneno yote na vitendo vyote. Habiib Abdillah Haddaad ameielezea kwa njia nyepesi kwani yeye ndiye ***mujaddid*** wa Tariqa yao".

Alikuwa na nyiradi za kila aina na zimetangaa duniani zikisomwa Mashariki na Magharibi, mashuhuri zaidi ikiwa ni *raatib* (*Raatibul-Haddaad*) yake na *wirdullatiif*. Baadhi ya nyiradi zake zimekusanywa kwenye kitabu *Wasilatul-Ibaad*. Pia ana diwani ambayo imekusanya elimu, mawaidha na dua, na hachoki mtu kwa kuisoma. Qasida zake zinasomwa sehemu mbali mbali duniani, ikiwa ni pamoja na Hadhramout, Indonesia, Misri, Syria na Afrika Mashariki.

Alikuwa na tabia njema kabisa, akimtakia kila mwislamu kheri, na haamki asubuhi wala kuchwewa na jua ila akiwa msafi wa moyo kwa watu wote. Hata alikuwa akisema kuwa hizi mali na kila nilichonacho ni kwa ajili ya kutoa, na kuwakirimu wenye haja na wanaostahiki. Alikuwa pia akisema, "Haki zetu tunasamehe, ama haki za Mwenyezi Mungu hatuwezi kusamehe". Alikuwa pia akisema: "Tunawasikia watu wakila chakula chetu na wanatutukana, lakini sisi hatuathiriki kwa hayo

wala hayatuhuzunishi bali tunawaombea". Alikuwa pia akisema: "Sisi hatumruhusu mtu atusifie wala hatupendi tutajwe ila kuwa ni Ahlil-bayt, tumeshikamana na elimu, na tuna utambuzi wa watu wa Tasawwuf na sisi hatutaki kudhihirika (kujionyesha)". Katika maneno yake mengine anasema: "Tariqa yetu ni kama tariqa ya Sheikh Umar Al-Attaas, mtu akitupa (zawadi) ya kitu huwa tunakaa kimya na hatumwombi, na wakija watoto wake kudai mali yake tunawaachia wao, watu wangapi wametuusia (tupewe) vitu hatukuvichukua, bali tumewagawia warithi wao".

Ama khofu yake kwa Mwenyezi Mungu, alikuwa hasikii aya, hadithi za Mtume(saw) au maneno ya Salaf yenye kujaza khofu ya Allah ila hulia sana, na hawezi kujizuia mpaka ndevu zake zinajaa machozi. Aliwahi kusomewa kitabu chake *Sabiil Iddikaar* akalia sana na uso wake ukabadilika rangi na kuwa mwekundu, kilipomalizika akasema, "Hizi ni sifa za Peponi tuko wapi sisi na (sifa) hizi? Matarajio yetu ni kuwa mbali na moto hata kama ikiwa juu ya uzio mrefu (mnyanyuko-*Aaraaf*) baina ya pepo na moto."

Alikuwa Habiib Haddaad akimpa mtu kazi ya kufanya, humwongezea ujira wake zaidi ya alivyokuwa akitarajia. Hata akisema, "Sisi tunakusudia kuwa afanye kibarua kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na sisi tunampa ujira kwa ajili ya Mwenyezi Mungu". Alimwambia mtu ambaye anashughulikia mashamba yake, "Tahadhari na kuwafukuza watu shambani kwangu kwa kutumia nguvu, akija mtu kuchukua kitu, umfahamishe tu kuwa ni mazao yetu, akichukua kutokana na kuwa na haja, basi mali zetu na vyote tunavyo vimiliki ni kwa ajili ya kutoa na kuwakirimu wenye haja na wanao stahiki. Na ikiwa kuja kwake ni kwa kutumia nguvu na kudhalilisha, basi kitendo chake kitamletea madhara mwenyewe, ima kwa haraka (sasa hivi/pale pale) au kwa baadaye".

Alikuwa akikaa na wageni wake na wanaomzuru akizungumza nao kwa bashasha, na huwaita kwa majina yao na akiwaliwaza. Akizungumza na watu kwa kadiri ya akili zao, na akimweka kila mtu kwenye daraja yake. Akikaa na mafakiri kwa furaha, akiwauliza haja zao na akijitahidi kuzikidhi kiasi cha uwezo wake. Alikuwa Habiib Haddaad akidumu kwenye vikao vyake juu ya kusoma elimu na kukumbushana elimu za

dini, na kuwazuia wanaokaa naye wasizungumze mambo ya haramu, kama kusengenya na kufitini watu, wala maneno ya dunia, akisema, “Tabia yangu inachukia kuzungumzia mambo ya kidunia tangu zamani, na inachukia kujionyesha na kujikalifisha kwa watu”. Akisema pia, “Musiniombe ushauri kwenye mambo ya kidunia, wala musinitajie ...inabidi iwe ni mambo ya akhera tu ...dunia ashauriwe mwengine asiyekuwa sisi”. Aliandikiwa na mmoja katika wanaompenda, kuwa mukiwa na haja au kitu chochote, mutuambie kwani sisi tuko kwenye utumishi wenu. Habiib Haddaad hakufurahi kwa maneno haya, na kusema, “Kwani sisi wafanya biashara hata tuwahitajie, sisi hatuna haja ya chochote kutoka kwao ila wamche Mwenyezi Mungu na watekeleze yaliyowalazimu katika haki za Mwenyezi Mungu na haki za waja wake. Hii ndio haja tunayo taka kwao”. Habiib Haddaad alikuwa akiwaangalia sana mayatima na wajane, akiwapa wanayohitaji kwenye maisha yao.

Habiib Haddaad alijenga misikiti mingi, miongoni mwayo ni msikiti wa Awwaabiin hapo Nuwaydira, msikiti wa Abraar hapo Sibayr, msikiti wa Fat-hi hapo Haawi, msikiti wa Ba Alawiy Seiyun, na msikiti wa Abdaal Shibaam.

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas-Mwenyezi Mungu amrehemu: "Mfuateni Habiib Abdillah Haddaad na wengine katika Salaf, na mujue kuwa hakuna aliyekuja na mfano wa aliyo kuja nayo Habiib Abdillah katika elimu yake, mwendo wake, ulimi wake na kalamu yake".

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas(ra), "Lazimianeni na kutalii vitabu vya Salaf Alawiyyiin na hakuna chenye kunufaisha kwenye kuongoza na kulingania kwa Mwenyezi Mungu zaidi ya hivyo. Na ambao katika Salaf hawazungumzi naibu wao amekuwa kalamu, ila Al-Habiib Abdillah bin Alawiy Haddaad kwani yeye amekusanya kulingania kwa mdomo, kalamu na nyendo".

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas(ra) baada ya kutaja vitabu vilivyotungwa na Habiib Abdillah Haddaad, “Ama Al-Habiib Abdillah Al-Haddaad katika kuandika ibara na kufikisha na kuongoza, hakuna katika Salaf mfano wake, Mwenyezi Mungu amemkusanyia

mdomo, kalamu na mwendo. Na yeye anazungumzia uimamu makhsusi kwenye Ahlil bayti,na kwenye Alawiyyiin hakuna aliye khusishwa kwa haya matatu na akayakusanya ila Al-Habiib Abdillah. Na pamoja na hayo Amemfanya kupendwa na viumbe. Je umesikia mtu ambaye anakimbia maneno ya Habiib Abdillah (yaani hayataki na kuwa mbali nayo) ila ambaye hana raghba ya kheri. Na kila siku yanaimbwa maneno yake (qasida zake) na zinafahamika upya maana zake."

Habiib Abdillah Haddaad alifariki usiku wa kuamkia Jumanne, tarehe 7 Dhul-Qa'ada mwaka 1103H. Na imepokewa kwamba katika ugonjwa wake wa mauti akiitaja sana hadithi ya Mtume(saw) iliyo mwishoni mwa Bukhariy, **"Maneno mawili yaliyo mepesi kwenye ulimi, mazito kwenye mizani, yanayo pendwa mno kwa Rahmani; *Subhanallah wa bihamdihi, Subhanallah Al-adhiim*".**

Al-Habiib Ahmad bin Zayn Al-Habashy:

Jina lake: Habiib Ahmad bin Zayn bin Alawiy bin Ahmad (Saahib Shiib) bin Muhammad bin Alawiy bin Abi Bakr Al-Habashy (Kwa sababu ya kukaa sana Habasha) bin Aliy bin Ahmad bin Muhammad (Asadullah) bin Hasan bin Aliy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam mpaka kwa Mtume(saw)-rehema na amani zimshukie.

Alizaliwa mwanzoni mwa mwaka 1069H Ghurfa na akalelewa huko na baba yake, akahifadhi Qur-ani, na alijitahidi tangu utotoni kutafuta elimu. Wakati wake Ghurfa haikuwa na wanachuoni wengi, akawa anakwenda kwa miguu kwenye miji ya karibu kama Shibam, Tariis, na Seiyun. Hata Tariim alikuwa akienda kwa miguu pamoja na mtumishi wake na wanabeba tende tu, kama chakula chao usiku na mchana. Huko Tariim mwanzoni alisoma kwa Habiib Abdallah bin Ahmad Balfaqiih kabla ya kujuana na Habiib Abdillah Haddaad. Alipofika kwa Habiib Abdillah Haddaad alitua kwake moja kwa moja, akasoma na kupata baraka zake, na kufuata ushauri wake hadi akashika mahala pake na wanafunzi wengi wa Habiib Haddaad wakaja kwake kusoma. Alisoma kwa Habiib Haddaad karibu miaka 40. Katika masheikh zake wengine ni Habiib Ahmad bin Umar Al-Hindawaan na Habiib Ahmad bin Hashim Al-Habashy. Masheikh zake wote walikuwa wakimpenda kwa jitihada yake kubwa, utambuzi wake na uhodari wake. Hata mara moja kwenye ziyara ya Nabii Huud(ra), Habiib Ahmad Al-Hindawaan alimwona Habiib Ahmad bin Zayn akiwa na bashasha na furaha na jamaa zake, akaitamka hadithi ya Mtume(saw), “Hakika Mwenyezi Mungu ana watu wenye pupa ya kutenda kheri katika viumbe wake, anawahuyisha kwenye afya na anawafisha kwenye afya”. (Tabraaniy), na nataraji wewe uko katika wao.’

Jitihada zake kwenye ibada zilianzia alipokuwa akitembea kwa miguu kwenda mji hadi mji kutafuta elimu. Alikuwa pia akizuru sana waliokwisha tangulia, akizuru Nabii Huud, Inaat na Bayt Jubair. Ama Tariim alikuwa akizuru Zanbal na akipenda kutembelea misikiti na sehemu walizokuwa wakifanya ibada Salaf wema walio tangulia. Alikaa sana Tarim akisoma kwa Habiib Haddaad. Mama yake

alikwenda kulalamika kuwa mtoto wake anakaa sana Tariim na kwamba anapata taabu (kwa kumkosa). Habiib Haddaad akamwambia awe anakaa Tariim siku 3 tu katika mwezi. Hili lilimsumbua sana Habiib Ahmad bin Zayn lakini akawa hana njia ya kufanya. Pia alikuwa akizuru sana Mash-had ya Handhalah iliyopo Buur, khasa akiweko Habiib Ahmad bin Hashim, na huenda hadi nyumbani kwake. Alikuwa pia akizuru Seiyun na Shibam akizuru misikiti yake na makaburi yake.

Habiib Ahmad bin Zayn alijenga misikiti mingi, hata Habiib Haddaad akimwita baba wa misikiti. Katika misikiti hiyo ni: Ba Alawiy na Rawdha iliyopo Ghurfa, Bahaa uliyoko Khal-i' Rashid, pamoja na kujenga misikiti katika vitongoji vingi miongoni mwake ni Jawha, Shiib Shuhooh, Jawad, Kharaabah, Ardha na Qaarah. Pia aliamirisha kwa kurekebisha majengo kwenye misikiti ya Ma'roof uliopo Shibaam, Masjid Rushd mkubwa, na masjid bin Ahmad uliopo Shibam. Alikuwa akiwaamrisha wakazi wake kuswali Ijumaa hata kama hawajatimia idadi watu 40, akiwa na makusudio ya kudhihirisha na kutangaza dini.

Alikuwa Habiib Ahmad akienda mji wowote au sehemu, hukusanyika watu wengi kwa ajili yake, na lazima mkusanyiko huo uwe ima na dhikri, au maulidi, au kusoma elimu au kutoa mawaidha kwani yeye alikuwa hachoki kusomesha hadi mwisho wa umri wake.

Habiib Ahmad bin Zayn alikuwa akichunga sana wakati wake kwa kuhakikisha haupiti bure ila anafanya jambo la kheir ima kuswali, kusoma Qur-ani, kusoma elimu, kuamrisha mema na kukataza mabaya au kulingania watu kwa Mwenyezi Mungu. Katika nyiradi zake alikuwa akileta kalima ya tawhiid, yaani *Laa ilaaha illa-Llahu*, mara 70,000 kila siku. Na hasikii kitu chochote cha fadhila katika matendo ya Mtume(saw) au ya waja wema walio tangulia ila hudumu juu yake. Wakati alipokuwa mtu mzima na akawa hawezi kusimama, akipata ukunjufu kidogo tu huswali kwa kusimama akitaka radhi za Mwenyezi Mungu. Hata kwenye utu uzima wake alikuwa hawachi kufanya mambo ya kheir na kuamka usiku akisoma Qur-ani mahala pake anapo lala na kusoma nyiradi.

Habiib Ahmad bin Zayn aliipa nyongo sana dunia na hakuwa na tamaa ya chochote katika maisha yake yote. Alikuwa hapendi kuzungumza mambo ya kidunia wala kuzungumzwa mbele yake. Aliwahi kumjia mtu mwenye ugonjwa na kutaka aombewe Mungu ili apone. Mtu huyo alisema kumwambia Habiib Ahmad bin Zayn, "nikipona nitakupa nusu ya mali yangu". Habiib Ahmad akamwangalia kwa hasira, kisha akasema, "Mwangalieni huyu mpumbavu, anatutajia mali, anahisi sisi tunaiona mali (kuwa ni kitu cha utukufu)? Au ina kima chochote mbele yetu". (Kisha akamwelekea) na kumwambia, "Wewe unataka tusikuombee dua wala tusikurehemu kwa maneno yako uliyotuambia". Mtu mmoja katika wanao soma alikwenda na kukaa kwake siku 3, hakuwahi kumsikia akitaja Dunia katika kikao chake chochote.Na alikuwa akitoa zaka hutoa mara mbili au mara tatu zaidi, na akisema: Mali yetu yote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Katika kisa chengine, alikuja mtu mwenye mali, akataka amchukue kuhiji na abebe yeye masurufu yote, lakini Habiib Ahmad akatoa udhuru wa kutokwenda. Yule mtu akamwuliza cha kumnunulia katika nguo au vingine. Habiib Ahmad bin Zayn akamwandikia kuwa hahitaji chochote ila maji ya Zamzam.

Alikuwa hana tamaa ya cheo, wala umashuhuri alioupata haukumzuia na tabia yake ya kusema haki kwa yeyote, wala hawatukuzi wenye vyeo. Ama madhalimu huwaambia wazi bila ya kuogopa. Alikuwa kiongozi mmoja akimwandikia na alikuwa dhalimu. Katika baadhi aliyoandika Habiib Ahmad ni haya: **"Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayo yafanya madhaalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatapokodoka macho yao".** (Ibrahim: 42).

Akichukua kibarua humlipa zaidi ya alivyokubaliana naye, khasa ikiwa kwenye jambo la kheri kama kujenga msikiti au kuandika kitabu. Hata amesikika mara nyingi akisema, "Mwenye kumchukua kibarua katika kazi yoyote kisha akashindana naye kwenye malipo kwa ujira ulio mdogo kuliko kazi yake hata kama akiridhia, ni dhulma, basi atanabahi na hayo". Hata siku moja alifanya kazi mtu mmoja ya kuhamisha

udongo kwenye baadhi ya misikiti yake, akauliza huwa analipwa kiasi gani, wakamtajia, akawaambia, “mlipeni mara mbili yake”.

Alikuwa pia akiwakirimu wageni khasa wakiwa ni watafutaji elimu au mafakiri na huwalisha chakula na kuzungumza nao kwa bashasha wakikaa siku kidogo au siku zaidi. Alikuwa pia akiwakirimu masharifu walio toka Tariim wakija kumzuru, pia wanafunzi wa Sheikh wake Habiib Haddaad.

Alipokuwa Ghurfa alikuwa anafanya karamu kubwa kubwa khasa kwenye mwezi wa Ramadhani, na wakihudhuria watu wengi wa mjini na wa nje. Akijiwa na mgeni ghafla huwa hajikalifishi na humwekea kile alichonacho. Ama watu wa serikali na watu wa mashamba ambao makusudio yao ni Dunia tu, hukaa nao kwa tabia njema na huzungumza nao kwa uzuri lakini hawawekei karamu kama za wageni wa elimu.

Alikuwa na pupa sana ya kuwarejesha watu kwenye haki. Pamoja na kujua hali za watu na tabia zao, alikuwa hawataji kwa majina bali huzungumza kwa upole na huruma na kuwalingania kwa njia bora kabisa kama ambavyo Mtume(saw) alivyokuwa akifanya. Ila kwenye baadhi ya wakati ikimshika ghera ya kidini na baya likafanyika kwa wazi, huwa hakuna wa kuweza kumzuia yeye na kusema na kukemea kwa ukali kabisa. Alikuja kwake mmoja wa masharifu akitaka aombewe asiadhibiwe kwa adhabu ya kisheria, akamwambia, “Vipi itaniwia mimi kufanya hayo? Na upanga wa sheria uko kwenye bega langu (au shingo yangu)?”

Habiib Ahmad bin Zayn alikuwa ni mtu mwenye subira, asiye na haraka kuwaapiza watu, bali husamehe na hawalipi ila kwa jema. Alipokuwa Ghurfa na kupata umashuhuri waliudhiwa walionasibika na yeye kwa kutukanwa na kupigwa. Akaja mtu mmoja mwenye cheo serikalini na kumshauri kuwa waadhibiwe wale waliofanya mabaya, akamkataza kata kata, na hakutaja tena kadhia hiyo. Hata wafuasi wake akiwahimiza kuwa wenye subira na kusamehe. Mmoja katika masharifu aliudhiwa na baadhi ya viongozi kwenye suala la mali yake hata akapata taabu sana. Yule sharifu akaja Ghurfa msikitini kwa Habiib Ahmad na kutaka kumwapiza yule kiongozi. Pale pale akatokezea Habiib Ahmad na kumwambia, “sema: Ewe Mwenyezi Mungu

mwongoe, Ewe Mwenyezi Mungu mtengeneze, Ewe Mwenyezi Mungu nikinge na shari yake, lakini usimwapize.”

Alifariki Alasiri tarehe 19 Shaaban, mwaka 1114H na kuzikwa hapo hapo Khal-i’ Raashid (sasa hivi maarufu kama Hawta).

Al-Habiib Umar bin Saggaaf Al-Saafiy Al-Saggaaf

Jina lake: Al-Habiib Umar bin Saggaaf bin Muhammad bin Umar bin Taha bin Umar bin Taha bin Umar Al-Saafiy bin Abdul-Rahman bin Muhammad bin Aliy bin Abdul-Rahman Saggaaf mpaka kwa Mtume(saw).

Alizaliwa Seiyun mwaka 1154, na kulelewa na baba yake na babu yake kwa mama yake Habiib Aliy bin Abdallah Saggaaf aliyemdiriki na kuchukua elimu kwa Habiib Haddaad. Katika masheikh zake wengine ni Habiib Hasan bin Aliy Al-Jufry wa Tariis, Habiib Muhammad bin Zayn bin Sumeit, Habiib Ja'afar bin Ahmad bin Zayn Al-Habashy, Habiib Hasan bin Abdillah Haddaad, Habiib Aydaroos bin Abdul-Rahman bin Abdallah Balfaqiih, na Habiib Hamid bin Umar.

Ama wanafunzi wake ni wengi mno, baadhi yao ni watoto wake, ndugu zake Muhammad, Hasan na Alawiy, na Habiib Saggaaf bin Muhammad bin Aydaroos Al-Jufriy, Habiib Tahir bin Husain bin Tahir, Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit, Habiib Hasan bin Saleh Al-Jufriy, Habiib Muhammad bin Ahmad bin Ja'afar Al-Habashy, Habiib Abdallah bin Husain bin Tahir, Sheikh Abdallah bin Sumayr na Sheikh Abdallah Ba Sawdan.

Ama kuhusu asili ya kuhamia kwa wajukuu wa Habiib Taha bin Umar Saggaf Seiyun na kufanya makazi yao hapo, tunanukuu maneno ya Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas-Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema: "Sultan Badr aliwaomba masharifu wa Tariim wakati wake wamhamishe mmoja wa watoto wao aje akae Seiyun. Wakamwambia Habiib Taha bin Umar bin Taha aende Seiyun, akawapa shuruti tatu (ili akubali kuhamia Seiyun, yaani wamwombee yapatikane mambo haya matatu), wasiache kuwa katika watoto wake wanavyuoni 40, iwe msikiti wake na uwanja wake sehemu ya Tariim na ipate utukufu wake (wa Tariim), na isipungue safu za wenye kuswali msikitini kwake na safu tatu, wakamkubalia na akaenda Seiyun."

Alijaaliwa kuwa na akili pevu na utambuzi wa hali ya juu tangu utotoni; aliandika mashairi kabla hajafikia umri wa miaka 7. Alikuwa akizungumza na masheikh zake na akifanya ***bahthi*** (tafiti za mas-ala)

pamoja nao naye akiwa na umri mdogo sana. Hata baba yake alimnyang'anya kitabu cha ibn Al-Muqriy na kukichana kwa kuona umri wake ni mdogo na atapatwa na kijicho kwa uhodari wake.

Alisimama kwenye kazi ya kufundisha na Da'awa. Wamechukua elimu kwake wanafunzi wengi. Alikuwa na darsa za kila siku katika fani za Fiq-hi, Hadithi na Tafsiri, pamoja na umahiri wake kwenye elimu za ala kama Nahau, Sarufi, lugha na mashairi. Ama Tasawwuf kilikuwa ndio chakula chake; akidumu juu ya vitabu vyake kama *Risaala*, *Awaarif*, *Lataaif Minan*, na vitabu vya Habiib Haddaad. Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy amesema kwamba masheikh wengi wa wakati wake wamenasibika na yeye, kwani alikusanya elimu ya hadithi na tasawwuf. Kisha akaendelea kusema, "Hata wakawa wakisomesha darasa au wakiandika kitabu na kusema amesema sheikh wetu, hawamkusudii mwengine ila yeye (Habiib Umar bin Saggaaf)".

Habiib Umar alikuwa ana jitihada kubwa kwenye ibada, pamoja na kushughulika kwake na kusomesha, na ndiye aliyekuwa Imaam wa msikiti wa Taha wakati wake. Alikuwa akizungumza na watu kwa wema, mwenye subira kubwa, na huruma juu ya watu pamoja na umaarufu alioupata.

Alihamia Suum (mji baina ya Seiyun na Tariis) mwisho wa umri wake na kuuamirisha mji huo, ambao ulishaachwa na kuwa kituo cha majambazi. Mji ukachangamka kwa kuja kwake, mashamba yakamea mazao, na nyumba zikajengwa.

Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas-Mwenyezi Mungu amrehemu, aliwahi kumtaja Habiib Umar bin Saggaaf Al-Saafiy akasema: "Yeye ndiye sheikh wa Muta-akhhiriina, wote wamechukua kwake; kama Habiib Hasan bin Saleh Al-Bahr, Habiib Tahir bin Husain, Habiib Abdallah bin Husain, Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit, Habiib Hadun bin Hud Al-Attaas, Habiib Umar Al-Baar wa mwisho, na mfano wao katika watu wa zama zao. Na alipo ingia Doan alipata umashuhuri mkubwa sana, na zikakusanyika zawadi za watu wa Doan kofia 500, shali na blanketi mizigo (twika) mitatu. Nikamwuliza mtoto wake Sayyidiiy Al-Habiib Sheikh bin Umar kwa yaliyo tajwa, akakiri hayo, na kusema: Nilikuwa na baba yangu kwenye kuingia kwake Doan, na

baada ya kufika Seiyun kwa siku tatu, alimwomba mama yangu shali kwa ajili ya watoto wadogo, akasema Sayyidiy baba yangu, tumeshatoa vyote tulivyo vipata, lau ungetuambia kabla tungekupa.”

Alifariki usiku wa kuamkia Jumatatu tarehe 20 Shawwaal, mwaka 1216, na alibebwa juu ya migongo ya watu toka Suum akisindikizwa na halaiki ya watu hadi Seiyun alikozikwa.

Al-Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit

Jina lake: Al-Habiib Ahmad bin Umar bin Zayn bin Alawiy bin Abdul-Rahman bin Abdallah bin Muhammad Sumeit bin Aliy bin Abdul-Rahman bin Ahmad bin Alawiy bin Faqiih Ahmad bin Abdul-Rahman bin Alawiy (Ammil Faqiih) bin Muhammad Sahib Mirbaat mpaka kwa Mtume(saw).

Alizaliwa mwaka 1177, na akasoma kwa baba yake Habiib Umar ambaye alimdiriki Habiib Abdillah Haddaad, kwani alipofariki Habiib Haddaad alikuwa na umri wa miaka 12. Katika jumla ya vitabu alivyosoma Habiib Ahmad kwa baba yake ni pamoja na *Ihyaa*, vitabu vya Habiib Haddaad, vitabu vya Habiib Ahmad bin Zayn, na vitabu vya ammi yake Habiib Muhammad bin Zayn, na vingine katika fani nyingi sana. Baada ya baba yake kufariki alilazimiana na Habiib Haamid bin Umar Haamid aliyepata maisha marefu. Na huyu na baba yake ndio masheikh zake wakubwa. Wengine aliosoma kwao ni Habiib Umar bin Saggaaf, Habiib Ahmad bin Hasan Al-Haddaad, Habiib Umar bin Abdul-Rahman Al-Baar wa pili, na mtoto wa ammi yake Habiib Abdul-Rahman bin Muhammad bin Zayn.

Mtu wa mwanzo kuhamia Shibam katika Bin Sumeit ni ammi yake Habiib Muhammad bin Zayn kwa ishara ya Habiib Ahmad bin Zayn Al-Habashy. Habiib Ahmad bin Zayn alimwambia, “Tumesikia kuwa Habiib Umar Al-Attaas amesema, hakika watu wa Shibam wakimjua walii watakuwa juu yake kama nzi wanavyokuwa juu ya asali. Na sisi hatuna shaka na wewe, tunataka kujaribu kwa (kukupeleka) wewe ... Makusudio yetu ukae Shibam unufaike na sisi. Na watu wanufaike na maneno yako, kama alivyosema Sheikh wetu Abdillah, chukua kwetu na uwaidhi watu”. Akatekeleza amri ya Sheikh wake, akafanya kazi ya da’awa na watu wakanufaika na yeye, hata Sheikh wake akamwambia, “Hakika kukaa kwako kwenye mji huu ni rehema ya Mwenyezi Mungu, na kabla yako hakudhihiri (kwenye mji huu) yeyote katika watu wa Tasawwuf ila alipata maudhi. Hawakusalimu (amri) watu wake ila kwa Habiib Abdillah Haddaad. Na sisi tuko juu ya nyayo zake, na wewe uko juu ya nyayo zetu”. Habiib Muhammad bin Zayn alifanya kazi kubwa

ya kufundisha fani za kila aina na akaandika vitabu vingi vyenye faida kubwa.

Na Habiib Ahmad bin Umar alifanya kazi kubwa ya kulingania kwa Mwenyezi Mungu. Bali alipokuwa akiifanya kazi hiyo alichukua ahadi kwa wanafunzi wake kuifanya kazi hiyo na kuwaambia kuwa ni kitendo bora kuliko vingine. Na akija mwanafunzi wake kumzuru mara ya pili humwuliza matendo aliyoyafanya katika Da'awa. Habiib Ahmad bin Umar aliombwa na mtu ruhusa kusafiri. Akamwambia, "Hamna ruhusa kusafiri ila ukiwa na nia ya kulingania kwa Mwenyezi Mungu". Aliweka utaratibu wa kusoma Sura ya Faatiha na Tashahhud baada ya adhana kwa sauti ili watu wajue na kuhifadhi. Akiwawekea watu muda maalumu wa kuwasomesha, na watu wa mashamba akiwapa siku yao ambayo huja kwake kusoma. Habiib Ahmad bin Umar aliwahi kuambiwa, usijikalifishe sana kwenye kulingania kwa Mwenyezi Mungu, akasema kuwaambia, "Masahaba wamejitolea mali zao na roho zao kwa ajili ya kuliweka juu neno la Mwenyezi Mungu, vipi mimi nisijikalifishe? Na mimi zaidi (nafanya nini? si) nazungumza kwa ulimi wangu!" Habiib Ahmad bin Umar hakuishia hapo, akawa anaeneza vitabu vidogo kwa ajili ya kusomesha na kuhifadhi, akiwahimiza wanavyuoni kuandika vitabu vyenye manufaa na kuvieneza kwa watu.

Katika vitabu ambavyo alikuwa akivihimiza ni *Fat-hur Rahman* cha Sheikh Ibn Ziyaad Al-Zabiidy, hata kikawa kinasomwa baada swala khasa asubuhi na alasiri, na wakati wa kunyanyua jeneza, na kwenye vikao vinavyo somwa maulidi, watu wote wakisoma kwa sauti moja, hata kilitangaa kwa watu kuwa ni uandishi wake kutokana na kukihimiza sana. Hata aliwahi kuuliza, "Akija Mtume(saw) akamwona mtu mmoja anasoma maulidi na mwengine anasoma *Fat-hur Rahman* atakaa kwa nani?" Akajibu mtu mmoja, "Atakaa kwa mwenye kusoma *Fat-hur Rahman"*. Akasema, "Basi juu yako kuanza na kilicho na umuhimu zaidi kabla ya chenye umuhimu, na weka pupa katika kuutumia wakati wako kwenye kutafuta elimu yenye manufaa."

Habiib Ahmad alikuwa akihimiza sana kuwasomesha mabinti wakiwa wadogo, na kuwasomesha akina mama; na husema, "Mke ni waziri, akitengenea watatengenea watoto wa kiume na wa kike, bila ya hivyo

wataharibika wote". Katika maneno yake anasema: "Afya ya kweli wakiwa familia yako wanataka uwasomeshe, na wanakung'ang'ania, na wanashtaki kwa wengine kwa kutokuwasomesha". Katika maneno yake amesema, "Akina mama na wenziwao wanasema kwa ulimi wa hali (si kwa maneno) kumwambia mwenye nyumba akitaka kutoka kwa ajili ya kumzuru walii au kikao cha elimu ambacho sio wajibu, ukiwachilia mbali kikao cha porojo, "Je, inakuwia utoke na ilhali sisi hatujui sheria za Kiislamu na wala hukai kutufundisha? Unajuaje, pengine mauti yatakuja kwa ghafla kwako au kwetu, na sisi tumejingika. Tutakukamata siku ya Kiyama tukikushtaki kwa Mwenyezi Mungu tukisema, 'Ewe Mwenyezi Mungu tuchukulie haki yetu kutoka kwake, kwani alitudhulumu hakutufundisha sheria za Kiislamu!'"

Hakuishia hapo tu Habiib Ahmad bin Umar bali alipangilia masuala ya uchumi, akawa anamwekea kila mwenye mali mtu aliye fukara ili amkopeshe na wagawane faida. Pia alikuwa akiomba dua sana na kuwahimiza watu kuomba wapate kiongozi wa nchi aliye mwadilifu, na akisikitika sana kwa kukosekana kwake.

Pamoja na kwamba hakuandika vitabu, lakini alihimiza wengi kuandika na yeye ndiye sababu kubwa ya kuvieneza, katika vitabu vilivyo andikwa kwa sababu yake ni:

- *Simtul-Iqyaan* sherhe ya *Riyadhatul-Sibyaan* kilichoandikwa na Sheikh Abdallah Ba Sawdan.
- *Kaafiy Al-talib* ufupisho wa *Silatil-Aqaarib*, asili ni ya Imaam Ibn Hajar, ufupisho ni wa Sheikh Abdallah bin Sumayr.
- *Mudhaakaratul-Tulaab fi qawaaid Al-Iraab* cha Sheikh Muhammad bin Abi Bakr mashuhuri kama Bakkaar katika nahau.
- Khutba ya Habiib Tahir, na sherhe yake ya Sheikh Abdallah Ba Sawdaan, na utungo wake ya Sheikh Ahmad bin Umar Ba Dhiib.
- Safina Najaa cha Sheikh Salim bin Abdallah bin Sumayr

Imepokewa kutoka kwa Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas alipopita Shibaam chini ya baadhi ya nyumba, alimsikia bibi mmoja akiendesha jiwe la kusaga huku akisoma alichohifadhi katika *Fat-hur Rahman* na kuisoma hadithi ya Jibriil mashuhuri iliyopokewa kutoka kwa Sayyidna Umar, akasimama akisikiliza na huku akiwa amepata mazingatio makubwa hadi akatokwa na machozi na kusema, "Amali yako uliifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ewe Ahmad bin Umar! Umemtoa Jibril mbinguni juu mpaka kwa huyu mama aliyekaa juu ya jiwe la kusaga."

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas-Mwenyezi Mungu amrehemu-kumwambia Habiib Ahmad bin Abu Bakr bin Sumeit, baada ya kumuusia yeye na wenzake kufanya kazi ya kulingania kwa Mwenyezi Mungu: "Je hamjasikia mfano wa wazi kuambiwa ambaye anataka kufundisha au kukumbusha, kwani wewe ni Ibn Sumeit ?. Jambo linalo onyesha kuwa kulingania kwa Mwenyezi Mungu ndio kazi yao kubwa, na Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit ameeneza bendera za kulingania kwa Mwenyezi Mungu na akajaalia kuwa na kichwa, miguu na mikono."

Amesema Habiib Ahmad bin Hasan(ra), "alikuja Shibaam Habiib Tahir bin Husain bin Tahir(ra), Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit akamwambia, "Muradi wetu ni kuwa uwakumbushe watu baada ya (swala ya) Ijumaa". Akaiandika khutba yake mashuhuri kabla ya kuswali Ijumaa na baada ya swala akapanda mimbarini na kuisoma.

Na kwenye maneno mengine ya Habiib Ahmad bin Hasan, "alipita mara moja mmoja wa masharifu kumpitia Habiib Ahmad bin Umar, akamuuliza, "Unakwenda wapi". Akamwambia nakwenda kuzuru pande za Kibla (Kaskazini). Akamwambia ukiwa unaenda kufanya ulinganiaji wa Mwenyezi Mungu na kufundisha watu basi sawa, ama sivyo hamna ruhusa (kwenda). Akasema yule sharifu nitalingania kwa Mwenyezi Mungu na nitafundisha watu. Akampa ruhusa na akalingania kwa Mwenyezi Mungu na kufundisha watu na akapata kabuli. Na ulingano wa Mwenyezi Mungu ulikuwa umelala (Habiib Ahmad bin Umar) akauamsha ukawa unaenda kwa miguu yake na mikono yake."

Habiib Alawiy bin Shihaab amesema, “Amesema mmoja katika wenye maarifa ya Mwenyezi Mungu, Da’awa ya Habiib Ahmad bin Umar imegonga masikioni (kwa watu) zaidi ya Da’wa ya Imaam Haddaad.”

Habiib Ahmad bin Umar alikuwa na wanafunzi wengi walioenea kila sehemu Hadhramout, bali imepokewa kuwa hakuna mwenye wanafunzi wengi na ambaye wakati wake wanavyuoni wote walimkubali kama Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit. Katika wanafunzi wake ni wanavyuoni 7 wenye jina la Abdallah nao ni: Sheikh Abdallah Ba Sawdan, Habiib Abdallah bin Aliy bin Shihaab, Habiib Abdallah bin Husain Balfaqiih, Habiib Abdallah bin Husayn bin Tahir, Habiib Abdallah bin Umar bin Yahya, Sheikh Abdallah bin Sa’ad bin Sumayr, na Habiib Abdallah bin Abi Bakr Aydeed. Wengine ni Habiib Hasan bin Saleh Al-Bahr, Sheikh Ahmad bin Umar Ba Dhiib, Habiib Muhsin bin Alawiy Saggaaf, na Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy.

Alifariki Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit siku ya Jumatano tarehe 17 Dhul-Qa’ada, mwaka 1257H na kuzikwa Jarb Haysam, makaburi maarufu Shibam.

Al-Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy

Jina lake: Al-Habiib Aydaroos bin Umar bin Aydaroos bin Abdul-Rahman bin Isa bin Muhammad bin Ahmad (Saahib Shiib) bin Muhammad bin Alawiy bin Abi Bakr Habashy, bin Aliy bin Ahmad bin Muhammad Asadullah bin Hasan Turabi, bin Aliy bin Al-Faqiih Muqaddam mpaka kwa Mtume-rehema na amani zimshukie.

Alizaliwa Ghurfa, siku ya Ijumaa tarehe 23 Muharram 1237H. Akalelewa na baba yake na ammi yake Habiib Muhammad bin Aydaroos. Akasoma kwa ammi yake Qur-ani na aqida za dharura (lazima kila mtu kuzijua). Alipo fariki ammi yake naye akiwa na miaka 10, akasoma kwa baba yake vitabu vya mwanzo katika fani za Fiq-hi na Nahau. Tangu utotoni ammi yake alikuwa akimchukua kuhudhuria darsa za Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit. Habiib Aydaroos alisafiri kwenda sehemu mbali mbali za Hadhramout kutafuta elimu. Alipokwenda Hijja alikutana na wanachuoni ambao alichukua kwao elimu. Masheikh zake ni wengi mno wanazidi 100, na amewataja baadhi yao kwenye kitabu *Iqdil Yawaaqit*. Miongoni mwao ni hawa watatu tuliowataja mwanzo, wengine ni: Habiib Muhammad bin Ahmad bin Ja'afar Al-Habashy, Habiib Hasan bin Saleh Al-Bahry, Habiib Abdallah bin Husain bin Tahir, Habiib Aliy bin Umar Saggaaf, Habiib Abdallah bin Aliy bin Shihaab, Habiib Ahmad bin Aliy Al-Juneid, Habiib Abdallah bin Husain Balfaqiih, na Sheikh Abdallah Ba Sawdaan.

Na wanafunzi wake pia ni wengi sana, tutawataja hapa baadhi yao tu: watoto wake, Habiib Salim bin Taha Al-Habashy, Habiib Ubeydillah bin Muhsin Saggaaf, Habiib Sheikhan bin Muhammad Al-Habashy, Sheikh Umar bin Awadh Sheibaan, Sheikh Hasan bin Awadh Mukhaddam, Habiib Abdallah bin Hasan Al-Bahry, Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas na Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy.

Habiib Aydaroos ndio marejeo ya watu wa Hadhramout kwenye *Isnaad*, bali ni marejeo ya dunia nzima wakati wake kama walivyo thibitisha hayo wanachuoni wenye kutegemewa. Alifanya kazi kubwa ya kuhifadhi mlolongo wa elimu hadi kwa Mtume(saw) na akaandika

vitabu ambavyo aliweka wazi humo sanad yake na sanad ya masheikh zake. Katika jumla ya vitabu hivyo ni *Iqdil Yawaaqiit*, na *Uquud La-aal*, pamoja na kwamba aliandika vitabu kwenye fani nyengine pia.

Habiib Aydaroos alikuwa ana tabia njema kabisa, alikuwa mwenye huruma kwa madhaifu, hata akienda kwenye ziyara ya Nabii Huud(as) huwa anakwenda pole pole kwa ajili ya kuwa sawa na wasio na uwezo na madhaifu. Hata akisafiri kwenda sehemu mbali mbali kama Tariim na Seiyun pamoja na utu uzima wake ni kwa sababu watu wanufaike na yeye, kwani ilikuwa ni wajibu wao ndio waje kumzuru, lakini yeye anakwenda kwao ili wapate manufaa na wapate kumfuata tabia zake njema na wapate baraka zake.

Alikuwa Habiib Aydaroos akijiwa na watu wenye umashuhuri na uongozi huwakirimu sana na hujitahidi kuwawekea vyakula vizuri, akaambiwa kwa nini munakalifisha nafsi zenu katika kuwalisha watu chakula kizuri wakati yanawatosha hata maji ya nyumbani kwenu, na hawa (wanao kuja kwenu) hawana makusudio ila kuwazuru na kuwaangalieni na inatosha hiyo kuwa ni ikraamu yao? Akasema (Habiib Aydaroos)-Mwenyezi Mungu amwie radhi, "Hakika watu wa zama hizi wamezoea chakula kizuri na hawawezi kukinai bila yake (chakula kizuri)". Anasema Habiib Ubeydillah bin Muhsin Al-Saggaaf mwenye kukusanya maneno yake: "Amehofia (Habiib Aydaroos) kwa kutokukinai kwao kwa alichonacho katika vyakula vya chini (ikiwa ina maana anawalisha chakula kizuri kuliko anacho kula mwenyewe), na ikawa ni sababu ya kuharibika nia zao njema kwa Al-Habiib, wakapungukiwa na baraka ambazo wangezipata kwa Al-Habiib. Na hilo si ajabu kwa watu wa zama hizi kutokana na upungufu wa elimu yao. kwani Al-Habiib-Mwenyezi Mungu amwie radhi-hata kama watu wa zama hizi wamekubaliana kwa kumtukuza na kumuenzi na kuwa na dhana nzuri sana juu yake, lakini tabia zao zimewazidia, wala si ajabu kwao kumili kwenye matamanio na dalili yake utamwona mmoja wao ukimwuliza juu ya ziyara yake kwa Al-Habiib kitu cha kwanza atakacho kwambia ni chakula alichokipata kwake kabla ya kukupa khabari ya faida alizo pata ambazo kwa ajili yake ndio anazuriwa. Kwa hili ndio utaelewa kuwa kufanya karamu kama hivi kwa Sayyidna (Habiib Aydaroos) ni kutokana na kuwa na rehema juu yao ili wapate

baraka kamili. Kama watu wagumu wa nyoyo na tabia katika Waarabu ambao Mtume(saw) akiwakaribisha kwa vitu vya kidunia mpaka ikawa mmoja wao anasema: Nilikuja kwako na hakuna niliyekuwa namchukia juu ya ardhi zaidi yako, na hivi sasa hakuna aliyejuu ya ardhi ninaye mpenda zaidi yako au kwa maana kama hii. Na hii ni kwa ikramu na kuhimili maudhi yao, na kwa ajili hii ndio wakaingia kwenye dini ya Mwenyezi Mungu vikundi kwa vikundi, na Sayyidna ana sehemu kubwa ya urithi wa Mtume(saw)-rehema na amani zimshukie." *Mwisho wa kunukuu.*

Aliwahi kuambiwa Habiib Aydaroos, hatujakusikieni mukimwamrisha wala kumkataza mtu maalumu wakati munajua anayofanya, kama walivyokuwa wakifanya wenye mwendo huu, akasema: "Hakika watu zama hizi tabia zao zimewashinda. Huenda ukimwamrisha mmoja wao au kumkataza kwa kumkusudia ataona uzito (wala hatokufuata), hata kama kabla ya hapo alikuwa akiahidi nafsi yake kuwa atafuata anayo ambiwa na kuacha aliyo katazwa." Na ndio maana Al-Habiib alikuwa akiamrisha na kukataza kwa jumla, na imepokewa kutoka kwa Mtume(saw) akisema: **"Vipi watu wanafanya hili ...vipi watu wanawacha lile?"**

Habiib Aydaroos alipata maudhi ya kila aina aliyoyapata kwa wakaazi wa mji wake Ghurfa, hata alitaka kuhama kwa maudhi aliyo pata lakini akaona bora asubiri na ataraji ujira kwa Mwenyezi Mungu. Habiib Aydaroos alipata umashuhuri mkubwa hadi wakawa wanamwonea hasadi na wakamchukia, mwisho wakaishia na kutumia uchawi, lakini yeye hakuwaapiza wala kuwaombea mabaya akimtegemea Mwenyezi Mungu kwa yote.

Alifariki Jumatatu Tarehe 9 Rajab 1314H, baada ya kuhimili athari ya uchawi aliofanyiwa kwa muda mrefu na alizikwa Ghurfa.

Al-Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy

Jina lake: Al-Habiib Aliy bin Muhammad bin Husain bin Abdallah bin Sheikh bin Abdallah bin Muhammad bin Husain bin Ahmad Saahib Shiib bin Muhammad bin Alawiy bin Abi Bakr Al-Habashy bin Aliy bin Ahmad bin Muhammad (Asadullah) bin Hasan (Turaabiy) bin Aliy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam mpaka kwa Mtume(saw)-rehema na amani zimshukie.

Alizaliwa Qasam siku ya Ijumaa tarehe 24 Shawwaal 1259H, baba yake na mama yake wote walifanya kazi ya Da'awa. Baba yake ni mwanachuoni aliyefanya kazi ya kusomesha na kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu. Alienda miji tofauti ndani ya Hadhramout akiwa hana kazi yoyote zaidi ya kulingania Dini, kumfundisha asiyejua na kumwongoza asiye na elimu. Masheikh zake ni wengi zaidi ya mia, kati yao ni Habiib Abdallah bin Husain bin Tahir na ndugu yake Habiib Tahir, Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit na wengine. Habiib Muhammad bin Husain alikubaliana na Habiib Abdallah bin Umar bin Yahya na Habiib Muhsin bin Alawiy Saggaaf na wakaandikishana pia kuwa "watajitahidi kwa kiasi cha uwezo wao kuwalingania ndugu zao katika masharifu na wengine (wasio masharifu) khasa kwenye wangwa wa Hadhramout, na kwamba watawahimiza kushikamana na elimu na matendo (yaliyolingana na elimu), na (kufanya) yale yaliyohimizwa na sheria tukufu, miongoni mwa matendo mema ..." Baadaye Habiib Muhammad bin Husain alihamia Makka na kushika wadhifa wa umufti na kufariki huko. Amesema Habiib Abdallah bin Husain bin Tahir: "Muhammad bin Husain ametekeleza kwa ukweli mlinganio wa Mwenyezi Mungu, Mtume-rehema na amani zimshukie- atamlipa kwenye watoto wake na watoto wa watoto wake, watakuwa mafaqihi wote".

Na kisa cha kuolewa mama yake Habiib Aliy, ni kuwa Habiib Muhammad bin Husain alienda Shibam akakutana na Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit na Habiib Umar bin Muhammad bin Sumeit akawauliza, "Je, muna mwalimu wa kike tunamhitaji afundishe kina mama?" Wakajibu, "Ndio". Je, unahitaji mwanamke wa kisharifu aliye mwalimu?" Akasema, "Ndio". Mama yake Habiib Aliy Habashy

alihama na familia yake na kuja Shibam wakapata kusoma chini ya uangalizi wa Habiib Ahmad bin Umar. Habiib Ahmad bin Umar akaenda kwa Habiib Husain bin Ahmad bin Al-Haadiy Al-Jufriy (babu yake Habiib Aliy upande wa mama) na kumwambia, "Amekuja sharifu mwanachuoni mwenye utukufu anamtaka binti yako Alawiyya amchukue, na apate kufundisha kina mama." Akakubali, wakamwuliza mahari, akasema kama ilivyo kawaida ya Ba Alawiy. Hawakuwa wenye uwezo, hata gharama za harusi, wala nguo walikuwa hawana, kila mmoja mwenye mapenzi ya masharifu akapeleka alichonacho. Hata chakula cha usiku watu walijitolea na kupeleka nyumbani kwao. Ikafanyika harusi usiku ule ule; na siku ya pili Habiib Muhammad bin Husain akampandisha ahli yake juu ya kipando huku akimwendesha. Wakafika Tariba, na alikuwa Habiib Muhammad bin Husain ana wake wawili kabla yake. Akaanza Habaaba na kazi ya kufundisha kina mama. Akamkuta bibi mmoja aliyekaribia siku zake za mwisho, hajawahi kuswali maisha yake, akamfundisha. Hazikupita siku tatu ila kulikuwa na safu nne za kina mama wanaswali nyuma yake. Baada ya siku kadhaa Habiib Muhammad bin Husain akampelekea khabari Habiib Ahmad bin Umar maendeleo ya Habaaba kusomesha kina mama. Habiib Ahmad bin Umar akamwambia mmoja wa watu wa Shibam, "Panda mimbarini na wasomee barua watu". Baada ya kupanda mimbarini na kuisoma, akasimama Habiib Ahmad bin Umar akasema, "Enyi watu wa Shibaam! Mulisema binti wa Al-Haadiy hakupata wa kumsindikiza, wallahi amesindikizwa na malaika".

Habiib Aliy aliwadiriki Habiib Abdallah bin Husain bin Tahir na Habiib Hasan bin Saleh Al-Bahry na kusoma kwao. Alisoma pia kwa Habiib Muhsin bin Alawiy Saggaaf, Sheikh Muhammad bin Abdallah Al-Khatiib Ba Rajaa, Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy, Sayyid Ahmad bin Zayniy Dahlaan wa Makka na Habiib Umar bin Abi Bakr Al-Jufriy wa Madina na masheikh wengine wengi. Ama masheikh zake wakubwa alio pata kwao faida zaidi ni wawili; baba yake na Habiib Abu Bakr bin Abdallah Al-Attaas. Habiib Aliy Habashy alikuwa na jitihada kubwa ya kusoma elimu na kutalii, alikuwa akitalii pamoja na kaka yake Habiib Husain sherehe 12 za kitabu cha *Minhaaj*!

Habiib Aliy Habashy alihamia Seiyun na kuanzisha darasa na kueneza elimu na Da'awa. Msikiti wa kwanza aliokuwa na darasa ulikuwa ni msikiti wa Hanbal. Darasa zake zilikuwa kwenye fani za lugha khasa Nahau (kwani yeye anahesabika kuwa ndio aliyehuisha Nahau Hadhramout kwa kuifundisha na kuitangaza), Fiq-hi, Hadiith na Tasawwuf. Mwenyezi Mungu akajaalia kabuli na wakawa wanahudhuria watu wengi. Pamoja na kufundisha alikuwa ni mtoaji mawaidha yenye kuathiri sana, na watu walikuwa wakilia sana na kutubia kwenye vikao vyake, hata mmoja wa wanafunzi wake anasema kuwa waadhi wake ulikuwa kama waadhi wa Sheikh Abdul-Kadir Jelaniy, kwani ulikuwa unakamua mioyo na kutoa machozi kutoka ndani kabisa ya macho. Alikaa karibu miaka 30 kwenye msikiti wa Hanbal akieneza elimu, dhikri na mafundisho ya dini.

Kisha akaanzisha Ribaat yake ambayo ndiyo ribaat ya kwanza Hadhramout nzima, na tunukuu maneno yake kwenye kuianzisha, "Niliazimia kujenga ribaat nikiwa na 30 ***qirsh*** (aina ya pesa ya zama hizo yenye thamani haba), nikamwambia rafiki yangu mpenzi Ahmad bin Aliy Makaarim na Ahmad bin Umar Hassaan, tunataka tusimamishe nembo ya elimu mjini kwetu, tusimamishe sura na Mwenyezi Mungu atasimamisha uhakika (***ma'naa***). Ninaazimia kujenga ribaat kwa ajili ya wenye kutafuta elimu, na tutawasimamia kwa nafaka kila atakayekaa ndani yake. Nikaanza kuijenga na khabari zikaenea kwa watu. Wakaona ajabu na hali yangu. Wakasema, 'Ali Habashy hana kitu (hohehahe) na nini uwezo wake wa kujenga ribaat'. Mwenyezi Mungu akanisaidia, mara akatokea mfanyabiashara wa mji akaleta 500 ***qirsh***, na akasema huu ni mchango wangu kwenye kujenga ribaat. Tulipo maliza kujenga ribaat, akaja ndugu yangu Hasan bin Ahmad Al-Aydaroos, akasema: Ewe Aliy! Lau ukiweza kutoa nafaka kwa wanaokaa ribaat miezi miwili tu inatutosha fakhari kwa walio tangulia, nikamwambia inshallah tutasimamia nafaka zao miaka mingi."

Akajenga pia msikiti wake Riyaadh na kujenga makazi yake karibu nao. Mwenyezi Mungu akajaalia kabuli na wakatoka wanavyuoni kutoka kwenye ribaat hiyo na wakaeneza elimu Hadhramout nzima, bali na sehemu zengine, na wakasimamia kufanya kazi ya Da'awa. Jina lake

likatangaa Dunia nzima kwa kazi kubwa aliyoifanya ya Da’awa na kueneza elimu.

Habiib Aliy Habashy alikuwa mkarimu kupita wakarimu wa zama zake na inatosha kuwa alilisha mji wa Seiyun mzima na miji iliyo karibu naye kwa muda wa miezi mitatu wakati ulipokumbwa na njaa. Na walipokuwa wakija kwake watu kutoka vijijini na mashambani hufungua milango ya nyumba yake, akiwalisha usiku na mchana pamoja na kuwafundisha yaliyo muhimu katika dini. Mwenyezi Mungu alimjaalia ukarimu mkubwa, katika wakati mmoja anakuwa na watu zaidi ya 50 nyumbani kwake ukiondoa wageni, walioko Ribaat zaidi ya watu sabini, wanaofanya kazi kwenye mashamba yake zaidi ya watu 60, na wote akiwalisha, wala hakuwahi kuchukua deni kwa mtu yeyote, wala hakukuwa na mtu mwenye kuwa na hisani juu yake (mfadhili), bali yeye ndiye aliyekuwa akiwafanyia hisani. Iliwahi kuhesabiwa katika miezi miwili na nusu vitu alivyotumia katika chakula vikafika gunia 20 za mchele, gunia 20 za ngano, gunia 20 za mahindi, na mapipa makubwa ya samli manne. Ama sukari aliyokuwa akitumia kwenye chai haikuweza kukadiriwa.

Habiib Aliy Habashy pia alianzisha maulidi ya Al-khamisi ya mwisho ya Rabiul-Awwal kila mwaka, ambayo ilipata kabuli kubwa na kuenea umashuhuri wake dunia nzima, hata watawala wakaogopa na kufanya kila njia kuifunga kwa ajili ya wingi wa watu wanaohudhuria na karamu kubwa isiyo na mfano Hadhramout. Na maulidi haya yalikuwa mashuhuri kwa mawaidha yaliyotoka kwake na baadhi ya wanavyuoni wengine maarufu wa Hadhramout kama Habiib Abdallah bin Muhammad Al-Habashy na Habiib Haamid bin Ahmad Al-Mihdhaar, na watu kuwa na unyenyekevu mkubwa, kutokwa na machozi na kutubia kwa ukweli, na ukunjufu wa moyo anaouhisi mwenye kuhudhuria. Na sasa hata baada ya miaka kadhaa tukihudhuria maulidi hayo Seiyun tunashuhudia waliohudhuria wakiwa na utulivu wa hali ya juu, wamenyenyekea, wakiwa wameinamisha vichwa vyao chini wakilia kwa kukumbuka makosa yao.

Al-Habiib Aliy Habashy alipata bahati ya kupendwa na watu sana kutoka kila sehemu, hata akisema, “Hiki ni kitu kutoka kwa Mwenyezi

Mungu Aliyetukuka, Aliyejaalia mahaba ya faqiir (yaani mwenyewe) kwenye mioyo ya watu. Watu wanatamani wapate maqamu kama haya (ya kwangu) na wako tayari kuyanunua kwa mali nyingi, lakini faqiri (yaani mwenyewe) yuko mbali kabisa na hayo, wala sipendi watu wanitukuze, wala waelekee kwangu, lakini hiki ni kitu alichokitaka Mwenyezi Mungu, siwezi kurudisha amri ya Mwenyezi Mungu".

Alifariki adhuhuri ya tarehe 20 Rabiul-Thani 1333H na kuzikwa Seiyun karibu na msikiti wake.

Al-Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas

Jina lake: Al-Habiib Ahmad bin Hasan bin Abdallah bin Aliy bin Abdallah bin Muhammad bin Muhsin bin Husain bin Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas bin Aqiil bin Salim bin Abdallah bin Abdul-Rahman bin Abdallah bin Abdul-Rahman Saggaaf mpaka kwa Mtume-rehema na amani zimshukie.

Alizaliwa Huraydha mwezi wa Ramadhani 1257H, akapoteza macho yake katika umri mdogo. Mwenyezi Mungu Akambarikia macho ya ndani na kupata hifadhi ya ajabu kwa kila alichokisikia katika elimu. Alianza kwa kuhifadhi baadhi ya sura za Qur-ani kwa babu yake Habiib Abdallah bin Aliy. Kisha babu yake akampeleka kwa Sheikh Faraj bin Umar bin Sabaah, ambaye alikuwa ni Haafidh, na mcha Mungu sana, alisuhubiana na Habiib Haadun bin Huud Al-Attaas na alikaa kwake Mash-had karibu miaka 8, ama Huraydha alikaa miaka 56 akifanya kazi ya kufundisha Qur-ani. Mwalimu huyu alikuwa akimpenda mno Habiib Ahmad bin Hasan, na wakiondoka watoto wote humwamrisha akariri darasa mara 40.

Katika masheikh zake wa mwanzo kabisa ni Habiib Saleh bin Abdallah bin Ahmad Al-Attaas bali ndiye mlezi wake katika dini na ndiye aliyemfungua fahamu yake na moyo wake. Anasema alipokuwa na umri wa miaka 5, akicheza na tope siku ya Ijumaa akaja Habiib Saleh na kumwambia, “Nenda kajitayarishe uvae juba lako uje kuswali Ijumaa, na kumsomea aya: **"Na anaye tukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo"**. (Hajj:32). Habiib Ahmad Al-Attaas anasema ndio mara ya kwanza kuisikia Qur-ani na akaihifadhi. Amesoma kwa sheikh wake huyu vitabu vingi vya awali, pamoja na *Ihyaa*, *Iidhaah Asraar Uloomul-Muqarrabiin*, *Risaalatul-Qushairiyya*, *Mukhtasar Al-Adhkaar ya Bahraq*, na *Shifaa* ya Qadhi Iyaadh.

Sheikh wake wa pili alikuwa ni Habiib Abu Bakr bin Abdallah bin Talib Al-Attaas, alisoma kwake baada ya Qur-ani; *Riyaadhatul-Sibyaan* ya Ramliy, *Hadiyyatul-Siddiiq* ya Habiib Abdallah bin Husain bin Tahir, na sehemu ya mwanzo ya *Jamiul-Saghiir*. Na yeye ndiye

aliyemwashiria kusoma kwa Habiib Muhammad bin Aliy bin Saggaaf aliyehamia Huraydha kutoka Seiyun kwa ajili ya kufundisha elimu.

Sheikh wake wa tatu ni Sayyid Ahmad bin Zayniy Dahlan ambaye alikutana naye alipo safiri kwenda Hijja mwaka 1274 ambaye alimhimiza kubaki Makka na kutafuta elimu. Yeye ndiye aliyemsimamia mambo yake alipokuwa Makka, na akimtanguliza juu ya wanafunzi wake wengine. Akasoma Tajwiid kwa Sayyid Aliy bin Ibrahim Al-Samannuudi kwa ishara ya sheikh wake Sayyid Dahlan. Kisha akasoma na kuhifadhi vitabu kuanzia vya mwanzo hadi vikubwa kwenye fani nyingi sana kwa Sayyid Ahmad bin Zayniy Dahlan na akaonyesha uhodari mkubwa, mpaka sheikh wake akamtaka ashike nafasi yake Makka ya kufundisha na utoaji fatwa. Lakini akatoa udhuru na kutaka arudi kwao baada ya kukaa Makka kwa miaka mitano, kwa kuwa watu wake wanamuhitaji. Sayyid Ahmad Dahlaan alikuwa akitoa maelezo marefu na kusherehesha darasa akihudhuria Habiib Ahmad bin Hasan kuliko akiwa hayupo, na akimwashiria Habiib Ahmad bin Hasan kuwa atakuwa kiongozi wa maulamaa wote katika zama zake bali atakuwa marejeo yao wote. Hata Habiib Umar bin Hasan Al-Haddaad amesema, kwamba Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas angekaa Makka angepata umashuhuri kama wa Ibn Hajar Al-Haitamiy, lakini (babu yake) Habiib Umar bin Abdul-Rahman alikuwa hapendi umashuhuri. Sayyid Ahmad Zayniy Dahlaan ni mjukuu wa Sheikh Abdul-Kadir Jelaniy, na baba yake alikuwa ni mtu mwenye kupenda wacha Mungu na mwenye itikadi nao, na alimchukua mtoto wake akiwa mdogo na kumpeleka kwa Habiib Muhammad bin Talib Al-Mihdhaar amwombee. Hata Habiib Abubakr Al-Ataas anasema kwamba Sayyid Ahmad Zayn alipata sana dua za Aali Ba Alawiy. Alikuwa pia akiwapenda Ahlil bayt na khasa Aali Ba Alawiy pamoja, na akiwakumbusha mwenendo wa wazee wao katika tabia njema na kushikamana na elimu na matendo (yanayoeandana na elimu). Hata akisema: “Hawa ni Ahlil-bayt wakipata manufaa watanufaisha na wengine”.

Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas anawahesabu masheikh zake wakubwa kuwa ni wanne, hawa watatu na Habiib Ahmad bin Muhammad Al-Mihdhaar wa Guwayrah. Pia alikuwa na masheikh wengine wengi sana ambao alichukua elimu kwao, miongoni mwao ni

Habiib Muhammad bin Husain Al-Habashy, Habiib Umar bin Abdallah Al-Jufriy wa Madina, Sheikh Muhammad bin Muhammad Al-Azb, Habiib Fadhl bin Alawiy bin Sahl wakati akiwepo Makka (baadaye alihamia Uturuki), Habiib Muhsin bin Alawiy Al-Saggaaf na Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy.

Habiib Ahmad Al-Attaas alifanya kazi kubwa sana ya Da'awa na kueneza elimu kwenye mji wake bali na Hadhramout nzima. Yeye pamoja na ndugu yake Habiib Aliy Habashy walikubaliwa na Hadhramout nzima kwa elimu na kulingania kwa Mwenyezi Mungu. Katika Da'awa yake hasa kwenye mashamba alikuwa akiwafanyia wepesi sana kwenye masuala ya dini. Mwenyezi Mungu alimjaalia elimu yenye ukunjufu sana. Na hiyo ni kutokana na hifdhi yake ya ajabu, kusoma vitabu vingi sana kuliko Sheikh yeyote aliyeko Hadhramout, pamoja na utambuzi na elimu ya zawadi (*ilmu ladunniy*) aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Amesema Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas(ra), "Nilipoingia Hudaydah nilikutana na Qadhi Muhammad Muhsin, kadhi wa mji ule na alikuwa karibu anahifadhi *Tuhfah* kwa moyo. Tukaanza kukumbushana, na ulimi wangu ukafunguka kwa baadhi ya elimu zisizo na mipaka maalum akasema Qadhi, "Subhanallah! Nyie masharifu wa Alawiyiin anakuja kwenu mtu mkubwa na anarejea akiwa mdogo, anakuja kwenu mwanachuoni anarudi mjinga (akiwa ana maana kuwa anajikuta yuko mbele ya mtu ambaye ana elimu kubwa sana kuliko ya kwake hadi yule mtu anajihisi kuwa hajui kitu)". Nikasema, "Yasikughuri uliyoyasikia, na haya hayakutokea ila kwa niya yako njema Mwenyezi Mungu ndio kayatamkisha haya kwa ulimi wangu".

Alikuwa akikusanya vitabu vya kila aina, akisomewa usiku na mchana kwenye maisha yake yote, akiwa nyumbani au safarini, na maktaba yake ilikuwa ndio maktaba kubwa kuliko zote hapo Hadhramout katika wakati (zama) wake.

Habiib Ahmad pia alikuwa ni kiongozi wa kabila lake, bali kiongozi mwenye kukubalika Huraydha na miji iliyo kuwa karibu naye. Alifanya kazi kubwa ya usuluhishi ukitokea ugomvi, na fitina baina ya makabila, hata alikuwa akitoa mali zake kwa ajili ya usuluhishi. Na neno lake

lilikuwa linakubaliwa na wote, hata kwa viongozi wa dola. Cheo hicho hakikumshughulisha. Aliendelea kusomesha na kufanya Da'awa kwa muda wa zaidi ya miaka 50. Hata alikuwa akisema, "Sisi hatuyapendi haya (uongozi wa watu), lakini tunafanya kazi za wazee wetu".

Wanafunzi wake ni wengi mno, kwani kama tulivyosema zaidi ya miaka 50 tangu aliporudi kutoka Haramain alikuwa akifanya kazi ya kusomesha na Da'awa. Baadhi yao ni: Habiib Abdallah bin Alawiy Al-Attaas, Habiib Ahmad bin Abdul-Rahman Saggaaf, Habiib Abdallah bin Tahir Al-Haddaad na ndugu yake Alawiy, Habiib Abdallah Shatiry, Sheikh Muhammad bin Awadh Ba Fadhl, Sheikh Umar bin Abi Bakr Ba Juneid, Habiib Mustafa bin Ahmad Al-Mihdhaar, Habiib Ahmad bin Sumeit na mtoto wake Habiib Umar na wengine wengi. Katika wanafunzi wake wa kuandikiana ni Sheikh Yusuf bin Ismail Al-Nabahaniy.

Habiib Ahmad Al-Attaas alikulia juu ya tabia njema na twaa (utii) ya Mwenyezi Mungu tangu utotoni. Hakuwa mwenye hasira, akiwachukulia kwa upole watu wa mashamba anaokaa nao, ilhali wengi wao wakiwa na tabia nzito ambazo zinahitaji subira kubwa. Hata mara moja alisuluhisha katika kesi moja, wakamsingizia kuwa hakufanya haki, na kumsema kwa maneno ambayo hayalingani na cheo chake. Pamoja na kwamba hafanyi usuluhishi hadi wamemkubali wagomvi wote, na akaitaja ile kadhia mbele yao na wao wakakubali yale aliyoyasema. Juu ya hayo yote akiambiwa kuwa fulani anakutajeni kwa ubaya, akijibu kuwa sisi hatuhisi chochote. Hata akisema kuwa sisi hatumtaki mtu kwa ajili ya haki zetu, na kama tuna haki yoyote huwa tunasamehe. Sisi tunataka wajue tu haki za Mwenyezi Mungu. Hata ilikuwa kawaida yake, akinunua kitu kama shamba, akaja mtu na akadai, anamkinaisha, na huenda akanunua shamba au mitende mara mbili au tatu kwa ajili ya kukata shina la uhasama.

Ama ukarimu, basi nyumba ya Habiib Ahmad Al-Attaas ilikuwa wazi kwa ajili ya wageni na wote wanaopita au kutua Huraydha. Ukarimu wake ulikuwa ni wa hali ya juu, pamoja na kuwa yeye mwenyewe akila chakula kidogo sana. Chakula chake zaidi kilikuwa ni mkate wa hamira na kahawa. Anasema, "Nilimwomba Mwenyezi Mungu ajaalie nyama

kwangu kama kitambaa, na mwanamke kama ukuta, kwa kuwa nilikuwa nina matamanio sana ya vitu hivyo, na Mwenyezi Mungu akanikubalia dua yangu." Hata aliwahi kulaumiwa na baadhi ya jamaa zake kwa kutoa sana pamoja na kwamba yeye si mwenye uwezo mkubwa. Akasema, "Mimi sijali hata kama nikitoa vyote nilivyonavyo katika siku moja." Akijiwa na wageni hujitahidi sana kuwakirimu, pamoja na kuwaangalia vipando vyao, na kuwapa zawadi kubwa kubwa za nguo, na kuwasaidia kwa kiasi anachoweza. Alikuwa akisema, "Sisi hatuoni uzito kwa mgeni hata kama akikaa mwaka, kinachotupa taabu ni kuwa nao muda wote, ama kumlisha na kumkabili kwa wema si gumu hata kidogo." Alikuwa akiletewa zawadi zinazo mkhusu yeye tu, katika nguo za kifakhari. Alikuwa huzivaa kidogo kisha huzitoa kwa wahitaji wala hajali thamani yake. Alikuwa akichukua kibarua humlipa zaidi ya matarajio yake na zaidi ya kazi yake. Sadaka zake nyingi huwa za siri, akiwapa wahitaji wakati wakimsalimia bila ya kujua mtu.

Jitihada zake kwenye ibada zilikuwa adimu sana. Akipunguza kula chakula hadi akija Sheikh wake Habiib Saleh Al-Attaas na kumsimamia hadi ale tende anazo mletea. Akifanya ibada usiku na mchana na nyiradi zake haziwachi pamoja na kushughulika kwake kwenye kufundisha, kutoa waadhi na kusuluhisha baina ya watu. Alikuwa na visimamo viwili usiku, kimoja katikati ya usiku na kingine karibu na alfajiri. Na akifika mji wowote huwa anaenda kuswali kwenye misikiti yote ili apate baraka za waliopata kuswali kabla kwenye misikiti ile. Na kama kuna madrasa huenda kwao, akawapa zawadi watoto na walimu wao, bali ilikuwa kila mwezi au miezi miwili huja nyumbani kwake wanafunzi wa vyuo na walimu wao. Yeye huwakirimu na kuwaamrisha walimu wao wawalakinie Swala watoto na huwahimiza washikamane na elimu na matendo ya kheri.

Alipohiji mara ya pili baada ya kufariki kwa Sayyid Ahmad Dahlan, alipata makaribisho makubwa na kukubaliwa na wanavyuoni wa Haramain na wasiokuwa wakaazi kwa ujuzi na ucha Mungu aliokuwa nao.

Katika maneno yake ya mwisho: "Allah Allah kwenye mgeni (mumfanyie wema), Allah Allah kwenye mgeni (mumfanyie wema),

musifanye ***takliif*** (musijilazimishe mazito) kwa ajili ya mgeni wala musikae nyuma kwake, na hakuna ambacho kitakwenda kinyume kwenu".

Alifariki Huraydha tarehe 6 Rajab 1334, na kuzikwa kwenye Quba la babu yake Habiib Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas.

Al-Habiib Abdallah Shatiry

Jina lake: Al-Habiib Abdallah bin Umar bin Ahmad bin Umar bin Ahmad bin Umar bin Ahmad bin Aliy bin Husain bin Muhammad bin Ahmad bin Umar bin Alawiy Shatiry, bin Aliy bin Ahmad bin Muhammad (Asadullah) bin Hasan (Turaabiy) bin Aliy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam mpaka kwa Mtume(saw).

Alizaliwa Tariim mwezi wa Ramadhan 1290. Alianza kusoma Tariim kwa Sheikh Muhammad bin Sulaiman Ba Hirmiy na mtoto wake Sheikh Abdul-Rahman, kisha akajiunga na madrasa iliyopo kwenye Qubba ya Sheikh Abdallah bin Sheikh Aydaroos, wasimamizi wake wakiwa Habiib Ahmad bin Muhammad Al-Kaaf na Habiib Sheikh bin Aydaroos bin Muhammad Al-Aydaroos. Akasoma kwao vitabu vya mwanzo kwenye fani za Fiq-hi na Tasawwuf na kuhifadhi Qur-ani. Kisha akalazimiana na Habiib Abdul-Rahman bin Muhammad Mash-hoor ambaye ndiye sheikh wake mkubwa. Masheikh zake wengine ni Habiib Alawiy bin Abdul-Rahman Mash-hoor, Habiib Abdallah bin Aydaroos bin Alawiy Al-Aydaroos, Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy na Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas. Alienda kwa Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy akasoma kwake kwenye ribaat yake kama alivyosoma kwa masheikh wengine hapo Seiyun.

Mwaka 1310 alienda Makka kutafuta elimu akasoma kwa wanavyuoni wengi akiwemo Habiib Husain bin Muhammad Al-Habashy, Sheikh Muhammad Said Ba Busail, Sayyid Abu Bakr Shataa, Sheikh Umar bin Abu Bakr Ba Juneid na Sheikh Said Al-Yamaniy. Alifanya jitihada kubwa alipokuwa Makka; halali zaidi ya masaa 2, na usiku na mchana akihudhuria darsa 13 kwenye fani mbali mbali kama Tafsiri, Hadiith, Fiq-hi, Balaagha, Mantiq, na Qira-aat.

Alirudi Tariim mwaka 1314H baada ya kuhimizwa na baba yake, kwani yeye bado alitaka kuendelea kusoma na hakutosheka na alichokipata, lakini akawa hana njia. Hapo Tariim akasimamia Ribaat, akisomesha bila ya kuchoka pamoja na kupangilia masomo na kuisimamia kwa muda wa miaka 50. Hakutoka nje ya Tariim ila kwa ajili ya ziyara za Da'awa nazo zikiwa ndani ya Hadhramout hadi alipofariki. Hakika

watu wa kila aina walipata manufaa kwa kusomesha kwake, na watu walitoka kila pembe ya Dunia kuja kusoma kwake; hivyo alipata wanafunzi wengi sana. Anasema mtoto wake Habiib Muhammad Mahdiy, kuwa walihesabu vijana waliosoma Ribaat tangu kuanzishwa hadi kufariki kwake wakafikia 13,000 na huenda wanafunzi wake wakazidi kuliko hawa. Hata Habiib Mustafa Al-Mihdhaar anasema elimu ya Shatiry imeenea kila sehemu. Habiib Abdallah bin Muhsin Al-Attaas wa Boogoor (Indonesia) anasema, Abdallah bin Umar Shatiry atafufuliwa umma peke yake, yeye na wanafunzi wake. Na maneno haya yanatiliwa nguvu na Hadithi ya Mtume(saw) aliyoyapokea Bayhaqiy na Abu Ya'aliy: **"Je, nisikufahamishe karimu kuliko aliye karimu, Mwenyezi Mungu ndiye karimu kuliko aliye karimu, na mimi ni mkarimu kuliko watoto wa Adam wote, na mkarimu zaidi baada yangu ni mtu aliyefundisha elimu, ikaenea elimu yake, atafufuliwa siku ya Kiyama umma peke yake".**

Baadhi ya darasa zake ni kama ifuatavyo:

- Darasa ya Ribaat baada ya Alfajiri, baada ya Adhuhuri, na baada ya Magharibi, hizi hazikukatika kwenye maisha yake yote ila kwa udhuru wa kisheria.
- Siku ya Jumatano na Jumamosi, darasa za jumla baada ya Ishraaq.
- Darasa ya Fiq-hi kwa watu makhsusi baada ya darasa ya jumla siku ya Jumatano na Jumamosi.
- Darasa ya Bayaan asubuhi siku ya Jumapili na Jumanne.
- Darasa ya Tafsiri msikiti wa Mihdhaar mwezi wa Ramadhan.

Alikuwa akihudhuria darasa na wakati hana hali nzuri ya kiafya, na akisema, "Tunahudhuria na huku tukiumwa na kichwa na maumivu yetu tukitegemea tupate shifaa kwa kusikia elimu." Hapendi wanafunzi wapoteze wakati wao, hata akipata uzito mkubwa akiwaita wanafunzi wake nyumbani. Hata mara moja alisema, "Musifikirie watoto wangu kuwa hatuna watu wanaotutaka tuhudhurie sana majalisi yao ya raha wakiwa na vyombo vya chai. Lakini sisi tunawacha hayo na

tunatanguliza kukutumikieni nyinyi, tukiwa na pupa ya kukunufaisheni na kukupeni faida.”

Alikuwa pia akienda kwenye vyuo vingine vya Tariim, akihudhuria vikao vya kutahini vijana na wakati mwengine akasimamia mwenyewe. Alikuwa hachoki kuwapa nasaha na kuwahimiza kufuata nyayo za watu wema waliotangulia. Wakati mwengine akisafiri na kwenda Inaat na kukaa wiki au wiki mbili akieneza elimu na kuangalia vyuo vinavyoendelea. Alikuwa akiwaambia wanaomsaidia kufundisha, “Mshukuruni Mwenyezi Mungu enyi watoto wangu, Ambaye amekuleteeni wanafunzi hawa kutoka sehemu za mbali, basi wasimamieni na jitoleeni kwa kiasi munacho weza katika kuwafundisha, kwani lau mmoja wenu angeambiwa nenda ewe fulani mji fulani au fulani ukafundishe, ingekuwa taabu kwake.”

Habiib Abdulla Shatiry alikuwa na tabia njema kabisa: mpole, mnyenyekevu na mwenye kuituhumu nafsi yake, wala hamdharau mtu, mkweli kwa wanavyuoni wenzake akiwapa hadhi yao wanayostahiki, hata akihudhuria darasa zao kwa heshima na utulivu. Alikuwa pia ni mwenye kusema ukweli pale inapohitajika, akisikia mtu amefanya kitu ambacho si kizuri, na akawa ni mwenye cheo au mali, basi humwendea nyumbani kwake na humnasihi akiwa naye peke yao.

Na katika tabia zake njema, alikuwa akiwaulizia wanafunzi wake, kuwaangalia na kuwarai kwa hali ya juu kabisa pamoja na kusubiri juu yao. Akiona aliyekosea humwita na kumkosoa kwa faragha, likikaririka lile kosa na akawa hasikii hapo humkanya mbele za wengine. Alikuwa akiwapenda sana wanafunzi, na akija Tariim katika wacha Mungu, humwomba azuru Ribat, huwakusanya wanafunzi wake, ili awatizame na awanasihi kwa yenye kusababisha kufaulu kwao. Alikuwa husema, “Unaonaje kama hawa wote wakawa wanavyuoni wenye kutenda kwa elimu yao, wenye kulingania kwa Mwenyezi Mungu, vipi itakuwa furaha ya Mustafa (Mtume(saw)) kwao? Na vipi watawanufaisha Umma Muhammadiyya?” Alikuwa akifurahi sana kumwona mwanafunzi akijitahidi kwenye utafuta elimu, akizungumza naye kwa mapenzi, akimwuliza maswali na kufanya naye utafiti wa mas-ala, hata akisema wakija wanafunzi wawili, mmoja na zawadi ya riali 1,000

lakini hana raghba na kusoma, na mwengine hakuja na kitu, lakini mwenye raghba kamili ya kusoma kwa jitihada zake zote, angekuwa amefurahi zaidi na huyu mwenye raghba kuliko yule aliye kuja na zawadi. Na akiwa na shughuli yoyote ya harusi au karamu huwaalika wanafunzi wake, na akitaka wawe kwenye chumba chenye masharifu na masheikh. Alikuwa akiwaulizia wale wasiohudhuria darasa, na huenda kwenye vyumba vyao kujua hali zao. Mara nyingi wakimwona anakuja na kuwaamsha wale waliolala kwa ajili ya swala ya Alfajiri. Waliomwona wanasema alikuwa akiwachukulia wanafunzi wake kama watoto wake, bali zaidi ya watoto wake. Akisikiliza mashtaka yao, huyu akitaka kitabu, huyu akimwomba ushauri, hata akichelewa sana kurudi nyumbani kwake kwa sababu ya wanafunzi, akiwa na subira kamili juu yao.

Alikuwa Habiib Abdallah Shatiry akiwakataza wanafunzi wake kwenda kwenye chumba cha mwengine bila ya kutaka faida ya kielimu, na husema, "Hakika nyie ni wenye kuondoka (kurudi nyumbani kwenu mukimaliza masomo), na radi zenu zikiwa juu ya mabega yenu, na familia zenu zinawahitajia, basi inatakiwa muhifadhi nyakati zenu, na kuutumia kwenye (kitu) kitakacho waletea manufaa".

Katika mwisho wa umri wake, alikuwa baada ya swala ya Alfajiri kila siku ila Jumanne, Al-khamisi na Ijumaa, huzungukia daira za darasa, ambazo zilikuwa karibu 9 au 10, na akiuliza walimu kama wamefika. Akiwa hajafika yeyote, hukaa yeye kwenye ile daira na kumtuma mtu kwenda kumwita mwalimu yule. Akishakuja huenda kwenye daira anayoichagua na kuwauliza wanachosoma, na kuuliza maswali kwenye somo lao, na hufanya nao utafiti na uchambuzi wa mas-ala kwenye kitabu wanachokisoma, mpaka anakuwa na uhakika kuwa wameelewa wanachokisoma; kisha huwahimiza na kuwatia mapenzi ya kutamani kusoma na wanafunzi huathirika na maneno yake. Na kila daira hutamani akae kwao Sheikh wao huyu, ili ajue maendeleo yao; na kila mwanafunzi hutaka kuonekana hodari kuliko mwenziwe. Hapo ndipo wanapofanya jitihada kwenye kutalii wakipata ladha ya kusoma na usiku na mchana huifanya moja, na ikawa hakai mtu Ribat miaka 3 tu, ila amehifadhi vitabu vingi kwenye fani tofauti.

Kwa kuwa hamna njia ya kuwataja wanafunzi wake wote, hapa tutataja baadhi ya walio mashuhuri ambao na wao pia wamefanya kazi ya kusomesha:

- Habiib Alawiy bin Abdallah bin Shihaab, ndiye aliyeshika nafasi yake kusomesha Ribaat hadi akafariki.
- Habiib Hasan bin Ismail Al-Haamid, mwasisi wa Ribaat ya Inaat.
- Habiib Abdallah bin Abdul-Rahman Aal Sheikh, mwasisi wa Ribaat ya Shihr.
- Habiib Aliy bin Tahir bin Yahya, mwasisi wa ma'ahadi ya dini Ghayl Ba Waziir.
- Habiib Muhammad bin Abdallah Al-Haddaar mwasisi wa Ribaat ya Baydhaa.
- Sheikh Mahfuudh bin Salim bin Uthman ambaye alilazimiana na Ribaat kwa miaka 60.
- Habiib Ahmad bin Umar Shatiry mwenye *Yaaqut Nafiis* aliye kiandika kwa ishara ya Sheikh wake huyu.
- Habiib Muhammad bin Salim bin Hafiidh, aliye andika vitabu vingi vyenye manufaa na mwenye kushughulika na elimu maisha yake yote.

Ama jitihada zake kwenye ibada, Habiib Abdallah Shatiry alikuwa akitoka katikati ya usiku akitembelea misikiti ya Salaf, akifanya ibada, kisha hurudi nyumbani bila ya kujulikana na mtu. Bali nyakati zake zote, ikiwa si kusomesha au kutoa waadhi, au kusuluhisha watu huwa yumo kwenye ibada. Na jinsi alivyokuwa ameshikamana na ibada aliwahi kusema anatamani mtu ashike sehemu yake amfanyie kazi yake (ya kufundisha na kulingania) na yeye apate faragha ya kufanya ibada tu. Ama mwezi wa Ramadhani humwachia mtu asimamie Ribaat na yeye hudumu juu ya ibada tu.

Habiib Abdallah Shatiry alisifiwa na masheikh zake na marafiki zake waliosoma naye. Imepokewa kuwa alikuwa akitembea Habiib Ahmad

bin Hasan Al-Attaas, akakutana na Habiib Abdallah Shatiry, akauliza nani, akajibu Abdallah Shatiry, akasema Habiib Ahmad bin Hasan, “Makaribisho mema yenye wasaa kwa mwanachuoni wa Tariim na Imaam wa Tariim na Khatibu wa Tariim.” Mwengine ni Habiib Saleh bin Abdallah Al-Haamid wa Nisaab, alisema kwenye barua aliyo mtumia Habiib Abdallah, “Na mumetuomba dua na kukuangalieni, basi wewe ewe mtoto wangu ni wajibu juu yetu kukuombea na kukuangalia kwa kusimama kwenye wadhifa huu, tunategemea kwako utafikia daraja tukufu, na Al-Habiib mkubwa(saw) atafurahi kwa kueneza Da’awa yake, na waja wema waliotangulia wote watafurahi”.

Alifariki tarehe 29 Jamaadal-Uula 1361H, na akazikwa Zanbal kwenye miguu ya mama yake, kama alivyousia.

AALI BA ALAWIY AFRIKA MASHARIKI

- Kuingia Uislamu Afrika Mashariki
- Makabila ya Ba Alawiy yaliyopo Afrika Mashariki
- Al-Habiib Saleh bin Alawiy Jamalillayl
- Al-Habiib Ahmad bin Abu Bakr bin Sumeit
- Al-Habiib Umar bin Ahmad bin Sumeit
- Sanad ya Aali Ba Alawiy

Kuingia Uislamu Afrika Mashariki.

Kwa hakika Uislamu uliingia Afrika Mashariki katika zama za mwanzo kabisa, lakini kutokana na kukosekana marejeo kauli zimegongana. **Riwaya moja** inasema kuwa Uislamu uliingia Afrika Mashariki kabla ya kufika Madina. **Kauli ya pili** inasema Uislamu ulifika Afrika Mashariki wakati wa ukhalifa wa Sayyidna Uthman. **Kauli ya tatu** inasema kuwa Uislamu uliingia Afrika Mashariki kwenye karne ya tatu kwa kupitia watu wa Shirazi. La muhimu ni kuwa Uislamu uliingia Afrika Mashariki kwenye karne za mwanzo, na kabla sana ya kuja dini ya kikristo au dini yoyote ile.

La pili ni kuwa waliohamia Afrika Mashariki walikuwa ni vikundi vitatu: Washirazi, hawa ndio wa mwanzo kabisa na ndio waliotawala Kilwa na sehemu nyingine. Kikundi cha pili kilikuwa ni watu wa Hadhramout. Kikundi cha tatu kilikuwa ni wa-Omani ambao walitawala Zanzibar na sehemu kubwa ya Afrika Mashariki.

Anasema Sayyid AbdulQadir Juneid, kwenye kitabu chake, "*Al-Islaam wal-Yamaniyyunal-Hadhaarim bi Sharq Afriiqiyya*", "Watu hawa wa Hadharimiy (wenyeji wa mji wa Hadharamout-Yemen) hawakuja kwenye miji hii (ya Afrika Mashariki) kwa ajili ya kutafuta ufalme, utawala au uongozi. Katu si hivyo, lakini wao walikuja wakiwa wamechukua bendera ya Uislamu, wakiwalingania watu kwenye Uislamu. Vile vile walikuja kwa ajili ya kufanya biashara halali ambayo itawapatia riziki halali. Hao ndio watu walio-iinua bendera ya Uislamu katika miji hii katika viza vya usiku na siku ngumu kwa misukosuko na shida. Hakika walisafiri safari zenye kuchosha na wakakumbana na magumu yenye kutia machungu kwa silaha ya azma zisizojua kuchoka wala kukimwa bila ya kutupia jicho utupu wa njia (mapori) na umbali wa kutoka eneo moja hadi jingine. Bila ya kuangalia uwepo wa vyombo vya usafiri, kwani hakukuwa na magari wala ndege ambazo wangelizitumia kwa kusafiria, wala hakukuwa na barabara za lami (kama ilivyo leo) kama ambavyo hazikuwepo taa za barabarani. Mtu (katika wao) alitembea kwa miguu umbali wa maili ndefu akivuka tambarare, mashamba na vijiji, akilala chini katika ardhi au katika mkeka/jamvi akilipata, akila anachokipata na kilichowepesika.

Unapoingia usiku, husimama akauhuisha kwa kumuabudu Mola wake Mlezi na kwa kusoma Qur-ani na kuandika (vitabu). Hali ilikuwa hivyo mpaka Uislamu ukakita mizizi katika nchi hizi na Bara lenye kiza likawa limefunikwa na mafundisho ya Uislamu kwa maongozi yake. Na mji wa Zanzibar ukawa ni welekeya wa wanafunzi wageni kutoka nchi mbali mbali za Kiafrika, kuanzia Msumbiji, Zaire na Malawi na ukawa ni chimbuko la mionzi ya nuru, uongofu na elimu iliyo zizagazia nchi za jirani yake.

Na vivyo hivyo ulikuwa mji wa Lamu nchini Kenya ni kimbilio wa watafuta elimu kutoka Somalia, Barawa na Maarika na maeneo ya ukanda huo. Kwa hivyo basi miji miwili hii; Zanzibar na Lamu imepata utukufu katika kueneza ustaarabu wa Kiislamu Afrika Mashariki na pwani zake. Katika uenezaji wa elimu na utapanyi wa mahubiri ya Uislamu, miji ya Zanzibar na Lamu ilishirikiana na Visiwa vya Comoro ambavyo imechimbuka humo nuru ya Uislamu, mafundisho yake, miongozo yake na maelekezo yake. Yote hayo yamepatikana kupitia fadhila za wahubiri hao wa Kihadhaarimi katika Alawiyyina na wasio Alawiyyina. Yalihitimu kupitia mikono yao mamilioni ya wakaazi wa nchi hizi na wakawa ni mifano ya elimu, maarifa na adabu tukufu na tabia njema za kiislamu. Baadhi yao walikuwa na tunzi nyingi katika elimu mbali mbali. Kupitia tunzi zao hizo wakawa na athari kubwa katika ulimwengu wa Kiislamu. Wengi katika Waafrika wakahifadhi kitabu cha Mwenyezi Mungu, Qur-ani Tukufu, kupitia juhudi zao.”

Mwisho wa kunukuu.

Makabila Ya Ba Alawiy yaliyopo Afrika Mashariki.

Aal Sheikh Abi Bakr bin Salim:
Tumeshaona tarjama ya Sheikh Abu Bakr bin Salim, na ikitajwa Aal Sheikh kwenye Ba Alawiy basi makusudio ni yeye.

Watu wa Hadhramout walifika Afrika Mashariki kupitia Somalia na Uhabeshi. Na katika makabila ya mwanzo kufika yalikuwa ni Aal Sheikh na Aal Jamalillayl.

Aal Sheikh Abi Bakr bin Salim walitua kwanza Pate, mji ulio karibu na Lamu. Wa mwanzo kuhama alikuwa Sayyid Ahmad bin Abi Bakr bin Abdallah bin Sheikhaan bin Husein bin Sheikh Abi Bakr. Mwengine katika Aal Sheikh ni Sayyid Saleh bin Muhammad bin Muhammad bin Ahmad bin Husein bin Sheikh Abi Bakr aliyepata kizazi kikubwa kwenye visiwa vya Comoro. Matumbo haya mawili yameenea sehemu mbali mbali za Afrika Mashariki.

Tumbo la tatu ni la Sayyid Aliy bin Sheikh Abi Bakr. Wengi wa hawa wako kwenye visiwa vya Comoro wakiwa wamehamia kutoka Pate. Katika walio mashuhuri kwenye zama zetu kwa elimu, ucha Mungu na kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu ni Sayyid Muhammad Ma'roof bin Sheikh Ahmad bin Abi Bakr bin Ahmad bin Abi Bakr bin Abdallah bin Salim bin Ahmad bin Abdallah bin Aliy bin Sheikh Abi Bakr. Huyu alikuwa mcha mungu mkubwa na aliyefanya kazi kubwa ya Da'awa. Yeye ndiye aliyeeneza tariqa ya Shadhiliyya Afrika Mashariki.

Wengine walio maarufu katika tumbo la Sayyid Aliy bin Sheikh Abu Bakr ni:

- Sayyid Ahmad bin Husain bin Saleh bin Abibakr bin Ahmad bin Abibakr mpaka mwisho wa nasabu. Huyu alikuwa mcha mungu mwenye kudumu juu ya nyiradi nyingi. Yeye ndiye aliyeweka utaratibu wa kuisoma Ratibul Attaas baada ya sala ya alasiri siku ya Alkhamisi hapo Msikiti Jibril, Unguja.
- Sayyid Haamid bin Mansab bin Aliy Aal Sheikh, ambaye alikuwa mwanachuoni mkubwa aliyeendeleza kusomesha fani mbali mbali za elimu za Dini misikitini Unguja na kufanya

Da'wa. Bwana huyu alikuwa pia hodari wa lugha ya Kiingereza na akiifundisha kwenye baadhi ya shule Unguja. Alifariki akiwa anasomesha darasa ya Tafsiri ya Qur'ani, ndani ya Msikiti Gofu, Unguja. Msikiti Gofu ni Msikiti wenye historia kubwa ya elimu za Dini na ucha Mungu katika ardhi ya Zanzibar. Wanavyuoni wengi wakubwa wa Zanzibar wamepitia hapo. Mtoto wake Sayyid Ahmad Haamid Mansab naye pia alikuwa mwanachuoni, aliyesoma Ribat ya Tariim takriban miaka 10, na baada ya kurudi akadumu juu ya kusomesha Dini Unguja hadi kufariki kwake.

- Sayyid Umar bin Abdallah bin Sheikh Ahmad maarufu kama Mwinyi Baraka-mwanachuoni na mlinganiaji mkubwa wa dini. Alikuwa mahiri wa lugha nyingi kama Kiingereza na Kifaransa, na akizitumia kwenye kutoa waadhi ziyada ya Kiarabu, Kiswahili na Kingazija. Aliwahi kuwa mwalimu mkuu wa Muslim Academy Unguja, na alishika nyadhifa mbali mbali za kiserikali Ngazija.

Katika masharifu wa Aal Sheikh ambao pia walifanya kazi kubwa ya kufundisha na Da'awa ni Sayyid Haadiy bin Ahmad bin Abdillah Al-Haddaar Aal Sheikh, aliyekuja kutoka Inaat, akafundisha Mombasa, kisha akawa kadhi Pemba na baadaye akahamia Ngazija (Comoro) wakati wa ukaazi wa Habiib Umar bin Sumeit huko. Aliendelea na kufundisha huko Comoro na baadaye akahamia Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kufariki huko.

Aal Jamalillayl

Asili ya Jamalillayl ni Sheikh Muhammad bin Hasan bin Muhammad Asadullah bin Hasan Turaabiy bin Aliy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam. Na sababu ya kuitwa Jamalillayl ni kuwa alikuwa akihuyisha usiku kwa ibada.

Masharifu wa Jamalillayl walihamia Pate kutoka Shihr kwenye karne ya Kumi Hijriy, na kutoka hapo ndipo wakatangaa Afrika Mashariki. Tumbo lililokuwa mashuhuri ni la Aal Abdul Rahman bin Ahmad bin

Abdallah bin Sheikh Muhammad Jamalillayl, na hawa wako wengi Ngazija na Kenya. Katika wa mwanzo kuhamia Afrika Mashariki ni Sayyid Harun bin Ahmad bin Abdul Rahman (tuliye mtaja hivi punde). Sayyid Abdul Kadir Junied ametaja tumbo la pili ambalo ni la Aal Ahmad bin Abdallah Ba Hassan bin Muhammad bin Salim bin Ahmad bin Abdul Rahman bin Aliy bin Sheikh Muhammad Jamalillayl, lakini amesema kuwa hawajulikani, huenda wakawepo lakini hawajijui kuwa ni masharifu.

Katika waliokuwa mashuhuri ni Sayyid Abul-Hasan (wa kwanza mashuhuri kama Mwinyi Ba Hasan) bin Ahmad bin Abdallah (Lulu) Jamalillayl aliyezikwa Ngazija, na Habiib Saleh bin Alwiy Jamalillayl ambaye alihamia Lamu, Kenya kutoka Ngazija. Na wote wawili wamefanya kazi kubwa ya kueneza elimu na kulingania kwa Mwenyezi Mungu. Wengine ni Sayyid Abul Hassan (wa pili) bin Ahmad Jamalillayl bin Abul Hasan (wa kwanza) mwanafunzi wa Habiib Ahmad bin Sumeit na Sheikh Said bin Dahman ambaye alifanya kazi kubwa ya kueneza elimu Zanzibar. Bwana huyu alikuwa mwanachuoni mkubwa na mwenye elimu ya *Taarikh* (Historia), na katika wanafunzi wake ni Sayyid Umar Abdallah (Mwinyi Baraka).

Wengine katika Jamallilayl ni Sayyid Abdul Fattaah bin Ahmad ndugu wa Abul Hasan, Sayyid Muhammad bin Alawiy bin Ahmad, Sayyid Mustafa bin Ja'afar, Sayyid Hasan bin Muhammad bin Hasan, na Sayyid Alawiy bin Abdul Wahhaab bin Abul Hasan.

Aal Aideed:

Aal Aideed ni wajukuu wa Sheikh Muhammad bin Aliy bin Muhammad bin Abdallah bin Faqiih Ahmad bin Abdul Rahman bin Alawiy Ammil Faqiih, aliye kuwa mashuhuri kama Mawla Aideed kwa sababu ya kufanya makazi yake Aideed na watu wakamfuata na ukaamirishwa kama kitongoji na kizazi chake kikachukua jina hilo.

Sayyid Abdul Kadir Juneid ametaja kuwa wako wengi Ngazija na Kenya ila haijahifadhiwa nasabu yao.

Katika walio mashuhuri ni Sayyid Muhammad bin Adnan bin Hamzah Aideed, aliyehamia Unguja kutoka Ngazija na kusoma kwa Habiib Umar bin Sumeit, Sheikh Sulayman bin Muhammad Al-Alawiy na masheikh wengine Unguja. Maisha yake yote yalikuwa kwenye kusoma na kufundisha tangu alipokuwa Unguja, na baadaye Morogoro na Dar-es-salaam ambapo alifariki tarehe 23 Rabiul Thani 1426.

Aal Ba Faqiih

Aal Ba Faqiih ni tumbo katika matumbo ya Aal Aideed tuliowataja kabla kwa kupitia watoto wake Sayyid Abdallah Al-A'yun Al-Nassaakh na Sayyid Alawiy.

Katika walio mashuhuri ni Sayyid Muhammad bin Alawiy bin Umar bin Ibrahim bin Ahmad Ba Faqiih. Mwengine ni Sayyid Abdillah bin Aliy bin Ahmad bin Ibrahim bin Ahmad bin Alawiy bin Abdul Rahman bin Aliy bin Sulayman bin Ahmad bin Abdallah Al-A'yun Al-Nassaakh bin Muhammad (Mawla Aideed) bin Aliy bin Muhammad bin Abdallah bin Faqiih Ahmad bin Abdul Rahman bin Alawiy Ammil Faqiih aliyekuwa mwenye istiqaama na akitajwa kwa wema na Habiib Umar bin Sumeit.

Aal Ba Faraj

Aal Ba Faraj ni wajukuu wa Sayyid Faraj bin Ahmad Masrafah bin Muhammad bin Abdallah bin Faqiih Ahmad bin Abdul Rahman bin Alawiy Ammil Faqiih.

Ametaja Sayyid AbdulQadir kuwa hakuna anayejulikana kwenye kabila hili.

Aal Saggaaf

Hawa ni wajukuu wa Sheikh Abdul Rahman Saggaaf ambaye tarjama yake imeshatangulia kwenye viongozi wa Ba Alawiy.

Wako matumbo matatu Afrika Mashariki:

- Aal Baytiy, wajukuu wa Sayyid Abu Bakr bin Ibrahim bin Abdul Rahman Saggaaf, katika walio maarufu ni Sayyid Muhsin bin Muhammad bin Alawiy bin Abdallah bin Muhammad bin Abdallah bin Salim Al-Baytiy
- Aal Sheikh bin Ismail bin Ibrahim Saggaaf, hawa hawajulikani kama alivyotaja Sayyid Abdul Kadir Juneid.
- Aal Al-Wahat, nao ni wajukuu wa Sayyid Hasan (Sahibul-Wahat) bin Sheikh Aliy bin Abi Bakr Sakaraan bin Abdul Rahman Saggaaf. Katika wa mwanzo kuja Siyu (Kenya) ni Sayyid Husain bin Muhammad Al-Majdhub bin Umar bin Hasan (Sahibul-Wahat) bin Sheikh Aliy. Katika walio maarufu ni Sayyid Abdul Rahman bin Ahmad bin Muhammad Al-Saggaaf aliyezaliwa Siyu na kutafuta elimu hapo na kuwa mahiri kwenye Fiq-hi, Nahau, Sarufi, Tafsiri na Hadiith. Kisha akahamia Unguja na kusoma kwa wanachuoni hapo. Alipata kuwa kadhi Unguja na Mombasa, pamoja na kueneza elimu kwa kusomesha na kulingania. Mwengine aliye mashuhuri ni Sayyid Ja'afar bin Zayn Al-Wahat Al-Saggaaf aliyezikwa karibu na msikiti wa Ijumaa Malindi, alikuwa ni mcha mungu na mwenye kudumu juu ya ibada. Na katika aliye maarufu kwa kukirimu wageni ni Sayyid Abdallah bin Hashim bin Zayn bin Muhammad bin Ja'afar bin Ahmad bin Muhammad bin Abdallah bin Aliy bin Hasan bin Sheikh Aliy bin Abi Bakr aliyezaliwa Somalia na kufariki Dar-es-salaam.

Aal Nadhiiry

Aal Nadhiiry ni wajukuu wa Sayyid Muhammad Al-Nadhiir bin Abdallah bin Umar (ibn Sanhajiyya, mama yake alikuwa ni wa kabila la Sanhajiya kutoka Himyar na ndio maana jina hili likawa mashuhuri kwake, na pia anajulikana kama *ahmarul-uyuun*) bin Abdul Rahman (mwenye msikiti wa Babutainah) bin Ahmad bin Alawiy bin Faqiih

Ahmad bin Abdul Rahman bin Alawiy Ammil Faqiih. Sababu ya kuitwa Nadhiir ni kwa sababu ya uzuri wake uliopindukia.

Wengi katika masharifu hawa wako Somalia na ametaja Sayyid Abdul Kadir kuwa wako baadhi yao Ngazija lakini hawajulikani.

Ama tumbo lililokuwa Unguja ni Qullateni, na hawa walihama kutoka Barawa (Somalia), babu yao aliitwa Qullateni kwa sababu ya ukarimu wake usio na kifani. Katika walio mashuhuri ni Sayyid Umar bin Muhammad Qullateni bin Mudh-hir bin Abi Bakr bin Aliy bin Abi Bakr bin Muhammad bin Abi Bakr bin Ahmad bin Muhammad Al-Nadhiiry mpaka mwisho wa nasabu. Bwana huyu aliipokea Tariqa ya Qaadiriyya kutoka kwa Sheikh Uweis wa Barawa, Somalia na alifanya kazi kubwa ya kuieneza Afrika Mashariki. Alikuwa mcha mungu na mwenye kudumu juu ya nyiradi. Kila mwaka inafanyika ziyara mfungo saba kwenye kuba lake. Alipata watoto mabwana Muhammad, Ahmad, Abu Bakr Shibly na Aliy.

Aal bin Sumeit

Kabila hili ni wajukuu wa Sayyid Muhammad Sumeit bin Aliy bin Abdul Rahman bin Ahmad bin Alawiy bin Faqiih Ahmad bin Abdul Rahman bin Alawiy Ammil Faqiih kama tunavyotaja kwenye tarjama ya Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit.

Katika walio hamia Unguja ni Habiib Zayn bin Ahmad bin Sumeit aliyezikwa Kiponda Unguja na kaburi lake ni maarufu.

Na katika waliohamia Ngazija ni Habiib Abubakr bin Abdallah bin Abdul Rahman bin Muhammad bin Zayn bin Sumeit aliye-eneza elimu na kufanya kazi kubwa ya Da'awa Afrika Mashariki, yeye na mtoto wake Habiib Ahmad na mjukuu wake Habiib Umar. Mwengine aliye kuja Dar-es-salaam ni Sayyid Muhammad bin Abdallah bin Tahir bin Sumeit aliyekuwa Imamu wa msikiti wa Ijumaa, Kitumbini Dar-es-salaam. Bwana huyu alihama Tanzania baada ya uhuru na kuelekea Kenya.

Aal Masiliy

Hawa ni wajukuu wa Sayyid Abdallah Masily bin Muhammad bin Alawiy Al-Shaybah bin Abdallah bin Aliy bin Sheikh Abdallah Ba Alawiy. Masiiliy ni kila sehemu inayopita mkondo wa maji ya mvua na huenda babu yao aliishi sehemu kama hiyo na likamkaa jina hilo.

Ametaja Habiib Ahmad bin Sumeit kama ilivyonukuliwa na Sayyid Abdul Kadir kuwa ni katika masharifu wa mwanzo kutoka Hadhramout tangu karne ya kumi Hijriy.

Wengi walioko Afrika Mashariki wanapitia kwa Sayyid Aliy bin Ahmad bin Abdallah Al-Masiily, na wako zaidi visiwa vya Comoros khasa Hinzwani, na pia Pemba, Unguja, Dar-es-salaam na Kenya. Katika aliowataja Sayyid Abdul Kadir ni Sayyid Ahmad bin Abdul Rahman bin Aydaroos bin Abdul Rahman bin Aydaroos bin Sultan Alawiy bin Abi Bakr bin Aliy bin Abi Bakr Al-Masiily bin Ahmad bin Sheikh bin Abi Bakr bin Aydaroos bin Aliy bin Ahmad aliyewahi kushika wadhifa wa uwaziri kwenye Serikali ya Unguja.

Aal Shatiriy

Hawa ni wajukuu wa Sayyid Alawiy Al-Shaatiriy bin Aliy bin Qaadhi Ahmad bin Muhammad Asadullah bin Hasan Turaabiy bin Aliy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam. Na sababu ya kuitwa Shaatiriy ni kuwa aligawana mali yake nusu kwa nusu na ndugu yake Sayyid Abu Bakr Al-Habashy.

Hawa waliingia Afrika Mashariki kupitia Uhabeshi na wako Lamu, Mombasa na Unguja. Ametaja Sayyid Saleh bin Muhammad Jamalillayl kwenye kitabu chake cha Riyaadh kuwa katika wanavyuoni wa Lamu ni Sayyid Alawiy bin Abi Bakr bin Abdallah Al-Shatiriy na mtoto wake Sayyid Abu Bakr, na Sayyid Muhammad bin Abi Bakr bin Abdallah Al-Shatiriy. Na katika walio mashuhuri Lamu ni Sayyid Abdallah bin Muhammad bin Sheikhan bin Abdallah bin Sheikhan bin

Umar bin Aydaroos bin Abdallah bin Umar bin Alawiy bin Aydaroos bin Umar bin Muhammad bin Alawiy Shatiriy.

Na ametaja Sayyid AbdulQadir kuwa wako Aal Shatiry Mafia lakini nasabu zao hazijahifadhiwa.

Ama Aal Shatiry waliopo Unguja wametoka Barawa, na katika walio fika Unguja ni Sayyid Muhammad Shatiry pamoja na mtoto wake Sayyid Abdallah, kisha Sayyid Muhammad akapata mtoto mwengine Sayyid Habiib, na wote wawili walisoma Unguja kwa wanavyuoni wa huko na kupata sehemu kubwa ya elimu. Sayyid Habiib alipata umashuhuri kwa elimu ya mirathi na akawa ndio marejeo kwa elimu hiyo Unguja, na wote wawili walipata kizazi kikubwa Unguja, amefariki Sayyid Abdallah mwaka 1379 na Sayyid Habiib 1385H.

Aal Bunumay

Kabila hili ni wajukuu wa Sayyid Abu Numay bin Abdallah bin Sheikh bin Aliy bin Abdallah Watab bin Muhammad Al-Munaffir bin Abdallah bin Muhammad bin Sheikh Abdallah Ba Alawiy. Na wako masharifu wa Kibunumay waliotawala Hijaaz ambao ni kizazi cha Sayyidna Hasan na huenda upande mmoja ukawa umechukua jina la mwenzake kwa kutabaruku.

Masharifu hawa walitua Kenya na Unguja. Katika walio mashuhuri Kenya ni Sayyid Abdallah bin Hamiid bin Mahmud bin Hamiid bin Mahmud bin Ahmad bin Mahmud bin Abdul Rahman bin Mahmud Mawla Tawiila bin Muhammad bin Abu Numay.

Ama Sayyid Ahmad bin Alawiy alitua Lamu, kisha alipopata mtoto Alawiy akahamia Unguja na akaishi muda mrefu na kufariki Unguja mwaka 1374. Sayyid Alawiy bin Ahmad bin Alawiy akapata watoto wengi mkubwa wao akiwa Sayyid Muhammad ambaye ndiye mwenye kushika maqamu ya Habiib Umar bin Sumeit Ngazija. Amemwoa mjukuu wake Habiib Umar, Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu na atunufaishe na yeye.

Katika matumbo ya Bunamay liko tumbo linaitwa Aal Shatiriy na ni wajukuu wa Sayyid Abu Bakr bin Abdul Rahman bin Mahmud bin Muhammad bin Abu Numay, na hawa asili yao ni mji wa Fuwwah karibu na Shihr, na wako wengi Afrika Mashariki.

Aal Attaas

Mtu wa kwanza kuitwa Attaas ni Sayyid Abdul Rahman bin Aqiil bin Salim bin Abdallah bin Abdul Rahman Saggaaf. Baadaye jina la Attaas likawa mashuhuri kwa mtoto wake Habiib Umar tuliye itaja tarjama yake kwenye viongozi wa Ba Alawiy.

Hawa ni katika masharifu waliohamia Afrika Mashariki kutoka Hadhramout, katika walio mashuhuri Kenya ni Sayyid Umar bin Ahmad bin Saleh bin Muhammad bin Aliy bin Muhsin bin Husain bin Umar bin Abdul Rahman Al-Attaas.

Katika walio mashuhuri Tanzania ni Sayyid Umar bin Salim bin Umar bin Salim Al-Attaas, naye ni mjukuu wa Sayyid Umar bin Salim Al-Attaas mwenye ziyara Shihr, naye ndiye mwasisi wa msikiti wa Ijumaa Dar-es-salaam na amezikwa karibu na msikiti huo. Yeye alikuwa ni mwenye kuheshimiwa na serikali ya Ujerumani wakati wa utawala wao. Ama mtoto wake Sayyid Salim alikuwa ndiye msuluhishi wa kesi za Waislamu, lakini huyu hakuishi sana ila alihamia Kenya.

Aal Aydaroos

Wa mwanzo kuitwa Aydaroos kama tulivyoona ni Sheikh Abdallah Al-Aydaroos bin Abi Bakr Sakaraan bin Abdul Rahman Saggaaf, na kizazi chake kikarithi jina hilo.

Katika waliohamia Afrika Mashariki kutoka Hadhramout ni Sayyid Muhsin bin Alawiy bin Husain bin Ahmad bin Umar bin Ahmad bin Abdul Rahman bin Muhammad bin Abdul Rahman bin Ahmad bin Husain bin Abdallah Al-Aydaroos. Huyu alifanya makazi yake Kilimanjaro na Moshi, akawa amesimama kulingania Dini na kuongoza

watu katika mwenendo na tabia nzuri za kiislamu. Walisilimu watu wengi sana katika mikono yake. Alijenga misikiti mitatu kwa ajili ya wakaazi wa miji hiyo katika mwaka 1913 (Miiladiya). Serikali ya Kijerumani iliyokuwa ikitawala Tanganyika wakati huo ilipanga njama ya kumwua, akakimbia na kuondoka.

Aal Basukutah

Aal Basukutah ni wajukuu wa Sayyid Hasan bin Ahmad Masrafah bin Muhammad bin Abdallah bin Faqiih Ahmad bin Abdul Rahman bin Alawiy Ammil Faqiih. Na lakabu ya Ba Sukutah huenda aliipata kwa kupenda kukaa kimya na kuwa mchache wa kuzungumza.

Ametaja Sayyid AbdulQadir Juneid kuwa wako idadi kubwa Kenya wanaonasibika na Sayyid Ibrahim bin Muhammad Hamduun bin Hasan Ba Sukutah.

Aal Habashy

Aal Al-Habashy ni wajukuu wa Sayyid Abu Bakr Al-Habashy bin Aliy bin Qaadhi Ahmad bin Muhammad Asadullah bin Hasan Turaabiy bin Aliy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam. Tumetaja tarjama ya baadhi yao hapa juu kwenye sehemu ya viongozi.

Katika walio mashuhuri Lamu ni Sayyid Salim bin Husain bin Alawiy bin Salim bin Talib bin Abdallah bin Muhammad bin Isa bin Muhammad bin Ahmad Sahibul-Shiib. Na huyu Habiib Isa bin Muhammad ni katika wanafunzi wa Habiib Umar bin Abdul Rahman Al-Attaas. Bwana huyu Sayyid Salim alikuwa ni katika wanachuoni mashuhuri huko Lamu. Amesoma pamoja na Sayyid Ahmad Badawiy bin Saleh Jamalillayl, na walikuwa na udugu wa kidini baina yao. Amefariki Sayyid Salim huko huko Lamu.

Aal Haddaad

Aal Haddaad ni katika kizazi cha Sayyid Ahmad bin Abu Bakr bin Ahmad Masrafah bin Muhammad bin Abdallah bin Faqiih Ahmad bin Abdul Rahman bin Alawiy Ammil Faqiih.

Katika waliozuru Unguja wakati wa Habiib Ahmad bin Sumeit ni Habiib Alawiy bin Tahir Al-Haddaad (katika wanafunzi wa Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas.)

Ama aliyefanya kazi kubwa ya Da'awa katika Aal Al-Haddaad ni Habiib Ahmad Mash-hoor bin Taha bin Aliy bin Abdallah bin Taha bin Abdallah bin Taha bin Umar (nduguye Habiib Abdillah Haddaad) bin Alawiy bin Muhammad bin Abdallah bin Muhammad bin Alawiy bin Ahmad Al-Haddaad. Alihamia Kenya kwenye ujana wake akamdiriki Habiib Saleh bin Alawiy Jamalillayl. Habiib Ahmad Mash-hoor alishikamana sana na Habiib Umar bin Sumeit. Alifanya kazi kubwa ya kusomesha na kulingania Dini (kufanya Da'wa). Ameacha athari kubwa Afrika Mashariki. Pamoja na kujishughulisha na biashara kwa ajili ya kutafuta riziki ya halali, Habiib Ahmad Mash-hoor alitembelea miji mingi ya Kenya kwa ajili ya Da'awa. Alifika hadi Uganda na Zaire na walisilimu mkononi mwake maelfu ya wakristo na wasio na dini. Habiib Ahmad Mash-hoor alifariki Jeddah mwaka 1416H na kuzikwa Makka.

Aal Al-Baar

Aal Al-Baar ni wajukuu wa Sayyid Aliy bin Aliy bin Alawiy bin Ahmad bin Al-Faqiih Al-Muqaddam, na ameitwa hivyo kwa sababu ya kumtii sana baba yake.

Sayyid Abdul Qadir ametaja kuwa wako idadi kubwa Kenya. Walihamia Kenya kutoka Uhabeshi, ila nasabu yao haijahifadhiwa.

Aal Al-Biidh

Aal Al-Biidh ni wajukuu wa Sayyid Ahmad bin Abdul Rahman bin Husain bin Aliy bin Muhammad bin Ahmad bin Al-Faqiih Al-Muqaddam, na huenda akawa amepata jina hilo kwa ajili ya kufunga siku nyeupe (13,14 na 15) ambazo ni Sunna kuzifunga kila mwezi.

Kabila hili lilihamia Kenya kutoka Shihr, na katika walio mashuhuri ni Sayyid Abdallah bin Said bin Salim Al-Biidh na mtoto wake Sayyid Said aliyeanzisha chuo cha Ghannaa Mambrui kilichotoa idadi kubwa ya wanafunzi. Baada ya kufariki kwake, chuo hiki kimeendelezwa na mtoto wake Sayyid Muhammad bin Said bin Abdallah Al-Biidh aliyeshika maqamu yake. Pamoja na kusomesha hapo chuoni, Sayyid Muhammad Al-Biidh amekuwa akifanya kazi kubwa ya Da'awa katika nchi zote za Afrika Mashariki. Sayyid Muhammad Al-Biidh amefariki 23 Safar 1434H.

Aal Musawa

Aal Al-Musawa ni wajukuu wa Sayyid Ahmad Al-Musaawa bin Muhammad Muqlaf bin Ahmad bin Abu Bakr Sakaraan bin Abdul Rahman Saggaaf.

Waliohamia Afrika Mashariki ni katika tumbo la Sayyid Ahmad bin Abibakr Sakaraan, kwani liko kabila jingine linaitwa Al-Musawa wanaonasibika na Sayyid Husain bin Abdul Rahman Saggaaf. Katika walio mashuhuri Tanga, Tanzania ni Sayyid Hashim bin AbdulQadir bin Husain bin Ahmad Al-Musawa bin Muhammad bin Abdul Rahman bin Muhammad bin Husain bin AbdulQadir bin Husain bin Ibrahim bin Ahmad bin Muhammad bin Ahmad bin Abibakr Sakaraan. Aliyehama kuja Afrika Mashariki ni baba yake Sayyid AbdulQadir bin Husain. Sayyid Hashim alipata watoto Husain, Ahmad, Muhammad na AbdulQadir na wote wamesoma elimu ya dini na nasabu yao imehifadhiwa.

Aal Al-Juneid

Aal Juneid ni wajukuu wa Sayyid Abu Bakr Al-Juneid bin Umar bin Abdallah bin Harun bin Hasan bin Aliy bin Muhammad Jamalillayl. Hawa wanatoka katika tumbo la Jamalillayl. Pia wanaitwa Ba Harun kwa kuwatofautisha na Al-Juneid Al-Akhdhar. Al-Juneid walipewa jina hili kwa ajili ya kutabaruku na Imaam Juneid bin Muhammad kiongozi wa Masufi, kama ambavyo ndugu yake Aliy alipewa jina la Al-Sariy kwa kutabaruku na Imaam Al-Sariy Al-Saqatiy. Kwenye Ba Alawiy pia kuna kabila la bin Sahl na babu yao alipewa jina hilo kwa kutabaruku na Imaam Sahl Al-Tustariy. Hii inaonyesha jinsi Ba Alawiy walivyowapenda na kushikamana na watu wa Tasawwuf.

Katika waliofika Tanzania ni Sayyid AbdulQadir bin AbdulRahman bin Umar bin AbdulRahman (Al-Saggaaf) bin Ahmad bin Aliy bin Harun bin Aliy bin Juneid bin Aliy bin Abibakr Al-Juneid. Bwana huyu alizaliwa na kusoma Tariim kwenye Ribaat kisha akahamia Uganda kwa ajili ya kufundisha na kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu. Lakini hakupata utulivu wa ukaazi Uganda. Alipokuwa anarudi Hadhramout alipitia Dar-es-salaam, Tanzania ili apate kumzuru ndugu yake Sayyid Saleh aliyekuwa mkaazi wa hapo. Mwenyezi Mungu akajaalia aendelee kukaa Dar-es-salaam mpaka mwisho wa umri wake kwa ajili ya kusomesha na kulingania Dini. Hapa Daressalaam, Sayyid AbdulQadir alifungua madrasa, akawa imamu wa msikiti wa Ijumaa Kitumbini na kuweka darasa msikitini hapo na nyumbani kwake kwa muda wa zaidi ya miaka 40 hadi alipofariki dunia katika mwezi wa Rabiul Thani 1427H. Pamoja na kufundisha Sayyid AbdulQKadir alihuyisha Tariqa ya Ba Alawiy na kuwa kiongozi bora kwa kuwahimiza watu kuifuata na kuonyesha mfano mzuri wa tabia njema. Aliwahimiza masharifu kuhifadhi nasabu yao tukufu na alisimamia kuithibitisha na kuwapatia baadhi yao vitambulisho vya uthibitisho. Pia aliweka darasa ya kusoma vitabu vya Ba Alawiy kwenye msikiti wa Rawdha kuwakumbusha mwenendo wa wazee wao, na hakuchoka kuwakumbusha wanaojinasibisha na Alawiyyiin tabia zao na mwenendo wao mtukufu.

Aal Al-Ahdal

Katika masharifu walio mashuhuri ambao si katika Ba Alawiy ni masharifu wa Al-Ahdal. Mabwana hawa asili yao ni mji wa Zabiid na Maraawia na kama tulivyoona kuwa Imamu Ahmad bin Isa alisafiri na babu wa Ahdal ambaye alitua Waadiy Sihaam.

Katika wa mwanzo kuhamia Mogadishu kutoka Marakah ni Sayyid Hasan bin Husain na wa mwanzo kuhamia Lamu kutoka Marakah ni Sayyid Aliy bin Abibakr bin Muhammad bin Hasan bin Husain bin Muhammad bin Aliy bin Ja'afar bin Abibakr bin Aliy bin Abibakr bin Abil Qasim bin Muhammad Al-Rumhiy. Wako idadi kubwa katika mji wa Lamu. Kuna matumbo kama saba, mashuhuri kati yao ni walii mkubwa Sayyid Muhammad bin Adnan bin Abibakr bin Ahmad bin Abibakr bin Hasan bin Aliy Al-Waliy Al-Zaahid. Bwana huyu amefariki na kuzikwa Lamu mwaka 1382H.

Makabila mengine aliyotaja Sayyid AbdulQadir Juneid ni Aal Ridaai', Aal Radiiniy, na Aal Rifaai'.

Na huenda yakawepo makabila mengine ambayo hatujayataja. Makusudio ni kukumbushana kuwa waliohamia Afrika Mashariki ni wengi katika Aal Ba Alawiy, na walifanya kazi kubwa ya kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu na kueneza elimu kwa wakaazi wake.

Al-Habiib Saleh bin Alawiy Jamalillayl

Jina lake kamili: Al-Habiib Saleh bin Alawiy bin Abdallah bin Hasan bin Ahmad bin Abdallah Tuyuur bin Ahmad bin Harun bin Ahmad bin Abdul Rahman bin Ahmad bin Abdallah bin Sheikh Muhammad (Jamalillayl) bin Hasan (Al-Muallim) bin Muhammad (Asadullah) bin Hasan (Turabi) bin Aliy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam mpaka kwa Mtume(saw).

Alizaliwa Ngazija mwaka 1269H, na akaanza kutafuta elimu kwa baba yake na wengine. Katika mwaka 1287H, alipokuwa na umri wa miaka 18, alisafiri kwenda Lamu kwa ajili ya matibabu. Huko Lamu alitanguliwa na ammi yake Al-Habiib Aliy bin Abdallah. Hapo alimuomba ruhusa baba yake aendelee kuishi Lamu. Akasoma kwa wanavyuoni waliokuweko hapo, wakiwemo Ammi yake Habiib Aliy bin Abdallah, Habiib Abu Bakr bin Abdul Rahman Aal Sheikh (maarufu kama Mwinyi Mansabu), Sheikh Aliy bin Muhammad Al-Muawiy, Habiib Alawiy bin Abu Bakr Shatiry, Sheikh Abu Bakr Al-Muawiy, na Sayyid Ahdal bin Abu Bakr Al-Ahdal.

Baada ya kufuzu kwenye masomo yake, Habiib Saleh alifanya kazi ya kufundisha na kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu na kusomesha darasa usiku na mchana bila ya kuchoka. Akapewa ardhi na sheikh wake Mwinyi Mansabu, akajenga msikiti na akauita Riyaadh. Hili ni jina la mwalimu wake wa kuandikiana Habiib Aliy Habashy. Hapo Riyaadh, Habib Saleh alianzisha Maulidi ya kila mwaka katika usiku wa kuamkia Ijumaa ya mwisho ya Rabiul-Awwal ikiwafikiana na siku anayofanya Habiib Aliy Habashy.

Bila shaka Habiib Saleh aliijenga Riyaadh kwa ucha Mungu kwani Mwenyezi Mungu alimtilia baraka wakatoka humo wanavyuoni wengi walioeneza elimu Afrika Mashariki, na waliofanya kazi kubwa ya ulinganiaji Dini ya Mwenyezi Mungu.

Habiib Saleh alipata watoto zaidi ya kumi. Aliyeendeleza kizazi chake ni Habiib Ahmad Badawiy. Ama Habiib Aidaroos (maarufu kama Mwinyi Aidaroos) alipata watoto wa kike tu. Habiib Ahmad Badawiy akapata watoto na wajukuu, wengi wao wakiwa wacha Mungu na

wenye kusimamia kazi za wazee wao za kufundisha na kueneza mlingano wa Mwenyezi Mungu.

Wanafunzi wa Habiib Saleh ni wengi sana, kwani alifanya kazi ya kufundisha umri wake wote. Wachache kati ya hao ni watoto wake Habiib Ahmad Badawiy na Habiib Aydaroos, Sheikh Abdallah Ba Kathiir, Sheikh Muhammad bin Aliy Mua'wiy, Sheikh Salim Juma'an, Sheikh Ali bin Hasan, na Sheikh Abdullatiif bin Uthman. Hawa wawili wa mwisho ni wakaazi wa Ngazija (Comoro).

Habiib Saleh alikuwa ni mtu mwenye unyenyekevu sana, akivaa nguo duni na akifagia msikiti, hata ambaye hamjui hawezi kumtambua ila akiambiwa.

Amefariki Habiib Saleh Lamu tarehe 2 Muharram 1354H akiwa na umri wa miaka 85, akazikwa jirani na Ammi yake Habiib Aliy bin Abdallah Jamalillayl.

Al-Habiib Ahmad bin Sumeit

Jina lake kamili: Al-Habiib Ahmad bin Abu Bakr bin Abdallah bin AbdulRahman bin Muhammad bin Zayn bin Alawiy bin AbdulRahman bin Abdallah bin Muhammad Sumeit bin Aliy bin AbdulRahman bin Ahmad bin Alawiy bin Faqiih Ahmad bin AbdulRahman bin Alawiy (Ammil Faqiih) bin Muhammad Sahib Mirbaat mpaka kwa Mtume(saw).

Wa kwanza kuhamia Afrika Mashariki ni baba yake Habiib Abu Bakr bin Abdallah, aliyehamia Unguja na kukaa muda mkubwa. Alikuwa analazimiana na msikiti wa Mzaham na kushika ukadhi Unguja. Baadaye alihamia Ngazija na kufariki huko. Katika jumla ya vitabu alivyo andika ni *Tiryaaqul-Naafi minal-amaa* sherehe ya kitabu cha *Babu Maa jaa'*.

Alizaliwa Habiib Ahmad bin Sumeit Ngazija siku ya Al-khamisi, mwezi 5 Rajab 1277H. Kwa hakika alibashiriwa baba yake na Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit kuwa atapata mtoto mwenye baka jeusi kwenye shavu lake, akawa baba yake kila akizaliwa mtoto anaangalia alama hiyo, hadi akaikuta kwa Habiib Ahmad, akampa jina la Ahmad kwa kutabaruku na aliyempa bishara Habiib Ahmad bin Umar. Habiib Ahmad bin Sumeit alianza kusoma Ngazija kwa Habiib Abul-Hasan (wa kwanza), na masheikh wengine. Kisha alisafiri kwenda Hadhramout akiwa na umri wa miaka 17 kwa ishara ya baba yake kabla ya kufariki. Akatafuta elimu akiwa ameshukia kwa Ammi zake Shibam. Kisha akisafiri kwenda sehemu nyengine za Hadhramout kama Tariim, Seiyun, Hawta, na Ghurfa. Katika masheikh zake ni Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy, Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy, Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas, Habiib Ubeydillah bin Muhsin Al-Saggaaf, Habiib AbdulRahman Mash-hoor, Habiib Abdallah bin Muhammad Al-Habashy wa Hawta, Habiib Sheikhan bin Muhammad Al-Habashy wa Ghurfa na Habiib Ahmad bin Muhammad Al-Mihdhaar wa Doan. Katika masheikh zake wa Misri ni Sayyid Muhammad Al-Kayaaliy Al-Halaby na Sheikh Muhammad Al-Anbaabiy, na Unguja alisoma Mantiq kwa Sayyid Abdul Husain Al-Mar'ashy Al-Tustariy.

Baada ya kuenda mji mmoja hadi mwengine akitafuta elimu, Habiib Ahmad bin Sumeit alirudi Ngazija (Comoro), akaoa na kuanza kazi ya kusomesha na kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu. Mfalme Barghash wa Zanzibar alipopata habari zake akamtaka aende Zanzibar na kuchukua uongozi wa Dini kama Kadhi Mkuu wa Zanzibar. Hivyo akaenda huko na akadumu kwenye ukadhi kwa miaka 3.

Mwaka 1303H alisafiri na kwenda Uturuki na kukaa huko karibu miezi sita, na alikutana na Habiib Fadhl bin Alawiy bin Sahl na kuchukuwa kwake elimu. Katika muda huo alitunukiwa nishani na Mfalme Abdul Majid wa Uturuki. Alizuru pia Misri na Haramain na kukutana na wanavyuoni na wacha Mungu wengi. Kisha akarudi Unguja na kupewa Ukadhi Mkuu kwa mara ya pili.

Pamoja na ukadhi alifanya kazi ya Da'awa na kuandika vitabu. Elimu yake na ulinganiaji dini wake ulienea Afrika Mashariki. Sayyid AbdulQadir Juneid amesema kuwa hakuna mwenye kushika kalamu au wino katika Afrika Mashariki ila amenasibika kwake moja kwa moja au kupitia ***wasita*** (watu walio kati).

Na Habiib Ahmad bin Sumeit, pamoja na kufanya kazi ya ukadhi na kushughulika na uandishi, hayo hayakumzuia kufanya Da'awa. Akahuyisha tariqa ya Ba Alawiy kwa upole na njia iliyo bora hadi mlingano wake ukaenea kwa wakaazi wa Afrika Mashariki. Alikuwa Habiib Ahmad bin Sumeit mwenye huruma kwa watu, akibeba maudhi yao kwa subira kubwa na hakabiliani nao ila kwa hekima na busara kubwa, akifuata nyendo za Mtume(saw). Hata mara moja mtoto wake alighadhibika kwa maudhi anayoyapata kwa watu, akamwambia, "ewe mtoto wangu hakika tariqa yetu ni subira na kuhimili, na baki ya umri wetu ni mtukufu mno kwa kuutumia katika kumjibu huyu na huyu". Hata mara moja mwanafunzi wake alijibizana na mtu kwa sababu ya kumsema vibaya sheikh wake, akamwita Habiib Ahmad mwanafunzi wake na kumwambia, "ukimsikia ananisema kwa chochote usimjibu, umwachilie mbali kwani hii ndio hali yake kwa miaka 25 na sijawahi kumjibu". Na pamoja na yote hayo akikutana naye hukabiliana naye kwa bashasha. Hata mara moja shekhe huyu alipata deni kubwa akawa hana uwezo wa kulipa, Habiib Ahmad akamtumia mtu anunue vitabu

vyake ili ampatie pesa za kulipa madeni yake, na baada ya muda akamrudishia vitabu vyake, na hayo yote aliyafanya bila ya kumjulisha kuwa ni yeye ndiye aliyemsaidia, na haya aliyafanya pamoja na kwamba shekhe huyu alikuwa akimtaja Habiib Ahmad kwa ubaya.

Mara moja alikutana na sheikh mmoja akamsema kwa maneno mabaya hata mwanafunzi aliyekuwa naye akawa anahisi anachomwa na mkuki tumboni mwake, lakini Habiib Ahmad hakumjibu kwa lolote ila kwa kusema, ahsante sheikh fulani. Kisha baada ya muda Habiib Ahmad akamwita yule mwanafunzi wake, na kumwambia twende tukamwombe msamaha sheikh fulani, alipofika kwake, yule sheikh akamwangukia miguuni na kumwomba msamaha huku akilia. Alipo haditihiwa kisa hiki mtoto wake Habiib Umar akasoma ubeti ulio na maana ifuatayo:

Tukiwa wagonjwa tunakujieni kukuzuruni,

Na mukikosea tunakuja kwenu tukitoa udhuru.

Katika wakati wa uongozi wake Habbib Ahmad kama Kadhi Mkuu wa Zanzibar palitokea maradhi ya ndui (Small Pox) na ikawa watu wengi wanakufa. Madaktari walitangaza dharura ya kuchanja kwa wakaazi wote wa Zanzibar. Watu wakakataa kuchanja kabisa. Serikali ikajaribu kila hila isiweze kuwalazimisha. Serikali ya kikoloni ya Uingereza ikachukua hatua mbili muhimu. Kwanza ilitoa amri ya kuzuia mikusanyiko yote ya watu. Ilipoona watu bado wanaendelea kufa kwa wingi ikapitisha sheria (decree) ya muda yakuzuia mikusanyiko katika Sala za Ijumaa na Jamaa. Ilipotolewa amri hiyo Habiib Ahmad bin Sumeit, akiwa kama Kadhi Mkuu wa Zanzibar na kiongozi wa waislamu Zanzibar na Afrika ya Mashariki, akaenda kwa Mtawala wa Kiingereza (British Resident) na kumtaka Serikali yake ifute amri ile ya watu kutohudhuria Sala za Jamaa na Ijumaa kwani ni amri ambayo waislamu watalazimika kuiasi. Amri ile ikafutwa, lakini Serikali ikamtaka msaada yeye Habiib Ahmad katika kumaliza tatizo liliopo la maradhi yanayosababisha maafa makubwa nchini. Viongozi wakamtaka Habiib Ahmad achanje mbele za watu kwa kujua kuwa watu watamfuata, naye akakubali kwa ajili ya maslahi ya watu. Viongozi wa Serikali wakamleta na gari akachanjwa mbele za halaiki ya watu wengi. Watu walipomwona tu kuwa amechanja, na wao wakajitokeza kuchanja

na kusema, kama ameridhia Habiib Ahmad bin Abubakr, basi na sisi kama yeye (tumeridhia). Watu wakachanjwa na, kwa namna hiyo, Serikali ikaweza kuyadhibiti maradhi ya Small Pox na kuyashinda.

Hekaya hii inaonyesha mambo matatu; la kwanza ni kuwa Habiib Ahmad bin Sumeit alikuwa ni mtu aliyekubaliwa na kupendwa sana na watu wa Zanzibar alikokuweko (na katika nchi jirani za Afrika ya Mashariki) kama kiongozi wao, na alikuwa akisikilizwa na watu wote na kutiiwa amri zake. Hii ni kwa sababu watu wametosheka juu ya elimu yake, ucha Mungu wake, na mapenzi na mustakbali mzuri alionao kwa watu wake. Hivyo watu walikuwa wanamsikiliza na kumtii bila maswali yoyote.

La pili ni kuwa Habiib Ahmad bin Sumeit alikuwa akiongoza watu kwa kutumia hekima za Qur'ani na Sunna. Alichofanya ili kuwafanya watu wachanje ni kufuata hekima ya Mtume(saw) pale alipozuiliwa kuingia Makka yeye na Masahaba wake na ikabidi wanyama wao waliowachukuwa kuwachinja katika Hijja, wawachinje hapo hapo Hudaybiyya. Masahaba walishagoma kuchinja pale wakitaka kupambana na Makureshi wa Makka na kuingia Makka kwenda kuhiji kama wanavyofanya Waarabu wengine. Waliamini kuwa hiyo ni haki yao na hawakuwa tayari kuikosa warudi Madina baada ya safari ndefu kutoka Madina hadi pale nje kidogo ya Makka. Lakini walipomuona Mtume(saw) mwenyewe amechinja, hawakuwa na jinsi. Hekima hiyo iliwafanya watekeleze amri waliotakiwa, na warudi Madina, bila ya kuingia Makka. Hivyo Habiib Ahmad bin Sumeit alikopia hekima hiyo ya Mtume(saw) akachanja yeye, na ndipo na watu wa Zanzibar wakakubali kuchanjwa.

La tatu ni kuwa Habiib Ahmad bin Sumeit alikuwa anakubaliwa na kuheshimiwa siyo tu na watu wa kawaida bali hata na Masheikh wengine wote nchini na, kwa sababu hiyo, akiheshimiwa na Viongozi wa Serikali. Hii ndio sababu waliona hakuna njia ya kupitisha hukumu yao baada ya kukataliwa na watu ila kwa kumtumia Habiib Ahmad bin Sumeit, pamoja na kwamba ni suala lenye manufaa kwa wakaazi wake. Hivyo, elimu ya kiwango cha juu kabisa, hekima kubwa, ucha Mungu, na tabia njema na mustakbali mzuri kwa watu vilimwezesha Habiib

Ahmad bin Sumeit kuwakusanya waislamu wote Afrika Mashariki kuwa na umoja ule hasa unaotakiwa katika Qur'ani chini ya kiongozi mmoja, yeye.

Habiib Ahmad bin Sumeit alikuwa ana uhusiano mzuri na watawala. Makusudio yake hayakuwa kwa ajili ya manufaa ya nafsi yake bali kwa ajili ya raia. Akawa anawaalika kwenye shamba lake na akiwapa chakula na vinywaji vizuri, na akisema kuwa hafanyi kwa ajili ya nafsi yake, bali wakubali maombezi (shafaa) yake kwa ajili ya watu, kwani wao wametawala miji hii. Hakupambana nao kwa silaha, bali aliwazidi kwa hekima, na wakawa wanafuata mashauri yake.

Habiib Ahmad bin Sumeit alipendwa na masheikh zake, wanafunzi wenzake, na watu wa zama zake khasa wakaazi wa Hadhramout. Walimtaka sana abaki Shibaam afanye kazi ya kufundisha na Da'awa kwa kufahamu uwezo wake na nia yake bora kwenye kazi yake. Hata Habiib Sheikh bin Muhammad Al-Habashy alimwambia Habiib Umar, "ni kidogo sana mfano wa baba yako, na Hadhramout inamhitajia sana". Habiib Aliy Habashy amesema: "Mwenyezi Mungu akiitakia Shibam uhai atamleta humo Ahmad bin Abi Bakr". Vile vile Habiib Abdallah bin Aydaroos Al-Ayadaroos amesema kumwambia Habiib Umar, "na baba yako tunajifakharisha naye na Hadhramout inamhitajia. Muradi wetu ni kuwa aje achimbe chemchem ndani yake". Na alipotajwa Habiib Ahmad bin Sumeit mbele ya Habiib Umar bin Abdallah Al-Habashy, akasema: "Je, hakuna hila yoyote ya kuamsha azma yake ya kutoka (Afrika na kuja Hadhramout)? Kwani Hadhramout inamhitajia sana, na pwani (ya Afrika Mashariki) haimstahiki kumpata Habiib huyu, hata kama anapata daraja kubwa kwa kusubiri juu ya watu wake".

Habiib Umar alipokutana na Habiib Umar bin Hamid Saggaaf, alimwambia, "Baba yako si mwenye kutafuta sana (elimu), lakini elimu zake nyingi ni kwa njia ya kufunguliwa (na Mwenyezi Mungu), na Habiib Aliy bin Muhammad (Al-Habashy) anamtaja na kumsifia sana." Na alipotajwa kwa ammi yake Habiib Taahir bin Abdallah bin Sumeit, akasema, "Hakuzaliwa kwenye Aali Muhammad bin Zayn (bin Sumeit) mfano wake, na ana elimu (za ziada) ambazo hazipo kwa wazee wake."

Habiib Ahmad bin Sumeit alipata wanafunzi wengi sana, miongoni mwao ni mtoto wake Habiib Umar, Sheikh Said bin Dahman, Sheikh Muhsin bin Aliy Barwaniy na wengine. Mwanafunzi wake mkubwa alikuwa Sheikh Abdallah Bakathiir ambaye alihamia Zanzibar kutoka Lamu.

Sheikh Abdalla Bakathiir alidumu juu ya kufundisha na kueneza elimu hapo Ukutani na Msikiti Gofu kwa wanafunzi kutoka nchi mbali mbali Afrika ya Mashariki hadi kufariki kwake. Yalikuweko mapenzi makubwa sana baina ya Sheikh Abdallah Bakathiir na sheikh wake Habiib Ahmad bin Sumeit. Alipofariki Sheikh Abdallah mwezi 14 Shaaban, 1343H, Habiib Ahmad hakuwa na raha wala utulivu na akafariki miezi miwili baada yake. Alifariki Sheikh Abdallah Bakathir mwezi 14 Shaaban 1343, na Habiib Ahmad bin Sumeit mwezi 13 Shawwaal mwaka huo huo.

Alipofariki Habiib Ahmad bin Sumeit serikali walitaka kufanya mazishi rasmi (ya Kiserikali). Waliwapanga askari nje ya nyumba yake, lakini wakashindwa kutekeleza kutokana na wingi wa watu na msongomano kwa ajili ya kulibeba jeneza lake. Kila mtu akitaka jeneza liwe juu ya bega lake. Na jeneza halikufika msikiti mkubwa wa Ijumaa wa Malindi ila ulijaa msikiti ndani na nje, hata juu ya sakafu, na njia zikafungwa. Watu waliomsalia walikuwa wengi mpaka hawakuweza kunyanyua mikono yao kwa ajili ya swala kutokana kukamatana mabega yao. Walisimama pamoja waislamu wa madhehebu tofauti wakiswalishwa na Sheikh Pate, Habiib Abu Bakr bin Ahmad Aal Sheikh. Habiib Ahmad alizikwa nje ya msikiti wa Ijumaa Malindi.

Al-Habiib Umar bin Ahmad bin Sumeit

Huyu ni mtoto wa Habiib Ahmad bin Sumeit. Alizaliwa Habiib Umar Itsandaa-Ngazija, mwisho wa Dhil Hijja mwaka 1303H. Akalelewa na mama yake, kwani baba yake alikuwa Unguja.

Alipofikia umri wa miaka 6, alisafirishwa kupelekwa Unguja kwa baba yake. Alipofika umri wa miaka 8 alisafirishwa na baba yake kupelekwa Hadhramout apate kusoma. Akashukia Shibam kwa ammi ya baba yake Habiib Tahir bin Abdallah bin Sumeit na mtoto wake Habiib Abdallah. Akaenda sehemu mbali mbali za Hadhramout kama Tarim, Seiyun, Hawta na Ghurfa kwa ajili ya kusoma. Masheikh zake ni wengi sana, miongoni mwao ni Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy, Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy, Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas, Habiib Abdallah bin Hasan bin Saleh Al-Bahr, Habiib Umar bin Muhammad Al-Haddaad, Habiib Tahir bin Abdallah bin Sumeit na mtoto wake Habiib Abdallah, Habiib Ubeydillah bin Muhsin Al-Saggaaf, Habiib Abdul Rahman bin Muhammad Mash-hoor na mtoto wake Habiib Aliy, Habiib Ahmad bin Abdul Rahman Saggaaf, Habiib Muhammad bin Salim Al-Sariy, Habiib Ahmad Al-Juneid bin Ahmad Al-Juneid, Sheikh Abu Bakr bin Ahmad Al-Khatiib, Sheikh Hasan bin Awadh Mukhaddam, Habiib Abdallah Shatiry, Habiib Salim bin Hafiidh, Habiib Abdul Bariy bin Sheikh Al-Aydaroos, Habiib Mustafa bin Ahmad Al-Mihdhaar. Na miongoni mwa masheikh zake wa Haramain (Makka na Madina), ni pamoja na Sheikh Umar bin Abi Bakr Ba Juneid, Sheikh Umar Hamdaan Al-Mahrisiy, na Habiib Husain bin Muhammad Al-Habashy. Baadaye akarudi Unguja akasoma kwa baba yake na baadhi ya masheikh, akiwemo Sheikh Abdallah Ba Kathiir, Sheikh Said bin Dahman na Habiib Saleh Jamalillayl wa Lamu.

Kisha alihamia Ngazija kwa ajili ya kusomesha na kutafuta riziki ya halali, hadi alipo fariki baba yake mwaka 1343H, Habiib Umar akaenda Unguja kwa ajili ya kuangalia urithi wa baba yake. Kabla ya kwenda alimkabidhi duka lake na mali zake mmoja katika ndugu zake baada ya kuandikiana naye. Huko Unguja akakuta hali imebadilika na baba yake amewacha madeni. Habiib Umar akalipa madeni yote na na kushughulikia mambo yote mengine. Alipomaliza kutekeleza wajibu

wake kwa marehemu baba yake akarudi Ngazija. Yule aliyemwachia mali zake alikataa kumrudishia. Habiib Umar akamwomba amrudishie kadiri ya madeni ya watu tu, lakini pia akakataa. Bali yule mtu akamtishia kuwa atamwua Habiib Umar. Kwa kitisho chake hicho, akakamatwa na kuhukumiwa kwenda jela miaka 5. Habiib Umar akaenda Serikalini na kuomba asamehewe. Akashurutiwa atie saini kuwa likimtokea lolote serikali haitahusika. Habiib Umar akatia saini na kuachiwa mdaiwa wake.

Alipoona kuwa ana madeni ya watu na Ngazija imeshakuwa sehemu ngumu ya kuishi, akasafiri kwenda Madagascar kwa ajili ya kutafuta riziki na ili apate kulipa madeni. Alipata mtihani mkubwa huko kwani alikuwa akilala msikitini, na hakuwa na familia yake.

Baada ya miaka 10 ya mitihani, Al-Habiib akamwomba Mwenyezi Mungu ampe faraja, dua yake ilikubaliwa kwani aliitwa na Mfalme wa Zanzibar na kupewa ukadhi wa Pemba. Huo ulikuwa mwaka 1355. Alifanya kazi hiyo kwa miaka 2. Kisha alihamishiwa Unguja kuendelea na Ukadhi. Mwaka wa 1362 akateuliwa kuwa Kadhi Mkuu wa Zanzibar.

Habiib Umar alikuwa mtu wa ajabu katika nafasi yake ya ukadhi na aliacha gumzo kubwa miongoni mwa masheikh wa Zanzibar hadi miaka hii ya sasa. Tisa kwa kumi ya hukumu za Habiib Umar zilikuwa ni usuluhishi. Kila waliokwenda kwake wakiwa na uhasama, waliondoka kwake wameshapatana, wenye furaha, na wako radhi kila mmoja kwa mwenziwe, yaani hawana kinyongo tena. Katika kazi kubwa aliyoifanya akiwa kadhi, ni kuanzisha idara ya kusimamia wakfu, kwani kulikuwa na baadhi ya misikiti haina wakfu, na mingine ina wakfu, akazikusanya zote chini ya idara moja na kusimamia mapato na matumizi kwa misikiti yote. Misikiti ikaamirishwa, iliyobomoka ikatengenezwa na masurufu yakatumika kwa njia bora kabisa.

Nyakati za likizo zake Habiib Umar alifanya safari nyingi kwenda Haramain (Makka na Madina), na Hadhramout kuwazuru ndugu zake na kupata baraka za wazee wake na masheikh zake. Al-Habiib pia alizuru Misri na kupata bahati ya kushuhudia athari za Mtume(saw) alipokwenda Mash-had ya Sayyidna Husain.

Uadilifu aliodumisha akiwa Kadhi Mkuu wa Zanzibar haukuwafurahisha watu wote. Baadhi ya wenye tamaa za kidunia walipata uzito mkubwa, wakawa wanaanzisha chokochoko na kueneza fitina. Baadhi ya watu, kutokana na kutokuridhia hukumu ya Uislamu, wakawa wanakata rufaa katika Mahkama kuu ya Serikali wakiwa hawana woga wa ghadhabu za Mwenyezi Mungu. Al-Habiib akaona ni bora aache wadhifa huo, na mwaka 1379H akajiuzulu. Tukizingatia hatua hiyo tutafahamu kuwa uamuzi huo ulihitaji ucha Mungu mkubwa sana. Bila shaka haikubaliki kuwa na mahakama nyengine juu ya Qur'ani na Sunna.

Baada ya kujiuzulu ukadhi, akaendelea kukaa Unguja, akifanya kazi ya kusomesha na kulingania Dini ya Mwenyezi Mungu. Alikuwa na darasa msikiti wa Ijumaa Malindi baada ya Alasiri akisomesha kitabu cha "*Fat-hul-mui'in*". Darsa hiyo ilikuwa ikihudhuriwa na watu wengi sana. Kati ya waliokuwa wakihudhuria walikuwemo viongozi wa Serikali, matajiri na wafanya biashara. Ilimdhihirikia kuwa wengi wa watu hao hawakuwa wakifahamu na kunufaika ipasavyo na darasa iliyokuwa ikiendelea pale kutokana kiwango kidogo mno cha elimu zao za Dini. Al-Habiib akatumia hekima ya kuwaita vijana wadogo wachache na akawa anawasomesha kitabu cha Safiinatul Najaa, kabla ya kuanza darsa hasa ya wakubwa. Hiyo ilikuwa ni hekima ili hao viongozi na matajiri wapate kujua hukumu za udhu, swala na nyenginezo. Al-Habiib pia alikuwa na darasa nyengine msikitini na nyumbani kwake.

Habiib Umar alikuwa na ucha Mungu ambao mfano wake haukuonekana katika ardhi ya Zanzibar. Aliwaathiri wengi sana kwa ucha Mungu wake. Aliwacha athari nyingi na mapenzi makubwa miongoni mwa waislamu wa Zanzibar na alikubalika kuwa ndiye kiongozi wa waislamu wa Zanzibar na Afrika ya Mashariki hata baada ya kujiuzulu Ukadhi Mkuu. Heshima yake haikuanguka.

Al-Habiib alihama Unguja mwaka 1385H, mwaka mmoja baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kuelekea Shihr, Yemen. Huko akajenga nyumba yake, na kuendelea na kazi yake ya Da'awa na vikao vya kheri. Mwaka 1387H alihamia Ngazija, baada ya kuombwa na wakaazi wake arudi kwao alikozaliwa, kwani wanamhitajia zaidi, na wana haki zaidi

ya kufaidika na yeye. Huko Comoro alijenga nyumba yake katika mji wa Itsandaa. Watu kutoka nchi mbali mbali walikuwa wanakwenda Comoro kumkusudia, Zikaenea baraka zake kwa watu wake, na akabaki Ngazija hadi kufariki kwake.

Alikuwa Al-Habiib ni mwenye tabia bora kabisa, mpole mwenye huruma juu ya kila mwislamu. Njia yake ya Da'awa ilikuwa ni ya kubashiri na sio kutisha au kuogopesha. Akiwazidishia watu dhana nzuri kwa Mwenyezi Mungu na kuwabashiria fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema zake. Hata ikawa mwenye huzuni huondoka kwake akiwa moyo wake umejaa uchangamfu, furaha, kumtegemea Mwenyezi Mungu na kumtaraji. Muda wote Al-Habiib alikuwa anaifanyia kazi hadithi ya Mtume(saw) inayosema, **"Wabashirieni (wapeni khabari njema watu) wala musiwakimbize (kwa kuwatisha kwenu)"**.

Katika maisha yake Al-Habiib aliipa nyongo sana dunia. Alionesha kwa vitendo kuwa dunia haina thamani yoyote mbele yake. Chochote alichokipata alikitumia kwenye njia za kheri. Yeye mwenyewe, nafsi yake, alikuwa na nyumba ya kupanga. Lakini wageni wake aliwajengea majumba ya kifakhari yakiwa na mabustani nje ya mji kwa ajili ya kuwakirimu na kuwafurahisha.

Al-Habiib pia alikuwa akiwapa moyo wanaosoma. Wakimaliza kitabu huwafanyia karamu kubwa kwenye sehemu za matembezi na akiwaalika wanavyuoni wahudhurie. Yote hayo alikuwa akifanya kwa gharama zake, kwa ajili ya kuitukuza elimu na kuwapa moyo wanaosoma waendelee na kazi hiyo tukufu. Alipoondoka Zanzibar aliacha nyumba na mashamba yake na hakushughulika na mali hiyo tena, wala kuiuliza, bali aliridhia hukumu ya Mwenyezi Mungu. Alipokuwa Ngazija na kupata pesa hakutumia kitu kwa ajili ya nafsi yake, bali aliweka mahodhi kwa ajili ya kutoa huduma ya maji safi kwa wakaazi wake na kuweka sadaka ya kudumu. Akiwasaidia mafakiri na wahitaji, na misaada yake ilienea kila alipokaa bali aliifikisha hadi Hadhramout kwa ndugu na jamaa zake. Al-Habiib pia alikuwa ni mtu mwenye subira sana juu ya mitihani aliyoipata katika kila hali. Hamwombei dua mbaya yeyote mwenye kumkosea bali husamehe na kumfanyia wema akifuata mwenendo wa Mtume(saw).

Al-Habiib Umar alijaaliwa kupata mapenzi makubwa katika mioyo ya watu, na kupata kabuli kubwa. Hii inaonyesha mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume(saw) wake juu yake, kwani amesema Mtume(saw): **“Hakika Mwenyezi Mungu akimpenda mja humwita Jibriil na kumwambia mimi nampenda fulani basi umpende na wewe. Anasema: kisha hupendwa na Jibriil, kisha hunadiwa mbinguni, atasema, hakika Mwenyezi Mungu anampenda fulani, basi mpendeni, watampenda watu wa mbinguni, kisha huwekewa kabuli ardhini ...”**

Alifariki Al-Habiib Itsandaa usiku wa kuamkia Jumanne tarehe 9 Safar 1396H ikiwafikiana na tarehe 10 Feb 1976M, akiwa na umri ulio karibia miaka 93. Akasindikizwa na halaiki ya watu na kuzikwa kwenye kuba la babu yake Habiib Abubakr bin Abdallah bin Sumeit.

Sanad ya Aali Ba Alawiy:

Sanad ya wakaazi wengi wa Afrika Mashariki imepitia kwa Habiib Umar bin Sumeit ambaye tumemtaja hapa juu, na yeye amechukua kwa baba yake Habiib Ahmad bin Sumeit ambaye amechukua kwa masheikh wa Hadhramout kama ambavyo silsila inavyoonyesha hapa chini.

Njia ya Sanad kupitia kwa wazee hadi kwa Mtume(saw).

Al-Habiib Umar bin Ahmad bin Sumeit anaitaja sanad yake kwenye kitabu "*Hadiyyatul Ikhwaan*"

“Na wa kwanza na wa mwisho tuliyechukua kwake ni

- bwana wangu na baraka yangu, baba (yangu) Allama Ahmad bin Abi Bakr bin Abdallah bin Sumeit naye
- kwa walio katika zama zake, wa mwisho wao akiwa maimamu wawili Qutb wawili, Aliy bin Muhammad bin Husain Al-Habashy na Ahmad bin Hasan bin Abdillah Al-Attaas,
- na wao kwa walio katika zama zao wa mwisho wao Imaam, Al-Qutb Aydaroos bin Umar Al-Habashy,
- naye kwa maimamu wawili Abdallah bin Husain bin Tahir na Hasan bin Saleh Al-Bahr na walio katika zama zao,
- kwa maimamu wawili Ahmad bin Umar bin Sumeit na AbdulRahman bin Alawiy Mawlal-Butaihaa na walio katika zama zao,
- kwa maimamu wawili Haamid bin Umar Haamid na Aliy bin Sheikh bin Shihaabul-Diin na walio katika zama zao,
- kwa Imaam Hasan bin Abdillah Al-Haddaad na aliye kwenye zama zake,
- kwa Imaam Abdillah bin Alawiy Al-Haddaad na aliye kwenye zama zake,

- kwa Imaam Umar bin AbdulRahman Al-Attaas na aliye kwenye zama zake,
- kwa Imaam Husain bin Sheikh Abu Bakr bin Saalim na aliye kwenye zama zake,
- kwa Sheikh Abu Bakr bin Saalim na aliye kwenye zama zake,
- kwa Imaam Sheikh Shihaabul-Diin bin AbdulRahman na aliye kwenye zama zake,
- kwa baba yake Imaam AbdulRahman bin Aliy na Sheikh Abu Bakr Al-Aydaroos na walio kwenye zama zao,
- kwa Imaam Sheikh Abdallah Aydaroos na ndugu yake Sheikh Aliy bin Abu Bakr,
- kwa baba yao Imaam Sheikh Au Bakr Sakaraan na ammi yao Imaam Sheikh Umar Al-Mihdhaar na walio katika zama zao
- kwa baba yao Sheikh AbdulRahman Al-Saggaaf na aliye kwenye zama zake,
- kwa baba yake Imaam Sheikh Muhammad bin Aliy Mawla Dawiila na aliye kwenye zama zake,
- kwa maimamu wawili masheikh wawili Abdallah na Aliy watoto wa Alawiy bin Al-Faqiih na walio katika zama zao,
- kwa baba yao Imaam Sheikh Alawiy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam na aliye kwenye zama zake,
- kwa baba yake Imaam, Sayyidna Al-Faqiih Al-Muqaddam Muhammad bin Aliy na aliye kwenye zama zake,
- kwa baba yake Sheikh Aliy bin Muhammad na aliye kwenye zama zake,
- kwa (baba yake) Imaam Sheikh Muhammad Saahib Mirbaat,
- kwa baba yake Sheikh Aliy Khaali Qasam

- kwa baba yake Sheikh Alawiy bin Muhammad,
- kwa baba yake Sheikh Muhammad bin Alawiy,
- kwa baba yake Imaam Alawiy bin Ubeydillah,
- kwa baba yake Imaam Ubeydillah bin bin Ahmad,
- kwa baba yake Imaam Al-Muhaajir ila Allah Ahmad bin Isa,
- kwa baba yake Imaam Isa bin Muhammad,
- kwa baba yake Imaam Muhammad bin Aliy,
- kwa baba yake Imaam Aliy Ureidhiy,
- kwa kaka yake Imaam Musa Al-Kaadhim, na wote wawili kwa kwa baba yao Imaam Ja'far Saadik,
- kwa Imaam Muhammad Al-Baaqir,
- kwa baba yake Imaam Zaynil Abidina Aliy bin Husain,
- kwa baba yake Sayyidna Imaam Husain Al-Sibti,
- kwa baba yake Sayyidna Amirul Muuminina Aliy bin Abi Talib-Mwenyezi Mungu autukuze uso wake-, na pia kwa mama yake Fatima Al-Zahraa-Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote-,
- kwa Mtume(saw) –Rehema na amani zimshukie-
- kwa Jibriil mwaminifu
- kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka na kutakasika."

Na Sayyid AbdulQadir Juneid ametengeneza na kupanga sanad hii, nasi tunaweka mchoro uliofanana na sanad aliyoiandika.


Sayyidna Muhammad RasooluLlah (SAW)
Sayyidna Aliy bin Abi Talib
Sayyidna Husain bin Aliy
Imaam Aliy Zaynil Abidina bin Husain
Imaam Muhammad Al-Baaqir bin Aliy
Imaam Ja'far Saadik bin Muhammad Al-Baaqir
Imaam Aliy Ureidhiy bin Ja'far Saadik
Imaam Muhammad bin Aliy Al-Ureidhiy
Imaam Isa Al-Naqiib bin Muhammad
Imaam Al-Muhaajir Ahmad bin Isa
Imaam Ubeydillah bin Ahmad bin Isa
Imaam Alawiy bin Ubeydillah
Imaam Muhammad Saahib Sawmaa' bin Alawiy
Imaam Alawiy bin Muhammad
Imaam Aliy Khaali Qasam bin Alawiy
Imaam Muhammad Saahib Mirbaat bin Aliy
Imaam Aliy bin Muhammad Saahib Mirbaat
Al-Faqiih Al-Muqaddam Muhammad bin Aliy
Sheikh Alawiy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam Muhammad
Sheikh Alawiy bin Alawiy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam
Sheikh Muhammad Mawla Dawiila bin Aliy
Sheikh Abdul Rahman Saggaaf bin Muhammad
Sheikh Abu Bakr Sakaraan bin Abdul Rahman Saggaaf
Sheikh Abdullah Aydaroos bin Abu Bakr
Sheikh Aliy bin Abu Bakr Sakraan
Sheikh Abdul Rahman bin Aliy bin Abu Bakr
Sheikh Ahmad bin Abdul Rahman bin Aliy
Sheikh Abu Bakr bin Salim
Sheikh Husain bin Abu Bakr bin Salim
Al-Habiib Umar bin Abdul Rahman Al-Attaas
Al-Habiib Abdillah bin Alawiy Al-Haddaad
Al-Habiib Hasan bin Abdillah Al-Haddaad
Al-Habiib Ahmad bin Hasan Al-Haddaad
Al-Habiib Abdul Rahman bin Abdullah Balfaqiih
Al-Habiib Alawiy bin Ahmad Al-Haddaad
Al-Habiib Abdul Rahman bin Alawiy Mawla Butaihaa
Al-Habiib Hasan bin Saleh Al-Jufriy
Al-Habiib Abdullah bin Umar bin Yahya
Al-Habiib Abdullah bin Husain Bal Faqiih
Al-Habiib Abdullah bin Husain bin Tahir
Al-Habiib Ahmad bin Aliy bin Haroon Al-Juneid
Al-Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy
Al-Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy
Al-Habiib Abdul Rahman bin Muhammad Mash-hoor
Al-Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas
Al-Habiib Ahmad bin Abdul Rahman Al-Saggaaf
Al-Habiib Alawiy bin Abdullah bin Shihaab
Al-Habiib Salim bin Hafiidh Aal Sheikh
Al-Habiib Ahmad bin Abu Bakr bin Sumeit
Al-Habiib Muhammad bin Hadiy Al-Saggaaf
Al-Habiib Abdallah bin Tahir Al-Haddaad
Al-Habiib Abdallah bin Umar Shatiry
Al-Habiib Umar bin Ahmad bin Sumeit

Njia ya pili ya sanad

Njia ya pili ya sanad ni kutoka kwa Al-Faqiih ikipitia kwa Sheikh Abu Madyan kwa wasita wa Sheikh AbdulRahman Al-Muq-a'd na Sheikh Abdallah Saleh Al-Maghribiy.

1. Al-Faqiih Al-Muqaddam Muhammad bin Aliy Ba Alawiy
2. Sheikh Abu Madyan Shua'yb bin Abil-Hasan Al-Tilmisaniy Al-Maghribiy
3. Sheikh Abu Ya-'zaa Al-Maghribiy
4. Sheikh Aliy bin Harazim au ibn Hirzihim
5. Sheikh Abubakr Muhammad bin Abdillah bin Al-Arabiy Al-Maa'firiy
6. Al-Imaam Abi Hamid Muhammad bin Muhammad Al-Ghazaliy Al-Tuusiy
7. Imaam Al-Haramain Abdul Malik bin Muhammad Al-Juwayniy
8. Imaam Muhammad bin Abdallah bin Yusuf bin Abdillah Al-Juwayniy
9. Imaam Abu Talib Al-Makkiy Muhammad bin Aliy bin Atiyya Al-Haarithiy mwandishi wa *Quut Al-Quluub*
10. Imaam Abubakr Shibliy
11. Imaam Abul-Qasim Juneid bin Muhammad
12. Imaam Abil Hasan Al-Sariy bin Al-Mughallis Al-Saqatiy
13. Imaam Ma'roof Al-Karkhy
14. Imaam Al-Habiib Al-Ajamiy
15. Imaam Al-Hasan Al-Basriy
16. Sayyidna Aliy bin Abi Talib
17. Mtume(saw) Muhammad-rehema na amani zimshukie.

Riwaya nyengine ni kutoka kwa Imaam Al-Ma'roof Al-Karkhy amechukua kutoka kwa Imaam Aliy Ridhaa, nae kutoka kwa baba yake Imaam Musa Al-Kaadhim, nae kutoka kwa baba yake Imaam Ja'afar Saadik. Nae kutoka kwa baba yake Imaam Muhammad Al-Baaqir, nae kutoka kwa baba yake Imaam Aliy Zainil Abidina, nae kutoka kwa baba yake Sayyidna Husain, nae kutoka kwa baba yake Sayyidna Aliy bin Abi Talib, nae kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-rehema na amani zimshukie.

MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA

Faharasa

UTANGULIZI: 2
YALIYOMO 4
UTUKUFU WA AHLIL BAYT 8
Aya za Qur-an zinazowaelezea Ahlil Bayt 9
Hadithi za Mtume(saw) zinazowaelezea Ahlil-bayt: 17
Mtume(saw) katuwachia kizazi chake: 17
Mahdy ni mjukuu wa Mtume(saw): 21
Ubora wa Ahlil-Bayti. 22
Kujihadhari na kuwachukia Ahlil-bayti. 25
Mwenye kuwafanyia wema atalipwa na Mtume(SAW). 27
Ahlul-Bayti watapata matatizo sana duniani 27
Maneno ya Masahaba na Salaf katika kuwazungumzia Ahlil-bayti. 28
Wajibu wa Ahlil-bayti: 31
Masahaba wa Mtume(SAW). 34
TARJAMA YA AHLIL KISAA 36
Mtume Muhammad (SAW): 37
Nasabu ya Mtume(saw): 37
Historia ya wazee wake: 38
Kisa cha nuru ya Mtume(saw): 39
Kushika mimba ya Mtume(saw) na kufariki kwa Bwana Abdillah: 39
Kuzaliwa kwake Mtume(saw): 40
Majina ya Mtume(saw): 40
Waliomnyonyesha Mtume(saw) 41
Kufariki Mama yake: 42
Kulelewa na Babu yake: 42
Kulelewa na Ammi yake: 42
Safari ya Shaam: 42
Kwenda Shaam kwa mali ya Bibi Khadija: 43
Kuolewa Bi. Khadija na Mtume(saw): 43
Kutetea madhaifu (wanyonge): 44
Kujenga Ka'aba: 46
Dalili za utume wake kabla ya kushuka kwa wahyi: 46
Jinsi ulivyokuwa ukishuka wahyi: 47
Kulingania Uislamu kwa siri: 48
Watu wa mwanzo kusilimu: 48

Kulingania kwa dhahiri: 48
Makureshi na mlingano wao kwa Abi Talib: 49
Kukatwa pande Baniy Hashim na Baniy Muttalib na kwenda kwao kwenye Shiib (kiunga cha) Abi Talib: 50
Kwenda Twaif: 52
Israi na Miiraji: 53
Maudhi aliyoyapata Mtume(saw) kutoka kwa washirikina: 53
Kulingania kwake wakati wa misimu: 54
Kuhama Mtume(saw) kwenda Madina: 56
Mwaka wa kwanza baada ya Kuhama: 59
Mwaka wa pili baada ya Kuhama: 60
Mwaka wa tatu baada ya kuhama: 60
Mwaka wa nne baada ya kuhama: 61
Mwaka wa tano baada ya kuhama: 61
Mwaka wa sita baada ya kuhama: 62
Mwaka wa saba baada ya kuhama: 62
Mwaka wa nane baada ya kuhama: 62
Mwaka wa tisa baada ya kuhama: 63
Mwaka wa kumi baada ya kuhama: 63
Mwaka wa kumi na moja baada ya kuhama: 63
Kufariki kwa Mtume(saw): 63
Kupigwa na butwaa kwa masahaba kwa kufariki Mtume(saw) na khutba ya Sayyidna AbuBakr: 65
Kuoshwa kwa Mtume(saw) na kuzikwa kwake: 66
Tabia njema za Mtume(saw): 66
Mifano ya Unyenyekevu wake: 67
Mfano wa Huruma yake: 67
Mifano ya Kusamehe kwake: 68
Mifano ya Ukarimu wake: 68
Mifano ya Ushujaa wake: 69
Mifano ya Ibada za Mtume(saw) na jitihada zake: 69
Mifano katika maisha yake na hali ya uduni aliyokuwa nayo: 70
Miujiza yake: 71
Utukufu wake juu ya manabii wengine: 71
Mapenzi ya Mtume(saw): 73
Kumpenda Mtume(saw) ni katika Imani: 73
Mwenye Kumpenda Mtume(saw) ataonja ladha ya Imani: 73
Kumpenda Mtume(saw) ni wajib: 73

Kumpenda Mtume(saw) kutasababisha kuwa naye siku ya Kiyama: 73
Mapenzi ya Mtume(saw) juu ya Waislamu: 75
Mapenzi ya Mtume(saw) juu ya watakao kuja baada yake na kumuamini: 75
Kumpenda Mtume(saw) ni kufuata aliyokuja nayo: 75
Kumwona Mtume(saw) usingizini: 76
Kutukuzwa kwake na masahaba wake na mapenzi yao juu yake: 76
Kufikishwa kwake salamu za umma wake: 77
Wakeze Mtume(saw)- Mamama wa Waislamu: 77
Mama Khadija bint Khuwaylid(ra). 77
Mama Sawda bint Zam-ah(ra). 79
Mama Aisha bint Abi Bakr(ra). 79
Mama Hafsa bint Umar bin Khattab(ra). 81
Mama Zaynab bint Khuzaymah(ra). 82
Mama Ummu Salamah Hind bint Abi Umayya Al-Makhzumiya(ra). 82
Mama Ummu Habiba Ramlah bint Abi Sufyaan(ra). 83
Mama Zaynab bint Jahsh(ra). 84
Mama Juwayriya bint Al-Harith(ra). 85
Mama Safiyya bint Huyay bin Akhtab(ra). 86
Mama Maymuna bint Al-Harith Al-Hilaaliyya. 87
Watoto wa Mtume(saw): 88
Bibi Zaynab(ra) 88
Bibi Ruqayya(ra) 90
Bibi Ummu Kulthuum(ra) 91
Ammi zake Mtume(saw): 93
Sayyidna Hamza bin Abdil Muttalib 93
Sayyidna Abbas bin Abdil Muttalib 95
Shangazi zake: 98
Sayyidatna Safiyya bint Abdil Muttalib 98
Sayyidatna Fatima. 99
Sayyidna Aliy 103
Kusilimu kwake 103
Kujitoa muhanga kwa ajili ya Mtume(saw) 103
Kupanda mabegani mwa Mtume(saw) 104
Kupendwa na Mwenyezi Mungu na Mtume(saw) wake na kila mwislamu 104
Ushujaa wake 106
Elimu yake 107

Udugu wake na Mtume(saw). 107
Mawla (Bwana) wa kila Muumini 108
Ucha Mungu wake na kuipa nyongo dunia. 109
Kumshirikisha Mtume(saw) kwenye wanyama wake wa sadaka. 111
Yaliyojiri baina ya masahaba. 111
Maneno ya Aali Ba Alawiy kuhusu yaliyojiri baina ya masahaba 112
Maneno ya Sayyidna Aliy kuhusu ukhalifa 116
Kuuawa kwake: 118
Wasiya wake wa mwisho. 119
Baadhi ya maneno yake ya Hikma. 119
Sayyidna Hasan bin Aliy 123
Kufariki kwake. 124
Wasiya wake kwa ndugu yake Bwana Husain. 125
Kizazi cha Sayyidna Hasan 125
Bwana Hasan Muthanna 125
Bwana Abdallah Al-Mahdh: 126
Bwana Muhammad Nafsul Zakiyya 127
Sayyidna Husain bin Aliy. 129
Maneno ya Ba Alawiy kuhusu kueleza kisa cha Bwana Husain. 130
ASILI YAO 134
Imaam Aliy Zainil Abidina: 135
Imaam Muhammad Baaqir. 141
Imaam Jaafar Saadik: 143
Imaam Aliy Ureidhy: 145
Imaam Muhammad bin Aliy: 146
Imaam Isa Naqiib: 147
WAASISI WA BA ALAWIY 148
Kuhamia kwao Hadhramout: 149
Maneno ya baadhi ya Ba Alawy kuhusu Al-Muhaajir. 153
Imaam Abdallah bin Ahmad bin Isa. 154
Kuthibitishwa nasabu yao. 155
Imaam Aliy bin Alawiy (Khaali Qasam). 156
Imaam Muhammad bin Aliy (Saahib Mirbaat) 157
Muhammad bin Aliy Ba Alawiy (Al-Faqiih Al-Muqaddam) 158
Maneno ya Ba Alawiy kuhusu Al-Faqiih Al-Muqaddam. 161
Tasawwuf: 163
Maneno ya wanavyuoni juu ya Tasawwuf 164
Maneno ya Aali Ba Alawiy kuhusu Tasawwuf 166

Tariqa ya Aali Ba Alawiy: 168
Maana ya kuwa Dhahir ni Ghazaaliya na Batin ni Shadhiliyya ... 170
Maneno ya Sheikh Yusuf Ismail Nabahaniy: 171
Maneno ya Sheikh Muhammad bin Ahmad Ba Jarfiil 172
Maneno ya Sheikh Ahmad (Shahiid) bin Abdallah Bafadhl 172
BAADHI YA VIONGOZI WA AALI BA ALAWIY 174
Sheikh Abdallah bin Alawiy bin Al-Faqiih Al-Muqaddam: 177
Sheikh Abdul-Rahman Saggaaf 181
Sheikh Umar Mihdhaar bin Abdul Rahman Saggaaf 184
Sheikh Abdallah Aydaroos bin Abi Bakr bin Abdul Rahman Saggaaf 187
Sheikh Abubakar Al-Adany bin Abdallah Aydaroos 190
Sheikh Abu bakr bin Salim 195
Al-Habiib Umar bin Abdul-Rahman Al-Attaas: 197
Al-Habiib Abdillah Al-Haddaad: 199
Al-Habiib Ahmad bin Zayn Al-Habashy: 207
Al-Habiib Umar bin Saggaaf Al-Saafiy Al-Saggaaf 212
Al-Habiib Ahmad bin Umar bin Sumeit 215
Al-Habiib Aydaroos bin Umar Al-Habashy 220
Al-Habiib Aliy bin Muhammad Al-Habashy 223
Al-Habiib Ahmad bin Hasan Al-Attaas 228
Al-Habiib Abdallah Shatiry 234
AALI BA ALAWIY AFRIKA MASHARIKI 240
Kuingia Uislamu Afrika Mashariki 241
Makabila Ya Ba Alawiy yaliyopo Afrika Mashariki 243
Aal Sheikh Abi Bakr bin Salim: 243
Aal Jamalillayl 244
Aal Aideed: 245
Aal Ba Faqiih 246
Aal Ba Faraj 246
Aal Saggaaf 246
Aal Nadhiiry 247
Aal bin Sumeit 248
Aal Masiliy 249
Aal Shatiriy 249
Aal Bunumay 250
Aal Attaas 251
Aal Aydaroos 251

Aal Basukutah 252
Aal Habashy 252
Aal Haddaad 253
Aal Al-Baar 253
Aal Al-Biidh 254
Aal Musawa 254
Aal Al-Juneid 255
Aal Al-Ahdal 256
Al-Habiib Saleh bin Alawiy Jamalillayl 257
Al-Habiib Ahmad bin Sumeit 259
Al-Habiib Umar bin Ahmad bin Sumeit 265
Sanad ya Aali Ba Alawiy: 270
Njia ya Sanad kupitia kwa wazee hadi kwa Mtume(saw). 270
Njia ya pili ya sanad 274